
ELLEN G. WHITE

# UZOEFU WA KIKRISTO

## NA MAFUNDISHO YA ELLEN.G.WHITE





## YALIYOMO


**1....UTOTO** ....................................................................................................4
AJALI ........................................................................................................
ELIMU…………………………………………………………………………
**2....UONGOFU** ....................................................................................................6
**3....MWANZO WA KAZI ZA HADHARA** ..................................................................... 10
**4. IMANI YA MAREJEO** ......................................................................................20
**5. KUKATA TAMAA** ..........................................................**Error! Bookmark not defined.**
**6. MAONO YANGU YA KWANZA** .......................................**Error! Bookmark not defined.**
**7. MAONO YA NCHI MPYA** ................................................................................ 65
**8. WITO WA KUSAFIRI** ....................................................... **Error! Bookmark not defined.**
**9. KUKUTANA NA USHUPAVU WA KIDINI** ......................................................... 43
**10. SABATO YA BWANA** ...................................................................................... 50
**11. NDOA NA KUFANYA KAZI WA PAMOJA** ...................**Error! Bookmark not defined.**
**12. PATAKATIFU PA MBINGUNI** ........................................................................ 55
**13. UPENDO WA MUNGU KWA WATU WAKE** .........................................................58
**14. KUTIWA MUHURI** ..........................................................................................60
**15. JARIBU LA IMANI YETU** ............................................... **Error! Bookmark not defined.**
**16. KWA KUNDI DOGO** ........................................................6**Error! Bookmark not defined.**
**17. KUTIKISWA KWA NGUVU ZA MBINGUNI** ....................................................... 66
**18. MAANDALIZI KWA AJILI YA MWISHO** ............................................................ 67
**19. MAPAMBANO NA UMASKINI** ...........................................................................68
**20. MAJALIWA YA MUNGU YANAYOTIA MOYO** ...........**Error! Bookmark not defined.**
**21. MAOMBI NA IMANI** ..........................................................................................76
**22. KUANZA KUCHAPISHA** ...................................................................................78
**23. KUTEMBELEA NDUGU** ......................................................................................81
**24. KUCHAPISHA TENA** ......................................................... **Error! Bookmark not defined.**
**25. KUONDOKA MICHIGANI** ....................................................................................93
**26. NJIA MBILI** ..................................................................................................... 95
**27. TAJI MBILI** ........................................................................................................98
**28. UMIZIMU WA KISASA** ...................................................................................... 102

29. MITEGO YA SHETANI ..... 104
30. PEPETO ..... 106
31. KUSAFIRI KATIKA NJIA NYEMBAMBA ..... 109
32. KUJITAYARISHA KWA AJILI YA HUKUMU ..... 112
33. MUUNDO NA MAENDELEO ..... Error! Bookmark not defined.
34. UPENDO WA MUNGU KWA KANISA ..... Error! Bookmark not defined.
35. KAZI YA UMISHENARI ..... Error! Bookmark not defined.
36. MIPANGO MIKUBWA ZAIDI ..... Error! Bookmark not defined.
37. KUPANUA KAZI KATIKA NCHI ZA KIGENI ..... Error! Bookmark not defined.
38. KUSAMBAZA KURASA ZILIZOCHAPWA ..... Error! Bookmark not defined.
39. MTAZAMO WA PAMBANO ..... Error! Bookmark not defined.
40. THAWABU YA JUHUDI YA DHATI ..... Error! Bookmark not defined.
KIAMBATISHO ..... Error! Bookmark not defined.
KUPIMWA KWA NENO LA MUNGU ..... Error! Bookmark not defined.
VYANZO ..... Error! Bookmark not defined.

KIMETAFSIRIWA KUTOKA KATIKA KITABU
CHRISTIAN EXPERIENCE OF EGW

**ASANTE KWA BABA WA MBINGUNI NA WATAFSIRI, WAHARIRI, WASHAURI, WASOMAJI, WANAUFUNDI**

**Nhandi Masunga-Dodoma, Tanzania**

**Daudi Masaka-Carolina, Marekani**
**Judi and John Mugane-Boston, Marekani**
**Lisa Lothian-New York, New York**
**Sandra Barron-Carolina, Marekani**
**Daniel Masaka-Jersey, Marekani**
**Grace Momadi-Masaka-Jersey, Marekani**

# 1. UTOTO

Nilizaliwa huko Gorham, jimbo la Maine, tarehe 26 Novemba 1827. Wazazi wangu, Robert na Eunice Harmon, waliishi katika jimbo hili kwa miaka mingi. Wakiwa bado katika umri wa ujana waligeuka na kuwa washiriki waaminifu na waliojitoa wa Kanisa la Methodist Episcopal. Ndani ya kanisa hilo walikuwa na nafasi ya heshima, na walijishughulisha kwa bidii kuwaleta wenye dhambi kwa Kristo na kuijenga kazi ya Mungu kwa kipindi cha miaka arobaini. Katika muda huo walipata furaha ya kuona watoto wao wote wanane wakimgeukia Kristo na kuunganishwa katika zizi Lake.**[CETsw 13.1]**

## AJALI

Nilipokuwa bado mtoto, wazazi wangu walihama kutoka Gorham kwenda Portland, jimbo la Maine. Huko, nilipokuwa na umri wa miaka tisa, nilipatwa na ajali ambayo ilikuja kuathiri maisha yangu yote. Nilipokuwa pamoja na dada yangu pacha na mmoja wa wanafunzi wenzetu, tulikuwa tukivuka uwanja wa wazi katika mji wa Portland, ndipo msichana mmoja aliyekuwa na umri wa takriban miaka kumi na mitatu alikasirishwa na jambo dogo lisilo na umuhimu, akarusha jiwe lililonipiga puani. Pigo hilo lilinifanya nipoteze fahamu, nikaanguka chini na  nikiwa nimezimia.**[CETsw 13.2]**

Nilipopata fahamu tena, nilijikuta katika duka la mfanyabiashara. Mtu mmoja mkarimu nisiyemfahamu alijitolea kunipeleka nyumbani kwa gari lake, lakini kwa kuwa sikuwa nimetambua jinsi nilivyokuwa dhaifu kutokana na jeraha langu, nilimwambia kwamba nilipendelea kutembea. Wale waliokuwapo hawakutambua kwamba nilikuwa nimejeruhiwa vibaya kiasi hicho, hivyo wakaniacha niende. Hata hivyo, baada ya kutembea umbali mfupi tu, nilianza kuhisi udhaifu na kizunguzungu.Dada yangu pacha, pamoja na mwanafunzi mwenzetu walinibeba na kunipeleka nyumbani.**[CETsw 13.3]**

Kwa muda fulani baada ya ajali hiyo, sikukumbuka jambo lolote lililotokea. Mama yangu alisema kwamba sikuonyesha dalili zozote za kutambua kilichokuwa kikiendelea, bali nililala nikiwa katika hali ya kupoteza fahamu kwa muda wa majuma matatu. Hakuna mtu, isipokuwa yeye peke yake, aliyedhani kwamba ningeweza kupona; lakini kwa sababu fulani alikuwa na imani kwamba ningeendelea kuishi.**[CETsw 14.1]**

Nilipopata fahamu tena, ilionekana kwangu kana kwamba nilikuwa nimelala tu. Sikukumbuka ajali ile, wala sikujua kilichokuwa kimesababisha ugonjwa wangu. Kwa ajili yangu, kilitengenezewa kitanda kikubwa cha watoto wachanga, na humo nililala kwa majuma mengi. Mwili wangu ulikuwa umedhoofika sana kiasi kwamba nilibaki ngozi na mifupa tu (kiunzi).**[CETsw 14.2]**

Wakati huo nilianza kumwomba Bwana aniandae kwa ajili ya kifo. Marafiki Wakristo walipotembelea familia yetu, walikuwa wakimuuliza mama yangu ikiwa alikuwa amezungumza nami kuhusu kufa. Niliposikia mazungumzo hayo, yaliamsha moyo wangu na kunifanya

nitafakari. Nilitamani kuwa Mkristo, na nikasali kwa bidii ili nipate msamaha wa dhambi zangu. Nilihisi amani ya moyo iliyotokana na jambo hilo, nami nikaanza kuwapenda watu wote, nikitamani kwamba wote wapate kusamehewa dhambi zao na kumpenda Yesu kama nilivyokuwa nikifanya mimi.**[CETsw 14.3]**

Nilipata nguvu taratibu sana. Nilipoanza kuwa na uwezo wa kushiriki katika michezo pamoja na marafiki zangu wadogo, nililazimika kujifunza somo chungu kwamba mara nyingi mwonekano wetu wa nje huleta tofauti katika namna tunavyotendewa na wenzetu.**[CETsw 14.4]**

**ELIMU**

Afya yangu ilionekana kuwa imeharibika kabisa bila matumaini ya kuimarika. Kwa muda wa miaka miwili sikuweza kupumua kupitia pua yangu, na niliweza kuhudhuria shule kwa shida sana. Ilionekana kuwa haiwezekani kwangu kusoma na kukumbuka yale niliyokuwa nimejifunza. Msichana yuleyule aliyekuwa chanzo cha mkasa wangu, aliteuliwa kuwa kiongozi wa darasa na mwalimu wetu, na miongoni mwa majukumu yake ilikuwa kunisaidia katika kuandika na masomo mengine. Daima alionekana kuwa na huzuni ya kweli kwa sababu ya jeraha kubwa alilonisababishia, ingawa nilikuwa mwangalifu nisimsimulishe wala kumkumbusha jambo hilo. Alikuwa mpole na mvumilivu kwangu, na alionekana kuwa mwenye huzuni na mwenye kutafakari aliponiona nikijitahidi kupata elimu huku nikikabiliwa na vikwazo vikubwa.**[CETsw 14.5]**

Mfumo wangu wa neva/fahamu ulikuwa umedhoofika sana, na mkono wangu ulikuwa ukitetemeka kiasi kwamba niliweza kuwa na maendeleo madogo sana katika kuandika; niliweza kutekeleza tu mazoezi rahisi ya mwandiko wa herufi kubwa na zisizo laini au za kupendeza. Nilipojitahidi kuelekeza akili yangu katika masomo yangu, herufi zilizokuwa kwenye ukurasa zilionekana kuungana pamoja, matone makubwa ya jasho yalisimama kwenye paji la uso wangu, na hali ya udhaifu pamoja na kizunguzungu vilinishika. Nilikuwa na kikohozi kibaya, na mwili wangu wote ulionekana kuwa umedhoofika.**[CETsw 15.1]**

Walimu wangu walinishauri niache shule, na nisiendelee na masomo yangu hadi afya yangu itakapokuwa imeimarika. Lilikuwa jaribu gumu zaidi katika maisha yangu ya ujana kukubali udhaifu wangu, na kuamua kwamba nilipaswa kuacha masomo yangu na kuachana na tumaini la kupata elimu.**[CETsw 15.2]**

## 2. UONGOFU

Mnamo Machi mwaka 1840, William Miller alitembelea Portland, jimbo la Maine, na kutoa mfululizo wa mihadhara kuhusu ujio wa pili wa Kristo. Mihadhara hiyo ilileta msisimko mkubwa, na kanisa la Kikristo lililokuwa katika Mtaa wa Casco, ambako hotuba hizo zilitolewa, lilijaa watu mchana na usiku. Hakukuwa na msisimko wa kupita kiasi uliotawala katika mikutano hiyo, bali hali ya unyenyekevu na kicho ilitawala mioyo ya wale waliosikiliza. Sio tu kwamba watu wa mjini pekee walionyesha shauku kubwa, bali pia watu wa vijijini walimiminika huko siku baada ya siku, wakileta vikapu vyao vya chakula cha mchana na kubaki kuanzia asubuhi hadi mwisho wa mkutano wa jioni.**[CETsw 16.1]**

Nikiwa pamoja na marafiki zangu, nilihudhuria mikutano hiyo. Bwana Miller alieleza unabii kwa usahihi mkubwa kiasi kwamba, iliwafanya wasikilizaji wake kusadiki moyoni. Alizungumzia vipindi vya kinabii, na akatoa ushahidi mwingi ili kutetea msimamo wake. Kisha maonyo yake mazito na yenye nguvu pamoja na maombi yake ya dhati kwa wale ambao hawakuwa tayari, yaliwafanya umati wa watu kubaki wakiwa wametulia na kuvutiwa kwa umakini sana, kana kwamba walikuwa wameshikwa na nguvu isiyoonekana.**[CETsw 16.2]**

### Uamsho wa Kiroho

Mikutano maalumu iliandaliwa ili wenye dhambi wapate nafasi ya kumtafuta Mwokozi wao na kujiandaa kwa ajili ya matukio ya kutisha yaliyokuwa karibu kutokea. Hofu na usadikisho vilienea katika mji mzima. Mikutano ya maombi ilianzishwa, na kulikuwa na mwamko mkubwa miongoni mwa madhehebu mbalimbali; na madhehebu yote kwa kiwango fulani yalihisi mvuto uliotokana na mafundisho kuhusu kuja kwa Kristo kulikokuwa karibu.**[CETsw 16.3]**

Wenye dhambi walipoalikwa kusogea mbele kwenye viti vya walio na shauku ya kutafuta wokovu, mamia waliitikia mwito huo; nami, nikiwa miongoni mwao, nilijikongoja katikati ya umati wa watu na kuchukua nafasi yangu pamoja na wale waliokuwa wakitafuta wokovu. Lakini moyoni mwangu kulikuwa na hisia kwamba nisingeweza kamwe kustahili kuitwa mtoto wa Mungu. Mara nyingi nilikuwa nimetafuta amani ile ipatikanayo ndani ya Kristo, lakini sikuweza kuupata ule uhuru nilioutamani. Huzuni kubwa sana ilikuwa imeutawala moyo wangu. Sikuweza kufikiria jambo lolote nililokuwa nimelifanya lililosababisha nijisikie hivyo; lakini ilionekana kwangu kwamba sikuwa mwema vya kutosha kuingia mbinguni, na kwamba jambo kama hilo lilikuwa kubwa mno kiasi cha kutoweza hata kulitarajia. **[CETsw 16.4]**

Kukosa kujiamini, pamoja na imani kwamba haingewezekana kwa mtu yeyote kuelewa hisia zangu, kulinifanya nishindwe kutafuta ushauri na msaada kutoka kwa marafiki zangu Wakristo. Hivyo nilizunguka bila sababu katika giza na kukata tamaa, huku wao, kwa kutoweza kutambua hali yangu ya ndani kutokana na ukimya wangu, walikuwa hawajui kabisa hali yangu halisi.**[CETsw 17.1]**

**Kuhesabiwa Haki kwa Imani**

Msimu wa joto (kiangazi) uliofuata, wazazi wangu walikwenda kwenye mkutano wa kambi wa Kanisa la Methodist huko Buxton, Maine, na walinichukua pamoja nao. Nilikuwa nimeazimia kabisa kumtafuta Bwana kwa bidii huko, na kupata, ikiwezekana, msamaha wa dhambi zangu. Kulikuwa na shauku kubwa moyoni mwangu ya kupata tumaini la Mkristo na amani ile inayopatikana kwa njia ya kuamini.**[CETsw 17.2]**

Nilitiwa moyo sana niliposikiliza hotuba iliyotokana na maneno haya, … "**nitaingia kwa mfalme, kinyume cha sheria; nami nikiangamia, na niangamie**." Esta 4: Katika maneno yake, mhubiri huyo alirejelea wale waliokuwa wakisitasita kati ya tumaini na hofu; watu waliotamani kuokolewa kutoka katika dhambi zao na kupokea upendo wa Kristo unaosamehe, lakini waliokuwa wameshikiliwa katika mashaka na utumwa kwa sababu ya woga na hofu ya kushindwa. Aliwashauri watu kama hao wajisalimishe kwa Mungu, na wategemee rehema Yake bila kuchelewa. Wangempata Mwokozi Mwenye neema, aliye tayari kuwanyoshea fimbo ya enzi ya rehema, kama vile Ahasuero alivyomnyoshea Esta ishara ya kibali chake. Kitu pekee kilichohitajika kutoka kwa mwenye dhambi, aliyekuwa akitetemeka mbele za Bwana wake, kilikuwa ni kunyoosha mkono wa imani na kuigusa fimbo ya enzi ya neema Yake. Mguso huo ulihakikisha msamaha na amani.**[CETsw 17.3]**

Wale waliokuwa wakingojea kujifanya kuwa wanastahili zaidi kupata kibali cha Mungu kabla hawajathubutu kudai ahadi za Mungu, walikuwa wakifanya kosa kubwa linaloweza kuleta maangamizi. Yesu pekee Ndiye anayetutakasa kutoka katika dhambi; Yeye pekee Ndiye anayeweza kusamehe makosa yetu. Yeye Ameahidi kwamba atasikiliza ombi na kujibu maombi ya wale wanaomjia kwa imani. Wengi wana wazo lisilo wazi kwamba ni lazima wafanye juhudi fulani kubwa ili wapate kibali cha Mungu. Lakini kujitegemea katika mambo ya kiroho ni bure kabisa. Ni kwa kuunganishwa tu na Yesu kwa njia ya imani ndipo mwenye dhambi anakuwa mtoto wa Mungu mwenye tumaini na imani. **[CETsw 18.1]**

Maneno haya yalinifariji, na kunipa ufahamu wa jambo nililopaswa kufanya ili niokolewe.

Sasa nilianza kuona njia yangu kwa uwazi zaidi, na giza lilianza kuondoka. Kwa bidii nilitafuta msamaha wa dhambi zangu, na nikajitahidi kujikabidhi kabisa kwa Bwana. Lakini mara nyingi akili yangu ilikuwa katika huzuni kubwa, kwa sababu sikuwa napata ile furaha kuu ya kiroho ambayo niliamini ingekuwa ushahidi wa kukubalika kwangu mbele za Mungu, na sikuweza kuthubutu kuamini kwamba nimeokoka bila kupata uzoefu huo. Nilihitaji sana maelekezo kuhusu usahili wa imani! **[CETsw 18.3]**

**Mzigo Uliondolewa**

Nilipokuwa nimeinama madhabahuni pamoja na wengine waliokuwa wakimtafuta Bwana, maneno yote yaliyokuwa moyoni mwangu yalikuwa: **"Nisaidie, Yesu; niokoe, la sivyo nitaangamia! Sitakoma kukuomba mpaka ombi langu litakaposikiwa na dhambi zangu zitakaposamehewa."** Nilihisi hali yangu ya uhitaji na kutokuwa na msaada kuliko nilivyowahi kuhisi hapo kabla. **[CETsw 18.4]**

Nilipopiga magoti na kusali, ghafla mzigo wangu uliondoka, na moyo wangu ukawa mwepesi. Mwanzoni nilihisi hofu ikinijia, nami nikajaribu kurudisha tena mzigo wangu wa huzuni. Ilionekana kwangu kwamba sikuwa na haki ya kujisikia mwenye furaha na shangwe. Lakini Yesu alionekana kuwa karibu sana nami; nilihisi kwamba ningeweza kumjia pamoja na huzuni zangu zote, misiba yangu na majaribu yangu, kama vile wale wahitaji walivyomjia kwa ajili ya kupata msaada alipokuwa duniani. Kulikuwa na uhakikisho moyoni mwangu kwamba Yeye alielewa majaribu yangu ya pekee na kwamba alihurumia hali yangu. Siwezi kamwe kusahau hakikisho hili la thamani la huruma na upole wa Yesu kwa mtu ambaye hakustahili hata kuangaliwa Naye. Katika kipindi hicho kifupi nilijifunza zaidi kuhusu tabia ya Mungu ndani ya Kristo kuliko nilivyowahi kujifunza hapo awali, nilipokuwa nimeinama pamoja na wale waliokuwa wakiomba. **[CETsw 18.5]**

Mmoja wa akina mama katika Israeli alinikaribia na kuniambia, **"Mtoto mpendwa, umempata Yesu?"** Nilikuwa karibu kujibu, **"Ndiyo,"** aliposema kwa mshangao, **"Hakika umempataYesu; amani Yake iko pamoja nawe, ninaiona katika uso wako!"** **[CETsw 19.1]**

Tena na tena nilijiuliza moyoni: **"Je, hii ndiyo dini kweli? Je, sijakosea?"** Ilionekana kuwa jambo kubwa mno kwangu kudai, na ilikuwa ni fursa (upendeleo) ya juu sana. Ingawa nilikuwa mwoga mno kuikiri waziwazi, nilihisi kwamba Mwokozi alikuwa amenibariki na kunisamehe dhambi zangu. **[CETsw 19.2]**

**Katika Upya wa Uhai**

Muda mfupi baada ya jambo hili, mkutano wa kambi ulimalizika, nasi tukaanza safari ya kurudi nyumbani. Akili yangu ilikuwa imejaa mahubiri, maonyo, na sala tulizokuwa tumesikia. Kila kitu katika maumbile kilionekana kuwa kimebadilika. Wakati wa mkutano huo, mawingu na

mvua vilitawala kwa sehemu kubwa ya muda, na hisia zangu zilikuwa zimeendana na hali ya hewa hiyo. Lakini sasa jua lilikuwa linang'aa kwa mwangaza na uwazi, likiifunika dunia kwa nuru na joto. Miti na nyasi vilikuwa na kijani kibichi kipya zaidi, na anga lilikuwa na rangi ya samawati iliyokolea zaidi. Dunia ilionekana kutabasamu chini ya amani ya Mungu. Vivyo hivyo, miale ya Jua la Haki ilikuwa imepenya mawingu na giza la akili yangu, na kuondoa huzuni iliyokuwa imetanda ndani yangu.**[CETsw 19.3]**

Ilionekana kwangu kwamba kila mtu lazima awe na amani pamoja na Mungu, na awe amejawa na Roho Wake. Kila kitu ambacho macho yangu yalitazama kilionekana kuwa kimebadilika. Miti ilikuwa mizuri zaidi, na ndege waliimba kwa utamu zaidi kuliko hapo awali; walionekana kumsifu Muumba wao kupitia nyimbo zao. Sikutamani kuzungumza, kwa hofu kwamba furaha hii ingeweza kuondoka, na ningepoteza ushahidi huo wa thamani wa upendo wa Yesu kwangu.**[CETsw 20.1]**

Maisha yangu yalionekana kwangu katika mwanga tofauti. Dhiki iliyokuwa imeufanya utoto wangu kuwa wa huzuni na giza ilionekana kuwa ilikuwa imenipata kwa rehema, kwa ajili ya mema yangu, ili kuugeuza moyo wangu kutoka katika ulimwengu na starehe zake zisizoridhisha, na kuuelekeza kwenye mvuto wa kudumu wa mbingu.**[CETsw 20.2]**

Muda mfupi baada ya kurudi kwetu kutoka kwenye mkutano wa kambi, mimi pamoja na wengine kadhaa tuliingizwa kanisani kwa kipindi cha matazamio. Akili yangu ilikuwa imejishughulisha sana na suala la ubatizo. Ingawa nilikuwa bado mdogo, niliweza kuona kwamba kulikuwa na namna moja tu ya ubatizo iliyothibitishwa na Maandiko, nayo ilikuwa ni kuzamishwa majini. Baadhi ya dada zangu wa Kimethodisti walijaribu bila mafanikio kunishawishi kwamba kunyunyiziwa maji ndiyo ulikuwa ubatizo wa kibiblia.**[CETsw 20.3]**

Hatimaye muda uliwekwa kwa ajili yetu kupokea ibada hii takatifu. Ilikuwa siku yenye upepo mkali tuliposhuka kwenda baharini, tukiwa idadi ya watu kumi na wawili ili kubatizwa. Mawimbi yalikuwa makubwa na yaligonga ufukwe kwa nguvu, lakini nilipouchukua msalaba huu mzito, amani yangu ilikuwa kama mto. Nilipotoka majini, nguvu zangu zilikuwa karibu kumalizika, kwa sababu nguvu za Bwana zilikuwa juu yangu. Nilihisi kwamba tangu wakati huo sikuwa tena wa ulimwengu huu, bali nilikuwa nimefufuka kutoka katika kaburi la maji na kuingia katika maisha mapya. **[CETsw 20.4]**

Siku hiyo hiyo, alasiri, nilipokelewa katika kanisa na kuwa mshiriki kamili.**[CETsw 20.5]**

# 3. MWANZO WA KAZI ZA HADHARA

Tena, nilitamani sana kuhudhuria shule na kufanya jaribio jingine la kupata elimu, hivyo nikaingia katika shule ya wasichana huko Portland. Lakini nilipojaribu kuendelea na masomo yangu, afya yangu ilidhoofika haraka, na ikawa wazi kwamba ikiwa ningesisitiza kuendelea kuhudhuria shule, ningefanya hivyo kwa gharama ya maisha yangu. Kwa huzuni kubwa nilirudi nyumbani kwetu.**[CETsw 21.1]**

Nilikuwa nimeona kuwa ilikuwa vigumu kufurahia mambo ya dini katika shule hiyo, kwa sababu nilizungukwa na mvuto mbalimbali uliokusudiwa kuiteka akili na kuiongoza mbali na Mungu. Kwa muda fulani nilihisi kutoridhika daima na hali yangu mwenyewe pamoja na kiwango changu cha maendeleo ya Kikristo, na sikuwa naendelea kutambua kwa ukamilifu hisia hai ya rehema na upendo wa Mungu. Hisia za kunikatisha tamaa zilikuwa zinanijia mara kwa mara, na jambo hilo lilinisababishia wasiwasi mkubwa moyoni.**[CETsw 21.2]**

## Kazi ya Marejeo Portland

Mnamo Juni mwaka 1842, Bwana Miller alitoa mfululizo wake wa pili wa mikutano ya hadhara katika kanisa la Mtaa wa Casco huko Portland. Niliona kuwa ni fursa kubwa kuhudhuria mikutano hiyo ya hadhara; kwa maana nilikuwa nimeingia katika hali ya kukata tamaa, na sikuwa najihisi kuwa tayari kukutana na Mwokozi wangu. Mfululizo huu wa pili wa mikutano ya hadhara ulileta msisimko mkubwa zaidi katika mji kuliko ule wa kwanza. Madhehebu mbalimbali yalifunga milango ya makanisa yao dhidi ya Bwana Miller, isipokuwa machache. Hotuba nyingi kutoka kwenye mimbari mbalimbali zilijaribu kufichua makosa yaliyodaiwa kuwa ya ushabiki wa kupindukia katika mafundisho ya mhubiri huyo; lakini umati wa wasikilizaji wenye shauku ulihudhuria mikutano yake, na wengi hawakuweza hata kuingia ndani ya jengo kwa vile nafasi haikutosha. Makusanyiko hayo yalikuwa na utulivu wa pekee na yalikuwa makini sana kusikiliza. **[CETsw 21.3]**

Namna ya Bwana Miller ya kuhubiri haikuwa ya kutumia maneno ya kupamba au ya ufasaha wa hali ya juu, bali alieleza mambo yaliyo wazi na yenye kushtua, yaliyowafanya wasikilizaji wake waamke kutoka katika hali yao ya kutojali na kutokuwa na tahadhari. Aliunga mkono kauli na mafundisho yake kwa ushahidi wa Maandiko alipokuwa akiendelea kueleza. Nguvu ya ushawishi iliambatana na maneno yake, kiasi kwamba yalionekana kwa kuthibitika kuwa yalikuwa maneno ya kweli.**[CETsw 21.4]**

Alikuwa mwenye adabu na huruma. Wakati kila kiti ndani ya jengo kilikuwa kimejaa, na jukwaa pamoja na sehemu zilizokuwa karibu na mimbari zilionekana kuwa zimejaa watu kupita

kiasi, nilimwona akitoka kwenye sehemu ya kuhubiri, akitembea katikati ya njia ya ukumbi, kisha akamshika mkono mzee au mwanamke dhaifu na kumtafutia mahali pa kukaa; halafu akarudi na kuendelea na mahubiri yake. Kwa kweli alistahili kuitwa **"Baba Miller,"** kwa sababu alikuwa mwenye utunzaji/kujali watu kwa namna ya pekee kwa wale kwa wale waliokuwa chini ya huduma yake. Alikuwa mwenye upendo katika mwenendo wake, mwenye tabia ya urafiki na moyo wa huruma.**[CETsw 23.1]**

Alikuwa mhubiri mwenye kuvutia, na maonyo yake, kwa Wakristo waliokiri imani pamoja na wale ambao hawakuwa wametubu, yalikuwa yenye kufaa na yenye nguvu. Wakati mwingine hali ya uzito na unyenyekevu mkubwa sana, kiasi cha kuleta huzuni, ilitawala katika mikutano yake. Hisia ya kwamba kulikuwa na pambano kuu liliokuwa linakaribia katika matukio ya wanadamu iliigusa mioyo ya umati wa wasikilizaji. Wengi walikubali ushawishi wa Roho wa Mungu. Nilimwona akishika mikono ya wazee wenye mvi na wanawake wazee wenye shauku na kuwatafutia viti wokovu wakiwa na hatua za kutetemeka; wale waliokuwa katika nguvu za ujana na ukomavu, pamoja na vijana na watoto, waliguswa sana. Milio ya maumivu, sauti za kulia, na sauti za kumsifu Mungu zilichanganyika kwenye madhabahu ya maombi.**[CETsw 23.2]**

Niliamini maneno yale mazito yaliyosemwa na mtumishi wa Mungu, na moyo wangu uliumia yalipopingwa au kufanywa kuwa jambo la mzaha. Mara nyingi nilihudhuria mikutano hiyo, na niliamini kwamba Yesu alikuwa karibu kuja katika mawingu ya mbingu; lakini jambo lililonitia wasiwasi mkubwa lilikuwa ni kuwa tayari kukutana Naye. Akili yangu ilikuwa ikitafakari daima kuhusu suala la utakatifu wa moyo. Zaidi ya mambo yote, nilitamani kupata baraka hii kuu, na kuhisi kwamba nilikuwa nimekubaliwa kabisa na Mungu.**[CETsw 23.3]**

**Maumivu ya moyoni na akilini**

Hadi wakati huu nilikuwa sijawahi kuomba mbele za watu hadharani, na nilikuwa nimeshawahi kusema maneno machache tu ya hofu na mashaka katika mikutano ya maombi. Sasa nilihisi kusukumwa moyoni kwamba nilipaswa kumtafuta Mungu kwa maombi katika mikutano yetu midogo ya kijamii. Jambo hili sikuthubutu kulifanya, kwa kuogopa kuchanganyikiwa na kushindwa kueleza mawazo yangu. Lakini wajibu huo uliwekwa moyoni mwangu kwa nguvu sana kiasi kwamba nilipojaribu kuomba kwa siri, nilionekana kana kwamba namdhihaki Mungu, kwa sababu nilikuwa nimeshindwa kutii mapenzi Yake. Kukata tamaa kulinijaa, na kwa muda wa majuma matatu marefu hakuna mwanga hata mmoja uliopenya giza lililonizunguka.**[CETsw 24.1]**

Mateso ya akili yangu yalikuwa makali sana. Wakati mwingine kwa usiku mzima sikuweza kuthubutu kufumba macho yangu, bali nilisubiri mpaka dada yangu pacha alipokuwa amelala usingizi mzito; kisha kwa utulivu nilitoka kitandani mwangu na kupiga magoti sakafuni, nikiomba kimya kimya, nikiwa na uchungu mkubwa usiosemeka ambao hauwezi kuelezwa kwa maneno. Vitisho vya jehanamu inayowaka milele vilikuwa daima mbele ya macho yangu. Nilijua kwamba haingewezekana kwangu kuishi kwa muda mrefu katika hali hii, wala sikuthubutu kufa na kukutana na hatima ile ya kutisha ya mwenye dhambi. Kwa wivu mkubwa nilitazama wale

waliotambua kwamba walikuwa wamekubaliwa na Mungu! Tumaini la Mkristo lilionekana kuwa la thamani kiasi gani kwa nafsi yangu iliyoteseka kwa maumivu makali!**[CETsw 24.2]**

Mara nyingi nilibaki nimeinama katika maombi karibu usiku kucha, nikilia kwa maumivu na kutetemeka kwa uchungu usioelezeka pamoja na hali ya kukata tamaa ambayo haiwezi kufafanuliwa kwa maneno. **“Bwana, nihurumie!”** lilikuwa ombi langu. Na kama yule mtoza ushuru maskini, sikuthubutu kuinua macho yangu kuelekea mbinguni, bali nilikiinamisha uso wangu sakafuni. Mwili wangu ulidhoofika sana na nguvu zangu zikapungua kwa kiasi kikubwa, lakini niliendelea kuficha mateso yangu na hali yangu ya kukata tamaa moyoni mwangu.**[CETsw 24.3]**

**Ndoto ya Hekalu na Mwana-Kondoo**

Nilipokuwa katika hali hii ya kukata tamaa, niliota ndoto ambayo iliathiri sana mawazo yangu. Niliota kwamba niliona hekalu ambalo watu wengi walikuwa wakilikimbilia. Ni wale tu waliokimbilia ndani ya hekalu hilo ndio ambao wangeokolewa wakati wa mwisho wa mambo yote; lakini wote waliobaki nje wangepotea milele. Makundi ya watu waliokuwa nje, ambao walikuwa wakiendelea na shughuli zao mbalimbali, waliwadhihaki na kuwakejeli wale waliokuwa wakiingia ndani ya hekalu hilo. Waliwaambia kwamba mpango huo wa usalama ulikuwa ni udanganyifu wa werevu tu, na kwamba kwa kweli hakukuwa na hatari yoyote ambayo walipaswa kuiepuka. Hata waliwashika baadhi ya watu kwa nguvu ili kuwazuia wasiingie haraka ndani ya kuta za hekalu hilo.**[CETsw 24.4]**

Kwa kuogopa kudhihakiwa, niliona ni afadhali kusubiri mpaka lile kundi la watu litawanyike, au mpaka niweze kuingia bila wao kuniona. Lakini badala ya kupungua, idadi yao iliongezeka zaidi. Kwa kuogopa kuchelewa, niliondoka nyumbani kwangu kwa haraka na kupenya katikati ya umati wa watu. Katika shauku yangu ya kufikia lile hekalu, sikutambua wala sikujali umati wa watu uliokuwa umenizunguka. **[CETsw 25.1]**

Nilipoingia ndani ya jengo hilo, niliona kwamba hekalu hilo kubwa lilikuwa limeegemezwa na nguzo moja kubwa sana, na juu ya nguzo hiyo alikuwa amefungwa Mwana-Kondoo aliyekuwa amejeruhiwa vibaya sana na kutokwa damu nyingi. Sisi tuliokuwapo tulionekana kujua kwamba Mwana-Kondoo huyo alikuwa ameteswa na kuumizwa kwa ajili yetu. Kila mtu aliyeingia ndani ya hekalu hilo alipaswa kufika mbele ya Mwana-Kondoo huyo na kukiri dhambi zake. Mbele kabisa ya Mwana-Kondoo huyo kulikuwa na viti vilivyoinuliwa, ambavyo juu yake kulikuwa kumeketi kundi la watu waliokuwa na sura za furaha sana. Mwanga wa mbinguni ulionekana kung’aa juu ya nyuso zao, nao walimsifu Mungu na kuimba nyimbo za shukrani zenye furaha nyingi ambazo zilifanana na muziki wa malaika. Hawa ndio waliokuwa wamekuja mbele ya Mwana-Kondoo, wakakiri dhambi zao, wakapokea msamaha, na sasa walikuwa wakisubiri kwa matarajio yenye furaha tukio fulani la kushangilia.**[CETsw 25.2]**

Hata baada ya kuingia ndani ya jengo hilo, hofu ilinijia, pamoja na hisia ya aibu kwamba nilipaswa kujinyenyekeza mbele ya watu hawa; lakini nilionekana kulazimishwa kusonga mbele. Polepole nilikuwa nikizunguka ile nguzo ili niweze kukabiliana na Mwana-Kondoo, ndipo tarumbeta iliposikika. Hekalu lilitikisika, na vilisikika vilio vya ushindi kutoka kwa watakatifu waliokusanyika. Mwangaza wa kutisha uliliangaza jengo lote; kisha ghafla kila kitu kikawa giza kuu. Wale watu wenye furaha walikuwa wametoweka wote pamoja na ule mwangaza, nami nilibaki peke yangu katika ukimya wa kutisha wa usiku. **[CETsw 25.3]**

Niliamka nikiwa katika uchungu mkubwa wa mawazo, na ilikuwa vigumu sana kujishawishi kwamba nilikuwa nimeota tu. Ilionekana kwangu kwamba hukumu yangu ilikuwa tayari imeamuliwa; kwamba Roho wa Bwana alikuwa ameniacha, na asingerejea tena kamwe.**[CETsw 25.1]**

**Ndoto ya Kumwona Yesu**

Muda mfupi baada ya hapo niliota ndoto nyingine. Nilionekana kuwa nimekaa katika hali ya kukata tamaa kabisa, nikiwa nimeufunika uso wangu kwa mikono yangu, huku nikitafakari hivi: "Kama Yesu angekuwa duniani, ningekwenda Kwake, ningejitupa miguuni Pake, na ningemweleza mateso yangu yote. Asingenikataa; angenihurumia, nami ningempenda na kumtumikia daima." **[CETsw 26.2]**

Wakati huo huo, mlango ulifunguka, na mtu mwenye sura nzuri na mwonekano wa kuvutia akaingia. Alinitazama kwa huruma, kisha akasema: "Je, ungependa kumwona Yesu? Yuko hapa, nawe unaweza kumwona ikiwa unatamani kufanya hivyo. Chukua kila kitu ulicho nacho, kisha unifuate."**[CETsw 26.3]**

Niliposikia maneno hayo, nilijawa na furaha isiyoelezeka, nami kwa hiari nilikusanya vitu vyangu vyote vidogo nilivyokuwa navyo, pamoja na kila kitu kidogo nilichokithamini sana, kisha nikamfuata mwongozi wangu. Aliniongoza mpaka kwenye ngazi iliyokuwa mwinuko mkali na iliyoonekana kuwa dhaifu sana. Nilipoanza kupanda ngazi hizo, alinionya niendelee kutazama juu, ili nisije nikapata kizunguzungu na kuanguka. Watu wengine wengi waliokuwa wakipanda ule mwinuko mkali walianguka kabla hawajafika kileleni.**[CETsw 26.4]**

Hatimaye tulifika kwenye ngazi ya mwisho, na tukasimama mbele ya mlango. Hapa mwongozi wangu aliniagiza niache vitu vyote nilivyokuwa nimevibeba pamoja nami. Kwa furaha niliweka vitu hivyo chini. Kisha akaufungua mlango na kuniambia niingie. Kwa muda mfupi tu nilijikuta nimesimama mbele ya Yesu. Hakukuwa na uwezekano wa kukosea kuitambua sura hiyo nzuri; ule mwonekano wa upendo na ukuu usingeweza kuwa wa mtu mwingine yeyote. Macho Yake yalipotulia juu yangu, nilijua mara moja kwamba Alifahamu kila jambo lililohusu maisha yangu, pamoja na mawazo yangu yote ya ndani na hisia zangu zote. **[CETsw 26.5]**

Nilijaribu kujisitiri nisitazamwe na macho Yake, kwa kuwa nilihisi kwamba singeweza kustahimili macho Yake yaliyochunguza kila kitu; lakini Alinikaribia akiwa na tabasamu, akaweka mkono Wake juu ya kichwa changu, kisha akasema: **"Usiogope."** Sauti Yake tamu

ilisisimua moyo wangu kwa furaha ambayo sikuwahi kuipata hapo awali. Nilikuwa na furaha nyingi kiasi kwamba sikuweza kutamka neno lolote, bali nilizidiwa na hisia, nikaporomoka na kulala kifudifudi miguuni Pake. Nilipokuwa nimelala pale bila nguvu, matukio ya uzuri na utukufu yalipita mbele yangu, nami nilionekana kana kwamba nilikuwa nimefikia usalama na amani ya mbinguni. Hatimaye nguvu zangu zilinirudia, nami nikainuka. Macho ya Yesu yenye upendo bado yalikuwa yamenielekea, na tabasamu Lake lilijaza nafsi yangu furaha. Uwepo Wake uliamsha ndani yangu heshima takatifu na upendo usioelezeka.**[CETsw 27.1]**

Mwongozi wangu sasa aliufungua mlango, nasi sote wawili tukatoka nje. Akaniambia nichukue tena vitu vyote nilivyokuwa nimeviacha nyuma. Baada ya kufanya hivyo, alinipa kamba ya kijani iliyokuwa imekunjwa kwa mviringo kwa uangalifu. Aliniagiza niiweke karibu na moyo wangu, na kila nilipotaka kumwona Yesu, niitoe kifuani mwangu na kuinyoosha mpaka mwisho wake. Alinionya nisiiruhusu ibaki imekunjwa kwa muda mrefu, ili isije ikafunga mafundo na kuwa vigumu kuinyoosha tena. Niliiweka ile kamba karibu na moyo wangu, kisha kwa furaha nikashuka kwenye ngazi nyembamba, nikimsifu Bwana na kuwaambia wote niliokutana nao mahali ambapo wangeweza kumpata Yesu. **[CETsw 27.2]**

Ndoto hii ilinipa tumaini. Kamba ile ya kijani iliwakilisha imani katika mawazo yangu, na uzuri pamoja na unyenyekevu wa kumtumaini Mungu vilianza kudhihirika ndani ya nafsi yangu.**[CETsw 28.1]**

**Huruma ya Kirafiki na Ushauri**

Sasa nilimweleza mama yangu huzuni zangu zote na mashaka yaliyokuwa yananisumbua. Kwa upole alinielewa, akanionyesha huruma na kunitia moyo, akinishauri niende kupata ushauri kwa Mzee Stockman, ambaye wakati huo alikuwa akihubiri fundisho la ujio wa Kristo huko Portland. Nilikuwa na imani kubwa kwake, kwa sababu alikuwa mtumishi wa Kristo aliyejitoa kwa moyo wake wote. Baada ya kusikiliza maelezo yangu, aliweka mkono wake kwa upendo juu ya kichwa changu, huku macho yake yakijaa machozi, kisha akasema: **"Ellen, wewe bado ni mtoto tu. Ulichopitia ni jambo la pekee sana kwa mtu wa umri wako mdogo. Lazima Yesu anakuandaa kwa kazi maalumu fulani." [CETsw 28.2]**

Kisha aliniambia kwamba hata kama ningekuwa mtu mzima mwenye umri mkubwa, na hivyo kusumbuliwa na mashaka na kukata tamaa, bado angeniambia kwamba alijua kuna tumaini kwangu kupitia upendo wa Yesu. Alisema kwamba maumivu makali ya moyoni na mawazoni niliyokuwa nimepitia yalikuwa ushahidi dhahiri kwamba Roho wa Bwana alikuwa akijitahidi kunivuta Kwake. Alieleza kwamba mwenye dhambi anapokuwa amefanywa mgumu na hatia, hatambui ukubwa wa kosa lake, bali hujidanganya kwamba yuko katika hali nzuri na kwamba hayuko katika hatari yoyote kubwa. Roho wa Bwana humwacha, naye huwa mzembe na asiyejali, au huendelea kwa ukaidi usio na tahadhari. Mtu huyu mwema aliniambia juu ya upendo wa Mungu kwa watoto Wake wanaokosea; kwamba badala ya kufurahia uharibifu wao, Yeye anatamani kuwavuta Kwake kwa imani rahisi na tumaini. Alisisitiza kwa kina juu ya upendo mkuu wa Kristo na mpango wa ukombozi. **[CETsw 28.3]**

Mzee Stockman alizungumza kuhusu bahati mbaya yangu ya awali, na akasema kwamba kwa kweli lilikuwa jambo lenye huzuni kubwa na mateso makali. Lakini aliniagiza niamini kwamba mkono wa Baba mwenye upendo haukuwa umeondolewa kwangu. Alisema kwamba katika maisha yajayo, wakati ukungu uliokuwa umefunika na kutia giza mawazo yangu wakati huo utakapokuwa umetoweka, nitatambua hekima ya uongozi wa Mungu ambao wakati huo ulionekana kuwa wa ukatili na wa ajabu usioeleweka. Yesu aliwaambia wanafunzi Wake," **Nifanyalo wewe hujui sasa; lakini utalifahamu baadaye."** Yohana 13:7 Katika wakati mkuu ujao, hatutaona tena kama vile tunavyoona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo, bali tutakutana uso kwa uso na mafumbo ya upendo wa Mungu. **[CETsw 28.4]**

**"Nenda kwa amani na ukiwa huru moyoni, Ellen,"** alisema; **"rudi nyumbani kwako ukimtumaini Yesu, kwa maana Yeye hatamnyima upendo Wake mtu yeyote anayemtafuta kwa kweli."** Kisha akaomba kwa bidii kwa ajili yangu, na ilionekana kwamba kwa hakika Mungu angeyajibu maombi ya mtumishi Wake mwaminifu, hata kama maombi yangu ya unyenyekevu yasingesikika. Mawazo yangu yalitulizwa sana, na utumwa wa huzuni wa mashaka na hofu uliondoka nilipokuwa nikisikiliza ushauri wa hekima na wenye upole kutoka kwa mwalimu huyu wa Israeli. Niliondoka mbele yake nikiwa nimefarijika na kutiwa moyo. **[CETsw 29.1]**

Katika dakika chache nilizopokea mafundisho kutoka kwa Mzee Stockman, nilipata ujuzi mwingi zaidi kuhusu upendo wa Mungu na huruma Yake yenye upole kuliko nilivyopata kutokana na mahubiri yote na mawaidha yote niliyowahi kuyasikiliza. **[CETsw 29.2]**

**Ombi Langu la Kwanza la Hadharani**

Nilirudi nyumbani, na tena nikaja mbele za Bwana, nikiahidi kufanya na kuvumilia jambo lolote ambalo Angehitaji kutoka kwangu, ikiwa tu tabasamu la Yesu lingeweza kuufurahisha moyo wangu. Wajibu ule ule ambao hapo awali ulikuwa umesumbua mawazo yangu uliwekwa tena mbele yangu—yaani, kuubeba msalaba wangu miongoni mwa watu wa Mungu waliokusanyika. Fursa haikukawia kupatikana; jioni hiyo kulikuwa na mkutano wa maombi nyumbani kwa mjomba wangu, ambao nilihudhuria. **[CETsw 29.3]**

Wengine walipopiga magoti kwa ajili ya maombi, nami nilipiga magoti pamoja nao huku nikitetemeka. Baada ya watu wachache kuomba, sauti yangu ilianza kusikika katika maombi kabla hata sijatambua nilichokuwa nikifanya. Katika wakati huo, ahadi za Mungu zilionekana kwangu kama lulu nyingi za thamani ambazo zilikuwa zinapatikana kwa kuziomba tu. Nilipokuwa nikiomba, mzigo na uchungu wa nafsi ambao nilikuwa nimeubeba kwa muda mrefu uliondoka, na baraka ya Bwana ilinijilia kama umande mwanana. Nilimsifu Mungu kutoka ndani kabisa ya moyo wangu. Kila kitu kilionekana kutoweka mbele yangu isipokuwa Yesu na utukufu Wake, nami nilipoteza ufahamu wa mambo yaliyokuwa yakiendelea kunizunguka. **[CETsw 29.4]**

Roho wa Mungu alinijia kwa nguvu nyingi sana kiasi kwamba sikuweza kurudi nyumbani usiku huo. Nilipozinduka na kutambua hali yangu, nilijikuta nikitunzwa/nikiangaliwa katika nyumba ya mjomba wangu, mahali ambapo tulikuwa tumekusanyika kwa ajili ya mkutano wa maombi. Mjomba wangu na shangazi yangu wote hawakuwa na uzoefu wa dini, ingawa mjomba wangu alikuwa amewahi kukiri imani hapo awali, lakini baadaye alikuwa ameanguka na kuacha msimamo wake wa kiroho. Niliambiwa kwamba alikuwa amesumbuliwa sana wakati nguvu za Mungu zilipokuwa juu yangu kwa namna ya pekee sana, na kwamba alikuwa akitembea huku na kule ndani ya nyumba, akiwa na huzuni kubwa na msongo wa mawazo moyoni mwake. **[CETsw 30.1]**

Nilipoanguka mara ya kwanza, baadhi ya watu waliokuwapo waliingiwa na hofu kubwa, na walikuwa karibu kwenda kumtafuta daktari, wakidhani kwamba nilikuwa nimepatwa na ugonjwa wa ghafla na hatari. Lakini mama yangu aliwaambia waniache, kwa sababu kwake na kwa Wakristo wengine wenye uzoefu ilikuwa wazi kwamba nguvu ya ajabu ya Mungu ndiyo iliyokuwa imenifanya nianguke. Niliporudi nyumbani siku iliyofuata, mabadiliko makubwa yalikuwa yametokea katika mawazo yangu. Ilionekana kwangu kwamba kwamba mimi sikuwa mtu yule yule aliyeondoka nyumbani kwa baba yangu jioni iliyotangulia. Andiko hili liliendelea kuwa akilini mwangu daima: "**Bwana Ndiye mchungaji wangu, Sitapungukiwa na kitu.**" Zaburi 23:1 Moyo wangu ulijaa furaha nilipokuwa nikiyarudia kwa sauti ya upole maneno haya.**[CETsw 30.2]**

**Mtazamo wa Upendo wa Baba**

Imani sasa ilitawala moyo wangu. Nilihisi upendo usioelezeka kwa Mungu, na nilikuwa na ushuhuda wa Roho Wake kwamba dhambi zangu zilikuwa zimesamehewa. Mtazamo wangu kuhusu Baba wa mbinguni ulibadilika. Sasa nilimtazama kama Mzazi Mwema na Mwenye upole, badala ya kumwona kama mtawala mkali anayewalazimisha wanadamu kumtii kwa upofu. Moyo wangu ulielekezwa Kwake kwa upendo wa kina na wa dhati. Kutii mapenzi Yake kulionekana kuwa furaha; ilikuwa jambo la kupendeza kuwa katika utumishi Wake. Hakuna kivuli chochote kilichofunika nuru iliyokuwa ikinifunulia mapenzi makamilifu ya Mungu. Nilihisi uhakikisho wa Mwokozi anayekaa ndani yangu, na nikatambua Ukweli wa yale ambayo Kristo alisema: "yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima." Yohana 8:12 **[CETsw 31.1]**

Amani yangu na furaha yangu vilikuwa tofauti sana na hali yangu ya awali ya giza na uchungu kiasi kwamba ilionekana kwangu kana kwamba nilikuwa nimeokolewa kutoka kuzimu na kuhamishiwa mbinguni. Hata niliweza kumsifu Mungu kwa ajili ya lile jambo la bahati mbaya lililokuwa limekuwa jaribu la maisha yangu, kwa sababu lilikuwa njia iliyofanya mawazo yangu yaelekezwe katika umilele. Kwa asili nilikuwa mwenye kiburi na mwenye tamaa ya mafanikio; huenda nisingekuwa tayari kuutoa moyo wangu kwa Yesu kama siyo mateso makali

yaliyokuwa yamenitenga, kwa namna fulani, na ushindi wa majivuno na mambo ya ubatili ya ulimwengu.**[CETsw 31.2]**

Kwa muda wa miezi sita hakuna kivuli chochote kilichofunika mawazo yangu, wala sikupuuza wajibu wowote nilioujua. Jitihada yangu yote ilikuwa kufanya mapenzi ya Mungu na kumweka Yesu pamoja na mbingu daima katika mawazo yangu. Nilishangazwa na kufurahi sana kwa sababu ya ufahamu ulio wazi niliokuwa nimepewa sasa kuhusu upatanisho na kazi ya Kristo. Sitajaribu kueleza zaidi hali za mawazo yangu; inatosha kusema kwamba mambo ya kale yalikuwa yamepita, na mambo yote yalikuwa yamekuwa mapya. Hakukuwa na wingu lolote la kuharibu furaha yangu kamili. Nilitamani kuwaambia wengine habari ya upendo wa Yesu, lakini sikuwa na hamu ya kushiriki katika mazungumzo ya kawaida na mtu yeyote. Moyo wangu ulikuwa umejaa sana upendo kwa Mungu na amani ile ipitayo ufahamu, kiasi kwamba nilifurahia kutafakari na kuomba.**[CETsw 31.3]**

**Kutoa Ushuhuda**

Usiku uliofuata baada ya kupokea baraka kubwa namna hiyo, nilihudhuria mkutano wa Waadventista. Wakati ulipofika kwa wafuasi wa Kristo kusema kwa ajili ya utetezi wa Bwana wao, sikuweza kukaa kimya, bali nilisimama na kueleza uzoefu wangu. Hakukuwa na wazo lolote lililoingia akilini mwangu kuhusu kile nilichopaswa kusema; lakini simulizi rahisi la upendo wa Yesu kwangu lilitoka kinywani mwangu kwa uhuru kamili. Moyo wangu ulikuwa na furaha kubwa kwa kuwa ulikuwa umewekwa huru kutoka katika utumwa wa kukata tamaa kuu na giza, kiasi kwamba nilisahau watu waliokuwa wamenizunguka, na nilionekana kana kwamba nilikuwa peke yangu pamoja na Mungu. Sikuwa na ugumu wowote wa kueleza amani yangu na furaha yangu, isipokuwa kwa machozi ya shukrani yaliyokuwa yakinizuia kuzungumza. **[CETsw 32.1]**

Mzee Stockman alikuwapo. Hivi karibuni alikuwa ameniona nikiwa katika hali ya kukata tamaa kabisa, na sasa aliponiona nimegeuzwa kutoka katika hali hiyo ya utumwa, alilia kwa sauti kubwa, akifurahi pamoja nami na kumsifu Mungu kwa ushahidi huu wa rehema Yake yenye upole na fadhili Zake za upendo. **[CETsw 32.2]**

Muda mfupi baada ya kupokea baraka hii kubwa, nilihudhuria mkutano wa kongamano katika kanisa la Kikristo, ambako Mzee Brown alikuwa mchungaji. Niliombwa kueleza uzoefu wangu, nami nilihisi siyo tu uhuru mkubwa wa kuzungumza, bali pia furaha, nilipokuwa nikisimulia kwa unyenyekevu hadithi yangu rahisi kuhusu upendo wa Yesu na furaha ya kukubaliwa na Mungu. Nilipokuwa nikizungumza, kwa moyo uliojaa unyenyekevu na macho yenye machozi, nafsi yangu ilionekana kuinuliwa kuelekea mbinguni katika roho ya shukrani.

Nguvu ya Mungu iliyoyeyusha mioyo iliwashukia watu waliokusanyika. Wengi walikuwa wakilia, na wengine wakimsifu Mungu. **[CETsw 32.3]**

Wenye dhambi walialikwa kusimama kwa ajili ya maombi, na wengi waliitikia mwito huo. Moyo wangu ulikuwa na shukrani nyingi kwa Mungu kwa ajili ya baraka Alizonipa, kiasi kwamba nilitamani wengine pia washiriki katika furaha hii takatifu. Mawazo yangu yalijikita sana kwa wale ambao huenda walikuwa wakiteseka chini ya hisia ya kutokupendezwa na Bwana na mzigo wa dhambi. Nilipokuwa nikisimulia uzoefu wangu, nilihisi kwamba hakuna mtu ambaye angeweza kupinga ushahidi wa upendo wa Mungu unaosamehe, ambao ulikuwa umeleta mabadiliko makubwa namna hii ndani yangu. Uhalisi wa uongofu wa kweli ulionekana wazi sana kwangu kiasi kwamba nilihisi kutaka kuwasaidia marafiki zangu vijana waingie katika nuru; na kila nafasi ilipopatikana nilitumia ushawishi wangu kwa ajili ya lengo hilo. **[CETsw 32.4]**

**Kuwahudumia Marafiki Vijana**

Nilikaa vikao pamoja na marafiki zangu vijana, ambao baadhi yao walikuwa na umri mkubwa zaidi yangu, na wachache walikuwa watu waliofunga ndoa. Baadhi yao walikuwa wenye ubatili na wasiojali; uzoefu wangu ulionekana kwao kama hadithi isiyo na maana, nao hawakuzingatia maombi yangu. Lakini niliamua kwamba juhudi zangu zisingekoma kamwe mpaka wapendwa hawa, ambao nilikuwa na shauku kubwa kwa ajili yao, wajisalimishe kwa Mungu. Nilitumia usiku kadhaa mzima katika maombi ya dhati kwa ajili ya wale ambao nilikuwa nimewatafuta na kuwakusanya kwa kusudi la kufanya kazi pamoja nao na kuomba pamoja nao. **[CETsw 33.1]**

Baadhi ya watu hawa walikuwa wamekutana nasi kwa sababu ya udadisi, ili kusikia yale ambayo ningesema; wengine walidhani kwamba nilikuwa nimepoteza akili kwa kuwa naendelea sana katika juhudi zangu, hasa kwa sababu wao wenyewe hawakuonyesha kujali jambo hilo. Lakini katika kila kikao chetu mdogo niliendelea kuwaonya na kuwaombea kila mmoja wao binafsi, mpaka wote walipomkabidhi Yesu maisha yao, wakikubali thamani ya upendo Wake unaosamehe. Kila mmoja wao alijitoa kwa Mungu. **[CETsw 33.2]**

Usiku baada ya usiku katika ndoto zangu nilionekana nikifanya kazi kwa ajili ya wokovu wa nafsi za watu. Katika nyakati hizo, watu fulani maalumu waliwasilishwa akilini mwangu; baadaye niliwatafuta na kuomba pamoja nao. Katika kila hali isipokuwa moja, watu hao walijitoa kwa Bwana. Baadhi ya ndugu zetu waliokuwa na mtazamo wa kawaida na wa tahadhari zaidi waliogopa kwamba nilikuwa na bidii kupita kiasi katika kutafuta uongofu wa nafsi. Lakini kwangu muda ulionekana kuwa mfupi sana kiasi kwamba iliwapasa wote waliokuwa na tumaini lenye baraka la kutokufa na waliokuwa wakitarajia kuja kwa Kristo upesi, kufanya kazi bila kukoma kwa ajili ya wale ambao bado walikuwa katika dhambi zao na waliosimama ukingoni mwa uharibifu wa kutisha.**[CETsw 33.3]**

Ingawa nilikuwa bado mdogo sana, mpango wa wokovu ulikuwa wazi sana akilini mwangu, na uzoefu wangu binafsi ulikuwa wa namna ya pekee sana kiasi kwamba, baada ya kutafakari jambo hilo, nilijua kwamba ilikuwa wajibu wangu kuendelea na juhudi zangu kwa ajili ya wokovu wa nafsi za thamani, na kuomba pamoja na kumkiri Kristo kila nafasi ilipotokea. Utu wangu wote ulijitoa kwa ajili ya utumishi wa Bwana wangu [nafsi yangu yote]. Haijalishi kwamba jambo gani lolote lingetokea, mimi nilidhamiria kumpendeza Mungu na kuishi kama mtu anayetarajia Mwokozi kuja na kuwazawadia waaminifu. Nilihisi kama mtoto mdogo anayemjia Mungu kama anavyomjia baba yake, na kumuuliza angependa nifanye nini. Kisha wajibu wangu ulipokuwa umewekwa wazi kwangu, jambo lililonipa furaha kubwa zaidi lilikuwa kuutimiza. Majaribu ya pekee yalinizunguka wakati mwingine. Wale waliokuwa na uzoefu mkubwa wa maisha kuliko mimi walijaribu kunizuia na kupunguza bidii ya imani yangu; lakini kwa tabasamu la Yesu lililokuwa likiangaza maisha yangu, na upendo wa Mungu uliokuwa moyoni mwangu, niliendelea na safari yangu kwa moyo wa furaha. **[CETsw 34.1]**

## 4. IMANI YA MAREJEO

Familia ya baba yangu bado iliendelea mara kwa mara kuhudhuria kanisa la Kimethodisti, pamoja na mikutano ya vikundi vya waumini iliyokuwa ikifanyika katika nyumba za watu binafsi. **[CETsw 35.1]**

**Uzoefu Katika Darasa**

Jioni moja mimi na kaka yangu Robert tulienda kwenye mkutano wa kikundi cha waumini. Mzee msimamizi wa kanisa alikuwapo. Wakati ulipofika zamu ya kaka yangu kutoa ushuhuda, alizungumza kwa unyenyekevu mkubwa, lakini kwa uwazi, kuhusu umuhimu wa kuwa na utayari kamili wa kukutana na Mwokozi wetu atakapokuja katika mawingu ya mbinguni akiwa na nguvu na utukufu mkuu. Kaka yangu alipokuwa akizungumza, nuru ya mbinguni iling'aa juu ya uso wake ambao kwa kawaida ulikuwa na rangi ya kupauka. Alionekana kana kwamba alikuwa ameinuliwa kiroho juu ya mazingira yaliyomzunguka wakati huo, na alizungumza kana kwamba alikuwa mbele ya uwepo wa Yesu.**[CETsw 35.2]**

Nilipoitwa ili nizungumze, nilisimama nikiwa na uhuru wa roho, moyo wangu ukiwa umejaa upendo na amani. Nilisimulia kisa cha mateso yangu makubwa niliyopitia chini ya ushawishi wa hatia ya dhambi, jinsi hatimaye nilivyopokea baraka niliyokuwa nimeitafuta kwa muda mrefu—yaani, kufanana kikamilifu na mapenzi ya Mungu—na nilieleza furaha yangu katika habari njema ya kuja upesi kwa Mkombozi wangu ili kuwachukua watoto Wake kwenda nyumbani. **[CETsw 35.3]**

Nilipomaliza kuzungumza, mzee msimamizi wa kikao aliniuliza kama haingekuwa jambo la kupendeza zaidi kuishi maisha marefu yenye manufaa, tukiwafanyia wengine mema, kuliko Yesu kuja upesi na kuwaangamiza wenye dhambi maskini. Nilijibu kwamba nilitamani sana kuja kwa Yesu. Ndipo dhambi ingekuwa imekwisha, nasi tungefurahia utakaso milele, bila kuwa na shetani wa kutujaribu na kutupotosha. **[CETsw 35.4]**

Baada ya mkutano kumalizika, nilitambua kwamba nilitendewa kwa namna isiyo ya upendo na wale ambao hapo awali walikuwa wema na wenye urafiki kwangu. Mimi na kaka yangu tulirudi nyumbani tukiwa na huzuni kwa sababu tulijiuliza kwanini hatueleweki ipasavyo na ndugu zetu, na kwa sababu fundisho la kuja kwa Yesu lililokuwa karibu lilikuwa limeamsha upinzani mkali namna hiyo mioyoni mwao. **[CETsw 35.5]**

**Tumaini lililobarikiwa**

Njiani kuelekea nyumbani tulizungumza kwa uzito kuhusu ushahidi wa imani yetu mpya na tumaini letu jipya. “Ellen,” alisema Robert, “je, tumedanganyika? Je, tumaini hili la kuonekana kwa Kristo upesi duniani ni uzushi, kiasi kwamba wachungaji na watu wanaodai kuwa na dini wanalipinga kwa ukali namna hii? Wanasema kwamba Yesu hatakuja kwa maelfu na maelfu ya miaka. Ikiwa hata hawa wanakaribia Ukweli, basi ulimwengu hauwezi kabisa kufikia mwisho wakati wa siku zetu.”**[CETsw 36.1]**

Sikuthubutu hata kwa muda mfupi kuupa moyo wangu nafasi ya kutokuamini, bali nilijibu kwa haraka: “Sina shaka hata kidogo kwamba fundisho linalohubiriwa na Bwana Miller ni Kweli. Ni nguvu kubwa kiasi gani inayoambatana na maneno yake! Ni ushawishi mkubwa kiasi gani unaofikishwa moja kwa moja moyoni mwa mwenye dhambi!” **[CETsw 36.2]**

Tulijadili jambo hilo kwa uwazi na unyofu tulipokuwa tukitembea njiani, na tukaamua kwamba ulikuwa wajibu wetu na pendeleo letu kutazamia kuja kwa Mwokozi wetu. Pia tuliona kwamba ingekuwa salama zaidi kujiandaa kwa ajili ya kuonekana Kwake, ili tuwe tayari kukutana Naye kwa furaha. Ikiwa kweli angekuja, hali ya wale waliokuwa wakisema sasa, **“Bwana wangu anakawia kuja,”** na ambao hawakuwa na shauku ya kumwona, ingekuwaje? Tulishangaa jinsi wachungaji walivyothubutu kutuliza hofu za wenye dhambi na wale waliokuwa wamerudi nyuma kwa kusema, **“Amani, amani!”** wakati ujumbe wa onyo ulikuwa ukitolewa katika nchi yote. Wakati huo ulionekana kwetu kuwa wa maana sana na wenye uzito mkubwa; tulihisi kwamba hatukuwa na muda wa kupoteza.**[CETsw 36.3]**

**“**Mti hujulikana kwa matunda yake,” alisema Robert. “Imani hii imetufanyia nini? Imetufanya tutambue kwamba hatukuwa tayari kwa ajili ya kuja kwa Bwana; kwamba tunapaswa kuwa na mioyo safi, la sivyo hatuwezi kukutana na Mwokozi wetu kwa amani. Imetuchochea kutafuta nguvu mpya na neema kutoka kwa Mungu.**[CETsw 36.4]**

“Imekufanyia nini wewe, Ellen? Je, ungekuwa vile ulivyo sasa kama usingalikuwa umesikia fundisho la kuja upesi kwa Kristo? Imeamsha tumaini gani moyoni mwako; imekupa amani, furaha, na upendo wa namna gani? Na kwangu mimi imefanya kila kitu. Nampenda Yesu, na ninawapenda Wakristo wote. Ninaipenda mikutano ya maombi. Ninapata furaha kubwa katika kusoma Biblia yangu na katika maombi.”**[CETsw 37.1]**

Sote wawili tulihisi tumeimarishwa na mazungumzo haya, na tuliamua kwamba hatungeruhusu mtu yeyote atugeuze kutoka katika imani yetu ya kweli juu ya Ukweli tuliouamini, wala kutoka katika tumaini lile lenye baraka la kuja kwa Kristo upesi katika mawingu ya mbinguni. Tulishukuru kwamba tuliweza kutambua nuru ile ya thamani, na kufurahi tunapolitazamia kuja kwa Bwana.**[CETsw 37.2]**

**Ushuhuda wa Mwisho Katika Darasa**

Muda mfupi baada ya hayo, tulihudhuria tena mkutano wa kikundi cha waumini. Tulitamani kupata nafasi ya kuzungumza kuhusu upendo wa thamani wa Mungu uliokuwa ukiihuisha nafsi zetu. Nilitamani hasa kueleza wema na rehema za Bwana kwangu. Mabadiliko makubwa yalikuwa yametokea ndani yangu kiasi kwamba niliona ilikuwa wajibu wangu kutumia kila nafasi ya kushuhudia upendo wa Mwokozi wangu.**[CETsw 37.3]**

Zamu yangu ya kuzungumza ilipofika, nilieleza ushahidi niliokuwa nao wa upendo wa Yesu, na kwamba nilikuwa nikitazamia kwa furaha kukutana na Mkombozi wangu hivi karibuni. Imani kwamba kuja kwa Kristo kulikuwa karibu kulikuwa kumeichochea nafsi yangu kumtafuta kwa bidii zaidi utakaso unaotokana na Roho wa Mungu.**[CETsw 37.4]**

Hapa kiongozi wa kikundi alinikatiza, akisema: **“Ulipokea utakaso kupitia Umethodisti, kupitia *Umethodisti*, dada, siyo kupitia fundisho lenye makosa.”[CETsw 37.5]**

Nilihisi nimelazimika kukiri ukweli kwamba haikuwa kupitia Umethodisti ambapo moyo wangu ulipokea baraka hiyo mpya, bali ilikuwa kupitia Kweli zenye kuchochea kuhusu kuonekana binafsi kwa Yesu. Kupitia Kweli hizo nilipata amani, furaha, na upendo mkamilifu. Hivyo ushuhuda wangu ulimalizika; huo ulikuwa ushuhuda wangu wa mwisho ambao ningetoa katika kikundi pamoja na ndugu zangu wa Kimethodisti. **[CETsw 37.6]**

Kisha Robert alizungumza kwa namna yake ya upole na unyenyekevu, lakini kwa njia iliyo wazi sana na yenye kugusa moyo kiasi kwamba baadhi ya watu walilia na kuguswa sana; lakini wengine walikohoa kwa ishara ya kutokubaliana, na walionekana kuwa na hali ya kutotulia kabisa. **[CETsw 38.1]**

Baada ya kuondoka katika kukutania, tulizungumza tena kuhusu imani yetu, na tukashangaa kwamba ndugu na dada zetu Wakristo wangeweza kushindwa kuvumilia hata neno moja linalohusu kuja kwa Mwokozi wetu. Tuliamua kwamba hatukupaswa tena kuhudhuria mikutano hiyo ya kikundi. Tumaini la kuonekana kwa Kristo katika utukufu lilijaza nafsi zetu, na lilijitokeza wazi kila tuliposimama kuzungumza. Ilikuwa dhahiri kwamba tusingeweza kuwa na uhuru katika mikutano hiyo ya kikundi; kwa sababu ushuhuda wetu ulizua kejeli na dhihaka ambazo tulizisikia mwishoni mwa mkutano, kutoka kwa ndugu na dada tuliowaheshimu na kuwapenda. **[CETsw 38.2]**

**Kutangaza Ujumbe wa Marejeo**

Waadventista walikuwa wakifanya mikutano wakati huo katika Ukumbi wa Beethoven. Baba yangu, pamoja na familia yake, walihudhuria mikutano hiyo mara kwa mara sana. Wakati wa ujio wa pili wa Kristo ulidhaniwa kuwa ungefika katika mwaka wa 1843. Muda uliokuwa umebaki kwa ajili ya nafsi kuokolewa ulionekana kuwa mfupi sana kiasi kwamba niliamua kufanya kila lililokuwa ndani ya uwezo wangu ili kuwaongoza wenye dhambi katika nuru ya ile Kweli. **[CETsw 38.3]**

Nilikuwa na dada wawili nyumbani—Sarah, ambaye alikuwa na umri mkubwa kuliko mimi kwa miaka kadhaa, na dada yangu pacha Elizabeth. Tulizungumza jambo hilo kati yetu, na tukaamua kutafuta fedha kadiri tunavyoweza, kisha tutumie fedha hizo kununua vitabu na vijitabu vya injili ili vigawiwe bure. Hilo ndilo jambo bora zaidi tuliloweza kufanya, na tulifanya jambo hilo dogo kwa furaha. **[CETsw 38.4]**

Baba yetu alikuwa mtengenezaji wa kofia, na kazi niliyogawiwa ilikuwa kutengeneza sehemu za juu za kofia hizo, kwa kuwa hiyo ndiyo ilikuwa sehemu rahisi zaidi ya kazi hiyo. Pia nilikuwa nikisuka soksi kwa malipo ya senti ishirini na tano kwa jozi moja. Moyo wangu ulikuwa dhaifu sana kiasi kwamba nililazimika kukaa nikiwa nimeegemezwa kitandani ili kufanya kazi hiyo; lakini siku baada ya siku nilikaa pale, nikifurahi kwamba vidole vyangu vilivyokuwa vikitetemeka vingeweza kufanya jambo fulani la kuleta kiasi kidogo cha fedha kwa ajili ya kazi ile niliyoipenda sana. Senti ishirini na tano kwa siku ndizo pekee nilizoweza kupata. Kwa uangalifu mkubwa nilikuwa naweka pembeni vipande vile vya thamani vya fedha nilivyopokea kama malipo, ambavyo vingetumika kununua machapisho ya kusoma ili kuwaelimisha na kuwaamsha wale waliokuwa gizani. **[CETsw 39.1]**

Sikuwa na jaribu lolote la kutumia mapato yangu kwa ajili ya kujifurahisha binafsi. Mavazi yangu yalikuwa rahisi; sikutumia chochote kwa ajili ya mapambo yasiyo ya lazima, kwa sababu kujionyesha kwa ubatili kulionekana kuwa ni dhambi machoni pangu. Hivyo, daima nilikuwa na kiasi kidogo cha fedha nilichokuwa nimehifadhi kwa ajili ya kununua vitabu vinavyofaa. Vitabu hivyo viliwekwa mikononi mwa watu wenye uzoefu ili wavipeleke sehemu mbalimbali. **[CETsw 39.2]**

Kila ukurasa wa machapisho hayo ulionekana kuwa wa thamani machoni pangu; kwa sababu ulikuwa kama mjumbe wa nuru kwa ulimwengu, ukiwaalika watu kujiandaa kwa tukio lile kuu lililokuwa karibu kutokea. Wokovu wa nafsi za watu ulikuwa mzigo wa mawazo yangu, na moyo wangu uliumia kwa ajili ya wale waliojidanganya kwamba walikuwa wanaishi katika usalama, wakati ujumbe wa onyo ulikuwa ukitolewa kwa ulimwengu.**[CETsw 39.3]**

**Suala la Kutokufa kwa Roho**

Siku moja nilisikiliza mazungumzo kati ya mama yangu na dada mmoja, kuhusu mahubiri waliyokuwa wamesikia hivi karibuni, yaliyokuwa yakifundisha kwamba nafsi haina kutokufa kwa asili. Baadhi ya aya za Biblia zilizotumiwa na mhubiri kama ushahidi zilirudiwa. Miongoni mwa hizo nakumbuka kwamba aya hizi zilinigusa sana: "roho ile itendayo dhambi itakufa." Ezekieli 18:4. "kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa; lakini wafu hawajui neno lolote Mhubiri 9:5. "kwa majira yake atakudhihirisha, Yeye aliyehimidiwa, Mwenye uweza peke yake, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana; ambaye Yeye peke yake hapatikani na mauti, amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa." 1 Timotheo 6:15, 16. "wale ambao kwa saburi katika kutenda mema wanatafuta utukufu na heshima na kutokuharibika, watapewa uzima wa milele." Warumi 2:7 . **[CETsw 39.4]**

**"Kwa nini,"** alisema mama yangu baada ya kunukuu kifungu hicho kilichotangulia, **"watafute kitu ambacho tayari wanacho?"** **[CETsw 40.1]**

Nilisikiliza mawazo haya mapya kwa shauku kubwa na kwa msisimko uliokuwa ukiniumiza moyoni. Nilipokuwa peke yangu pamoja na mama yangu, nilimuuliza kama kweli aliamini kwamba nafsi haifi. Jibu lake lilikuwa kwamba aliogopa huenda tulikuwa tumekosea kuhusu jambo hilo, kama vile tulivyokuwa tumekosea kuhusu mambo mengine pia. **[CETsw 40.2]**

"Lakini mama," nilisema, "je, kweli unaamini kwamba nafsi hulala kaburini mpaka wakati wa ufufuo? Je, unafikiri kwamba Mkristo anapokufa haendi mara moja mbinguni, wala mwenye dhambi haendi kuzimu?" **[CETsw 40.3]**

Alijibu: "Biblia haitupi ushahidi wowote kwamba kuna kuzimu inayowaka milele. Kama mahali kama hapo pana kweli, lingetajwa katika Kitabu Kitakatifu." **[CETsw 40.4]**

"Kwa nini, mama!" nililia kwa mshangao, "haya ni maneno ya ajabu kutoka kwako! Ikiwa unaamini fundisho hili lisilo la kawaida, usimruhusu mtu yeyote kulijua; kwa sababu ninaogopa kwamba wenye dhambi watapata uhakika wa uongo kupitia imani hii, na kamwe hawatatamani kumtafuta Bwana." **[CETsw 40.5]**

"Ikiwa hili ni fundisho la kweli la Biblia," alijibu, "badala ya kuzuia wokovu wa wenye dhambi, litakuwa njia ya kuwavuta kwa Kristo. Ikiwa upendo wa Mungu hautamshawishi mwasi kujisalimisha, hofu ya kuzimu ya milele haitamsukuma kutubu. Zaidi ya hayo, haionekani kuwa njia inayofaa ya kuongoza nafsi kwa Yesu kwa kutumia mojawapo ya hali za chini kabisa za

akili—yaani, hofu kuu yenye kudhalilisha. Upendo wa Yesu huvuta; utaitawala hata mioyo iliyo migumu zaidi." **[CETsw 40.6]**

Ilikuwa ni miezi kadhaa baada ya mazungumzo hayo kabla sijapata kusikia tena jambo lolote zaidi kuhusu fundisho hili; lakini katika kipindi hicho mawazo yangu yalikuwa yamejishughulisha sana na suala hilo. Niliposikia likihubiriwa, niliamini kwamba lilikuwa Kweli. Tangu nuru kuhusu usingizi wa wafu iliponijia akilini mwangu, fumbo lililokuwa limeufunika ufufuo liliondoka, na tukio hilo kuu lenyewe likaanza kuonekana kuwa na umuhimu mpya na wa hali ya juu. Mara nyingi mawazo yangu yalikuwa yamesumbuliwa na juhudi za kupatanisha thawabu au adhabu ya mara moja kwa wafu pamoja na Ukweli usiopingika wa ufufuo na hukumu ya wakati ujao. Kama wakati wa kufa roho iliingia katika furaha ya milele au mateso ya milele, basi kulikuwa na haja gani ya ufufuo wa ule mwili unaooza kaburini? **[CETsw 41.1]**

Lakini imani hii mpya na yenye uzuri ilinifundisha sababu iliyowafanya waandishi waliovuviwa kusisitiza sana kuhusu ufufuo wa mwili; ilikuwa ni kwa sababu utu wote ulikuwa umelala kaburini. Sasa niliweza kutambua wazi upotovu wa msimamo wetu wa awali kuhusu jambo hili. **[CETsw 41.2]**

**Kutembelewa na Mchungaji**

Familia yetu yote ilikuwa na shauku kubwa kuhusu fundisho la kuja kwa Bwana upesi. Baba yangu alikuwa amesimama kama mmoja wa nguzo za kanisa la Kimethodisti. Alikuwa amehudumu kama mhamasishaji wa kiroho, na pia kama kiongozi wa mikutano iliyofanyika katika nyumba za watu waliokuwa mbali na mji. Hata hivyo, mchungaji wa Kimethodisti alitufanyia ziara maalumu, na akatumia nafasi hiyo kutujulisha kwamba imani yetu na Umethodisti haviwezi kupatana. Hakutuuliza sababu zetu za kuamini tulivyoamini, wala hakurejelea Biblia ili kutushawishi kwamba tulikuwa tumekosea; bali alisema tu kwamba tulikuwa tumekubali imani mpya na ya ajabu ambayo Kanisa la Kimethodisti lisingeweza kuikubali.**[CETsw 41.3]**

Baba yangu alijibu kwamba lazima mchungaji huyo alikuwa amekosea kwa kuita fundisho hili kuwa ni fundisho jipya na la ajabu; kwa sababu Kristo Mwenyewe, katika mafundisho Yake kwa wanafunzi Wake, alikuwa amefundisha kuhusu ujio Wake wa pili. Alisema: **"Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi Mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe Kwangu; ili nilipo Mimi, nanyi mwepo."** (Yohana 14:2, 3) Alipochukuliwa kwenda mbinguni, wakati wafuasi Wake waaminifu walipokuwa wakimtazama Bwana wao aliyekuwa akitoweka machoni mwao, **"tazama, watu wawili wakasimama karibu nao, wenye nguo nyeupe,kasema, Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni."** (Matendo 1:10, 11) **[CETsw 43.1]**

**"Na zaidi ya hayo,"** alisema baba yangu, huku akizidi kupata msisimko kwa sababu ya jambo alilokuwa akizungumzia, **"**Paulo aliyevuviwa aliandika barua ili kuwafariji ndugu zake huko Thesalonike, akisema: **'na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa Kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza Wake katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu Zake; Yeye atakapokuja ili kutukuzwa katika watakatifu Zake, na kustaajabiwa katika wote waliosadiki katika siku ile'** (2 Wathesalonike 1:7-10) **'Kwa sababu Bwana Mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele. Basi, farijianeni kwa Maneno hayo.'** (1 Wathesalonike 4:16-18) **[CETsw 43.2]**

"Huu ndio ushahidi wenye mamlaka kuu kwa ajili ya imani yetu. Yesu na mitume Wake walizungumzia ujio wa pili kwa furaha na ushindi; na malaika watakatifu walitangaza kwamba Kristo, aliyepaa kwenda mbinguni, atarudi tena. Hili ndilo kosa letu—kuamini Neno la Yesu na wanafunzi Wake. Hili ni fundisho la zamani sana, wala halina doa lolote la uzushi."**[CETsw 44.1]**

Mchungaji huyo hakujaribu kurejelea hata andiko moja ambalo lingethibitisha kwamba tulikuwa tumekosea, bali alijitetea kwa kusema kwamba hakuwa na muda wa kutosha. Alitushauri tujiondoe kwa utulivu kanisani na tuepuke aibu ya kufanyiwa kesi ya kanisa. Tulijua kwamba baadhi ya ndugu zetu wengine walikuwa wakitendewa vivyo hivyo kwa sababu hiyo hiyo, na hatukutaka ionekane kwamba tulikuwa na aibu kukiri imani yetu, au kwamba hatungeweza kuitetea kwa Maandiko; hivyo wazazi wangu walisisitiza kwamba waelezwe sababu za ombi hilo.**[CETsw 44.2]**

Jibu pekee lililotolewa lilikuwa kauli isiyo wazi kwamba tulikuwa tumekiuka kanuni za kanisa, na kwamba jambo bora zaidi lilikuwa kujiondoa wenyewe kwa hiari ili kuepuka kesi. Tulijibu kwamba tulipendelea kufanyiwa mkutano wa majadiliano au kesi rasmi, na tukataka kujua ni dhambi gani tuliyoshtakiwa nayo, kwa kuwa tulikuwa na dhamiri safi kwamba hatukufanya kosa lolote kwa kutazamia na kupenda kuonekana kwa Mwokozi.**[CETsw 44.3]**

## 5. KUKATA TAMAA

Kwa uangalifu mkubwa na kwa kutetemeka mioyoni mwetu, tulikaribia wakati ambao Mwokozi wetu alitarajiwa kuonekana. Kwa bidii takatifu tulitafuta, kama watu wa Mungu, kutakasa maisha yetu ili tuwe tayari kukutana Naye wakati wa kuja Kwake. Mikutano iliendelea kufanyika katika nyumba za watu binafsi katika sehemu mbalimbali za mji, ikiwa na matokeo mema sana. Waumini walitiwa moyo kuwafanyia kazi ya kuongoa marafiki zao na ndugu zao, na idadi ya waongofu ilikuwa ikiongezeka siku baada ya siku. **[CETsw 45.1]**

**Mikutano katika Ukumbi wa Beethoven**

Licha ya upinzani kutoka kwa wachungaji na makanisa, Ukumbi wa Beethoven uliokuwa katika mji wa Portland ulikuwa ukijaa watu kila usiku; hasa siku za Jumapili kulikuwa na mkusanyiko mkubwa sana. Watu wa tabaka zote walimiminika katika mikutano hiyo. Matajiri na maskini, wakuu na watu wa kawaida, wachungaji na waumini wa kawaida, wote walikuwa na shauku ya kusikia wenyewe fundisho la ujio wa pili wa Kristo kwa sababu mbalimbali. Wengi walifika lakini, kwa kuwa hakukuwa na nafasi ya kusimama, waliondoka wakiwa wamekatishwa tamaa.**[CETsw 45.2]**

Mpangilio wa mikutano hiyo ulikuwa rahisi. Kwa kawaida mahubiri mafupi na yenye kueleweka yalitolewa kwanza, kisha nafasi ilitolewa kwa ajili ya mawaidha ya jumla. Kwa kawaida kulikuwa na utulivu mkubwa kabisa ambao ungewezekana kupatikana katika mkusanyiko mkubwa namna hiyo. Bwana aliizuia roho ya upinzani wakati watumishi Wake walipokuwa wakieleza sababu za imani yao. Wakati mwingine mhubiri alikuwa na uwezo mdogo wa kibinadamu, lakini Roho wa Mungu aliupa uzito na nguvu ukweli Wake. Uwepo wa malaika watakatifu ulionekana kuhisiwa katika mkusanyiko huo, na idadi ya waumini ilikuwa ikiongezeka kila siku katika kundi hilo dogo la waumini.**[CETsw 45.3]**

Katika tukio moja, wakati Mzee Stockman alipokuwa akihubiri, Mzee Brown, mchungaji wa Kikristo wa Kibaptisti, alikuwa ameketi madhabahuni akisikiliza mahubiri hayo kwa shauku kubwa. Aliguswa sana moyoni, na ghafla uso wake ukawa mweupe kama wa mtu aliyekufa. Alitikisika akiwa kwenye kiti chake, na Mzee Stockman alimshika mikononi mwake wakati tu alipokuwa akianguka chini. Kisha akamlaza kwenye sofa iliyokuwa nyuma ya madhabahu, ambapo alilala bila nguvu mpaka mahubiri yalipomalizika.**[CETsw 45.4]**

Baada ya hapo aliinuka; uso wake bado ulikuwa umepauka, lakini ulikuwa unang’aa kwa nuru iliyotoka kwa Jua la Haki. Kisha alitoa ushuhuda wenye kugusa sana. Alionekana kupokea upako mtakatifu kutoka juu. Kwa kawaida alikuwa mtu wa kuzungumza polepole, mwenye mtazamo wa bidii na asiyeonyesha msisimko wa kupita kiasi. Lakini katika tukio hili, maneno yake yenye uzito na yaliyotamkwa kwa utulivu yalikuwa yamebeba nguvu mpya.**[CETsw 46.1]**

Alieleza uzoefu wake kwa unyenyekevu mkubwa na kwa uaminifu kiasi kwamba wengi waliokuwa na chuki kubwa waliguswa mpaka wakalia. Roho wa Mungu alionekana katika

maneno yake na kuonekana wazi katika uso wake. Kwa furaha takatifu na ujasiri mkubwa alitangaza kwamba alikuwa amelichukua Neno la Mungu kuwa mshauri wake; kwamba mashaka yake yalikuwa yameondolewa kabisa na imani yake ilikuwa imethibitishwa. Kwa bidii aliwaalika ndugu zake wachungaji, washiriki wa kanisa, wenye dhambi, na wasioamini waichunguze Biblia wenyewe, na akawasihi wasimruhusu mtu yeyote kuwageuza kutoka katika kusudi lao la kujua Ukweli.**[CETsw 46.2]**

Alipomaliza kuzungumza, wale waliotamani maombi ya watu wa Mungu waliombwa wasimame. Mamia ya watu waliitikia mwito huo. Roho Mtakatifu alishuka juu ya mkusanyiko huo. Mbingu na dunia zilionekana kukaribiana. Mkutano uliendelea mpaka saa za usiku zilipokuwa zimeenda sana. Nguvu ya Bwana ilionekana juu ya vijana, wazee, na watu wa umri wa kati.**[CETsw 46.3]**

Mzee Brown hakukatiza uhusiano wake na Kanisa la Kikristo wakati huo wala baadaye, bali aliheshimiwa sana na watu wake. **[CETsw 46.4]**

**Matarajio ya Furaha**

Tulipokuwa tukirudi nyumbani kwa njia mbalimbali, sauti ya mtu akimsifu Mungu ilitufikia kutoka upande mmoja, na kana kwamba ilikuwa ikijibiwa, sauti nyingine kutoka upande mwingine na tena upande mwingine ilisikika ikisema: “Utukufu kwa Mungu, Bwana anatawala!” Watu walirudi majumbani mwao wakiwa na sifa za Mungu midomoni mwao, na sauti hiyo ya furaha ilisambaa katika utulivu wa hewa ya usiku. Hakuna aliyeshiriki katika mikutano hiyo ambaye angeweza kusahau matukio hayo yenye mvuto mkubwa. **[CETsw 47.1]**

Wale wanaompenda Yesu kwa kweli wanaweza kuelewa hisia za wale waliokuwa wakitazamia kwa hamu kubwa sana kuja kwa Mwokozi wao. Wakati wa matarajio ulikuwa umekaribia. Wakati ambao tulitumaini kukutana Naye ulikuwa karibu sana. Tulikikaribia kipindi hicho kwa utulivu wenye heshima na uzito. Waumini wa kweli walikuwa wakifurahia ushirika mtamu pamoja na Mungu—ikiwa ni mwanzo wa amani ambayo wangekuwa nayo katika maisha yale mazuri yajayo. Hakuna yeyote aliyepitia tumaini hili na imani hii ambaye angeweza kusahau saa zile za thamani za kungojea. **[CETsw 47.2]**

Kwa sehemu kubwa, shughuli za kidunia ziliachwa kwa muda wa majuma kadhaa. Tulichunguza kwa makini kila wazo na kila hisia ya mioyo yetu, kana kwamba tulikuwa katika kitanda cha kifo na tulikuwa karibu kufumba macho yetu milele kwa mambo ya dunia. Hakukuwa na utengenezaji wa “mavazi ya kupaa” kwa ajili ya tukio hilo kuu; tulihisi kwamba tulihitaji ushahidi wa ndani unaoonyesha kwamba tulikuwa tayari kukutana na Kristo. Na mavazi yetu meupe yalikuwa usafi wa nafsi, yaani tabia iliyosafishwa kutoka katika dhambi kwa damu ya upatanisho ya Mwokozi wetu.**[CETsw 47.3]**

**Siku za Mashaka**

Lakini wakati wa matarajio ulipita. Huu ulikuwa mtihani wa kwanza mkubwa uliowapata wale waliokuwa wameamini na kutumaini kwamba Yesu angekuja katika mawingu ya mbinguni. Kukatishwa tamaa kwa watu wa Mungu waliokuwa wakingojea kulikuwa kukubwa sana. Wenye dhihaka walishangilia ushindi, na wakawavuta wale waliokuwa dhaifu na waoga kujiunga nao. Baadhi ya watu waliokuwa wameonekana kuwa na imani ya Kweli walionekana kwamba walikuwa wamechochewa tu na hofu; na sasa ujasiri wao ulirudi baada ya muda wa matarajio kupita. Kwa ujasiri walijiunga na wenye dhihaka, wakitangaza kwamba hawakuwa kamwe wamedanganyika kiasi cha kuamini kwa kweli fundisho la Miller, ambaye walimwita mshupavu mwendawazimu. Wengine, ambao kwa asili walikuwa watu wa kubadilika-badilika au wasiosimamia msimamo wao, waliliacha jambo hilo kimya kimya.**[CETsw 47.4]**

Tulikuwa katika hali ya mashaka na kukatishwa tamaa, lakini hatukuiacha imani yetu. Wengi bado walishikilia tumaini kwamba Yesu asingekawia sana kuja Kwake; Neno la Bwana lilikuwa hakika, lisingeweza kushindwa. Tulihisi kwamba tulikuwa tumetimiza wajibu wetu, na kwamba tuliishi kulingana na imani yetu ya thamani; tulikuwa tumekatishwa tamaa, lakini hatukuvunjika moyo. Ishara za nyakati zilionyesha kwamba mwisho wa mambo yote ulikuwa karibu; hivyo ilitupasa kukesha na kujiweka tayari kwa ajili ya kuja kwa Bwana wakati wowote. Ilitupasa kungoja kwa tumaini na imani, bila kupuuza kukutana pamoja kwa ajili ya mafundisho, kutiana moyo, na kufarijiana, ili nuru yetu iweze kuangaza katika giza la ulimwengu. **[CETsw 49.1]**

**Kosa Katika Kuhesabu Muda:** Hesabu yetu ya wakati wa unabii ilikuwa rahisi sana na wazi kiasi kwamba hata watoto wangeweza kuielewa. Kuanzia tarehe ya amri ya mfalme wa Uajemi, inayopatikana katika Ezra 7, ambayo ilitolewa mwaka wa 457 kabla ya Kristo, miaka 2300 ya Danieli 8:14 ilidhaniwa kuwa ingemalizika mwaka 1843. Kwa hiyo, tulitarajia mwisho wa mwaka huo kuwa wakati wa kuja kwa Bwana. Tulikatishwa tamaa sana mwaka huo ulipopita kabisa, na Mwokozi hakuja. **[CETsw 49.2]**

Mwanzoni haikutambuliwa kwamba ikiwa amri hiyo haikutolewa mwanzoni mwa mwaka 457 K.K., basi miaka 2300 isingekamilika mwishoni mwa mwaka 1843. Lakini baadaye iligunduliwa kwamba amri hiyo ilitolewa karibu na mwisho wa mwaka 457 K.K.; kwa hiyo kipindi cha unabii kilipaswa kufikia majira ya mwisho ya mwaka 1844. Hivyo maono hayo ya wakati hayakuwa yamechelewa, ingawa yalionekana kana kwamba yamechelewa. Tulijifunza kutegemea maneno ya nabii: "Maana njozi hii bado ni kwa wakati ulioamriwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake, wala haitasema uongo; ijapokawia, ingojee; kwa kuwa haina budi kuja, haitakawia." (Habakkuki 2:3) **[CETsw 50.1]**

Mungu aliwajaribu na kuwathibitisha watu Wake kwa kupita kwa wakati mwaka wa 1843. Kosa lililofanyika katika kuhesabu vipindi vya unabii halikugunduliwa mara moja, hata na wasomi waliopinga maoni ya wale waliokuwa wakitazamia kuja kwa Kristo. Wasomi walikubali kwamba Bwana Miller alikuwa sahihi katika hesabu yake ya muda, ingawa walimpinga kuhusu tukio ambalo lingetokea mwishoni mwa kipindi hicho. Lakini wao pamoja na watu wa Mungu waliokuwa wakingojea walikuwa katika kosa moja kuhusu suala la muda.**[CETsw 50.2]**

Wale waliokuwa wamekatishwa tamaa hawakuachwa gizani kwa muda mrefu; kwa sababu walipochunguza vipindi vya unabii kwa maombi ya dhati, kosa liligunduliwa, na ufuatiliaji wa kalamu ya unabii ukaendelea kupitia kipindi kile cha kuchelewa. Katika matarajio ya furaha ya kuja kwa Kristo, kuchelewa kulikoonekana katika utimilifu wa maono hakukuwa kumezingatiwa, na jambo hilo likawa mshangao wenye huzuni na usiotarajiwa. Hata hivyo, jaribu hilo lilikuwa la lazima ili kuwajenga na kuwaimarisha waumini wa kweli katika Ukweli.**[CETsw 50.3]**

**Tumaini Lililohuishwa**

Sasa matumaini yetu yalielekezwa katika kuja kwa Bwana mwaka wa 1844. Huu pia ulikuwa wakati wa ujumbe wa malaika wa pili, ambaye, akiruka katikati ya mbingu, alipaza sauti: "Umeanguka, umeanguka Babeli mji ule ulio mkubwa." (Ufunuo 14:8) Ujumbe huo ulitangazwa kwanza na watumishi wa Mungu katika majira ya kiangazi ya mwaka 1844. Matokeo yake yalikuwa kwamba wengi waliyaacha makanisa yaliyoanguka. Kuhusiana na ujumbe huu, "kilio cha usiku wa manane" kilitolewa: "Tazama, Bwana arusi anakuja; tokeni mwende kumlaki." Katika kila sehemu ya nchi, nuru ilitolewa kuhusu ujumbe huu, na mwito huo uliwaamsha maelfu ya watu. Ulienda kutoka mji mmoja hadi mwingine, kutoka kijiji kimoja hadi kingine, na kufikia hata maeneo ya mbali ya vijijini. Uliwafikia watu wenye elimu na vipawa, pamoja na wale waliokuwa watu wa kawaida na wanyenyekevu.**[CETsw 50.4]**

Huu ulikuwa mwaka wenye furaha zaidi katika maisha yangu. Moyo wangu ulijaa matarajio ya furaha; lakini nilihisi huruma kubwa na wasiwasi kwa ajili ya wale waliokuwa wamekata tamaa na hawakuwa na tumaini katika Yesu. Sisi kama watu tuliungana katika maombi ya dhati, tukimwomba Mungu atupe uzoefu wa Kweli na ushahidi usioweza kukosewa kwamba tumekubaliwa Naye.**[CETsw 51.1]**

**Jaribu la Imani**

Tulihitaji uvumilivu mkubwa sana, kwa sababu wenye dhihaka walikuwa wengi. Mara nyingi tulikaribishwa kwa maneno ya kejeli yaliyohusu kukatishwa tamaa kwetu hapo awali. Makanisa ya kawaida yalitumia kila njia kuzuia imani ya kuja kwa Kristo upesi isienee. Hakukuwa na uhuru uliotolewa katika mikutano yao kwa wale waliothubutu kutaja tumaini la kuja kwa Kristo lililokuwa karibu. Wale waliodai kumpenda Yesu kwa dharau walikataa habari kwamba Yeye waliyemdai kuwa Rafiki yao mkuu alikuwa karibu kuwatembelea. Walikasirika na kuchukizwa dhidi ya wale waliotangaza habari za kuja Kwake, na ambao walifurahia kwamba wangemwona upesi katika utukufu Wake. **[CETsw 51.1]**

**Kipindi cha Maandalizi**

Kila wakati ulionekana kwangu kuwa wa umuhimu mkubwa sana. Nilihisi kwamba tulikuwa tukifanya kazi kwa ajili ya umilele, na kwamba wale waliokuwa wazembe na wasiojali

walikuwa katika hatari kubwa sana. Imani yangu haikuwa na wingu lolote la mashaka, na nilijishikilia mwenyewe katika ahadi za thamani za Yesu. Alikuwa amewaambia wanafunzi Wake: **"Ombeni, nanyi mtapokea."** Niliamini kwa uthabiti kwamba chochote nilichokiomba kulingana na mapenzi ya Mungu, hakika ningepokea. Nilijinyenyekeza miguuni pa Yesu, moyo wangu ukiwa katika upatanifu na mapenzi Yake. **[CETsw 52.2]**

Mara nyingi nilitembelea familia mbalimbali, na kufanya nao maombi ya dhati wale waliokuwa wamelemewa na hofu na kukata tamaa. Imani yangu ilikuwa na nguvu kiasi kwamba sikutilia shaka hata kwa muda mfupi kwamba Mungu angejibu maombi yangu. Bila ubaguzi wowote, baraka na amani ya Yesu zilishuka juu yetu kama jibu la maombi yetu ya unyenyekevu, na mioyo ya wale waliokuwa wamekata tamaa ilijazwa furaha kupitia nuru na tumaini. **[CETsw 52.3]**

Kwa kuchunguza mioyo yetu kwa bidii na uadilifu na kwa maungamo ya unyenyekevu, tulifika kwa maombi hadi wakati wa matarajio. Kila asubuhi tulihisi kwamba kazi yetu ya kwanza ilikuwa kuhakikisha ushahidi kwamba maisha yetu yalikuwa sawa mbele za Mungu. Tulitambua kwamba ikiwa hatukuwa tukisonga mbele katika utakatifu, bila shaka tungeanza kurudi nyuma. Upendo wetu na kujaliana kwetu sisi kwa sisi viliongezeka; tuliomba sana pamoja na kwa ajili ya kila mmoja wetu. Tulikutanika katika bustani za matunda na maeneo yenye miti ili kuwa na ushirika na Mungu na kumtolea maombi yetu, tukihisi uwepo Wake kwa ukamilifu zaidi tulipokuwa tumezungukwa na kazi Zake za asili. Furaha ya wokovu ilikuwa muhimu kwetu kuliko chakula na kinywaji chetu. Ikiwa mawingu yangetanda juu ya akili zetu, hatukuthubutu kupumzika wala kulala mpaka mawingu hayo yalipoondolewa kwa hakikisho la kwamba tumekubaliwa na Bwana.**[CETsw 53.1]**

**Kupita kwa Wakati Uliotarajiwa**

Watu wa Mungu waliokuwa wakingojea walikaribia saa ile ambayo kwa furaha kubwa walitumaini kwamba furaha yao ingetimia kwa kuja kwa Mwokozi. Lakini tena muda huo ulipita bila Yesu kuonekana. Ilikuwa ni hali ya kukatishwa tamaa kwa uchungu iliyowapata kundi lile dogo ambalo imani yake ilikuwa imara sana na tumaini lake lilikuwa kubwa sana. Lakini tulishangaa kuona kwamba tulikuwa na uhuru mkubwa katika Bwana, na kwamba tuliimarishwa sana kwa nguvu na neema Yake. **[CETsw 54.1]**

Hata hivyo, uzoefu wa mwaka uliotangulia ulijirudia kwa kiwango kikubwa zaidi. Kundi kubwa la watu liliacha imani yao. Baadhi ya wale waliokuwa na uhakika mkubwa sana walijeruhiwa sana katika kujivunia kwao kiasi kwamba walitamani kuukimbia ulimwengu. Kama Yona, walimlalamikia Mungu, na wakachagua kufa kuliko kuishi. Wale waliokuwa wamejenga imani yao juu ya ushahidi wa watu wengine, badala ya Neno la Mungu, sasa walikuwa tayari tena kubadilisha maoni yao. Jaribu hili kuu la pili lilifunua wingi wa mabaki yasiyofaa yaliyokuwa yamevutwa katika mkondo wenye nguvu wa imani ya ujio, na ambayo yalikuwa yamesafirishwa kwa muda pamoja na waumini wa kweli na watendakazi wenye bidii. **[CETsw 54.2]**

Tulikatishwa tamaa, lakini hatukuvunjika moyo. Tuliamua kujizuia kulalamika dhidi ya jaribu hilo gumu ambalo kupitia hilo Bwana alikuwa akitusafisha na uchafu kama chuma kinavyosafishwa, na kututakasa kama dhahabu katika tanuru. Tulidhamiria kujinyenyekeza kwa uvumilivu katika mchakato wa utakaso ambao Mungu aliona kuwa wa lazima kwetu, na kungoja kwa tumaini lenye subira Mwokozi awakomboe watu Wake waliokuwa wamejaribiwa na waaminifu.**[CETsw 54.3]**

Tulikuwa thabiti katika imani kwamba kuhubiri wakati maalumu wa unabii kulitokana na Mungu. Ni jambo hilo lililowafanya watu wachunguze Biblia kwa bidii, na kugundua kweli ambazo hapo awali hawakuwa wameziona. Yona alitumwa na Mungu kutangaza katika barabara za Ninawi kwamba ndani ya siku arobaini mji huo ungeangamizwa; lakini Mungu alikubali unyenyekevu wa watu wa Ninawi, na akaongeza muda wao wa majaribu. Hata hivyo, ujumbe ambao Yona aliutoa ulitumwa na Mungu, na Ninawi ilijaribiwa kulingana na mapenzi Yake. Ulimwengu uliliona tumaini letu kuwa ni udanganyifu, na kukatishwa tamaa kwetu kuwa matokeo ya kushindwa kwake; lakini ingawa tulikosea kuhusu tukio ambalo lilipaswa kutokea katika kipindi hicho, kwa kweli hakukuwa na kushindwa kwa maono yale yaliyoonekana kuchelewa.**[CETsw 54.4]**

Wale waliokuwa wakitazamia kuja kwa Bwana hawakuachwa bila faraja. Walikuwa wamepata maarifa ya thamani kupitia kuchunguza kwa kina Neno la Mungu. Mpango wa wokovu ulikuwa umeeleweka wazi zaidi kwao. Kila siku waligundua uzuri mpya katika kurasa takatifu, na kuona upatanifu wa ajabu uliopita katika Maandiko yote; kila aAndiko likieleza lingine, na hakuna Neno lolote lililotumiwa bila kusudi. **[CETsw 55.1]**

Kukatishwa tamaa kwetu hakukuwa kukubwa kama ule wa wanafunzi wa Yesu. Wakati Mwana wa Adamu alipoingia Yerusalemu kwa ushindi, walitarajia kwamba angevikwa taji na kuwa mfalme. Watu walimiminika kutoka maeneo yote yaliyokuwa karibu, wakipaza sauti: **"Hosana kwa Mwana wa Daudi!"** (Mathayo 21:9) Na makuhani na wazee walipomsihi Yesu awanyamazishe wale watu, Yeye alitangaza kwamba ikiwa wangekaa kimya, hata mawe yangepiga kelele, kwa sababu unabii ulipaswa kutimia. Hata hivyo, baada ya siku chache tu, wanafunzi hao hao walimwona Bwana wao mpendwa, ambaye waliamini kwamba angeutawala ufalme wa Daudi, akiwa ametundikwa juu ya msalaba wenye ukatili mbele ya Mafarisayo waliokuwa wakimdhihaki na kumtukana. Matumaini yao makubwa yalivunjika, na giza la kifo likawazunguka. Lakini Kristo alikuwa mwaminifu kwa ahadi Zake. Faraja aliyowapa watu Wake ilikuwa tamu sana, na thawabu ya wale waaminifu na wenye kushikilia Kweli ilikuwa kubwa. **[CETsw 56.1]**

Bwana Miller na wale waliokuwa wameungana naye walidhani kwamba **kutakaswa kwa Patakatifu** kunakotajwa katika Danieli 8:14 kulimaanisha kusafishwa kwa dunia kwa moto kabla haijawa makao ya watakatifu. Walidhani kwamba jambo hili lingetokea wakati wa ujio wa pili wa Kristo; kwa hiyo tulitazamia tukio hilo mwishoni mwa siku 2300, yaani miaka 2300. Lakini baada ya kukatishwa tamaa kwetu, Maandiko yalichunguzwa kwa uangalifu mkubwa, kwa maombi na tafakari ya dhati. Baada ya kipindi cha kusubiri kwa mashaka, nuru ilianza kumulika giza letu; mashaka na kutokuwa na uhakika viliondolewa. **[CETsw 56.2]**

Badala ya unabii wa Danieli 8:14 kumaanisha kutakaswa kwa dunia, sasa ilikuwa wazi kwamba ulielekeza kwenye kazi ya mwisho ya Kuhani wetu Mkuu huko mbinguni, kukamilishwa kwa upatanisho, na maandalizi ya watu wa Mungu ili waweze kusimama katika siku ya kuja Kwake.**[CETsw 56.3]**

## 6. MAONO YANGU YA KWANZA

Haikupita muda mrefu baada ya kupita kwa wakati huo mwaka wa 1844, ndipo nilipopewa maono yangu ya kwanza. Nilikuwa nimemtembelea Bi. Haines huko Portland, dada mpendwa katika Kristo ambaye moyo wake ulikuwa umeunganishwa na wangu; tulikuwa wanawake watano, wote tukipiga magoti kwa utulivu kwenye madhabahu ya familia kwa ajili ya ibada. Tulipokuwa tukiomba, nguvu ya Mungu ilinijia kwa namna ambayo sikuwahi kuipitia hapo awali.**[CETsw 57.1]**

Nilionekana nimezungukwa na nuru, na kuinuliwa juu zaidi na zaidi kutoka duniani. Niligeuka kutafuta watu wa marejeo (Waadventista) waliokuwa duniani, lakini sikuweza kuwaona. Ndipo sauti ikaniambia: **"Tazama tena, na tazama juu kidogo zaidi."** Nilipoinua macho yangu, niliona njia nyembamba na iliyonyooka, iliyoinuliwa juu sana kuliko dunia. Katika njia hiyo watu wa marejeo walikuwa wakisafiri kuelekea mji uliokuwa mwisho wa njia hiyo. Walikuwa na nuru kubwa iliyowekwa nyuma yao mwanzoni mwa njia hiyo, ambayo malaika aliniambia ilikuwa **"Kilio cha usiku wa manane-Midnite Cry."** (Tazama Mathayo 25:6) Nuru hiyo iliangaza njia yote, na kutoa mwanga kwa miguu yao ili wasijikwae. **[CETsw 57.2]**

Ikiwa wangeendelea kumtazama Yesu, aliyekuwa mbele yao akiwa anawaongoza kwenda mjini ule, wangekuwa salama. Lakini baada ya muda baadhi yao walichoka, na kusema kwamba mji huo ulikuwa mbali sana, na kwamba walitarajia kuwa wamekwisha kufika humo mapema. Ndipo Yesu angewatia moyo kwa kuinua mkono Wake wa kulia wenye utukufu; na kutoka katika mkono Wake kulitoka nuru iliyowamulikia kundi la waamini wa ujio. Nao wakapaza sauti: **"Haleluya!"** Wengine kwa ujasiri wa kiburi waliikataa nuru iliyokuwa nyuma yao, wakisema kwamba haikuwa Mungu aliyekuwa amewaongoza mpaka hapo. Nuru iliyokuwa nyuma yao ikazimika, na kuacha miguu yao katika giza kamili. Wakajikwaa, wakapoteza alama ya njia na macho yao yakaacha kumtazama Yesu tena, kisha wakaanguka kutoka kwenye njia ile kwenda katika dunia ya chini yenye giza na uovu. **[CETsw 57.3]**

Muda mfupi baadaye tulisikia sauti ya Mungu kama sauti ya maji mengi, iliyotujulisha siku na saa ya kuja kwa Yesu. Watakatifu walio hai, waliokuwa 144,000 kwa idadi, waliifahamu na kuielewa sauti hiyo; lakini waovu walidhani ilikuwa ni radi na tetemeko la nchi. Mungu aliposema wakati huo, alimimina juu yetu Roho Mtakatifu, na nyuso zetu zikaanza kung'aa na kuangaza kwa utukufu wa Mungu, kama uso wa Musa ulivyong'aa aliposhuka kutoka Mlima Sinai. **[CETsw 58.1]**

Wale 144,000 wote walitiwa muhuri, na walikuwa wameungana kikamilifu. Kwenye vipaji vya nyuso zao palikuwa pameandikwa: **"Mungu, Yerusalemu Mpya,"** na kulikuwa na nyota yenye utukufu iliyokuwa na jina jipya la Yesu. Katika hali yetu ya furaha na utakatifu, waovu walikasirika sana, na wangekimbia kwa nguvu ili kutukamata na kututia gerezani. Lakini tuliponyoosha mkono wetu kwa Jina la Bwana, walianguka chini bila nguvu. Ndipo ulipofika wakati ambapo sinagogi la Shetani lilijua kwamba Mungu alikuwa ametupenda sisi ambao tuliweza kuoshana miguu, na kusalimiana sisi kwa sisi kwa busu takatifu. Nao walisujudu miguuni petu.**[CETsw 58.2]**

Muda mfupi baadaye macho yetu yalielekezwa upande wa mashariki, kwa sababu lilikuwa limetokea wingu dogo jeusi, lenye ukubwa karibu nusu ya kiganja cha mkono wa mtu, ambalo sote tulijua kuwa lilikuwa ishara ya Mwana wa Adamu. Sote tulilitazama lile wingu kwa ukimya wa heshima na utakatifu lilipokuwa likikaribia, likazidi kuwa jepesi, lenye utukufu, na kuendelea kuwa lenye utukufu zaidi, mpaka likawa wingu kubwa jeupe. Sehemu ya chini ya wingu hilo ilionekana kama moto; upinde wa mvua ulikuwa juu ya wingu hilo, huku kulizunguka maelfu kumi ya malaika, wakiimba wimbo mzuri sana. Juu ya wingu hilo aliketi Mwana wa Adamu. Nywele Zake zilikuwa nyeupe na zilizojikunja/zilizojisokota, zikiwa zimeanguka juu ya mabega Yake; na juu ya kichwa Chake palikuwa na taji nyingi. Miguu Yake ilikuwa na sura kama ya moto; katika mkono Wake wa kulia alikuwa na mundu mkali, na katika mkono Wake wa kushoto palikuwa na tarumbeta ya fedha. Macho Yake yalikuwa kama mwali wa moto, yakichunguza watoto Wake kabisa ndani na nje. Ndipo nyuso zote zikawa na weupe kwa hofu, na wale ambao Mungu alikuwa amewakataa wakafunikwa na giza. Kisha sisi sote tukalia: **"Ni nani atakayeweza kusimama? Je, vazi langu ni safi lisilo na doa?"** Ndipo malaika wakaacha kuimba, na kukawa na ukimya wa kutisha kwa muda fulani. Kisha Yesu akasema: **"Wale walio na mikono safi na mioyo safi wataweza kusimama; neema Yangu yawatosha."** Kwa maneno hayo nyuso zetu zikaangaza, na furaha ikajaza kila moyo. Malaika wakapiga sauti ya juu zaidi na kuanza kuimba tena, huku lile wingu likizidi kulikaribia dunia. **[CETsw 58.3]**

Ndipo tarumbeta ya fedha ya Yesu ikasikika, alipokuwa akishuka juu ya lile wingu lililofunikwa na miali ya moto. Aliangalia makaburi ya watakatifu waliolala, kisha akainua macho na mikono Yake kuelekea mbinguni, akalia: **"Amkeni! Amkeni! Amkeni, ninyi mlalao mavumbini, na kuinuka."** Ndipo pakatokea tetemeko kubwa sana la nchi. Makaburi yakafunguka, na wafu wakatoka wakiwa wamevikwa kutokufa. Wale 144,000 walipaza sauti: **"Haleluya!"** walipowatambua marafiki zao waliokuwa wameporwa kutoka kwao kwa njia ya kifo. Na wakati huo huo sisi tulibadilishwa na kuchukuliwa pamoja nao kwenda kumlaki Bwana hewani. **[CETsw 59.1]**

Sote tuliingia ndani ya lile wingu pamoja, na tukatumia siku saba tukipanda kuelekea bahari ya kioo. Huko Yesu alileta taji, na kwa mkono Wake mwenyewe wa kulia akaziweka juu ya vichwa vyetu. Alitupatia vinubi vya dhahabu na matawi ya ushindi. Huko kwenye bahari ya kioo wale 144,000 walisimama katika umbo la mraba kamili. Baadhi yao walikuwa na taji zenye

kung'aa sana, wengine taji ambazo hazikung'aa sana. Baadhi ya taji zilionekana kuwa nzito kwa sababu zilikuwa zimejaa nyota, huku nyingine zikiwa na nyota chache tu. Lakini wote waliridhika kabisa na taji zao. Wote walikuwa wamevikwa mavazi meupe yenye utukufu yaliyotoka mabegani hadi miguuni. Malaika walikuwa wametuzunguka pande zote tulipokuwa tukitembea juu ya bahari ya kioo kuelekea lango la mji. Yesu aliinua mkono Wake mkuu wenye utukufu, akalishika lango la lulu, akalifungua kutoka kwenye bawaba zake zinazong'aa, kisha akatuambia: **"Mmefua mavazi yenu katika damu Yangu, mkasimama imara kwa ajili ya Kweli Yangu; ingieni."** Sote tuliingia ndani, na tulihisi kwamba tulikuwa na haki kamili ya kuwa katika mji ule. **[CETsw 59.2]**

Huko tuliona **mti wa uzima** na **kiti cha enzi cha Mungu**. Kutoka katika kiti cha enzi kilitoka mto safi wa maji, na kila upande wa mto huo kulikuwa na mti wa uzima. Upande mmoja wa mto kulikuwa na shina la mti, na upande mwingine kulikuwa na shina lingine; yote mawili yalikuwa ya dhahabu safi, yenye uwazi. Mwanzoni nilifikiri niliona miti miwili. Lakini nilipotazama tena, niliona kwamba ilikuwa imeungana juu na kuwa mti mmoja. Hivyo ulikuwa ni **mti wa uzima** uliokuwa kila upande wa mto wa uzima. Matawi yake yalipinda kuelekea mahali tuliposimama, na matunda yake yalikuwa yenye utukufu; yalionekana kama dhahabu iliyochanganywa na fedha. **[CETsw 60.1]**

Sote tulienda chini ya mti ule, na tukaketi ili kutazama utukufu wa mahali pale. Ndipo ndugu **Fitch** na **Stockman**, ambao walikuwa wamehubiri injili ya ufalme, na ambao Mungu alikuwa amewaweka kaburini ili awaokoe, walikuja kwetu na kutuuliza ni mambo gani tuliyopitia wakati wao walipokuwa wamelala. Tulijaribu kukumbuka kwa bidii majaribu yetu makubwa zaidi, lakini yalionekana kuwa madogo sana yakilinganishwa na uzito wa utukufu ulio mkuu mno na wa milele uliokuwa umetuzunguka. Hivyo hatukuweza hata kuyaeleza, bali sote tukapaza sauti: "Haleluya! Mbingu zina thamani inayozidi sana gharama yoyote tuliyolipa!" Kisha tukagusa vinubi vyetu vya utukufu, na kufanya matao ya mbinguni yasikike kwa sauti za sifa. **[CETsw 61.1]**

Baada ya kutoka katika maono, kila kitu kilionekana kimebadilika. Giza lilienea juu ya kila kitu nilichokitazama. Oh, jinsi ulimwengu huu ulivyoonekana kuwa wenye giza kwangu! Nililia nilipojikuta tena hapa, na nilihisi kutamani kurudi nyumbani. Nilikuwa nimeona ulimwengu bora zaidi, na jambo hilo liliufanya ulimwengu huu usiwe na mvuto tena kwangu. **[CETsw 61.2]**

Nilisimulia maono haya kwa waumini huko Portland, ambao walikuwa na imani kamili kwamba yalitoka kwa Mungu. Wote waliamini kwamba Mungu alikuwa amechagua njia hii, baada ya kukatishwa tamaa kukubwa kwa mwezi wa Oktoba, ili kuwafariji na kuwaimarisha watu Wake. Roho wa Bwana aliambatana na ushuhuda huo, na hali ya umilele ilitanda juu yetu. Hofu takatifu isiyoweza kusemwa ilinijaa moyoni, kwamba mimi nikiwa kijana mdogo na dhaifu kiasi hicho, nilikuwa nimechaguliwa kuwa chombo ambacho Mungu angekitumia kuwapa nuru

watu Wake. Nilipokuwa chini ya nguvu za Bwana, nilijazwa furaha, nikihisi kana kwamba nimezungukwa na malaika watakatifu katika nyua tukufu za mbinguni, ambako kuna amani na furaha yote. Lakini ilikuwa mabadiliko ya huzuni na uchungu kuamka na kurudi katika hali halisi ya maisha ya mwanadamu mwenye kufa, asiye na umilele. **[CETsw 61.3]**

## 7. MAONO YA NCHI MPYA

Tukiwa na Yesu akiwa mbele yetu, sote tulishuka kutoka katika mji ule kwenda duniani, juu ya mlima mkubwa na wenye nguvu sana. Mlima huo haukuweza kumbeba Yesu, hivyo ukagawanyika, na kukawa na uwanda mkubwa. Kisha tuliangalia juu na kuona mji ule mkuu, wenye misingi kumi na miwili, na malango kumi na mawili—matatu kila upande—na malaika katika kila lango. Sote tukapaza sauti: **"Mji! Mji ule mkuu! Unakuja, unakuja kutoka kwa Mungu, kutoka mbinguni!"** Nao ukaja na kukaa mahali pale tuliposimama. **[CETsw 62.1]**

Ndipo tukaanza kutazama vitu vya utukufu vilivyokuwa nje ya mji. Huko niliona nyumba nyingi zenye utukufu mkubwa, zilizokuwa na mwonekano kama wa fedha, zikiwa zimeegemezwa juu ya nguzo nne zilizopambwa kwa lulu zenye uzuri wa ajabu. Nyumba hizo zingekaliwa na watakatifu. Katika kila nyumba kulikuwa na rafu ya dhahabu. Niliona watakatifu wengi wakiingia katika nyumba hizo, wakavua taji zao zinazong'aa na kuziweka juu ya rafu, kisha wakaenda nje kwenye mashamba yaliyokuwa karibu na nyumba zao kufanya kazi fulani na ardhi. Lakini haikuwa kama tunavyofanya kazi na ardhi hapa duniani; La! La! Nuru tukufu iliangaza kuzunguka vichwa vyao, nao waliendelea kupaza sauti na kutoa sifa kwa Mungu.**[CETsw 62.1]**

Niliona pia shamba jingine lililojaa aina zote za maua. Nilipoyachuma, nilisema: **"Hayatawahi kunyauka."** Kisha nikaona shamba la nyasi ndefu, lenye uzuri wa ajabu sana. Lilikuwa na rangi ya kijani kibichi hai, na lilikuwa na mwangaza wa fedha na dhahabu lilipoyumba kwa fahari kwa utukufu wa Mfalme Yesu. Baadaye tuliingia katika shamba lililojaa kila aina ya wanyama: simba, mwana-kondoo, chui, na mbwa-mwitu, wote wakiwa pamoja kwa umoja mkamilifu. Tulipita katikati yao, nao walitufuata kwa amani. Kisha tuliingia katika msitu, lakini haukuwa kama misitu yenye giza tuliyo nayo hapa duniani; la, la. Ulikuwa na nuru na utukufu kila mahali. Matawi ya miti yalitikisika huku na huku, na sote tukasema: **"Tutakaa salama nyikani, na kulala katika misitu."** Tulipita ndani ya msitu huo, kwa sababu tulikuwa njiani kuelekea Mlima Sayuni. **[CETsw 62.3]**

Tulipokuwa tukisafiri, tulikutana na kundi la watu ambao pia walikuwa wakitazama utukufu wa mahali pale. Niliona rangi nyekundu ikiwa kama mpaka kwenye mavazi yao; taji zao zilikuwa zenye kung'aa sana, na mavazi yao yalikuwa meupe kabisa. Tulipowasalimia, nilimuuliza Yesu walikuwa nani. Akasema kwamba walikuwa **wafia dini waliouawa kwa ajili Yake.** Pamoja nao kulikuwa na kundi lisilohesabika la watoto wadogo; wao pia walikuwa na mpaka mwekundu kwenye mavazi yao. **[CETsw 63.1]**

Mlima Sayuni ulikuwa mbele yetu. Juu ya mlima huo kulikuwa na hekalu lenye utukufu, na kuzunguka hekalu hilo kulikuwa na milima mingine saba, ambayo juu yake ilimea maua a waridi na ya mayungiyungi. Niliona watoto wadogo wakipanda juu ya milima hiyo, au kama walipenda, walitumia mabawa yao madogo na kuruka hadi kileleni, kisha wakachuma maua yasiyonyauka kamwe. Kulikuwa na kila aina ya miti iliyozunguka hekalu ili kupamba mahali pale: mti wa msonobari, mti wa miberoshi, mzeituni, mihadasi, mkomamanga, na mtini uliokuwa umeinama kwa uzito wa matunda yake yaliyokomaa kwa wakati wake. Miti hiyo yote iliufanya mahali pale kuwa penye utukufu mwingi. Tulipokuwa karibu kuingia katika hekalu takatifu, Yesu aliinua sauti Yake yenye upendo akasema: **"Ni wale 144,000 tu wanaoingia mahali hapa."** Nasi tukapaza sauti: **"Haleluya!"** **[CETsw 63.2]**

Hekalu hili lilisimamiwa na nguzo saba, zote za dhahabu yenye uwazi, zilizopambwa kwa lulu zenye uzuri wa ajabu. Mambo ya ajabu niliyoyaona huko siwezi kuyaeleza. Laiti ningekuwa na uwezo wa kuzungumza kwa lugha ya Kanaani, ndipo ningeweza kueleza hata kidogo kuhusu utukufu wa ulimwengu bora ule. Niliona huko meza za mawe ambazo juu yake majina ya wale 144,000 yalikuwa yamechongwa kwa herufi za dhahabu.**[CETsw 63.3]**

Baada ya kutazama utukufu wa hekalu, tulitoka nje, na Yesu akatuacha, akaenda mjini. Muda mfupi baadaye tulisikia tena sauti Yake yenye kupendeza ikisema: **"Njooni, enyi watu Wangu, mmetoka katika dhiki kuu, na mmetenda mapenzi Yangu; mliteseka kwa ajili Yangu; njooni mle chakula cha jioni, kwa maana nitajifunga na kuwahudumia."** Tukapaza sauti: **"Haleluya! Utukufu!"** kisha tukaingia ndani ya mji. **[CETsw 64.1]**

Niliona meza ya fedha safi; ilikuwa ndefu kwa maili nyingi, lakini macho yetu yaliweza kuona sehemu yake yote. Niliona matunda ya mti wa uzima: mana, lozi, tini, makomamanga, zabibu, na aina nyingine nyingi za matunda. **[CETsw 64.2]**

Nilimwomba Yesu aniruhusu nile matunda hayo. Akasema: "Si kwa ajili ya sasa. Wale wanaokula matunda ya nchi hii hawarudi tena duniani. Lakini baada ya muda mfupi, ikiwa mtakuwa waaminifu, mtakula matunda ya mti wa uzima na kunywa maji ya chemchemi." Kisha akasema: **"Ni lazima urudi tena duniani, na uwaeleze wengine yale niliyokufunulia."** Ndipo malaika akanichukua kwa upole na kunishusha tena katika ulimwengu huu wenye giza.**[CETsw 64.3]**

## 8. WITO WA KUSAFIRI

Katika maono yangu ya pili, karibu wiki moja baada ya maono ya kwanza, Bwana alinipa mtazamo wa majaribu ambayo nilipaswa kuyapitia, na akaniambia kwamba nilipaswa kwenda kuwaeleza wengine yale aliyokuwa amenifunulia. Nilionyeshwa kwamba kazi yangu ingekutana na upinzani mkubwa, na kwamba moyo wangu ungeshikwa na maumivu makubwa; lakini neema ya Mungu ingenitosha kunisitiri katika hayo yote. **[CETsw 65.1]**

Baada ya kutoka katika maono hayo, nilifadhaika sana, kwa sababu yalinionyesha wajibu wangu wa kwenda kwa watu na kuwasilisha ukweli. Afya yangu ilikuwa dhaifu sana kiasi kwamba nilikuwa katika maumivu ya mwili karibu kila wakati, na kwa hali ilivyoonekana nilikuwa na muda mfupi tu wa kuishi. Nilikuwa na umri wa miaka kumi na saba tu, nilikuwa mdogo na dhaifu, sikuwa nimezoea kushirikiana na watu, na kwa asili nilikuwa mwenye haya na anayejitenga kiasi kwamba kukutana na watu wageni kulikuwa jambo lenye maumivu kwangu. **[CETsw 65.2]**

Kwa siku kadhaa, na hata hadi usiku wa manane, niliomba kwamba mzigo huu niondolewe na uwekwe juu ya mtu mwingine mwenye uwezo zaidi wa kuubeba. Lakini nuru ya wajibu haikubadilika, na maneno ya malaika yaliendelea kusikika masikioni mwangu: “Wajulishe wengine yale niliyokufunulia.” **[CETsw 65.3]**

Hapo awali, Roho wa Mungu aliponihimiza kufanya wajibu fulani, nilikuwa nimeinuka juu ya udhaifu wangu, nikisahau hofu na haya yote kwa kufikiria upendo wa Yesu na kazi ya ajabu aliyokuwa amenifanyia. **[CETsw 65.4]**

Lakini kazi hii niliyoonyeshwa ilionekana kuwa haiwezekani kwangu kuifanya. Kuijaribu kulionekana kama kushindwa kabisa. Majaribu yaliyohusiana nayo yalionekana kuwa makubwa kuliko uwezo wangu wa kuyavumilia. Ningewezaje mimi, mtoto wa umri mdogo, kwenda kutoka mahali pamoja hadi pengine, na kuwaeleza watu zile Kweli takatifu za Mungu? Moyo wangu ulijawa na hofu kubwa nilipofikiria jambo hilo. Ndugu yangu Robert, aliyekuwa amenizidi umri kwa miaka miwili tu, asingeweza kuandamana nami, kwa sababu afya yake ilikuwa dhaifu, na alikuwa na woga mkubwa kuliko mimi. Hakuna jambo lolote ambalo lingeweza kumshawishi kuchukua hatua hiyo. Baba yangu alikuwa na familia ya kuitunza, na asingeweza kuacha shughuli yake; lakini mara nyingi alinihakikishia kwamba ikiwa Mungu alikuwa ameniita kufanya kazi mahali pengine, asingekosa kunifungulia njia. Lakini maneno hayo ya kunitia moyo hayakunipa faraja kubwa katika moyo wangu uliokuwa umekata tamaa. Njia iliyokuwa mbele yangu ilionekana imezungukwa na matatizo ambayo sikuweza kuyashinda.**[CETsw 65.5]**

Nilitamani kifo kama njia ya kuachiliwa kutoka katika majukumu yaliyokuwa yananikabili. Hatimaye amani tamu ambayo nilikuwa nimeifurahia kwa muda mrefu iliniondoka, na kukata tamaa kukaanza tena kuutawala moyo wangu.**[CETsw 66.1]**

### Kutiwa Moyo na Ndugu

Kundi la waumini huko Portland halikujua kuhusu mapambano ya ndani ya moyo wangu yaliyokuwa yamenifikisha katika hali hii ya kukata tamaa. Lakini walijua kwamba kwa sababu fulani akili yangu ilikuwa imelemewa, na walihisi kwamba hali hiyo ilikuwa kosa upande wangu, kwa kuzingatia jinsi Bwana alivyokuwa amejidhihirisha kwangu kwa neema kubwa. Mikutano ilifanyika nyumbani kwa baba yangu, lakini huzuni yangu ya moyoni ilikuwa kubwa kiasi kwamba sikuhudhuria kwa muda fulani. Mzigo wangu ulizidi kuwa mzito mpaka maumivu ya roho yangu yalionekana kuwa zaidi ya uwezo wangu wa kubeba. **[CETsw 66.2]**

Hatimaye nilishawishiwa kuhudhuria mojawapo ya mikutano hiyo nyumbani kwangu. Kanisa lilifanya hali yangu kuwa jambo maalumu la maombi. Baba Pearson, ambaye katika uzoefu wangu wa awali alikuwa amepinga mafunuo ya nguvu za Mungu juu yangu, sasa aliomba kwa bidii kwa ajili yangu, na akanishauri nijisalimishe mapenzi yangu kwa mapenzi ya Bwana. Kama baba mwenye upendo, alijaribu kunitia moyo na kunifariji, akiniambia niamue kuamini kwamba sikuwa nimeachwa na Rafiki wa wenye dhambi. **[CETsw 66.3]**

Nilijihisi dhaifu sana na mwenye kukata tamaa kiasi kwamba sikuweza kufanya juhudi yoyote maalumu kwa ajili yangu mwenyewe, lakini moyo wangu uliungana na maombi ya marafiki zangu. Sikujali tena sana kuhusu upinzani wa ulimwengu, na nilikuwa tayari kutoa dhabihu yoyote ikiwa tu kibali cha Mungu kingeweza kurudishwa kwangu. **[CETsw 67.1]**

Wakati maombi yalipokuwa yakitolewa kwa ajili yangu, ili Bwana anipe nguvu na ujasiri wa kubeba ujumbe huo, giza zito lililonizunguka likaondoka. Nuru ya ghafla ikanijia. Kitu kilichoonekana kwangu kama mpira wa moto kilinigonga moja kwa moja juu ya moyo wangu. Nguvu zangu ziliondolewa, nami nikaanguka chini. Nilionekana kuwa katika uwepo wa malaika. Mmoja wa viumbe hao watakatifu akarudia tena maneno: "Wajulishe wengine yale niliyokufunulia." **[CETsw 67.2]**

Baba Pearson, ambaye hakuweza kupiga magoti kwa sababu ya ugonjwa wa baridi yabisi, alishuhudia tukio hilo. Nilipopata fahamu vya kutosha kuona na kusikia, alisimama kutoka kwenye kiti chake, akasema: "Nimeona jambo ambalo sikuwahi kutarajia kuliona. Mpira wa moto ulishuka kutoka mbinguni, na ukampiga dada Ellen Harmon moja kwa moja moyoni. Nimeuona! Nimeuona! Siwezi kamwe kulisahau. Limebadilisha utu wangu wote. Dada Ellen, uwe na ujasiri katika Bwana. Baada ya usiku huu sitawahi kuwa na shaka tena. Kuanzia sasa tutakusaidia, wala hatutakuvunja moyo."**[CETsw 67.3]**

**Hofu ya Kujikweza**

Hofu moja kubwa iliyokuwa imenilemea ni kwamba ikiwa ningetii wito wa wajibu, na kwenda kujitangaza kuwa nimependelewa na Aliye Juu, nikiwa na maono na mafunuo kwa ajili ya watu, huenda ningeshindwa na **kujikuza kwa dhambi**, na kuinuliwa juu kuliko nafasi ambayo ilinipasa kuwa nayo. Hilo lingesababisha nikose kibali cha Mungu, na kupoteza roho yangu. Nilikuwa nimejua visa vya watu waliopitia hali hiyo, na moyo wangu ulitetemeka nilipofikiria jaribu hilo gumu. **[CETsw 67.4]**

Sasa nilisihi kwamba ikiwa nilipaswa kwenda na kueleza yale ambayo Bwana alikuwa amenionyesha, nilindwe dhidi ya kujikweza kupita kiasi. Malaika akasema: "Maombi yako yamesikiwa, na yatajibiwa. Ikiwa uovu huu unaouogopa utakutishia, mkono wa Mungu utanyooshwa ili kukuokoa; kwa njia ya mateso atakuvuta Kwake, na kuhifadhi unyenyekevu wako. Upeleke ujumbe kwa uaminifu; vumilia mpaka mwisho, nawe utakula matunda ya mti wa uzima na kunywa maji ya uzima." **[CETsw 68.1]**

Baada ya kupata tena fahamu zangu kuhusu mambo ya dunia hii, nilijitoa kwa Bwana, nikiwa tayari kufanya mapenzi Yake, lolote ambalo lingekuwa. **[CETsw 68.2]**

**Miongoni mwa Waumini huko Maine**

Haikuchukua muda mrefu kabla Bwana aliponifungulia njia ya kwenda pamoja na shemeji yangu kuwatembelea dada zangu huko Portland, maili thelathini kutoka nyumbani kwangu. Nilipokuwa huko nilipata nafasi ya kutoa ushuhuda wangu. Kwa muda wa miezi mitatu koo langu na mapafu yangu yalikuwa yameathirika sana kiasi kwamba ningeweza kuzungumza

kidogo tu, na kwa sauti ya chini na iliyokwaruza. Katika tukio hilo nilisimama katika mkutano na kuanza kuzungumza kwa kunong'ona. Niliendelea hivyo kwa takribani dakika tano, ndipo maumivu na kizuizi vilipoondoka. Sauti yangu ikawa wazi na yenye nguvu, nami nikazungumza kwa urahisi na uhuru kamili kwa karibu saa mbili. Baada ya kumaliza ujumbe wangu, sauti yangu ilipotea tena mpaka niliposimama mbele ya watu tena; ndipo uponyaji huo wa ajabu ulirudiwa tena. Nilikuwa na hakikisho la daima kwamba nilikuwa nikifanya mapenzi ya Mungu, na niliona matokeo makubwa yakifuatana na juhudi zangu.**[CETsw 68.3]**

Njia ilifunguliwa kwa majaliwa ya Mungu ili niende sehemu ya mashariki ya Maine. Ndugu William Jordan alikuwa akienda Orrington kwa ajili ya shughuli za biashara, akiwa ameandamana na dada yake, na nilihimizwa kwenda pamoja nao. Kwa kuwa nilikuwa nimemuahidi Bwana kutembea katika njia ambayo angenifungulia, sikuweza kukataa. Roho wa Mungu aliambatana na ujumbe nilioutoa mahali hapo. Mioyo ya watu ilifurahi katika kweli, na wale waliokuwa wamekata tamaa walitiwa moyo na kutiwa nguvu ili waifufue imani yao. **[CETsw 69.1]**

Huko Orrington nilikutana na Mzee James White. Alikuwa anawajua marafiki zangu, na yeye mwenyewe alikuwa akijishughulisha na kazi ya kuokoa roho. **[CETsw 69.2]**

Pia nilitembelea Garland, ambako idadi kubwa ya watu walikusanyika kutoka maeneo mbalimbali ili kusikia ujumbe wangu. **[CETsw 69.3]**

Muda mfupi baada ya hapo nilienda Exeter, kijiji kidogo kisichokuwa mbali na Garland. Huko mzigo mzito ulikaa juu yangu, ambao sikuweza kuondolewa nao mpaka nilipokuwa nimeeleza yale niliyoonyeshwa kuhusu baadhi ya watu waliokuwa na msimamo wa ushupavu wa kidini waliokuwepo mahali hapo. Nilitangaza kwamba walikuwa wamedanganyika kwa kufikiri kwamba walikuwa wakiongozwa na Roho wa Mungu. Ushuhuda wangu uliwachukiza sana watu hao pamoja na wale waliowaunga mkono.**[CETsw 69.4]**

Muda mfupi baada ya hapo nilirudi Portland, nikiwa nimetoa ushuhuda ambao Mungu alikuwa amenipa, na nikiona kibali Chake katika kila hatua niliyopiga.**[CETsw 69.5]**

**Jibu la Maombi**

Katika majira ya kuchipua ya mwaka 1845, nilifanya ziara kwenda Topsham, Maine. Katika tukio moja, idadi kubwa ya watu tulikusanyika katika nyumba ya Ndugu Stockbridge Howland. Binti yake mkubwa, Bi. Frances Howland, ambaye alikuwa rafiki yangu mpendwa sana, alikuwa mgonjwa wa homa ya rheumatiki (homa ya baridi yabisi) na alikuwa chini ya uangalizi wa daktari. Mikono yake ilikuwa imevimba sana kiasi kwamba viungo vyake havikuweza kutofautishwa. Tulipokuwa tumeketi pamoja tukizungumzia hali yake, Ndugu Howland aliulizwa ikiwa alikuwa na imani kwamba binti yake angeweza kuponywa kwa

kujibiwa kwa maombi. Alijibu kwamba angejaribu kuamini kwamba hilo lingewezekana, na muda mfupi baadaye akasema wazi kwamba kweli aliamini kuwa lingeweza kutokea. **[CETsw 69.6]**

Sote tulipiga magoti na kumwomba Mungu kwa bidii kwa ajili yake. Tulishikilia ahadi hili: **"Ombeni, nanyi mtapokea."** (Yohana 16:24) Baraka ya Mungu iliambatana na maombi yetu, nasi tukapata uhakikisho kwamba Mungu alikuwa tayari kumponya yule aliyekuwa akiteseka. Mmoja wa ndugu waliokuwapo akapaza sauti akisema: **"Je, yupo dada hapa mwenye imani ya kwenda kumshika mkono, na kumwambia ainuke kwa Jina la Bwana?"** **[CETsw 71.1]**

Dada Frances alikuwa amelala katika chumba cha juu, na kabla hajamaliza kusema maneno hayo, Dada Curtis alikuwa tayari akipanda ngazi. Aliingia katika chumba cha mgonjwa akiwa na Roho wa Mungu juu yake, akamshika yule mgonjwa mkononi, akasema: **"Dada Frances, kwa jina la Bwana inuka, na uwe mzima."** Uhai mpya ukaingia katika mishipa ya yule msichana mgonjwa. Imani takatifu ikautawala moyo wake, na kwa kuitikia msukumo huo, akainuka kutoka kitandani, akasimama kwa miguu yake, na kutembea ndani ya chumba, akimsifu Mungu kwa uponyaji wake. Muda mfupi baadaye alivaa nguo zake na kushuka katika chumba tulichokuwa tumekusanyika, uso wake ukiwa unang'aa kwa furaha isiyoweza kusemwa na shukrani nyingi. **[CETsw 71.2]**

Asubuhi iliyofuata alikula kifungua kinywa pamoja nasi. Muda mfupi baadaye, wakati Mzee White alipokuwa akisoma sura ya tano ya kitabu cha Yakobo kwa ajili ya ibada ya familia, daktari aliingia ukumbini, na kama kawaida yake akaenda juu kumtembelea mgonjwa wake. Alipomkosa huko, alishuka haraka. Akiwa na uso wa mshangao na hofu, alifungua mlango wa jiko kubwa ambako sisi sote tulikuwa tumeketi, pamoja na mgonjwa wake akiwa nasi. Alimtazama kwa mshangao mkubwa, na hatimaye akasema: **"Kwa hiyo Frances amepona!"** **[CETsw 71.3]**

Ndugu Howland akajibu: **"Bwana ndiye aliyemponya."** Kisha msomaji akaendelea na sehemu ya sura aliyokuwa amekatishwa: **"Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana."** (Yakobo 5:14) Daktari alisikiliza akiwa na sura iliyoonyesha mchanganyiko wa mshangao na kutokuamini. Akatikisa kichwa, kisha akaondoka haraka chumbani. **[CETsw 72.1]**

Siku hiyo hiyo Dada Frances alisafiri kwa farasi maili tatu, akarudi nyumbani jioni. Ingawa hali ya hewa ilikuwa ya mvua, hakupata madhara yoyote, na aliendelea kuimarika haraka katika afya yake. Baada ya siku chache, kwa ombi lake mwenyewe, aliongozwa kwenda majini na kubatizwa. Ingawa hali ya hewa na maji vilikuwa vya baridi sana, hakupata madhara yoyote. Tangu wakati huo aliachiliwa kabisa kutoka katika ugonjwa huo, na akaendelea kufurahia afya yake ya kawaida.**[CETsw 72.2]**

## 8. KUKUTANA NA USHUPAVU WA KIDINI (USHUPAVU ULIOPITILIZA)

Niliporudi Portland, kulikuwa na ushahidi wa madhara makubwa yaliyosababishwa na ushupavu wa kidini. Wengine walionekana kufikiri kwamba dini ilikuwa na maana ya msisimko mkubwa na makelele mengi. Walizungumza kwa namna iliyowakera wasioamini, na hivyo kuwa na ushawishi wa kuamsha chuki dhidi yao wenyewe na dhidi ya mafundisho waliyokuwa wakiyafundisha. Kisha walifurahi kwamba waliteswa kwa ajili ya imani yao. Wasioamini hawakuweza kuona uthabiti wowote katika mwenendo wa namna hiyo. Ndugu katika baadhi ya maeneo walizuiwa kukusanyika kwa ajili ya mikutano. Watu wasio na hatia waliteseka pamoja na wale waliokuwa na makosa. **[CETsw 73.1]**

Mara nyingi nilibeba moyo wenye huzuni na mzigo mzito. Ilionekana kuwa jambo la ukatili sana kwamba kazi ya Kristo ingejeruhiwa kwa sababu ya mwenendo wa watu hawa wasio na busara. Hawakuwa wakiharibu roho zao wenyewe tu, bali pia walikuwa wakiweka doa juu ya kazi ya Mungu ambalo halikuwa rahisi kuondolewa. Na Shetani alipendezwa sana na jambo hilo. Alifurahia kuona kweli ukishughulikiwa na watu wasiotakaswa; kuona Kweli ikichanganywa na makosa, kisha vyote kwa pamoja vikakanyagwa mavumbini. Aliitazama kwa ushindi hali ya machafuko na kutawanyika kwa watoto wa Mungu. **[CETsw 73.2]**

Tulitetemeka kwa ajili ya makanisa ambayo yangekabiliwa na roho hii ya ushupavu. Moyo wangu uliumia kwa ajili ya watu wa Mungu. Je, wangeweza kudanganywa na kuongozwa mbali na shauku hii ya uongo? Kwa uaminifu nilitoa maonyo niliyopewa na Bwana; lakini yalionekana kuwa na matokeo madogo, isipokuwa kuwafanya watu hawa waliokuwa na mitazamo mikali iliyopitiliza, wanitazame kwa wivu.**[CETsw 73.3]**

### Unyenyekevu wa Uongo

Kulikuwa na baadhi ya watu waliodai kuwa na unyenyekevu mkubwa, na waliunga mkono wazo la kutambaa sakafuni kama watoto, wakisema kwamba huo ulikuwa ushahidi wa unyenyekevu wao. Walidai kwamba maneno ya Kristo katika **Mathayo 18:1-6** yalipaswa

kutimizwa kihalisi katika kipindi hiki walipokuwa wakimngojea Mwokozi wao arudi. Walikuwa wakitambaa kuzunguka nyumba zao, barabarani, juu ya madaraja, na hata ndani ya kanisa lenyewe.**[CETsw 73.4]**

Niliwaambia wazi kwamba jambo hilo halikuhitajika. Unyenyekevu ambao Mungu anautafuta kutoka kwa watu Wake unaonyeshwa kwa maisha yanayofanana na Kristo, si kwa kutambaa sakafuni. Mambo yote ya kiroho yanapaswa kushughulikiwa kwa heshima takatifu. Unyenyekevu na upole vinaendana na maisha ya Kristo, lakini vinapaswa kuonyeshwa kwa njia yenye heshima na staha. **[CETsw 74.1]**

Mkristo huonyesha unyenyekevu wa kweli kwa kuonyesha upole wa Kristo, kwa kuwa tayari daima kuwasaidia wengine, kwa kusema maneno ya wema, na kwa kutenda matendo yasiyo ya ubinafsi, ambayo huinua na kuheshimisha ujumbe mtakatifu zaidi uliowahi kuletwa katika ulimwengu wetu.**[CETsw 74.2]**

**Mafundisho ya Imani ya "Kutofanya Kazi"-Doctrine of No Work!**

Kulikuwa na baadhi ya watu huko Paris, Maine, walioamini kwamba kufanya kazi ilikuwa dhambi. Bwana alinipa karipio kwa ajili ya kiongozi wa kosa hili, akitangaza kwamba alikuwa akienda kinyume na Neno la Mungu kwa kujiepusha na kazi, kwa kusisitiza makosa yake kwa wengine, na kwa kuwashutumu wote ambao hawakuyakubali mafundisho yake. Alikataa kila ushahidi ambao Bwana alimpa ili kumshawishi kuhusu kosa lake, na aliazimia kutobadilisha mwenendo wake. Alifanya safari ngumu, akitembea umbali mrefu kwenda mahali ambapo angepokea tu matusi na dharau, kidhani kwamba kwa kufanya hivyo alikuwa akiteseka kwa ajili ya Kristo. Hisia zake binafsi ziliongoza maamuzi yake, na akili pamoja na hukumu ya busara viliwekwa kando.**[CETsw 74.3]**

Niliona kwamba Mungu angefanya kazi kwa ajili ya wokovu wa watu Wake; kwamba mtu huyu aliyepotoshwa angejidhihirisha hivi karibuni, ili wote wenye mioyo ya uaminifu waone kwamba hakuwa akiendeshwa na roho sahihi, na kwamba mwenendo wake ungefikia mwisho haraka. Muda mfupi baadaye mtego huo ulivunjika, naye akawa na ushawishi mdogo sana zaidi juu ya ndugu. Aliyashutumu maono hayo kuwa yalitoka kwa Shetani, na akaendelea kufuata hisia zake mwenyewe mpaka akili yake ikachanganyikiwa, na marafiki zake wakalazimika kumzuia. Hatimaye alitengeneza kamba kutoka katika baadhi ya matandiko yake, ambayo aliitumia kujinyonga. Wafuasi wake wakafikia kutambua udanganyifu wa mafundisho yake.**[CETsw 74.4]**

**Heshima na Hadhi ya Kazi**

Mungu aliweka utaratibu kwamba viumbe alioviumba vifanye kazi. Juu ya jambo hili furaha yao hutegemea. Hakuna yeyote katika eneo kubwa la uumbaji wa Mungu aliyeumbwa

kuwa kiumbe asiye na kazi. Furaha yetu huongezeka na uwezo wetu huendelea kukua tunapojishughulisha na kazi yenye manufaa. **[CETsw 75.1]**

Utendaji huleta nguvu. Maelewano kamili yanaenea katika ulimwengu wa Mungu. Viumbe wote wa mbinguni wako katika shughuli endelevu; na Bwana Yesu, katika kazi Yake ya maisha, ametupa mfano kwa kila mmoja. Alizunguka **"akitenda mema."** Mungu ameweka sheria ya kutenda kwa utii. Kwa utulivu lakini bila kukoma, vitu vilivyoumbwa na Mungu hutekeleza kazi vilivyowekewa. Bahari iko katika mwendo wa kudumu. Nyasi inayoota, ambayo leo ipo na kesho hutupwa motoni, hutimiza kusudi lake kwa kuvika mashamba uzuri. Majani husogea, ingawa hakuna mkono unaoonekana kuyagusa. Jua, mwezi, na nyota vina manufaa na utukufu katika kutimiza kazi yao. **[CETsw 75.2]**

Kila wakati mfumo wa mwili huendelea kufanya kazi yake. Siku baada ya siku moyo hupiga, ukifanya kazi yake ya kawaida iliyoamriwa, bila kukoma ukisukuma damu yake nyekundu kwenda sehemu zote za mwili. Utendaji, utendaji, unaonekana kutawala katika mfumo mzima wa viumbe hai. Na mwanadamu, ambaye akili na mwili wake viliumbwa kwa mfano wa Mungu, lazima awe mwenye shughuli ili kutimiza nafasi yake aliyowekewa. Hapaswi kuwa mvivu. Uvivu ni dhambi. **[CETsw 75.3]**

**Jaribu Kuu**

Katika kipindi cha uzoefu wangu wa kukabiliana na ushupavu wa kidini, nilipitia jaribu kubwa sana. Ikiwa Roho wa Mungu alimshukia mtu yeyote katika mkutano, na mtu huyo akamtukuza Mungu kwa kumsifu, baadhi ya watu walipaza sauti wakidai kwamba huo ulikuwa ushawishi wa kishetani unaoteka akili (mesmerism, hyponotism au animal magnetism ni udanganyifu wa akili au ushawishi wa kisaikolojia). Na ikiwa Bwana alipendezwa kunipa maono katika mkutano, baadhi yao walisema kwamba hayo yalikuwa matokeo ya msisimko au ushawishi wa kishetani unaoteka akili. **[CETsw 76.1]**

Nikiwa nimehuzunika na kuvunjika moyo, mara nyingi nilikwenda peke yangu mahali pa faragha ili kumimina moyo wangu mbele Yake ambaye huwaalika waliochoka na kulemewa waje wapate pumziko. Imani yangu iliposhikilia ahadi, Yesu alionekana kuwa karibu sana. Nuru tamu ya mbingu ilinizunguka, nami nilihisi kana kwamba nimezungukwa na mikono ya Mwokozi wangu, kisha nilichukuliwa katika maono. Lakini nilipowaeleza yale ambayo Mungu alikuwa amenifunulia nikiwa peke yangu, mahali ambapo hakuna ushawishi wa kibinadamu ungeweza kunigusa, nilihuzunika na kushangaa kusikia baadhi ya watu wakidokeza kwamba wale waliokuwa karibu zaidi na Mungu ndio waliokuwa katika hatari kubwa zaidi ya kudanganywa na Shetani.**[CETsw 76.2]**

Baadhi yao walitaka kunifanya niamini kwamba hakuna Roho Mtakatifu, na kwamba uzoefu wote ambao watu watakatifu wa Mungu walikuwa wameupata ulikuwa tu matokeo ya mesmerism au udanganyifu wa Shetani. **[CETsw 76.3]**

Wale waliokuwa wamechukua mitazamo mikali kuhusu baadhi ya vifungu vya Maandiko, wakijizuia kabisa kufanya kazi, na kuwakataa wote ambao hawakukubali mawazo yao juu ya jambo hili na mambo mengine yanayohusu wajibu wa kidini, walinishutumu kwamba nilikuwa nikifuata desturi za dunia. Kwa upande mwingine, Waadventista wa jina tu walinishutumu kwa ushupavu wa kidini, na niliwakilishwa kwa uongo kuwa kiongozi wa ushupavu ule ambao nilikuwa nikijitahidi daima kuuzuia. **[CETsw 76.4]**

Nyakati mbalimbali ziliwekwa kwa ajili ya kuja kwa Bwana, na watu walihimizwa kuzikubali. Lakini Bwana alinionesha kwamba nyakati hizo zingepita, kwa sababu wakati wa taabu lazima utokee kabla ya kuja kwa Kristo. Na kila mara tarehe ilipowekwa na ikapita, imani ya watu wa Mungu ingedhoofishwa. Kwa sababu ya jambo hili nilishtakiwa kuwa mimi ndiye mtumishi mwovu aliyesema: **"Bwana wangu anakawia kuja."** (Mathayo 24:48) **[CETsw 77.1]**

Mambo haya yote yalilemea sana roho yangu, na katika hali hiyo ya machafuko wakati mwingine nilijaribiwa kutilia shaka uzoefu wangu mwenyewe. **[CETsw 77.2]**

Asubuhi moja wakati wa ibada ya familia, nguvu za Mungu zilianza kunishukia, na wazo likanijia akilini kwamba huo ulikuwa ni ushawishi wa kishetani unaoteka akili, nami nikaupinga. Mara hiyo hiyo nikawa bubu, na kwa muda mfupi nikapoteza ufahamu wa mambo yote yaliyokuwa yananizunguka. Kisha nikaonyeshwa dhambi yangu ya kutilia shaka nguvu za Mungu, na kwamba kwa sababu ya kufanya hivyo nilipigwa na ukimya. Lakini niliambiwa kwamba ulimi wangu ungefunguliwa ndani ya saa ishirini na nne. Kadi ilionyeshwa mbele yangu, ambayo juu yake yaliandikwa kwa herufi za dhahabu sura na mistari ya **Maandiko hamsini ya Biblia**. **[CETsw 77.3]**

Baada ya kutoka katika maono, nilitoa ishara nipewe ubao wa kuandikia, nikaandika kwamba nilikuwa bubu, pia yale niliyoyaona, na kwamba nilihitaji Biblia kubwa. Nilichukua Biblia, na kwa urahisi nikapata vifungu vyote nilivyoviona kwenye ile kadi. **[CETsw 78.1]**

Siku hiyo nzima sikuweza kuzungumza. Asubuhi iliyofuata mapema, roho yangu ilijazwa furaha, na ulimi wangu ulifunguliwa ili kupaza sifa kuu kwa Mungu. Tangu wakati huo sikuthubutu tena kutilia shaka wala kupinga nguvu za Mungu hata kwa muda mfupi, haijalishi wengine wangenifikiriaje. **[CETsw 78.2]**

Mpaka wakati huo sikuwa na uwezo wa kuandika. Mkono wangu uliokuwa ukitetemeka haukuweza kushika kalamu kwa uthabiti. Nilipokuwa katika maono, malaika aliniamuru

niandike maono hayo. Nilitii, na nikaandika kwa urahisi. Mishipa yangu iliimarika, na tangu siku hiyo mpaka sasa mkono wangu umekuwa thabiti.**[CETsw 78.3]**

| The Fifty Texts | | |
|---|---|---|
| Luka1:20 | Wafilipi 2:13-15 | Mark 17, 18 |
| Yohana 16:15 | Waefeso 6:10-13 | John -27 |
| Matendo 2:4 | Waefeso 6:14-18 | John 13-15 |
| Matendo 4:29, 30 | Waefeso 4:32 | John 7, 8 |
| Matendo 4:31 | 1 Petro 1:22 | Mark 3-25 |
| Mathayo 7:6 | Yohana13:34, 35 | Rom 8:38, 3 |
| Mathayo 7:7-12 | 2 Wakorintho 13:5 | Rev n 3:7- |
| Mathayo 7:15 | 1 Wakorintho 3:10, 11 | Rev n 14:4 |
| Mathayo 24:24 | 1 Wakorintho 3:12, 13 | Phili ns 3:20 |
| Wakolosai 2:6, 7 | Matendo 20:28-30 | Jam 7, 8 |
| Wakolosai 2:8 | Wagalatia 1:6-9 | Phili ns 3:21 |
| Waebrania 10:35-37 | Luka 12:3-7 | Rev n 14:1 |
| Waebrania10:38, 39 | Luka 4:10, 11 | Heb 4:9 |
| Waebrania 4:10, 11 | 2 Wakorintho 4:6-9 | Rev n 21:2 |
| Waebrania 4:12 | 2 Wakorintho 4:17, 18 | Rev n 14:1 |
| Wafilipi 1:6 | 1 Petro 1:5-7 | Rev n 22:1 |
| Wafilipi 1:27-29 | 1 Wathesalonike 3:8 | |

**Maonyo ya Kuwa Waaminifu**

Ilikuwa msalaba mkubwa kwangu kuwaeleza waliokosea yale niliyoonyeshwa kuhusu wao. Ilinisababishia huzuni kubwa kuwaona wengine wakisumbuliwa au kuumizwa. Na nilipolazimika kutoa ujumbe huo, mara nyingi niliupunguza ukali wake, na kuufanya uonekane kuwa wenye upole na unaofaa zaidi kwa mtu huyo kadiri nilivyoweza. Kisha nilikwenda peke yangu na kulia kwa uchungu wa roho. Nilitazama wale ambao walionekana kujali roho zao wenyewe tu, na nilifikiri: **"Kama ningekuwa katika hali yao, nisingelalamika."** Ilikuwa jambo gumu sana kueleza ushuhuda wa wazi na unaogusa ambao Mungu alinipa. Kwa wasiwasi nilifuatilia matokeo yake. Na ikiwa wale waliokemewa wangeinuka dhidi ya karipio hilo, kisha wakaupinga ukweli, maswali haya yalianza kujitokeza moyoni mwangu: **Je, nilitoa ujumbe ule kama nilivyopaswa? Je, haingewezekana kuwepo njia nyingine ya kuwaokoa?** Kisha huzuni kubwa kama hiyo ilinilemea moyoni kwamba mara nyingi nilihisi kifo kingekuwa mjumbe wa kukaribishwa, na kaburi lingekuwa mahali pazuri pa kupumzika.**[CETsw 78.4]**

Sikutambua kwamba nilikuwa si mwaminifu kwa kuuliza maswali na kutilia shaka kwa namna hiyo, wala sikuona hatari na dhambi ya mwenendo huo, mpaka nilipochukuliwa katika maono na kuletwa mbele za Yesu. Alinitazama kwa usulioonyesha kutoridhika, kisha akaugeuza uso Wake mbali nami. Haiwezekani kueleza hofu na maumivu makali niliyoyahisi wakati huo. Nilianguka kifudifudi mbele Zake, lakini sikuwa na uwezo wa kutamka hata neno moja. Lo! Jinsi nilivyotamani kufunikwa na kujificha nisione tena uso ule wa kutisha uliokuwa umenikunjia ndita! Ndipo nilipoweza kutambua, kwa kiasi fulani, jinsi watakavyohisi wale

watakaopotea watakapolia milima na miamba, "Tuangukieni, tusitirini, mbele za uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na hasira ya Mwana-Kondoo." Ufunuo 6:16.**[CETsw 79.1]**

Muda mfupi baadaye malaika alinielekeza nisimame, na yale niliyoyaona mbele ya macho yangu hayawezi kuelezwa kikamilifu. Mbele yangu kulikuwa na kundi la watu waliokuwa na nywele zilizochafuka na mavazi yaliyokuwa yameraruliwa, na nyuso zao zilionyesha hali ya kukata tamaa na hofu kuu. Walinisogelea karibu, wakayasugua mavazi yao juu ya mavazi yangu. Nilipotazama mavazi yangu, niliona kwamba yalikuwa yametiwa madoa ya damu. Mara nyingine nilianguka chini kama mtu aliyekufa mbele ya miguu ya malaika aliyekuwa akiandamana nami. Sikuwa na sababu hata moja ya kujitetea, nami nilitamani sana kuondoka mahali pale Patakatifu.**[CETsw 79.2]**

Malaika akaniinua na kunisimamisha, kisha akasema, "Hali hii si yako sasa; bali tukio hili limeonyeshwa mbele yako ili ujue jinsi hali yako itakavyokuwa ikiwa utapuuza kuwatangazia wengine yale ambayo Bwana amekufunulia. Lakini ikiwa utakuwa mwaminifu mpaka mwisho, utakula matunda ya mti wa uzima, na utakunywa maji ya mto wa maji ya uzima. Itakubidi upitie mateso mengi, lakini neema ya Mungu yakutosha."**[CETsw 79.3]**

Ndipo nikajisikia kuwa tayari kufanya yote ambayo Bwana angenitaka nifanye, ili nipate kibali Chake, wala nisije nikahisi tena uso Wake wenye hali ya kutokuridhika.**[CETsw 80.1]**

**Muhuri wa Kibali cha Mungu**

Hizo zilikuwa nyakati za taabu nyingi. Kama tusingesimama imara wakati huo, tungekuwa tumefanya **kuanguka kwa imani yetu**. Baadhi walisema kwamba tulikuwa wakaidi; lakini tulilazimika kukaza nyuso zetu kama jiwe la gumegume, wala tusigeuke kwenda upande wa kulia au wa kushoto. **[CETsw 80.2]**

Kwa miaka mingi tulifanya kazi kupinga chuki na kushinda upinzani ambao wakati mwingine ulitishia kuwazidi nguvu wabebaji waaminifu wa kiwango cha kweli—mashujaa wa kiume na wa kike wa imani. Lakini tuligundua kwamba wale waliokuwa wakimtafuta Mungu kwa unyenyekevu na kwa mioyo iliyovunjika na kutubu, waliweza kutofautisha kati ya kweli na uongo. "atawaongoza katika hukumu, Wenye upole atawafundisha njia yake." **Zaburi 25:9.** **[CETsw 80.3]**

Mungu alitupa uzoefu wa thamani katika siku hizo. Tulipoletwa katika mapambano ya karibu na nguvu za giza, jambo ambalo lilitokea mara nyingi, tuliweka kila jambo mbele ya Msaidizi Mkuu. Tuliomba tena na tena kwa ajili ya nguvu na hekima. Hatukutaka kukubali kushindwa; tulihisi kwamba msaada lazima uje. Na kwa njia ya imani katika Mungu, silaha za adui ziligeuzwa dhidi yake mwenyewe. Ushindi mkuu ulipatikana kwa ajili ya kazi ya kweli,

nasi tulitambua kwamba Mungu hakutupa Roho Wake kwa kipimo kidogo. Kama kusingekuwa na ushahidi huu maalumu wa upendo wa Mungu, kama asingekuwa ameweka muhuri Wake juu ya kweli kwa kudhihirisha Roho Wake kwa namna hiyo, huenda tungevunjika moyo. Lakini uthibitisho huu wa uongozi wa Mungu, uzoefu huu hai katika mambo ya Mungu, ulitutia nguvu ili tupigane kwa ujasiri katika vita vya Bwana. Waumini waliweza kuona kwa uwazi zaidi jinsi Mungu alivyokuwa ameandaa njia yao, akiwaongoza katikati ya majaribu, masikitiko, na mapambano makali. Walizidi kuwa na nguvu kadiri walivyokutana na kushinda vikwazo, na walipata uzoefu wa thamani katika kila hatua waliyopiga mbele.**[CETsw 80.4]**

**Masomo Kutoka Wakati Uliopita**

Katika miaka ya baadaye nimeonyeshwa kwamba nadharia za uongo zilizotolewa zamani hazijaachwa kabisa. Wakati nafasi nzuri itakapojitokeza, zitafufuliwa tena. Tusisahau kwamba kila kitu kitakachoweza kutikiswa kitatikiswa. Adui atafanikiwa kuangusha imani ya baadhi ya watu, lakini wale walio waaminifu kwa kanuni hawatatikiswa. Watasimama imara katikati ya majaribu na vishawishi. Bwana ameonyesha makosa haya; na wale ambao hawatambui mahali ambapo Shetani amejiingiza wataendelea kuongozwa katika njia za uongo. Yesu anatuita tuwe macho, na kuyatia nguvu yale yaliyosalia ambayo yako karibu kufa. **[CETsw 81.1]**

Hatuitwi kuingia katika mabishano na wale wanaoshikilia nadharia za uongo. Mabishano hayana faida. Kristo hakuwahi kuingia katika mabishano ya aina hiyo. **"Imeandikwa"** ndio silaha iliyotumiwa na Mkombozi wa ulimwengu. Tudumu karibu na Neno. Tumruhusu Bwana Yesu na wajumbe Wake washuhudie. Tunajua kwamba ushuhuda wao ni wa Kweli. **[CETsw 81.2]**

Kristo yuko juu ya kazi zote za uumbaji Wake. Katika nguzo ya moto, aliwaongoza wana wa Israeli; macho Yake yaliona yaliyopita, yaliyopo, na yajayo. Anapaswa kutambuliwa na kuheshimiwa na wote wanaompenda Mungu. Amri Zake zinapaswa kuwa nguvu inayotawala katika maisha ya watu Wake. **[CETsw 81.3]**

Mjaribu huja na dhana kwamba Kristo ameondoa kiti Chake cha heshima na mamlaka na kukipeleka katika eneo fulani lisilojulikana, na kwamba wanadamu hawahitaji tena kusumbuliwa na kuinua tabia Yake na kutii sheria Yake. Anadai kwamba wanadamu wanapaswa kuwa sheria kwa ajili yao wenyewe. Mawazo haya ya udanganyifu huinua nafsi ya mwanadamu na kumfanya Mungu asiwe na maana. Kizuizi na udhibiti wa maadili katika familia ya wanadamu huharibiwa. Kuzuia maovu kunazidi kudhoofika zaidi na zaidi. Ulimwengu haumpendi wala hawamchi Mungu. Na wale wasiompende na wasiomcha Mungu, hivi karibuni watapoteza kabisa hisia ya wajibu wao kwa wenzao. Wanakuwa bila Mungu na bila tumaini katika ulimwengu.**[CETsw 81.4]**

Walimu wale ambao kila siku hawaruhusu Neno la Mungu katika lifanye kazi maishani mwao, wako katika hatari kubwa sana. Hawana ujuzi wa wokovu wa Mungu wala wa Kristo. Ni wale wasioishi kulingana na Kweli ndio wanaopendelea zaidi kubuni mawazo ya udanganyifu ili kujaza muda na kuchukua umakini ambao ulipaswa kutolewa kwa kujifunza Neno la Mungu. Ni kosa la kutisha kwetu kupuuza kujifunza Biblia ili kuchunguza nadharia zinazopotosha, ambazo zinaondoa mawazo kutoka katika maneno ya Kristo na kuyaelekeza kwenye mafundisho ya uongo yaliyotungwa na wanadamu.**[CETsw 83.1]**

Hatuhitaji mafundisho ya kubuni au kufikirika kuhusu asili (nafsi) ya Mungu. Kile ambacho Mungu anataka tujue kumhusu kimefunuliwa katika Neno Lake na katika matendo Yake. Vitu vya kupendeza vya asili vinafunua tabia Yake na uwezo Wake kama Muumba. Hivyo ni zawadi Yake kwa wanadamu, ili kuonyesha nguvu Zake na kuonyesha kwamba Yeye ni Mungu wa upendo. Lakini hakuna mtu aliyepewa mamlaka kusema kwamba Mungu Mwenyewe kwa nafsi Yake Yupo ndani ya ua, jani, au mti. Vitu hivi ni kazi za mikono ya Mungu, vikifunua upendo Wake kwa wanadamu. **[CETsw 83.2]**

Kristo Ndiye ufunuo mkamilifu wa Mungu. Wale wanaotamani kumjua Mungu, wajifunze kazi na mafundisho ya Kristo. Kwa wale wanaompokea na kumwamini, Yeye huwapa uwezo wa kufanyika wana wa Mungu.**[CETsw 83.3]**

## 10. SABATO YA BWANA

Nilipokuwa nikitembelea New Bedford, Massachusetts, mwaka 1846, nilifahamiana na Mzee Joseph Bates. Alikuwa ameikubali imani ya Marejeo ya Kristo (Advent) mapema, na alikuwa mfanyakazi mwenye bidii katika kazi hiyo. Nilimkuta akiwa ni Mkristo wa kweli mwenye heshima, mwenye adabu na fadhili. **[CETsw 85.1]**

Mara ya kwanza aliposikia nikizungumza, alionyesha kupendezwa sana. Baada ya mimi kumaliza kuzungumza, alisimama na kusema: “Mimi ni Tomaso mwenye mashaka. Siamini katika maono. Lakini kama ningeweza kuamini kwamba ushuhuda ambao dada ameueleza usiku wa leo kwa kweli ulikuwa sauti ya Mungu kwetu, ningekuwa mtu mwenye furaha zaidi kuliko wote walio hai. Moyo wangu umeguswa sana. Ninaamini kwamba msemaji huyu ni mnyofu, lakini siwezi kueleza kuhusu jinsi alivyoonyeshwa mambo ya ajabu aliyotuambia.”**[CETsw 85.2]**

Mzee Bates alikuwa akitunza **Jumamosi**, siku ya saba ya juma, na alitusisitizia kwamba hiyo ndiyo Sabato ya kweli. Mimi sikuona umuhimu wake wakati huo, na nilifikiri kwamba alikuwa amekosea kwa kusisitiza amri ya nne kuliko zile amri nyingine tisa. **[CETsw 85.3]**

Lakini Bwana alinipa maono kuhusu **Patakatifu pa mbinguni**. Hekalu la Mungu lilifunguliwa mbinguni, nami nikaonyeshwa **Sanduku la Mungu** lililofunikwa na **Kiti cha Rehema**. Malaika wawili walikuwa wamesimama upande mmoja na mwingine wa Sanduku hilo la Agano, huku mabawa yao yakiwa yamekunjuliwa juu ya Kiti cha Rehema, na nyuso zao zikielekea kwenye kiti. Malaika aliyekuwa akiniongoza aliniambia kwamba jambo hili liliwakilisha jeshi lote la mbinguni likiitazama **sheria ya Mungu** kwa hofu na heshima kuu, sheria ambayo ilikuwa imeandikwa kwa kidole cha Mungu.**[CETsw 85.4]**

Yesu aliinua kifuniko cha sanduku, nami nikaona **mbao za mawe** ambazo juu yake zilikuwa zimeandikwa **amri kumi**. Nilishangaa sana nilipoona kwamba **amri ya nne** ilikuwa katikati kabisa ya zile amri kumi, ikiwa imezungukwa na mng’ao laini wa nuru. Malaika alisema: “Hii ndiyo amri pekee kati ya zile kumi inayomtambulisha Mungu aliye hai, ambaye aliumba mbingu na nchi na vitu vyote vilivyomo ndani yake.”**[CETsw 85.5]**

Misingi ya dunia ilipowekwa, ndipo pia msingi wa Sabato uliwekwa. Nilionyeshwa kwamba kama Sabato ya Kweli ingekuwa imetunzwa, kamwe kusingekuwa na mtu asiyeamini Mungu wala mpinga Mungu. Utunzaji wa Sabato ungekuwa umeulinda ulimwengu dhidi ya ibada ya sanamu. **[CETsw 86.1]**

Amri ya nne imekanyagwa chini; kwa hiyo tumeitwa **kuziba pengo lililopo katika sheria** na kusimamia Sabato iliyotiwa unajisi. Mtu wa dhambi, ambaye alijiinua juu ya Mungu na kufikiri kubadilisha majira na sheria, ndiye aliyeleta mabadiliko ya Sabato kutoka siku ya saba kwenda siku ya kwanza ya juma. Kwa kufanya hivyo alifanya **pengo katika sheria ya**

**Mungu.** Kabla tu ya siku kuu ya Mungu, ujumbe unatolewa ili kuwaonya watu warudi kwenye uaminifu wao kwa sheria ya Mungu, ambayo mpinga Kristo ameivunja. Uangalifu lazima uelekezwe kwenye pengo hilo katika sheria, kwa njia ya mafundisho na mfano wa maisha. **[CETsw 86.2]**

Nilionyeshwa kwamba ahadi za thamani zilizomo katika **Isaya 58:12-14** zinawahusu wale wanaofanya kazi ya kurejesha Sabato ya Kweli. **[CETsw 87.1]**

Nilionyeshwa kwamba **malaika wa tatu**, anayehubiri amri za Mungu na imani ya Yesu, anawakilisha watu wanaopokea ujumbe huu na kuinua sauti ya onyo kwa ulimwengu ili kutunza amri za Mungu na sheria Yake kama **mboni ya jicho**. Na kwamba kwa kuitikia onyo hili, wengi wangeikubali **Sabato ya Bwana.** **[CETsw 87.2]**

## 11. NDOA NA KUFANYA KAZI PAMOJA

Tarehe **30 Agosti, 1846**, nilifunga ndoa na Mzee **James White**. Mzee White alikuwa amepata uzoefu mkubwa katika harakati za Marejeo (Advent), na kazi zake za kutangaza Kweli ilikuwa imebarikiwa na Mungu. Mioyo yetu iliunganishwa katika kazi hiyo kuu, na pamoja tulisafiri na kufanya kazi kwa ajili ya wokovu wa roho. **[CETsw 88.1]**

**Kuthibitishwa kwa Imani**

Mwezi **Novemba, 1846**, nilihudhuria pamoja na mume wangu mkutano huko **Topsham, Maine**, ambapo Mzee **Joseph Bates** alikuwapo. Wakati huo bado hakuamini kikamilifu kwamba maono yangu yalikuwa kutoka kwa Mungu. Mkutano huo ulikuwa kipindi cha kuvutia sana. Roho wa Mungu alinijilia; nilifunikwa katika maono ya utukufu wa Mungu, na kwa mara ya kwanza nilipewa kuona sayari nyingine. Baada ya kutoka katika maono, nilisimulia yale niliyoyaona. Ndipo Mzee Bates akaniuliza kama nilikuwa nimejifunza elimu ya nyota (astronomy). Nilimwambia kwamba sikumbuki kamwe kusoma au kuchunguza elimu ya nyota. Kisha akasema: **"Hili ni jambo la Bwana."** Uso wake uliangaza kwa nuru ya mbinguni, naye akalihubiria kanisa kwa nguvu.**[CETsw 88.2]**

Kuhusu mtazamo wake juu ya maono hayo, Mzee Bates alisema yafuatayo: **[CETsw 88.3]**

"Ingawa sikuweza kuona jambo lolote ndani yake lililopingana na Neno, bado nilihisi hofu na nilijaribiwa sana, na kwa muda mrefu sikuwa tayari kuamini kwamba yalikuwa zaidi ya matokeo ya hali ya mwili wake kuwa dhaifu na kudhoofika kwa muda mrefu." **[CETsw 88.4]**

"Kwa hiyo nilitafuta nafasi mbele ya wengine, wakati akili yake ilipoonekana kuwa huru kutoka katika msisimko (nje ya mikutano), ili kumuuliza maswali mengi na kumchunguza yeye pamoja na marafiki zake waliokuwa wakifuatana naye, hasa dada yake mkubwa, ili nipate ukweli kama ingewezekana." "Katika ziara nyingi alizofanya huko New Bedford na Fairhaven tangu wakati huo, wakati wa mikutano yetu, nimemwona akiwa katika maono mara nyingi, na pia huko Topsham, Maine; na wale waliokuwapo katika baadhi ya matukio hayo yenye msisimko wanajua vizuri jinsi nilivyosikiliza kila neno kwa shauku kubwa, na jinsi nilivyotazama kila mwendo ili kugundua udanganyifu au ushawishi wa kishetani unaoteka akili." "Ninamshukuru Mungu kwa nafasi niliyopata pamoja na wengine kushuhudia mambo haya. Sasa naweza kusema kwa ujasiri kwa ajili yangu mwenyewe. Ninaamini kwamba kazi hii ni ya Mungu, na imetolewa ili kuwafariji na kuwatia nguvu watu Wake 'waliotawanyika, walioteswa, na waliokataliwa,' tangu kufungwa kwa kazi yetu ... mwezi Oktoba, 1844."**[CETsw 88.1]**

**Maombi ya Bidii na Yenye Matokeo**

Wakati wa mkutano huko Topsham, nilionyeshwa kwamba ningeteseka sana, na kwamba tungepitia jaribu la imani yetu baada ya kurudi Gorham, mahali ambapo wazazi wangu walikuwa wakiishi wakati huo. **[CETsw 89.1]**

Tuliporudi, nilishikwa na ugonjwa mkali sana, na niliteseka kupita kiasi. Wazazi wangu, mume wangu, na dada zangu waliungana katika maombi kwa ajili yangu, lakini niliendelea kuteseka kwa muda wa wiki tatu. Mara nyingi nilizimia kana kwamba nimekufa, lakini kwa jibu la maombi ya watu, nilipata nafuu tena. Maumivu yangu yalikuwa makali sana kiasi kwamba niliwasihi wale waliokuwa karibu nami wasiombe tena kwa ajili yangu; kwa sababu nilifikiri kwamba maombi yao yalikuwa yanaongeza muda wa mateso yangu. Majirani zetu walikata tamaa wakadhani nitakufa. Kwa muda fulani Bwana aliruhusu imani yetu ijaribiwe. **[CETsw 89.2]**

Ndugu na Dada Nichols, kutoka Dorchester, Massachusetts, walikuwa wamesikia kuhusu mateso yangu, na mwana wao Henry alikuja Gorham akiwa amebeba vitu vya kunifariji. Wakati wa ziara yake, marafiki zangu waliungana tena katika maombi kwa ajili ya kupona kwangu. Baada ya wengine kuomba, Ndugu Henry Nichols alianza kuomba kwa bidii kubwa sana; na nguvu za Mungu zilipokuwa juu yake, alisimama kutoka magotini mwake, akaja upande wangu wa pili wa chumba, akaweka mikono yake juu ya kichwa changu, akisema: **“**Dada Ellen, Yesu Kristo akufanye uwe mzima.” Kisha akaanguka nyuma, akiwa amelemewa na nguvu za Mungu. Niliamini kwamba kazi hiyo ilikuwa ya Mungu, na maumivu yakaondoka. Roho yangu ilijazwa na shukrani na amani. Maneno yaliyokuwa moyoni mwangu yalikuwa: “Hakuna msaada mwingine kwetu isipokuwa kwa Mungu. Tunaweza kuwa na amani tu unapopumzika ndani Yake na kusubiri wokovu Wake.”**[CETsw 89.4]**

**Kazi Huko Massachusetts**

Wiki chache baada ya jambo hili, tulipokuwa njiani kwenda Boston, tulipanda meli huko Portland. Dhoruba kali ilitokea, nasi tulikuwa katika hatari kubwa. Lakini kwa rehema ya Mungu sote tulifika salama nchi kavu. **[CETsw 90.1]**

Kuhusu kazi zetu huko Massachusetts mwezi Februari na juma la kwanza la Machi, mume wangu aliandika kutoka Gorham, Maine, tarehe **14 Machi, 1847**, muda mfupi baada ya kurudi nyumbani: **[CETsw 90.2]**

“Tulipokuwa mbali na marafiki zetu hapa kwa karibu majuma saba, Mungu amekuwa mwenye rehema kwetu. Amekuwa nguvu yetu baharini na nchi kavu. Ellen amekuwa na afya nzuri zaidi kwa muda wa majuma sita yaliyopita kuliko alivyokuwa kwa miaka sita iliyopita. Sisi sote tuna afya njema....”**[CETsw 90.3]**

“Tangu tulipoondoka Topsham, tumepitia nyakati ngumu. Pia tumekuwa na vipindi vingi vya utukufu, vya mbinguni, na vya kutuburudisha. Kwa ujumla, hii imekuwa mojawapo ya safari bora zaidi tulizowahi kufanya huko Massachusetts. Ndugu zetu huko New Bedford na Fairhaven waliimarishwa sana na kuthibitishwa katika Kweli na nguvu za Mungu. Ndugu katika maeneo mengine pia walibarikiwa sana.”**[CETsw 90.4]**

## 12. PATAKATIFU PA MBINGUNI

Katika mkutano uliofanyika siku ya Sabato, tarehe **3 Aprili, 1847**, nyumbani kwa Ndugu Stockbridge Howland, tulihisi roho ya pekee ya maombi. Na tulipokuwa tukiomba, Roho Mtakatifu alitujilia. Tulikuwa na furaha kubwa. Muda mfupi baadaye nilitenganishwa na mambo ya dunia, nami nikafunikwa katika maono ya utukufu wa Mungu. **[CETsw 91.1]**

Niliona malaika akiruka kwa haraka kuja kwangu. Kwa upesi alinichukua kutoka duniani mpaka katika mji mtakatifu. Katika mji huo niliona hekalu, nami nikaingia ndani yake. Nilipita kupitia mlango kabla sijafika kwenye pazia la kwanza. Pazia hilo liliinuliwa, nami nikaingia katika **Patakatifu**. Hapa niliona madhabahu ya uvumba, kinara chenye taa saba, na meza iliyokuwa na Mikate ya Wonyesho. Baada ya kuona utukufu wa Patakatifu, Yesu aliinua pazia la pili, nami nikaingia katika **Patakatifu pa Patakatifu**. **[CETsw 91.2]**

Katika Patakatifu pa Patakatifu niliona sanduku; juu yake na pembeni zake kulikuwa na dhahabu safi kabisa. Kila mwisho wa Sanduku kulikuwa na kerubi mzuri, akiwa amenyosha mabawa yake juu yake. Nyuso zao zilielekeana, nao walitazama chini. Katikati ya wale malaika kulikuwa na chetezo cha dhahabu. Juu ya Sanduku la Agano, mahali ambapo malaika walikuwa wamesimama, kulikuwa na utukufu mkali sana ulioonekana kama kiti cha enzi ambacho Mungu alikuwa anakaa. Yesu alisimama karibu na sanduku hilo, na wakati maombi ya watakatifu yalipofika Kwake, uvumba uliokuwa katika chetezo ulianza kuvuta moshi; naye aliyatoa maombi yao pamoja na moshi wa uvumba mbele za Baba Yake. **[CETsw 91.3]**

Katika Sanduku hilo kulikuwa na chungu cha dhahabu kilichokuwa na mana, fimbo ya Haruni iliyochipuka, na mbao za mawe ambazo zilikunjamana kama kitabu. Yesu alizifungua, nami nikaona zile Amri Kumi zilizoandikwa juu yake kwa kidole cha Mungu. Kwenye ubao mmoja kulikuwa na amri nne, na kwenye ubao mwingine kulikuwa na amri sita. Amri nne zilizokuwa kwenye ubao wa kwanza zilikuwa zikimetameta kuliko zile sita. Lakini ile ya nne, yaani **amri ya Sabato**, ilikuwa iking'aa kuliko zote; kwa maana Sabato ilikuwa imetengwa ili ihifadhiwe kwa heshima ya jina takatifu la Mungu. Sabato takatifu ilionekana yenye utukufu; nuru ya utukufu ilikuwa imeizunguka pande zote. Niliona kwamba amri ya Sabato haikusulubishwa msalabani. Kama ingekuwa hivyo, basi zile amri nyingine tisa pia zingekuwa zimesulubishwa; na tungekuwa na uhuru wa kuzivunja zote, pamoja na ile ya nne. Niliona kwamba Mungu hakuibadilisha Sabato, kwa maana Yeye habadiliki. Lakini papa aliibadilisha kutoka siku ya saba kwenda siku ya kwanza ya juma; kwa sababu alitabiriwa kuwa angebadilisha majira na sheria. **[CETsw 91.4]**

Niliona kwamba kama Mungu angebadilisha Sabato kutoka siku ya saba kwenda siku ya kwanza, basi angebadilisha maandishi ya amri ya Sabato yaliyoandikwa juu ya zile mbao za mawe, ambazo sasa ziko ndani ya Sanduku katika Patakatifu pa Patakatifu pa hekalu la mbinguni;

na yangeandikwa hivi: **“Siku ya kwanza ndiyo Sabato ya Bwana, Mungu wako.”** Lakini niliona kwamba yaliandikwa vilevile kama yalivyoandikwa wakati ule kwenye mbao za mawe kwa kidole cha Mungu, na kukabidhiwa kwa Musa katika Mlima Sinai: **“Lakini siku ya saba ndiyo Sabato ya Bwana, Mungu wako.”** Niliona kwamba Sabato takatifu ndiyo, na itaendelea kuwa, **ukuta wa kutenganisha kati ya Israeli wa kweli wa Mungu na wasioamini**; na kwamba Sabato ndiyo jambo kuu litakalounganisha mioyo ya watakatifu wapendwa wa Mungu wanaosubiri. **[CETsw 93.1]**

Niliona kwamba Mungu ana watoto ambao bado hawaioni na hawaishiki Sabato. Hawajakataa nuru iliyotolewa juu yake. Na mwanzoni mwa wakati wa taabu, tulijazwa na Roho Mtakatifu tulipotoka kwenda kutangaza Sabato kwa ukamilifu zaidi. Hili liliwakasirisha makanisa na Waadventista wa jina tu, kwa sababu hawakuweza kuipinga Kweli ya Sabato. Wakati huo wateule wa Mungu wote waliona wazi kwamba tulikuwa na Kweli, nao wakatoka na kuvumilia mateso pamoja nasi. Niliona **upanga, njaa, tauni, na machafuko makubwa katika nchi**. Waovu walifikiri kwamba sisi ndio tulikuwa tumesababisha hukumu hizo kuwapata, nao wakaungana kupanga kutuondoa duniani, wakifikiri kwamba kwa kufanya hivyo maovu yangekoma. **[CETsw 93.2]**

Katika wakati wa taabu, sisi sote tulikimbia kutoka mijini na vijijini, lakini tulifuatwa na waovu waliovamia nyumba za watakatifu wakiwa na mapanga. Walinyanyua mapanga yao ili kutuua, lakini mapanga yakavunjika na kuanguka chini yakiwa hayana nguvu kama majani makavu. Ndipo sisi wote tukamlilia Mungu mchana na usiku kwa ajili ya ukombozi, na kilio chetu kikafika mbele za Mungu. **[CETsw 95.1]**

Jua likachomoza, na mwezi ukasimama mahali pake. Vijito vya maji vikakoma kutiririka. Mawingu mazito na meusi yakatokea, yakigongana yenyewe kwa yenyewe. Lakini kulikuwa na sehemu moja iliyo wazi yenye utukufu uliotulia, ambapo sauti ya Mungu ilitoka kama maji mengi, ikazitikisa mbingu na nchi. Anga likafunguka na kufungwa, likiwa katika msukosuko. Milima ikatikisika kama mwanzi upeponi, na kutupa nje miamba mikubwa iliyochongoka kila upande. Bahari ikachemka kama sufuria, na kutupa mawe juu ya nchi. **[CETsw 95.2]**

Na Mungu alipokuwa akisema **siku na saa ya kuja kwa Yesu**, na kutoa **agano la milele kwa watu Wake**, alisema sentensi moja, kisha akanyamaza, huku maneno hayo yakisambaa duniani kote. Israeli wa Mungu walisimama wakiwa wameelekeza macho yao juu, wakisikiliza maneno yaliyotoka kinywani mwa Yehova na kusambaa duniani kama milio mikubwa ya radi. Ilikuwa hali ya kutisha na yenye utukufu mkuu. Mwishoni mwa kila sentensi, watakatifu walipaza sauti wakisema: **“Utukufu! Haleluya!”** Nyuso zao ziling’aa kwa utukufu wa Mungu; nazo zikaangaza kama uso wa Musa ulivyoangaza aliposhuka kutoka Sinai. Waovu hawakuweza kuwatazama kwa sababu ya utukufu huo. Na wakati baraka zisizo na mwisho zilipotangazwa juu ya wale waliomheshimu Mungu kwa kuitunza Sabato yake takatifu, kukawa na mshangao mkubwa wa ushindi dhidi ya **mnyama na sanamu yake**. **[CETsw 95.3]**

Ndipo **miaka elfu (Jubilii/Yubile)** ilipoanza, wakati ambapo nchi ingetulia na kupumzika. Nilimwona mtumwa mwaminifu akiinuka kwa ushindi na furaha, akitikisa na kuondoa minyororo iliyokuwa imemfunga, wakati bwana wake mwovu akiwa katika mshangao na kuchanganyikiwa, kwa maana waovu hawakuweza kuelewa maneno ya sauti ya Mungu.**[CETsw 96.1]**

Muda mfupi baadaye lilitokea lile wingu kubwa jeupe. Lilionekana kuwa lenye kupendeza kuliko wakati mwingine wowote uliopita. Juu yake aliketi **Mwana wa Adamu**. Mwanzoni hatukumwona Yesu juu ya lile wingu, lakini lilipokaribia dunia tuliweza kuuona mwili Wake wa kupendeza. Wingu hili, lilipoonekana mara ya kwanza, lilikuwa **ishara ya Mwana wa Adamu mbinguni**. **[CETsw 96.2]**

Sauti ya Mwana wa Mungu ikawafufua watakatifu waliolala, wakiwa wamevikwa **kutokufa kwa utukufu**. Watakatifu waliokuwa hai walibadilishwa kwa muda mfupi, nao wakachukuliwa pamoja nao ndani ya gari la mawingu. Lilionekana lenye utukufu mwingi lilipokuwa likipaa juu. Kila upande wa lile gari kulikuwa na mabawa, na chini yake kulikuwa na magurudumu. Na gari hilo lilipopanda juu, magurudumu yake yakasema: **"Mtakatifu,"** na mabawa yake yaliposogea yakasema: **"Mtakatifu,"** na msafara wa malaika watakatifu waliolizunguka lile wingu wakasema: **"Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi."**Nao watakatifu waliokuwa ndani ya lile wingu wakasema: **"Utukufu! Haleluya!"** Kisha lile gari likapaa juu kuelekea katika mji mtakatifu. Yesu akafungua malango ya mji wa dhahabu, akatuongoza kuingia ndani. Huko tulikaribishwa, kwa sababu tulikuwa tumeshika **"amri za Mungu,"** na tulikuwa na **"haki ya kuuendea mti wa uzima."** (Ufunuo 14:12; 22:14.) **[CETsw 96.3]**

## 13. UPENDO WA MUNGU KWA WATU WAKE

Nimeuona upendo wa huruma ambao Mungu anao kwa watu Wake, nao ni mkuu sana. Niliwaona malaika wakiwa juu ya watakatifu, wakiwa wamekunjua mabawa yao kuwazunguka. Kila mtakatifu alikuwa na malaika anayemhudumia. Ikiwa watakatifu walilia kwa sababu ya kukata tamaa, au walikuwa katika hatari, malaika waliokuwa wakiwahudumia daima waliruka haraka kwenda juu ili kupeleka habari hiyo; na malaika waliokuwa mjini waliacha kuimba. Ndipo Yesu angemwagiza malaika mwingine ashuke kuwafariji, kuwalinda, na kujaribu kuwazuia wasitoke katika njia nyembamba. Lakini kama hawakutii uangalizi wa malaika hao, na hawakukubali kufarijiwa nao, bali wakaendelea kupotea, malaika hao wangeonekana wenye huzuni na kulia. Wangebeba habari hiyo kwenda juu, na malaika wote waliokuwa mjini wangelia, kisha kwa sauti kubwa waseme: **"Amina."** Lakini kama watakatifu wangeweka macho yao kwenye thawabu iliyokuwa mbele yao, na kumtukuza Mungu kwa kumsifu, basi malaika wangebeba habari za furaha kwenda mjini, nao malaika waliokuwa mjini wangepiga vinubi vyao vya dhahabu na kuimba kwa sauti kubwa: **"Haleluya!"** na matao ya mbinguni yangesikika yakijaa nyimbo zao nzuri.**[CETsw 97.1]**

Kuna utaratibu mkamilifu na maelewano kamili katika mji mtakatifu. Malaika wote walioagizwa kuitembelea dunia wanashika **kadi ya dhahabu**, ambayo huionyesha kwa malaika walioko kwenye malango ya mji wanapoingia na kutoka. Mbinguni ni mahali pazuri. Natamani kuwa huko na kumwona Yesu wangu mpendwa, ambaye alitoa maisha Yake kwa ajili yangu, na kubadilishwa kuwa mfano Wake wa utukufu. Laiti ningekuwa na maneno ya kueleza utukufu wa ulimwengu ule mzuri unaokuja! Nina kiu ya mito ya maji ya uzima inayoufurahisha mji wa Mungu wetu.**[CETsw 97.2]**

Bwana amenionyesha maono ya **malimwengu mengine**. Nilipewa mabawa, na malaika akaniongoza kutoka mjini kwenda mahali palipokuwa penye mwangaza na utukufu. Nyasi za mahali hapo zilikuwa za kijani kibichi zenye uhai, na ndege waliokuwa huko waliimba nyimbo tamu. Wakazi wa mahali hapo walikuwa wa ukubwa mbalimbali; walikuwa wenye heshima, wakuu, na warembo. Walikuwa na **mfano kamili wa Yesu**, na nyuso zao zilikuwa zikimeta kwa furaha takatifu, zikionyesha uhuru na furaha ya mahali hapo. Nilimuuliza mmoja wao kwa nini walikuwa warembo au wanaovutia kwa uzuri zaidi kuliko wale walioko duniani. Jibu lake lilikuwa: **"Tumeishi katika utii mkamilifu kwa amri za Mungu, na hatukuanguka kwa kutotii kama wale walioko duniani."[CETsw 97.3]**

Kisha nikaona miti miwili. Mmoja ulifanana sana na **mti wa uzima ulioko mjini**. Matunda ya yote mawili yalionekana mazuri, lakini matunda ya mmoja wa miti hiyo hawakuruhusiwa kula. Walikuwa na uwezo wa kula matunda ya miti yote miwili, lakini walikatazwa kula yale ya mti mwingine. Ndipo malaika aliyekuwa pamoja nami akaniambia: **"Hakuna yeyote katika mahali hapa aliyewahi kuonja mti uliokatazwa; lakini kama wangekula, wangeanguka." [CETsw 98.1]**

Kisha nilipelekwa kwenye ulimwengu mmoja uliokuwa na **mbalamwezi saba (moons)** . Huko nilimwona **Henoko mwema wa zamani**, ambaye alihamishwa bila kuona mauti. Kwenye mkono wake wa kulia alikuwa amebeba **tawi la mtende lenye utukufu**, na kwenye kila jani kulikuwa kumeandikwa neno: **“Ushindi.”** Kichwani mwake kulikuwa na taji nyeupe yenye kung’aa sana. Kwenye majani ya taji hiyo, na katikati ya kila jani, kulikuwa kumeandikwa: **“Usafi.”** Kuzunguka taji hiyo kulikuwa na mawe ya rangi mbalimbali yaliyong’aa kuliko nyota, nayo yaliakisi mwanga juu ya maandishi na kuyafanya yaonekane makubwa zaidi. Nyuma ya kichwa chake kulikuwa na utepe ulioshikilia taji hilo, na juu ya utepe huo palikuwa pameandikwa: **“Utakatifu.”** Juu ya taji hiyo kulikuwa na taji nyingine nzuri iliyong’aa kuliko jua. Nilimuuliza kama hapa ndipo mahali alipochukuliwa kutoka duniani. Akasema: **“Sivyo; mji ndio makao yangu, nami nimekuja kutembelea mahali hapa.”** Alitembea katika mahali hapo kana kwamba palikuwa nyumbani kwake kabisa. Nilimsihi malaika aliyekuwa pamoja nami aniruhusu nibaki mahali hapo. Sikuweza kuvumilia wazo la kurudi tena katika ulimwengu huu wenye giza. Ndipo malaika akaniambia: **“Lazima urudi, na kama utakuwa mwaminifu, wewe pamoja na wale 144,000 mtapata nafasi ya kutembelea malimwengu yote na kuona kazi za mikono ya Mungu.”[CETsw 98.2]**

## 14. KUTIWA MUHURI

Wakati wa kufungua Sabato takatifu, tarehe 5 Januari 1849, tulijikusanya katika maombi pamoja na familia ya Ndugu Belden huko Rocky Hill, Connecticut, na Roho Mtakatifu akatushukia. Nilichukuliwa katika maono hadi **Patakatifu pa Patakatifu**, ambako nilimwona Yesu akiendelea kuwaombea Israeli. Chini ya vazi Lake kulikuwa na **kengele na komamanga, kengele na komamanga**. Kisha nikaona kwamba Yesu hatatoka katika Patakatifu pa Patakatifu mpaka kila hukumu iwe imeamuliwa, ama kwa ajili ya wokovu au maangamizi. Na kwamba ghadhabu ya Mungu haiwezi kuja mpaka Yesu amalize kazi yake katika Patakatifu pa Patakatifu, avue mavazi Yake ya ukuhani, na kujivika mavazi ya kisasi.**[CETsw 100.1]**

Ndipo Yesu atatoka katikati ya Baba na wanadamu, na Mungu hatanyamaza tena, bali atamimina ghadhabu yake juu ya wale waliokataa kweli yake. Niliona kwamba **hasira ya mataifa, ghadhabu ya Mungu, na wakati wa kuhukumu wafu** vilikuwa vitu tofauti na vilivyotenganishwa, kimoja kikifuata kingine. Pia niliona kwamba Mikaeli alikuwa bado hajainuka, na kwamba wakati wa taabu, ambao haujawahi kutokea, ulikuwa bado haujaanza. Mataifa sasa yanaanza kukasirika, lakini wakati Kuhani wetu Mkuu atakapomaliza kazi Yake katika Patakatifu, atasimama, atavaa mavazi ya kisasi, ndipo mapigo saba ya mwisho yatamiminwa. **[CETsw 100.2]**

Niliona kwamba wale malaika wanne wangezuia pepo nne mpaka kazi ya Yesu katika patakatifu itakapokamilika, ndipo mapigo saba ya mwisho yangekuja. Mapigo haya yatawakasirisha waovu dhidi ya wenye haki. Watafikiri kwamba sisi ndio tumesababisha hukumu za Mungu kuwajia, na kwamba wakituondoa duniani, mapigo hayo yatasimama. Amri itatolewa ya kuwaua watakatifu, jambo ambalo litawafanya walie mchana na usiku wakimwomba Mungu awaokoe. Huu ndio utakuwa **wakati wa taabu ya Yakobo**.
(Mwanzo 32.) Ndipo watakatifu wote watamlilia Mungu kwa uchungu mkubwa wa roho, nao wataokolewa kwa sauti ya Mungu. Wale **144,000** watashinda. Nyuso zao zitaangazwa kwa utukufu wa Mungu. **[CETsw 100.4]**

Kisha nikaonyeshwa kundi la watu waliokuwa wakilia kwa uchungu mkubwa. Juu ya mavazi yao palikuwa pameandikwa kwa herufi kubwa: **"Umepimwa katika mizani, nawe umeonekana kuwa umepunguka."** Nikauliza kundi hili lilikuwa ni akina nani. Malaika akaniambia: **"Hawa ndio wale waliokuwa wakishika Sabato zamani, lakini wakaiacha."** Niliwasikia wakilia kwa sauti kubwa: **"Tuliamini kuhusu kuja Kwako, na tulifundisha juu ya ujio kwa bidii."** Na walipokuwa wakisema hayo, macho yao yalitazama mavazi yao na kuona maandishi yale, ndipo wakalia kwa sauti kubwa. Niliona kwamba walikuwa wamekunywa maji ya kina kirefu, kisha wakayachafua mabaki yake kwa miguu yao—yaani, waliikanyaga Sabato

chini ya miguu yao. Ndiyo sababu walipimwa katika mizani na kuonekana wamepunguka.**[CETsw 101.1]**

Kisha malaika aliyekuwa pamoja nami akanielekeza tena mjini, ambako niliwaona malaika wanne wakiruka kuelekea lango la mji. Walikuwa karibu kumpa malaika wa langoni **kadi ya dhahabu**, ndipo nikaona malaika mwingine akiruka kwa haraka sana kutoka upande wa utukufu mkuu, akiwapigia kelele kwa sauti kubwa wale malaika wengine, huku akipunga kitu mkononi mwake juu na chini. Nilimwomba malaika aliyekuwa pamoja nami anieleze maana ya kile nilichokiona. Akaniambia kwamba sikuweza kuona zaidi wakati huo, lakini muda mfupi baadaye angenionyesha maana ya mambo yale niliyoyaona. **[CETsw 101.2]**

Jumamosi (Sabato) alasiri mmoja wetu alikuwa mgonjwa, naye akaomba maombi ili apone. Sisi sote tuliungana kumwomba **Yule Tabibu ambaye hajawahi kushindwa kumponya mgonjwa yeyote**. Nguvu ya uponyaji iliposhuka, na yule mgonjwa akaponywa, Roho akaja juu yangu, nami nikachukuliwa katika maono.**[CETsw 101.3]**

Niliona malaika wanne waliokuwa na kazi ya kufanya duniani, nao walikuwa njiani kwenda kuitimiza. Yesu alikuwa amevaa mavazi ya ukuhani. Aliwatazama kwa huruma watu Wake waliosalia, kisha akainua mikono yake na kwa sauti iliyojaa huruma kuu akasema: **"Damu Yangu, Baba, damu Yangu! Damu yangu! Damu Yangu!"** Ndipo nikaona nuru kali sana ikitoka kwa Mungu aliyekuwa ameketi juu ya kile kiti kikubwa cheupe cha enzi, na nuru hiyo ikamzunguka Yesu pande zote. Kisha nikaona malaika akiruka kutoka kwa Yesu akiwa na agizo, akielekea kwa haraka kwa wale malaika wanne waliokuwa na kazi ya kufanya duniani. Alikuwa akipunga kitu mkononi mwake juu na chini, huku akipiga kelele kwa sauti kubwa: **"Shikilieni! Shikilieni! Shikilieni! Shikilieni! Mpaka watumishi wa Mungu watakapotiwa muhuri kwenye vipaji vya nyuso zao."** Nilimuuliza malaika aliyekuwa pamoja nami maana ya kile nilichosikia, na kile ambacho wale malaika wanne walikuwa karibu kufanya. Akaniambia kwamba ni Mungu anayezizuia nguvu hizo, na kwamba amewapa malaika wake mamlaka juu ya mambo ya duniani.**[CETsw 102.1]** **[CETsw 101.3]**

Malaika wale wanne walikuwa wamepewa uwezo kutoka kwa Mungu wa kushikilia pepo nne, na walikuwa karibu kuziachia. Lakini wakati mikono yao ilikuwa ikilegea, na pepo hizo nne zilikuwa karibu kuvuma, jicho la huruma la Yesu liliwatazama masalio wale ambao bado hawakuwa yametiwa muhuri. Ndipo Yesu akainua mikono Yake kwa Baba na kumsihi, akisema kwamba alikuwa amemwaga damu Yake kwa ajili yao. Kisha malaika mwingine akaagizwa kuruka haraka kwenda kwa wale malaika wanne na kuwaambia: "Shikeni, mpaka watumishi wa Mungu watakapotiwa muhuri kwa muhuri wa Mungu aliye hai kwenye vipaji vya nyuso zao." **[CETsw 102.2]**

## 15. JARIBU LA IMANI YETU

Katika wakati huu wa majaribu tunahitaji kutiana moyo na kufarijiana na kila mmoja wetu. Majaribu ya Shetani sasa ni makubwa kuliko wakati mwingine wowote, kwa sababu anajua kwamba muda wake ni mfupi, na kwamba hivi karibuni kila hukumu itaamuliwa, ama kwa uzima au kwa mauti. Sasa si wakati wa kuzama chini kwa sababu ya kukata tamaa na majaribu; tunapaswa kustahimili mateso yetu yote na kumtumaini Mungu Mwenyezi wa Yakobo kwa moyo wote. Bwana amenionyesha kwamba **neema Yake inatosha kwa majaribu yetu yote**; na ingawa majaribu hayo ni makubwa kuliko hapo awali, lakini tukimtegemea Mungu kikamilifu, tunaweza kushinda kila jaribu na kwa neema Yake tutatoka tukiwa washindi. **[CETsw 103.1]**

Ikiwa tutashinda majaribu yetu, na kupata ushindi dhidi ya vishawishi vya Shetani, basi tunavumilia jaribu la imani yetu, ambalo ni la thamani kuliko dhahabu, na tunakuwa wenye nguvu zaidi na tayari zaidi kukabiliana na jaribu linalofuata. Lakini ikiwa tutakata tamaa na kujiweka wenyewe kwenye vishawishi vya Shetani, tutazidi kuwa dhaifu na hatutapata thawabu kwa ajili ya jaribu hilo, wala hatutakuwa tumejiandaa vizuri kwa jaribu linalofuata. Kwa njia hii tutazidi kudhoofika zaidi na zaidi, hadi kuwekwa mateka na Shetani kwa mapenzi yake. **[CETsw 103.2]**

Ni lazima tuvae silaha zote za Mungu, na tuwe tayari wakati wowote kwa ajili ya vita dhidi ya nguvu za giza. Majaribu na mitihani yanapotujia kwa nguvu, na tumwendee Mungu, tukimlilia katika maombi. Hatatufukuza hali tukiwa mikono mitupu, bali atatupatia neema na nguvu za kushinda, na kuvunja nguvu za adui. Laiti wote wangeweza kuona mambo haya katika mwanga wake halisi, na kuvumilia mateso kama askari wema wa Kristo! Ndipo Israeli ingesonga mbele, ikiwa na nguvu katika Mungu, na katika uwezo wa nguvu Zake. **[CETsw 103.3]**

Mungu amenionyesha kwamba aliwapa watu Wake kikombe kichungu cha kunywa, ili kuwatakasa na kuwaosha. Ni kinywaji kichungu, na wanaweza kukifanya kiwe kichungu zaidi kwa kunung'unika, kulalamika, na kusikitika. Lakini wale wanaokipokea kwa namna hiyo lazima wapewe kikombe kingine, kwa maana kile cha kwanza hakijatimiza kusudi lake moyoni. Na ikiwa kile cha pili hakitatimiza kazi hiyo, basi watapewa kingine tena, na kingine, mpaka kitimize kusudi lake; la sivyo wataachwa wakiwa wachafu na wasio safi moyoni. Niliona kwamba kikombe hiki kichungu kinaweza kutiwa utamu kwa njia ya uvumilivu, kustahimili, na maombi; na kwamba kitakuwa na matokeo yaliyokusudiwa katika mioyo ya wale wanaokipokea kwa njia hiyo, na Mungu ataheshimiwa na kutukuzwa. **[CETsw 103.4]**

Si jambo dogo kuwa Mkristo, na kukubaliwa na kuthibitishwa na Mungu. Bwana amenionyesha baadhi ya watu wanaodai kuwa na ukweli wa sasa, lakini maisha yao hayaendani na madai yao. Wana kiwango cha uchaji wa Mungu kilicho chini sana, na wanapungukiwa sana na utakatifu wa Biblia. Baadhi yao hujihusisha na mazungumzo ya bure na yasiyofaa, na wengine hujiachilia kwa maonyesho ya kiburi cha nafsi. Hatupaswi kutarajia kuzipendeza nafsi zetu wenyewe, kuishi na kutenda kama ulimwengu, kufurahia anasa zake, na kushirikiana na wale walio wa ulimwengu, halafu tutawale pamoja na Kristo katika utukufu. **[CETsw 104.1]**

Ni lazima tushiriki mateso ya Kristo hapa duniani, ikiwa tunataka kushiriki utukufu Wake baadaye. Ikiwa tunatafuta maslahi yetu wenyewe, jinsi tunavyoweza kujipendeza zaidi, badala ya kutafuta kumpendeza Mungu na kusogeza mbele kazi Yake tukufu yenye mateso, tutamvunjia Mungu heshima na kulidhalilisha jambo takatifu tunalodai kulipenda. Tumebakiwa na muda mfupi tu wa kufanya kazi kwa ajili ya Mungu. Hakuna jambo linalopaswa kuwa la thamani sana kiasi cha kushindwa kulitoa dhabihu kwa ajili ya wokovu wa kundi lililotawanyika na lililoteseka la Yesu. Wale wanaofanya agano na Mungu kwa dhabihu sasa, hivi karibuni watakusanywa nyumbani kushiriki thawabu kubwa, na kuimiliki ufalme mpya milele na milele. **[CETsw 104.2]**

Ee, na tuishi kikamilifu kwa ajili ya Bwana, na kuonyesha kwa maisha yaliyo na mpangilio mzuri na mwenendo wa kimungu kwamba tumekuwa pamoja na Yesu, na kwamba sisi ni wafuasi Wake wapole na wanyenyekevu. Ni lazima tufanye kazi wakati kungali mchana, kwa maana wakati usiku wa giza wa shida na mateso utakapokuja, itakuwa imechelewa kufanya kazi kwa ajili ya Mungu. Yesu Yuko katika hekalu Lake takatifu, na sasa anakubali dhabihu zetu, maombi yetu, na maungamo yetu ya makosa na dhambi zetu; Naye atasamehe makosa yote ya Israeli, ili yaweze kufutwa kabla hajaondoka katika patakatifu. Yesu atakapoondoka patakatifu, wale walio watakatifu na wenye haki wataendelea kuwa watakatifu na wenye haki; kwa maana dhambi zao zote zitakuwa zimefutwa, na watakuwa wametiwa muhuri kwa muhuri wa Mungu aliye hai. Lakini wale wasio haki na wachafu wataendelea kuwa wasio haki na wachafu; kwa maana wakati huo hakutakuwa tena na kuhani katika patakatifu wa kutoa dhabihu zao, maungamo yao, na maombi yao mbele ya kiti cha enzi cha Baba. Kwa hiyo, jambo lolote linalopaswa kufanyika ili kuokoa roho kutoka kwenye dhoruba inayokuja ya ghadhabu, lazima lifanyike kabla Yesu hajaondoka katika Patakatifu pa Patakatifu pa hekalu la mbinguni.**[CETsw 105.1]**

## 16. KWA KUNDI DOGO

**Ndugu wapendwa:** Bwana alinipa maono tarehe 26 Januari, 1850, ambayo nitayasimulia. Niliona kwamba baadhi ya watu wa Mungu ni wapumbavu na wamelala kiroho, na wako nusu tu katika hali ya kuamka; hawatambui wakati tunaoishi sasa, na kwamba ... baadhi yao wako katika hatari ya kusombwa na kuangamizwa. Nilimsihi Yesu awaokoe, awavumilie kwa muda mfupi zaidi, na awaonyeshe hatari yao kubwa, ili waweze kujiandaa kabla haijawa milele kuchelewa. Malaika alisema: **"Uharibifu unakuja kama tufani kubwa."** Nilimsihi malaika awaonee huruma na kuwaokoa wale wanaoupenda ulimwengu huu, ambao wamejifunga na mali zao, na hawakuwa tayari kuziacha na kutoa dhabihu ili kuwawezesha wajumbe kusonga mbele kwenda kuwalisha kondoo wenye njaa waliokuwa wanaangamia kwa kukosa chakula cha kiroho.**[CETsw 105.2]**

Nilipowaona roho maskini zikifa kwa kukosa Ukweli wa sasa, na baadhi ya wale waliodai kuamini Ukweli wakiwa wanaziacha zife kwa kuzuia njia zinazohitajika ili kuendeleza kazi ya Mungu, jambo hilo lilikuwa chungu sana kwangu, nami nikamsihi malaika aniondolee maono hayo. Niliona kwamba wakati kazi ya Mungu ilipohitaji baadhi ya mali zao, kama yule kijana aliyemjia Yesu (Mathayo 19:16-22), waliondoka wakiwa na huzuni; na kwamba hivi karibuni mjeledi wa gharika ungepita na kufagia mali zao zote, na ndipo ingekuwa imechelewa kutoa dhabihu za vitu vya duniani na kujiwekea hazina mbinguni.

Kisha nilimwona Mkombozi mtukufu, mwenye uzuri na upendo; kwamba aliacha makao ya utukufu, akaja katika ulimwengu huu wa giza na upweke, ili kutoa maisha Yake ya thamani na kufa, Yeye Mwenye haki kwa ajili ya wasio haki. Alivumilia dhihaka kali na kupigwa mijeledi kwa ukatili, alivaa taji la miiba iliyosokotwa, na katika bustani alitokwa na matone makubwa ya damu, wakati mzigo wa dhambi za ulimwengu wote ulikuwa juu Yake. Malaika akauliza: **"Kwa ajili ya nini?"** Ee, niliona na kuelewa kwamba ilikuwa kwa ajili yetu; kwa sababu ya dhambi zetu Aliteseka mambo haya yote, ili kwa damu Yake ya thamani atuokoe kwa ajili ya Mungu!

Kisha tena waliletwa mbele yangu wale ambao hawakuwa tayari kutumia mali za ulimwengu huu ili kuokoa roho zinazopotea kwa kuwapelekea ukweli, wakati Yesu akiwa amesimama mbele za Baba akisihi kwa damu Yake, mateso Yake, na kifo Chake kwa ajili yao. Wakati huo huo wajumbe wa Mungu walikuwa wakingojea, wakiwa tayari kubeba ukweli wa wokovu, ili watu wapate kutiwa muhuri kwa muhuri wa Mungu aliye hai. Ni jambo gumu kwa baadhi ya wale wanaodai kuamini ukweli wa sasa kufanya hata jambo dogo kama kuwapa wajumbe fedha ya Mungu mwenyewe, ambayo Amewakopesha ili wawe mawakili wake.

Yesu mwenye mateso, upendo Wake mkuu kiasi kwamba ulimfanya kutoa maisha Yake kwa ajili ya mwanadamu, aliletwa tena mbele yangu; pia maisha ya wale wanaodai kuwa wafuasi Wake, ambao walikuwa na mali za dunia hii, lakini waliona kuwa ni jambo kubwa sana kusaidia kazi ya wokovu. Malaika alisema: **"Je, watu wa namna hii wanaweza kuingia mbinguni?"** Malaika mwingine akajibu: **"Hapana, kamwe, kamwe, kamwe. Wale ambao hawapendezwi na kazi ya Mungu duniani, hawawezi kamwe kuimba wimbo wa upendo wa ukombozi kule juu."** Niliona kwamba kazi ya haraka ambayo Mungu alikuwa akiifanya duniani ingekamilishwa upesi katika haki, na kwamba wajumbe walipaswa kusonga mbele kwa haraka ili kuwatafuta kundi lililotawanyika.

Kutetemeka kukuu kulikuwa kumeanza na kungeendelea, na wote ambao hawakuwa tayari kusimama kwa ujasiri na bila kuyumba kwa ajili ya ukweli, na kutoa dhabihu kwa ajili ya Mungu na kazi Yake, wangesukumwa nje. Malaika alisema: **"Mnadhani kwamba mtu yeyote atalazimishwa kutoa dhabihu? Hapana, hapana. Lazima iwe sadaka ya hiari. Itawagharimu vyote ili kuinunua shamba."** Nilimlilia Mungu awaokoe watu Wake, ambao baadhi yao walikuwa wakizimia na kufa. Kisha nikaona kwamba hukumu za Mwenyezi Mungu zilikuwa zinakuja kwa haraka, nami nikamsihi malaika aseme kwa lugha yake kwa watu. Akasema: **"Ngurumo zote na radi zote za Mlima Sinai hazitawasukuma wale ambao hawatasukumwa na kweli zilizo wazi za Neno la Mungu; wala ujumbe wa malaika hautawaamsha."**

Kisha nikaona uzuri na upendo wa Yesu. Vazi Lake lilikuwa jeupe kuliko weupe wote. Hakuna lugha inayoweza kuelezea utukufu Wake na uzuri Wake uliotukuka. Wote, wote wanaozishika amri za Mungu, wataingia kupitia malango ya kuingia katika mji, na watakuwa na haki ya kuufikia mti wa uzima, na watakuwa daima katika uwepo wa Yesu mpendwa, ambaye uso Wake unang'aa kuliko jua la mchana.

Nilielekezwa kumwangalia Adamu na Hawa katika Edeni. Walikula matunda ya mti uliokatazwa, wakafukuzwa kutoka bustanini, kisha upanga wa moto ukawekwa kuzunguka mti wa uzima, ili wasije wakala matunda yake na kuwa wenye dhambi wasiokufa. Mti wa uzima ulikusudiwa kuendeleza hali ya kutokufa. Nilimsikia malaika akiuliza: "Ni nani katika jamaa ya Adamu aliyepita ule upanga wa moto na akala matunda ya mti wa uzima?" Nilimsikia malaika mwingine akijibu: "Hakuna hata mmoja katika jamaa ya Adamu aliyepita ule upanga wa moto na kula mti huo; kwa hiyo hakuna mwenye dhambi asiyeweza kufa. Roho itendayo dhambi itakufa

kifo cha milele, kifo kitakachodumu milele, ambacho hakitakuwa na tumaini la ufufuo; ndipo ghadhabu ya Mungu itatulizwa."

"Watakatifu watapumzika katika mji mtakatifu, na kutawala kama wafalme na makuhani kwa miaka elfu moja; kisha Yesu atashuka pamoja na watakatifu juu ya Mlima wa Mizeituni, na mlima huo utapasuka katikati, na kuwa uwanda mkubwa kwa ajili ya Paradiso ya Mungu kukaa juu yake. Sehemu iliyobaki ya dunia haitasafishwa mpaka mwisho wa miaka hiyo elfu moja, wakati wafu waovu watakapofufuliwa, na kukusanyika kuuzunguka mji. Miguu ya waovu haitaweza kamwe kuinajisi dunia iliyofanywa mpya. Moto utashuka kutoka kwa Mungu kutoka mbinguni na kuwateketeza; utawaunguza kabisa, mizizi na matawi. Shetani ndiye mzizi, na watoto wake ndio matawi. Moto ule ule utakaowateketeza waovu, ndio utakaosafisha dunia."

## 17. KUTIKISWA KWA NGUVU ZA MBINGUNI

Tarehe 16 Desemba, 1848, Bwana alinipa maono kuhusu kutetemeka kwa nguvu za mbinguni. Niliona kwamba wakati Bwana aliposema **"mbingu"** alipokuwa akitoa ishara zilizorekodiwa na Mathayo, Marko, na Luka, alimaanisha mbingu halisi; na aliposema **"nchi"**, alimaanisha dunia.Nguvu za mbinguni ni jua, mwezi, na nyota. Hizo ndizo zinazotawala katika mbingu. Nguvu za dunia ni zile zinazotawala juu ya dunia. Nguvu za mbinguni zitatetemeshwa kwa sauti ya Mungu. Ndipo jua, mwezi, na nyota zitasogezwa kutoka mahali pake. Hazitaondoka, bali zitatetemeshwa kwa sauti ya Mungu.

Mawingu mazito na meusi yalikuja juu, yakagongana yenyewe kwa yenyewe. Anga likagawanyika na kurudi nyuma; kisha tuliweza kutazama juu kupitia nafasi iliyo wazi katika kundi la nyota la Orion, ambako sauti ya Mungu ilitokea. Mji mtakatifu utashuka kupitia nafasi hiyo iliyo wazi. Niliona kwamba nguvu za dunia sasa zinatetemeshwa, na kwamba matukio yanakuja kwa mpangilio. Vita, na habari za vita, upanga, njaa, na magonjwa ya kuambukiza ndivyo vitakavyoanza kutikisa nguvu za dunia; kisha sauti ya Mungu itatikisa jua, mwezi, na nyota, na pia dunia hii. Niliona kwamba kutetemeka kwa nguvu huko Ulaya siyo, kama wengine wanavyofundisha, kutetemeka kwa nguvu za mbinguni, bali ni kutetemeka kwa mataifa yenye hasira.

## 18. MAANDALIZI KWA AJILI YA MWISHO

Tarehe 14 Mei, 1851, niliona uzuri na upendo wa Yesu. Nilipoutazama utukufu Wake, wazo halikuja akilini mwangu kwamba ningewahi kutenganishwa na uwepo Wake. Niliona mwanga ukitoka katika utukufu uliomzunguka Baba, na ulipokaribia karibu nami, mwili wangu ulitetemeka na kutikisika kama jani. Nilifikiri kwamba kama ungeendelea kunikaribia ningetoweka kabisa; lakini ule mwanga ulinipita. Ndipo niliweza kupata kwa kiasi fulani ufahamu wa Mungu mkuu na wa kutisha ambaye tunapaswa kushughulika Naye. Niliona jinsi baadhi ya watu wanavyokuwa na mawazo hafifu kuhusu utakatifu wa Mungu, na jinsi wanavyolitumia bure jina Lake takatifu na la kuheshimiwa, bila kutambua kwamba ni Mungu, Mungu mkuu na wa kutisha, ambaye wanazungumza juu Yake. Wakati wa kuomba, wengi hutumia maneno yasiyo na heshima na yasiyofaa, ambayo humhuzunisha Roho mpole wa Bwana, na kusababisha maombi yao kuzuiwa yasifikie mbingu.

Pia niliona kwamba wengi hawatambui wanavyopaswa kuwa ili kuishi mbele za Bwana bila kuhani mkuu katika patakatifu, wakati wa dhiki. Wale wanaopokea muhuri wa Mungu aliye hai, na kulindwa wakati wa dhiki, lazima waakisi kikamilifu sura ya Yesu.

Niliona kwamba wengi walikuwa wakipuuzia maandalizi muhimu sana yanayohitajika, na walikuwa wakitazamia wakati wa **"kuburudishwa"** na **"mvua ya mwisho"** kuwafanya wafae kusimama katika siku ya Bwana, na kuishi mbele Zake. Ee, ni wangapi nilioona wakati wa dhiki wakiwa hawana mahali pa kujisitiri! Walikuwa wamepuuza maandalizi yaliyohitajika; kwa hiyo hawakuweza kupokea kiburudisho ambacho wote wanapaswa kuwa nacho ili kuwafanya wafae kuishi mbele ya Mungu mtakatifu.

Wale wanaokataa kuchongwa na manabii, na kushindwa kutakasa roho zao kwa kutii ukweli wote, na ambao wako tayari kuamini kwamba hali yao ni nzuri zaidi kuliko ilivyo kweli, watafika wakati wa kumwagwa kwa mapigo. Ndipo wataona kwamba walihitaji kuchongwa na

kusawazishwa kwa ajili ya jengo. Lakini wakati huo hakutakuwa tena na muda wa kufanya hivyo, wala hakutakuwa na Mpatanishi wa kusihi hukumu yao mbele za Baba. Kabla ya wakati huo, tangazo hili lenye uzito wa kutisha litakuwa limetolewa: **"Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa."** (Ufunuo 22:11)

Niliona kwamba hakuna mtu anayeweza kushiriki katika **"kiburudisho"** hicho, isipokuwa apate ushindi juu ya kila dhambi inayomzingira: juu ya kiburi, ubinafsi, kupenda dunia, na kila neno na tendo lisilo sahihi. Kwa hiyo, tunapaswa kusogea karibu zaidi na zaidi kwa Bwana, na kutafuta kwa bidii maandalizi yale yanayotuwezesha kusimama katika vita katika siku ya Bwana. Wote wakumbuke kwamba Mungu ni mtakatifu, na kwamba hakuna isipokuwa viumbe watakatifu watakaoweza kuishi mbele za uwepo Wake milele.

## 19. MAPAMBANO NA UMASKINI

Huko Gorham, Maine, tarehe 26 Agosti, 1847, mtoto wetu wa kwanza wa kiume, **Henry Nichols White**, alizaliwa. Mwezi Oktoba, Ndugu na Dada Howland wa Topsham walitupatia kwa wema sehemu ya nyumba yao, jambo ambalo tulilikubali kwa furaha, na tukaanza maisha ya nyumbani kwa kutumia samani tulizoazimwa. Tulikuwa maskini, na tulipitia nyakati ngumu sana. Tulikuwa tumeazimia kutowategemea wengine, bali kujitegemeza wenyewe, na kuwa na kitu cha kuwasaidia wengine. Lakini hatukufanikiwa kifedha. Mume wangu alifanya kazi kwa bidii sana akibeba mawe kwenye reli, lakini hakuweza kupata malipo yaliyokuwa yanastahili kwa kazi yake. Ndugu na Dada Howland walitugawia kwa hiari kila walipoweza; lakini wao pia walikuwa katika hali ngumu ya maisha. Waliamini kikamilifu ujumbe wa kwanza na wa pili, na walikuwa wametoa kwa ukarimu mali zao ili kuendeleza kazi, mpaka wakawa wanategemea kazi yao ya kila siku.

Mume wangu aliacha kazi ya kubeba mawe, akachukua shoka lake akaenda msituni kukata kuni za kamba. Akiwa na maumivu ya kudumu ubavuni mwake, alifanya kazi kuanzia asubuhi mapema mpaka giza lilipoingia ili kupata karibu senti hamsini kwa siku. Tulijitahidi kudumisha moyo wa ujasiri na kumtumaini Bwana. Sikulalamika. Asubuhi nilihisi kumshukuru Mungu kwa kutulinda katika usiku mwingine uliopita, na jioni nilimshukuru kwa kutuhifadhi katika siku nyingine.

Siku moja, chakula chetu kilipokwisha, mume wangu alikwenda kwa mwajiri wake ili kupata fedha au chakula. Ilikuwa siku yenye dhoruba, naye alitembea maili tatu kwenda na kurudi akiwa kwenye mvua. Alirudi nyumbani akiwa amebeba begi la vyakula mgongoni mwake, lililofungwa katika sehemu mbalimbali, akiwa amepita kwa njia hiyo katika kijiji cha Brunswick,

ambako mara nyingi alikuwa amehubiri. Alipoingia nyumbani, akiwa amechoka sana, moyo wangu ulizama ndani yangu. Hisia yangu ya kwanza ilikuwa kwamba Mungu alikuwa ametutelekeza. Nilimwambia mume wangu: **"Je, tumefikia hali hii? Je, Bwana ametuacha?"** Sikuweza kuzuia machozi yangu, nami nililia kwa sauti kwa saa nyingi, mpaka nikazimia. Maombi yalitolewa kwa ajili yangu. Baada ya muda mfupi nilihisi ushawishi wa kutia moyo wa Roho wa Mungu, nami nilijutia kwamba nilikuwa nimeanguka chini ya hali ya kukata tamaa. Tunatamani kumfuata Kristo na kuwa kama Yeye; lakini wakati mwingine tunazimia chini ya majaribu, na tunabaki mbali Naye. Mateso na majaribu hutukaribisha karibu na Yesu. Tanuru huteketeza takataka na kuifanya dhahabu ing'ae zaidi.

Wakati huo nilionyeshwa kwamba Bwana alikuwa ametujaribu kwa ajili ya wema wetu, na kutuandaa kufanya kazi kwa ajili ya wengine. Alikuwa akitikisa kiota chetu, ili tusije tukatulia katika hali ya starehe. Kazi yetu ilikuwa kufanya kazi kwa ajili ya roho za watu. Kama tungefanikiwa kifedha, nyumba ingekuwa mahali pazuri sana kiasi kwamba tungekuwa hatutaki kuiacha.

Majaribu yaliruhusiwa kutupata ili kutuandaa kwa ajili ya mapambano makubwa zaidi ambayo tungekutana nayo katika safari zetu. Baada ya muda mfupi tulipokea barua kutoka kwa ndugu katika majimbo mbalimbali, wakitualika tuwatembelee; lakini hatukuwa na uwezo wa kusafiri kutoka nje ya jimbo. Jibu letu lilikuwa kwamba njia haikuwa imefunguliwa mbele yetu. Nilifikiri kwamba haingewezekana kwangu kusafiri pamoja na mtoto wangu. Hatukutaka kuwategemea wengine, na tulikuwa waangalifu kuishi kulingana na uwezo wetu. Tulikuwa tumeazimia kuteseka kuliko kuingia katika madeni.

Mtoto mdogo Henry hivi karibuni aliugua sana, na hali yake ikawa mbaya haraka kiasi kwamba tuliingiwa na hofu kubwa. Alilala katika hali ya kulegea sana; Alipumua kwa haraka na kwa shida. Tulimpa dawa lakini hazikusaidia. Ndipo tukamwita mtu mwenye uzoefu katika magonjwa, naye akasema kwamba kupona kwake kulikuwa na mashaka. Tulikuwa tumemwombea, lakini hakukuwa na mabadiliko. Tulitumia kisingizio cha mtoto kama sababu ya kutokusafiri na kufanya kazi kwa ajili ya mema ya wengine, na tuliogopa kwamba Bwana alikuwa karibu kumwondoa. Kwa mara nyingine tena tulimjia Bwana kwa maombi, tukimsihi awe na huruma juu yetu, na kuokoa maisha ya mtoto. Tukaweka ahadi kwa uzito mbele Zake kwamba tutakwenda mbele, tukimtumaini Mungu, popote atakapotutuma.

Maombi yetu yalikuwa ya dhati na ya kusihi kwa uchungu mkubwa. Kwa imani tulidai ahadi za Mungu, na tuliamini kwamba alisikiliza vilio vyetu. Nuru kutoka mbinguni ilianza kupenya mawingu na kutuangazia. Maombi yetu yalijibiwa kwa neema. Tangu saa hiyo mtoto alianza kupata nafuu.

**Ziara ya Kwanza Connecticut**

Tukiwa Topsham tulipokea barua kutoka kwa Ndugu E. L. H. Chamberlain wa Middletown, Connecticut, akitusihi tuhudhurie mkutano wa konferensi katika jimbo hilo mwezi Aprili, 1848. Tuliamua kwenda ikiwa tungeweza kupata fedha za safari. Mume wangu alimaliza hesabu na mwajiri wake, na akagundua kwamba alikuwa anastahili kupokea dola kumi. Dola tano kati ya hizo nilinunua nguo ambazo tulizihitaji sana, kisha nikafanyia koti la mume wangu marekebisho kwa kulishona viraka, hata kuunganisha viraka juu ya viraka, kiasi kwamba ilikuwa vigumu kutambua kitambaa cha awali kwenye mikono ya koti. Tulibakiwa na dola tano za kutupeleka hadi Dorchester, Massachusetts.

Sanduku letu lilikuwa na karibu kila kitu tulichokuwa nacho duniani; lakini tulifurahia amani ya moyo na dhamiri safi, na vitu hivi tulivithamini kuliko starehe za kidunia.

Tukiwa Dorchester tulifika nyumbani kwa Ndugu Otis Nichols. Tulipoondoka, Dada Nichols alimkabidhi mume wangu dola tano, ambazo zililipia nauli yetu hadi Middletown, Connecticut. Tulikuwa wageni huko Middletown, kwa kuwa hatukuwahi kumwona hata mmoja wa ndugu wa imani katika Connecticut. Kati ya fedha zetu tulikuwa tumebakiwa na senti hamsini tu. Mume wangu hakuthubutu kutumia fedha hizo kukodi gari, kwa hiyo alilibeba sanduku letu na kulitia juu ya rundo refu la mbao katika eneo la karibu la kuhifadhia mbao, kisha tukaendelea kutembea tukitafuta mtu mwenye imani kama yetu. Muda si muda tulimpata Ndugu Chamberlain, ambaye alituchukua kwenda nyumbani kwake.

**Konferensi Huko Rocky Hill**

Konferensi ya Rocky Hill ilifanyika katika chumba kikubwa ambacho hakikuwa bado kimekamilika cha nyumba ya Ndugu Albert Belden. Katika barua aliyomwandikia Ndugu Stockbridge Howland, mume wangu aliandika kuhusu mkutano huo kama ifuatavyo:

“Aprili 20, Ndugu Belden alituma gari lake lenye farasi wawili hadi Middletown kwa ajili yetu na ndugu waliotawanyika katika mji huo. Tulifika mahali hapa karibu saa kumi jioni, na baada ya muda mfupi Ndugu Bates na Gurney wakafika. Tulikuwa na mkutano jioni hiyo ukiwa na watu wapatao kumi na tano. Ijumaa asubuhi ndugu waliendelea kuja mpaka tukawa karibu hamsini. Hawa hawakuwa wote wameikubali kweli kikamilifu. Mkutano wetu siku hiyo ulikuwa wa kuvutia sana. Ndugu Bates aliwasilisha amri za Mungu kwa uwazi, na umuhimu wake ulisisitizwa kwa ushuhuda wenye nguvu. Neno lilikuwa na matokeo ya kuwaimarisha wale waliokuwa tayari katika kweli, na kuwaamsha wale ambao hawakuwa wamefanya uamuzi kamili.”

**Kupata Fedha za Kwenda Magharibi mwa New York**

Miaka miwili kabla ya wakati huo, nilikuwa nimeonyeshwa kwamba wakati fulani wa baadaye tungeitembelea sehemu ya magharibi ya New York. Na sasa, muda mfupi baada ya kumalizika kwa konferensi ya Rocky Hill, tuliombwa kuhudhuria mkutano mkuu huko Volney, New York, mwezi Agosti. Ndugu Hiram Edson alituandikia kwamba ndugu huko walikuwa wengi wao maskini, na kwamba hangeweza kutuahidi kwamba wangeweza kusaidia sana kugharamia safari yetu, lakini angefanya kile alichoweza. Hatukuwa na fedha za kusafiria. Afya ya mume wangu ilikuwa dhaifu, lakini njia ilifunguka kwake kufanya kazi katika mashamba ya nyasi, naye akaamua kukubali kazi hiyo.

Ilionekana wakati huo kwamba tulipaswa kuishi kwa imani. Kila tulipoamka asubuhi, tulipiga magoti kando ya kitanda chetu na kumwomba Mungu atupe nguvu za kufanya kazi siku hiyo, na hatukuwa na amani bila kupata uhakikisho kwamba Bwana alikuwa amesikia maombi yetu. Kisha mume wangu aliendа mbele akitumia mundu kukata nyasi kwa nguvu ambazo Mungu alimpa. Usiku aliporudi nyumbani, tuliendelea tena kumsihi Mungu atupe nguvu za kupata fedha kwa ajili ya kueneza kweli. Katika barua aliyomwandikia Ndugu Howland, tarehe 2 Julai, 1848, alieleza uzoefu huu hivi:

“Leo kuna mvua, kwa hiyo sikati nyasi, vinginevyo nisingeweza kuandika. Nakata nyasi siku tano kwa ajili ya wasioamini, na Jumapili kwa ajili ya waumini, kisha napumzika siku ya saba; kwa hiyo nina muda mchache sana wa kuandika... Mungu hunipa nguvu ya kufanya kazi kwa bidii siku nzima... Ndugu Holt, Ndugu John Belden, na mimi tumechukua ekari mia moja za nyasi za kukata, kwa malipo ya senti themanini na saba na nusu kwa kila ekari, na tunajigharamia chakula chetu wenyewe. Asifiwe Bwana! Natumaini kupata dola chache hapa zitakazotumika katika kazi ya Mungu.”

Kutokana na kazi yake katika shamba la nyasi, mume wangu alipata dola arobaini. Kwa sehemu ya fedha hizo tulinunua nguo muhimu, na tukabakiwa na fedha za kutosha kutupeleka magharibi mwa New York na kuturudisha tena.

Afya yangu ilikuwa dhaifu, na haikuwezekana kwangu kusafiri huku nikimtunza mtoto wetu. Kwa hiyo tulimwacha mtoto wetu mdogo Henry, aliyekuwa na umri wa miezi kumi, huko Middletown kwa Dada Clarissa Bonfoey. Ilikuwa jaribu kubwa kwangu kutengana na mtoto wangu, lakini hatukuthubutu kuruhusu upendo wetu kwake utuzuie kufuata njia ya wajibu. Yesu aliutoa uhai Wake ili kutuokoa. Ni jinsi gani sadaka yoyote tunayoweza kutoa ni ndogo ikilinganishwa na sadaka Yake!

**Konferensi Huko Volney**

Mkutano wetu mkuu wa kwanza katika magharibi mwa New York, ulioanza tarehe 18 Agosti, ulifanyika huko Volney, katika ghala la Ndugu David Arnold. Kulikuwa na watu

wapatao thelathini na watano waliohudhuria—marafiki wote walioweza kukusanywa katika sehemu hiyo ya jimbo. Lakini miongoni mwa watu hao haikupatikana hata wawili waliokuwa na msimamo mmoja. Baadhi yao walikuwa wameshikilia makosa makubwa, na kila mmoja alisisitiza kwa nguvu maoni yake mwenyewe, akidai kwamba yalikuwa yanapatana na Maandiko.

Tofauti hizi za ajabu za maoni zilileta mzigo mzito moyoni mwangu. Niliona kwamba makosa mengi yalikuwa yakiwasilishwa kama kweli. Ilionekana kwangu kwamba Mungu alikuwa akidharauliwa. Huzuni kubwa ilinilemea rohoni, nami nikazimia chini ya mzigo huo. Baadhi yao waliogopa kwamba nilikuwa nakaribia kufa. Ndugu Bates, Chamberlain, Gurney, Edson, na mume wangu waliomba kwa ajili yangu. Bwana aliyasikia maombi ya watumishi Wake, nami nikapata nguvu tena.

Kisha nuru ya mbinguni ikashuka juu yangu, na mara nikawa nimeondolewa katika mambo ya dunia. Malaika wangu aliyekuwa pamoja nami aliniwekea mbele baadhi ya makosa ya wale waliokuwapo, na pia ukweli uliokuwa ukipingana na makosa yao. Maoni hayo yaliyotofautiana, ambayo walidai kwamba yalikuwa yanapatana na Maandiko, yalitokana na tafsiri zao wenyewe za mafundisho ya Biblia. Niliagizwa kuwaambia kwamba walipaswa kuacha makosa yao, na kuungana katika kweli za **ujumbe wa malaika wa tatu**.

Mkutano wetu ulifungwa kwa ushindi. Ukweli ulipata ushindi. Ndugu zetu waliacha makosa yao na kuungana katika ujumbe wa malaika wa tatu, na Mungu aliwabariki sana na kuwaongezea idadi yao. [Baada ya kurudi kutoka magharibi mwa New York mwezi Septemba, 1848, Mzee na Bi. White walisafiri kwenda Maine, ambako walifanya mkutano pamoja na waumini tarehe 20–22 Oktoba. Huu ulikuwa mkutano wa Topsham, ambapo ndugu walianza kuomba kwamba njia ifunguliwe kwa ajili ya kuchapisha kweli zilizohusiana na ujumbe wa marejeo.

Baada ya mwezi mmoja, mwezi Novemba, 1848, walikuwa pamoja na kikundi kidogo cha ndugu na dada waliokusanyika katika konferensi huko Dorchester, karibu na Boston, Massachusetts. Ilikuwa katika mkutano huu ambapo nuru ilipokelewa kuhusu wajibu wa Mzee James White wa kuchapisha kweli za ujumbe wa malaika wa tatu.]

**Ziara kwa Ndugu Snow**

Kutoka Volney tulisafiri kuelekea Port Gibson, umbali wa maili sitini, ili kuhudhuria mwaliko mwingine tarehe 27 na 28 Agosti. Mume wangu aliandika katika barua aliyomwandikia Ndugu Hastings tarehe 26 Agosti: "Tukiwa njiani, tulisimama nyumbani kwa Ndugu Snow huko Hannibal. Mahali hapo kulikuwa na roho nane au kumi za thamani. Ndugu Bates, Ndugu na Dada Edson, na Ndugu Simmons walikaa nao usiku huo. Asubuhi Ellen alichukuliwa katika maono, na wakati alipokuwa katika maono, ndugu wote waliingia. Mmoja wao hakuwa pamoja nasi katika kweli ya Sabato, lakini alikuwa mnyenyekevu na mwema. Ellen alisimama akiwa

katika maono, akaichukua Biblia kubwa, akaiinua mbele za Bwana, akazungumza kutoka ndani yake, kisha akaipeleka kwa ndugu huyo mnyenyekevu na kuiweka mikononi mwake. Aliipokea huku machozi yakimtiririka kifuani. Kisha Ellen akarudi na kukaa karibu nami. Alikuwa katika maono kwa muda wa saa moja na nusu, wakati huo wote hakupumua kabisa. Ilikuwa wakati wa kugusa moyo sana. Wote tulilia sana kwa furaha. Tulimwacha Ndugu Bates pamoja nao, kisha tukaja mahali hapa pamoja na Ndugu Edson."

## 20. MAJALIWA YA MUNGU YANAYOTIA MOYO

Tena niliitwa kujikana nafsi kwa ajili ya wokovu wa roho. Tulipaswa kutengana na mtoto wetu mdogo Henry, na kwenda mbele kutumika bila masharti katika kazi hiyo. Afya yangu ilikuwa dhaifu sana, na kama ningemchukua mtoto wangu pamoja nami, bila shaka angechukua sehemu kubwa ya muda wangu. Ilikuwa jaribu kubwa, lakini sikuthubutu kumruhusu awe kizuizi katika njia ya wajibu. Niliamini kwamba Bwana alikuwa amemhifadhi alipokuwa mgonjwa sana, na kwamba kama ningemruhusu anizuie kufanya wajibu wangu, Mungu angemwondoa kwangu. Nikiwa peke yangu mbele za Bwana, nikiwa na moyo wa huzuni na machozi mengi, nilimwacha, na nikamkabidhi mtoto wangu wa pekee ili atunzwe na mwingine.

Tulimwacha Henry katika familia ya Ndugu Howland, ambao tuliwaamini kabisa. Walikuwa tayari kubeba mizigo, ili sisi tuwe huru kadiri iwezekanavyo kufanya kazi katika kazi ya Mungu. Tulijua kwamba wangeweza kumtunza Henry vizuri zaidi kuliko ambavyo sisi tungeweza kufanya ikiwa tungemchukua katika safari zetu. Tulijua kwamba ilikuwa kwa manufaa yake kuwa na makao ya kudumu na nidhamu thabiti, ili tabia yake nzuri na ya upole isiharibiwe.

Ilikuwa jambo gumu kutengana na mtoto wangu. Uso wake mdogo wenye huzuni nilipomwacha ulikuwa mbele yangu mchana na usiku; lakini kwa nguvu za Bwana niliweka mawazo hayo pembeni, na kutafuta kuwafanyia wengine mema.

Kwa miaka mitano familia ya Ndugu Howland ilibeba jukumu lote la kumlea Henry. Walimtunza bila malipo yoyote, wakimpatia mavazi yake yote, isipokuwa zawadi moja niliyokuwa nikimpelekea mara moja kwa mwaka, kama Hana alivyompelekea Samweli.

**Kuponywa kwa Gilbert Collins**

Asubuhi moja mwezi Februari, 1849, wakati wa ibada za familia katika nyumba ya Ndugu Howland, nilionyeshwa kwamba ilikuwa wajibu wetu kwenda Dartmouth, Massachusetts. Muda mfupi baadaye, mume wangu alikwenda posta, na akarudi akiwa na barua kutoka kwa Ndugu Philip Collins, akitusihi twende Dartmouth, kwa sababu mtoto wao wa kiume alikuwa mgonjwa sana. Tulienda mara moja, na tukakuta kwamba mvulana huyo, aliyekuwa na umri wa miaka kumi na mitatu, alikuwa amekuwa mgonjwa kwa muda wa wiki tisa kutokana na kikohozi cha kifaduro, na alikuwa amedhoofika kiasi cha kubaki kama mifupa tu. Wazazi wake walidhani kwamba alikuwa na ugonjwa wa kifua kikuu, na walikuwa na huzuni kubwa wakifikiri kwamba mwana wao wa pekee angechukuliwa kutoka kwao.

Tuliungana katika maombi kwa ajili ya mvulana huyo, na tukamsihi Bwana kwa dhati amwokoe na kifo. Tuliamini kwamba angepona, ingawa kwa mtazamo wa kibinadamu hakukuwa na uwezekano wowote wa kupona kwake. Mume wangu alimwinua mikononi mwake, huku akitembea chumbani akisema kwa sauti: “Hutakufa, bali utaishi!” Tuliamini kwamba Mungu atatukuzwa katika uponyaji wake.

Tuliondoka Dartmouth, na tukawa mbali kwa muda wa karibu siku nane. Tuliporudi, Gilbert mdogo alitoka kutupokea. Alikuwa ameongezeka uzito wa pauni nne. Tulikuta familia yote ikifurahi ndani ya Mungu kwa sababu ya udhihirisho huu wa neema ya Mungu.

**Kuponywa kwa Dada Temple**

Baada ya kupokea ombi la kumtembelea Dada Hastings wa New Ipswich, New Hampshire, ambaye alikuwa akiteseka sana, tuliliweka jambo hilo kuwa mada ya maombi, na tukapata ushahidi kwamba Bwana angeenda pamoja nasi. Tukiwa njiani tulisimama Dorchester, katika familia ya Ndugu Otis Nichols, nao wakatuambia kuhusu mateso ya Dada Temple wa Boston. Kwenye mkono wake alikuwa na kidonda kilichokuwa kikimsumbua sana. Kilikuwa kimeenea hadi sehemu ya kukunja kiwiko. Alikuwa ameteseka kwa maumivu makali sana, na alikuwa ametumia njia za kibinadamu bila kupata msaada wowote. Jaribio la mwisho la matibabu lilikuwa limesababisha ugonjwa huo kuhamia kwenye mapafu yake, na alihisi kwamba kama asingepata msaada wa haraka, ugonjwa huo ungeishia kuwa kifua kikuu.

Dada Temple alikuwa ameacha ujumbe kwamba twende na kumwombea. Tulienda kwa hofu na kutetemeka, kwa kuwa tulikuwa tumetafuta bure uhakikisho kwamba Mungu angefanya kazi kwa ajili yake. Tuliingia katika chumba cha mgonjwa, tukitegemea tu ahadi zilizo wazi za

Mungu. Mkono wa Dada Temple ulikuwa katika hali mbaya kiasi kwamba hatukuweza kuugusa, hivyo tulilazimika kumimina mafuta juu yake. Kisha tuliungana katika maombi, na kudai ahadi za Mungu. Maumivu na uchungu viliondoka kwenye mkono huo wakati tulipokuwa tukiomba, na tulimwacha Dada Temple akifurahi katika Bwana. Tuliporudi baada ya siku nane, tulimkuta akiwa na afya njema, na akifanya kazi kwa bidii kwenye beseni la kufulia.

**Familia ya Leonard Hastings**

Tulikuta familia ya Ndugu Leonard Hastings ikiwa katika huzuni kubwa. Dada Hastings alitupokea akiwa na machozi, akisema: "Bwana amewatuma kwetu wakati wa hitaji kubwa sana." Alikuwa na mtoto mchanga aliyekuwa na umri wa karibu wiki nane, ambaye alikuwa akilia kila mara anapokuwa macho. Hali hii, pamoja na afya yake mbaya sana, ilikuwa ikimaliza nguvu zake haraka.

Tulimwomba Mungu kwa bidii kwa ajili ya mama huyo, tukifuata maagizo yaliyotolewa katika kitabu cha Yakobo, nasi tukapata uhakika kwamba maombi yetu yalisikiwa. Yesu alikuwa katikati yetu ili kuvunja nguvu za Shetani na kumweka huru aliyekuwa amefungwa. Lakini tulikuwa na hakika kwamba mama huyo asingeweza kupata nguvu nyingi mpaka kilio cha mtoto kingekoma. Tulimpaka mtoto mafuta na kumwombea, tukiwa na imani kwamba Bwana angewapa mama na mtoto wote amani na pumziko. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa. Kilio cha mtoto kilikoma, na tuliwaacha wote wawili wakiwa katika hali nzuri. Shukrani za mama huyo hazingeweza kuelezeka kwa maneno.

Mazungumzo yetu na familia hiyo mpendwa yalikuwa ya thamani sana. Mioyo yetu iliunganishwa pamoja; hasa moyo wa Dada Hastings uliunganishwa na wangu, kama vile mioyo ya Daudi na Yonathani ilivyokuwa imeunganishwa. Umoja wetu haukuvunjika wakati wote wa maisha yake.

**Maji ya Uzima—Ndoto**

Mume wangu alihudhuria mikutano huko New Hampshire na Maine. Wakati alipokuwa hayupo, nilikuwa na wasiwasi mwingi, nikiogopa kwamba angepata kipindupindu, ambacho wakati huo kilikuwa kimeenea. Lakini usiku mmoja niliota kwamba wakati watu wengi waliokuwa karibu nasi walikuwa wakifa kutokana na kipindupindu, mume wangu alipendekeza kwamba twende matembezini. Tulipokuwa tukitembea, niliona kwamba macho yake yalikuwa mekundu kama yenye damu, uso wake ulikuwa na wekundu, na midomo yake ilikuwa myeupe. Nilimwambia kwamba niliogopa angekuwa rahisi kushambuliwa na kipindupindu. Akasema: "Tembea mbele kidogo zaidi, nami nitakuonyesha dawa ya uhakika ya kipindupindu."

Tulipoendelea kutembea, tulifika kwenye daraja lililokuwa juu ya kijito cha maji. Ghafla aliacha kunifuata na akaruka ndani ya maji mpaka akapotea machoni. Niliogopa; lakini muda

mfupi baadaye alitokea tena, akiwa ameshika glasi ya maji yaliyokuwa yakimetameta. Akanywa na kusema: “Maji haya huponya kila aina ya magonjwa.” Akaruka tena ndani ya maji na kutoweka machoni, kisha akaleta glasi nyingine ya maji safi na yaliyo wazi, na alipoiinua akarudia maneno yale yale.

Nilihuzunika kwa sababu hakunipa baadhi ya hayo maji. Akasema: “Kuna chemchemi ya siri chini kabisa ya mto huu ambayo huponya kila aina ya magonjwa, na wote wanaopata maji hayo lazima waruke wenyewe kwa imani. Hakuna mtu anayeweza kuyapata kwa ajili ya mwingine. Kila mmoja lazima ajitafutie mwenyewe.” Alipokunywa glasi ya maji, niliutazama uso wake. Rangi ya uso wake ilikuwa nzuri na ya kawaida. Alionekana kuwa na afya na nguvu. Nilipoamka, hofu zangu zote ziliondoka, nami nikamkabidhi mume wangu katika uangalizi wa Mungu mwenye rehema, nikiwa na imani kamili kwamba Mungu angemrudisha kwangu salama.

## 21. MAOMBI NA IMANI

Mara nyingi nimeonyeshwa kwamba watoto wa Bwana hupuuza sana maombi, hasa maombi ya faraghani; kwamba wengi hawatumii imani ile ambayo ni haki yao na wajibu wao kuitumia, mara nyingi wakisubiri hisia zile ambazo imani pekee inaweza kuleta. Hisia si imani; mambo haya mawili ni tofauti. Imani ni yetu kuitumia, lakini hisia za furaha na baraka ni za Mungu kutoa. Neema ya Mungu huja kwa nafsi kupitia njia ya imani hai, na imani hiyo tuna uwezo wa kuitumia.

Imani ya kweli hushikilia na kudai baraka iliyoahidiwa kabla haijadhihirika na kuhisiwa. Tunapaswa kupeleka maombi yetu kwa imani ndani ya pazia la pili, na kuiacha imani yetu ishike baraka iliyoahidiwa, na kuidai kuwa ni yetu. Kisha tunapaswa kuamini kwamba tunapokea baraka hiyo, kwa sababu imani yetu imeishika, na kulingana na neno la Mungu ni yetu. **“Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.” Marko 11:24.** Hapa ndipo ilipo imani, imani tupu, kuamini kwamba tunapokea baraka hiyo hata kabla hatujaiona au kuifurahia. Wakati baraka iliyoahidiwa inapodhihirika na kufurahiwa, imani humezwa. Lakini wengi hudhani kwamba wana imani nyingi wanaposhiriki kwa wingi katika Roho Mtakatifu, na kwamba hawawezi kuwa na imani isipokuwa wahisi nguvu ya Roho. Watu kama hao huchanganya imani na baraka inayokuja kupitia imani.

Wakati hasa wa kutumia imani ni pale tunapohisi tumepungukiwa na Roho. Wakati mawingu mazito ya giza yanapoonekana kuizunguka akili, huo ndio wakati wa kuiacha imani hai ipenye gizani na kuyatawanya mawingu hayo.

Imani ya kweli hutegemea ahadi zilizomo katika Neno la Mungu, na wale tu wanaolitii Neno hilo wanaweza kudai ahadi zake tukufu. "**Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa." Yohana 15:7. "lo lote tuombalo, twalipokea kwake, kwa kuwa twazishika amri zake, na kuyatenda yapendezayo machoni pake." 1 Yohana 3:22.**

Tunapaswa kuwa watu wa maombi ya faraghani sana. Kristo ndiye mzabibu, sisi ni matawi. Na kama tunataka kukua na kustawi, ni lazima daima tuvute utomvu na lishe kutoka kwa Mzabibu ulio Hai; kwa maana tukitengwa na Mzabibu hatuna nguvu.

Nilimuuliza malaika kwa nini hakukuwa na imani na nguvu zaidi katika Israeli. Akasema: "Mmeuachilia mkono wa Bwana mapema mno. Shikeni maombi yenu kwa nguvu mbele ya kiti cha enzi, na mshikilie kwa imani thabiti. Ahadi ni hakika. Aminini kwamba mnayapokea yale mnayoomba, nayo mtakuwa nayo." Kisha nikaonyeshwa habari za Eliya. Alikuwa mwanadamu mwenye hisia kama sisi, naye aliomba kwa bidii. Imani yake ilivumilia jaribu. Mara saba aliomba mbele za Bwana, na hatimaye wingu likaonekana.

Niliona kwamba tulikuwa tumezitilia mashaka ahadi za hakika, na kumuumiza Mwokozi kwa ukosefu wetu wa imani. Malaika akasema: "Vaeni silaha ….zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu." Waefeso 6:16 Ikiwa adui anaweza kuwaongoza waliokata tamaa kuondoa macho yao kutoka kwa Yesu, na kuyaelekeza kwao wenyewe, wakitafakari juu ya kutostahili kwao badala ya kutafakari juu ya kustahili kwa Yesu, upendo Wake, sifa Zake, na rehema Yake kuu, basi ataiondoa ngao ya imani yao, na kufanikisha kusudi lake; wataachwa wazi kwa majaribu yake yenye moto. Kwa hiyo walio dhaifu wanapaswa kumtazama Yesu na kumwamini; ndipo watakapotumia imani.

## 21. KUANZA KUCHAPISHA

Katika mkutano uliofanyika Dorchester, Massachusetts, mwezi Novemba 1848, nilikuwa nimepewa maono kuhusu kutangazwa kwa ujumbe wa kutiwa muhuri, na kuhusu wajibu wa ndugu zetu kuchapisha nuru iliyokuwa ikiangaza katika njia yetu.

Baada ya kutoka katika maono hayo, nilimwambia mume wangu: “Nina ujumbe kwa ajili yako. Unapaswa kuanza kuchapisha karatasi ndogo na kuituma kwa watu. Ianze ikiwa ndogo; lakini watu watakaposoma, watakutumia fedha ambazo zitatumika kuchapisha, na itafanikiwa tangu mwanzo. Kutoka katika mwanzo huu mdogo nilionyeshwa kwamba itakuwa kama vijito vya nuru vinavyozunguka dunia yote.”

Tulipokuwa Connecticut katika majira ya kiangazi ya mwaka 1849, mume wangu alihisi kwa kina kwamba wakati ulikuwa umefika kwake kuandika na kuchapisha ukweli wa sasa. Alitiwa moyo sana na kubarikiwa alipofanya uamuzi huo. Lakini tena alianza kuwa na mashaka na wasiwasi, kwa sababu hakuwa na fedha hata kidogo. Kulikuwa na watu waliokuwa na mali, lakini walichagua kuzihifadhi kwao wenyewe. Hatimaye alikata tamaa, na akaamua kutafuta shamba la nyasi ili akate nyasi apate fedha.

Alipotoka nyumbani, mzigo mzito ulimjia, nami nikazimia. Maombi yalifanyika kwa ajili yangu, nami nikabarikiwa na kuchukuliwa katika maono. Nilionyeshwa kwamba Bwana alikuwa amembariki na kumtia nguvu mume wangu kufanya kazi shambani mwaka mmoja uliopita; kwamba alikuwa ametumia vizuri fedha alizopata huko; na kwamba angepata mara mia katika maisha haya, na kama angekuwa mwaminifu, angepokea thawabu kubwa katika ufalme wa Mungu. Lakini Bwana asingempa tena nguvu za kufanya kazi shambani, kwa maana alikuwa na kazi nyingine kwa ajili yake. Na ikiwa angejaribu kwenda shambani, angeangushwa na ugonjwa;

lakini alipaswa kuandika, kuandika, kuandika, na kuendelea kwa imani. Mara moja alianza kuandika, na alipofikia sehemu ngumu ambayo ilihitaji kueleweka, tuliungana katika maombi kwa Mungu ili tupate ufahamu wa maana halisi ya Neno Lake.

**Gazeti la "Present Truth"**

Siku moja mwezi Julai, mume wangu alirudi nyumbani kutoka Middletown akiwa amebeba nakala elfu moja za toleo la kwanza la gazeti lake. Mara kadhaa, wakati machapisho yalipokuwa yakipangwa kwa ajili ya uchapishaji, alikuwa ametembea kwenda Middletown umbali wa maili nane na kurudi; lakini siku hii alikuwa ameazima farasi na gari la Ndugu Belden ili aweze kuleta karatasi hizo nyumbani.

Karatasi hizo za thamani zilizokuwa zimechapishwa zililetwa ndani ya nyumba na kuwekwa sakafuni. Kisha kikundi kidogo cha watu waliokuwa na shauku kilikusanyika, nasi tukapiga magoti kuzunguka hizo karatasi, kwa mioyo ya unyenyekevu na machozi mengi, tukamsihi Bwana aruhusu baraka Zake ziwe juu ya wajumbe hawa waliochapishwa wa kweli.

Baada ya kukunja karatasi hizo, na mume wangu kufunga na kuandika anwani za nakala kwa wale wote aliodhani wangekuwa tayari kuzisoma, aliziweka katika begi la mkononi na kuzibeba kwa miguu hadi posta ya Middletown.

Katika miezi ya Julai, Agosti, na Septemba, matoleo manne ya gazeti hilo yalichapishwa huko Middletown. Kila toleo lilikuwa na kurasa nane. [Ukubwa wa kila ukurasa ulikuwa karibu inchi sita kwa tisa na nusu.] Kabla ya karatasi hizo kutumwa kwa posta, kila mara ziliwekwa mbele za Bwana, na maombi ya dhati yaliyochanganyika na machozi yalitolewa kwa Mungu, ili baraka Zake ziambatane na wajumbe hao wa kimya wa kweli. Mara tu baada ya kutumwa kwa toleo la kwanza, tulipokea barua zilizokuwa na fedha za kuendeleza uchapishaji wa gazeti hilo, pamoja na habari njema kwamba watu wengi walikuwa wameikubali kweli.

Pamoja na kuanza kazi hii ya uchapishaji, hatukuacha kazi yetu ya kuhubiri kweli. Bali tuliendelea kusafiri kutoka mahali hadi mahali, tukitangaza mafundisho yaliyokuwa yametuletea nuru kubwa na furaha. Tuliwatia moyo waamini, tukasahihisha makosa, na kuweka mambo katika utaratibu kanisani. Ili kuendeleza kazi ya uchapishaji na wakati huohuo kuendelea na kazi yetu katika maeneo mbalimbali, gazeti hilo lilihamishwa mara kwa mara kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

**Ziara ya Maine**

Tarehe 28 Julai, 1849, mtoto wangu wa pili, James Edson White, alizaliwa. Alipokuwa na umri wa wiki sita, tulienda Maine. Tarehe 14 Septemba tulihudhuria mkutano huko Paris. Ndugu Bates, Chamberlain, na Ralph walikuwepo, pamoja na ndugu na dada kutoka Topsham.

Nguvu za Mungu zilishuka kama ilivyokuwa siku ya Pentekoste, na watu watano au sita waliokuwa wamedanganywa na kuongozwa katika makosa na ushupavu wa kidini, walianguka chini kifudifudi. Wazazi waliungama kwa watoto wao, na watoto waliungama kwa wazazi wao na kwa mmoja na mwingine. Ndugu J. N. Andrews alisema kwa hisia kubwa: "Ningebadilishana makosa elfu moja kwa ajili ya ukweli mmoja." Tukio la namna hiyo la kuungama na kumsihi Mungu msamaha tumeliona mara chache sana. Mkutano huo, ambao ulikuwa mwanzo wa siku bora kwa watoto wa Mungu huko Paris, ulikuwa kama sehemu yenye majani mabichi jangwani kwao. Bwana alikuwa akimuandaa Ndugu Andrews kwa ajili ya matumizi makubwa katika siku zijazo, na alikuwa akimpa uzoefu ambao ungekuwa wa thamani kubwa katika huduma yake ya baadaye.

**Kuendelea Kwa Imani**

Katika mkutano uliofanyika huko Topsham, baadhi ya ndugu waliokuwepo walionyesha hamu yao ya kutaka tutembelee tena Jimbo la New York; lakini afya yangu dhaifu ilinilemea moyo wangu. Niliwaambia kwamba sikuweza kuthubutu kwenda isipokuwa Bwana angenitia nguvu kwa ajili ya kazi hiyo. Waliomba kwa ajili yangu, na mawingu ya kukata tamaa yakatawanyika, lakini sikupata nguvu ile niliyotamani sana. Niliamua kuendelea kwa imani na kwenda, nikishikilia ahadi hii: **"Neema yangu yakutosha."**

Katika safari ya kwenda New York, imani yetu ilijaribiwa, lakini tulipata ushindi. Nguvu zangu ziliongezeka, nami niliweza kumshangilia Mungu. Wengi walikuwa wameikubali kweli tangu ziara yetu ya kwanza, lakini kulikuwa na mengi yaliyopaswa kufanywa kwa ajili yao, na nguvu zetu zote zilihitajika katika kazi iliyokuwa ikifunguka mbele yetu.

**Kazi Huko Oswego**

Katika miezi ya Oktoba na Novemba, wakati tulipokuwa tukisafiri, gazeti lilikuwa limesimamishwa kwa muda; lakini mume wangu bado alikuwa na mzigo moyoni wa kuandika na kuchapisha. Tulikodi nyumba huko Oswego, tukakopa samani kutoka kwa ndugu zetu, na tukaanza kuishi kama familia. Huko mume wangu aliandika, akachapisha, na kuhubiri.

## 23. KUTEMBELEA NDUGU WAUMINI

Tulipokuwa Oswego, New York, mwanzoni mwa mwaka 1850, tuliombwa kutembelea Camden, mji uliokuwa karibu maili arobaini upande wa mashariki. Kabla ya kwenda huko, nilionyeshwa kikundi kidogo cha waumini waliokuwa mahali pale. Miongoni mwao nilimwona mwanamke mmoja aliyedai kuwa na uchaji mwingi wa Mungu, lakini alikuwa mnafiki na alikuwa akiwadanganya watu wa Mungu.

### Mkutano wa Camden

Asubuhi ya Sabato, watu kadhaa walikusanyika kwa ajili ya ibada, lakini yule mwanamke mdanganyifu hakuwepo. Nilimuuliza dada mmoja kama hao ndio waumini wote waliokuwa katika eneo hilo. Akasema ndiyo. Yule mwanamke ambaye nilikuwa nimemwona katika maono aliishi maili nne kutoka mahali hapo, na yule dada hakumfikiria kabisa. Lakini muda mfupi baadaye aliingia, nami mara moja nilimtambua kuwa ndiye yule mwanamke ambaye Bwana alikuwa amenionyesha tabia yake halisi.

Wakati wa mkutano, alizungumza kwa muda mrefu sana, akisema kwamba alikuwa na upendo mkamilifu, kwamba alikuwa na utakatifu moyoni, kwamba hakuwa na majaribu wala vishawishi, bali alikuwa na amani kamili na kujisalimisha kikamilifu kwa mapenzi ya Mungu.

Baada ya mkutano nilirudi nyumbani kwa Ndugu Preston nikiwa na huzuni kubwa moyoni. Usiku huo niliota ndoto kwamba chumba cha siri kilichokuwa kimejaa takataka kilifunguliwa mbele yangu, nami nikaambiwa kwamba kazi yangu ilikuwa kukisafisha. Kwa mwanga wa taa niliondoa takataka hizo, na nikawaambia wale waliokuwa pamoja nami kwamba chumba hicho kingeweza kujazwa tena na vitu vya thamani zaidi.

Jumapili asubuhi tulikutana na ndugu waumini. Mume wangu alisimama ili kuhubiri juu ya mfano wa wanawali kumi. Hakupata uhuru wa kuzungumza, hivyo akapendekeza tufanye

muda wa maombi. Tukapiga magoti mbele za Bwana na kuomba kwa bidii. Wingu la giza likaondolewa, nami nikachukuliwa katika maono. Tena nilionyeshwa hali ya mwanamke huyu. Alionyeshwa kwangu akiwa katika giza kamili. Yesu alimkunjia uso wake wa kukasirika yeye na mume wake. Uso huo wa kukemea na kuhuzunisha ulinifanya nitetemeke. Niliona kwamba alikuwa ametenda kama mnafiki, akidai utakatifu huku moyo wake ukiwa umejaa uchafu.

Baada ya kutoka katika maono, nilisimulia kwa kutetemeka, lakini kwa uaminifu, kile nilichoonyeshwa. Yule mwanamke alisema kwa utulivu: "Ninafurahi kwamba Bwana anaujua moyo wangu. Anajua kwamba ninampenda. Kama moyo wangu ungeweza kufunguliwa ili muuone, mngeona kwamba ni safi na umetakasika."

Mawazo ya baadhi ya watu yalichanganyikiwa. Hawakujua kama waumini kile ambacho Bwana alikuwa amenionyesha, au kuruhusu mwonekano wa nje uzidi ushuhuda nilioutoa.

Muda mfupi baada ya hapo, hofu kubwa ilimshika yule mwanamke. Hofu ya kutisha ilimjia, naye akaanza kuungama. Hata aliende nyumba kwa nyumba kwa majirani zake ambao hawakuamini, na akaungama kwamba yule mwanaume aliyekuwa akiishi naye kwa miaka mingi hakuwa mume wake; kwamba alikuwa amekimbia kutoka Uingereza, akamwacha mume mwema na mtoto mmoja. Aliungama matendo mengine mengi mabaya aliyokuwa ameyafanya. Toba yake ilionekana kuwa ya kweli, na katika baadhi ya mambo alirudisha vitu alivyokuwa amevichukua kwa njia isiyo halali.

Matokeo ya tukio hili yalikuwa kwamba ndugu na dada wa Camden, pamoja na majirani zao, waliimarishwa kikamilifu katika imani kwamba Mungu alikuwa amenifunulia mambo niliyosema, na kwamba ujumbe huo ulipewa kwao kwa rehema na upendo, ili kuwaokoa kutoka katika udanganyifu na makosa hatari.

**Huko Vermont**

Katika majira ya kuchipua ya mwaka 1850, tuliamua kutembelea Vermont na Maine. Nilimwacha mtoto wangu mdogo Edson, aliyekuwa na umri wa miezi tisa wakati huo, chini ya uangalizi wa Dada Bonfoey, huku sisi tukiendelea na safari yetu ili kufanya mapenzi ya Mungu. Tulifanya kazi kwa bidii sana, tukivumilia shida nyingi ili kufanikisha mambo machache tu. Tuliwakuta ndugu na dada waumini wakiwa wametawanyika na katika hali ya kuchanganyikiwa. Karibu kila mmoja alikuwa ameathiriwa na kosa fulani, na wote walionekana kuwa na bidii kwa ajili ya mawazo yao wenyewe. Mara nyingi tuliteseka kwa uchungu mkubwa wa moyo tulipokutana na watu wachache sana waliokuwa tayari kusikiliza kweli ya Biblia, huku kwa shauku wakishikilia makosa na ushupavu wa kidini. Tulilazimika kufanya safari ngumu ya maili arobaini kwa gari la abiria (*stagecoach*) ili kufika Sutton, mahali ambapo tulikuwa tumepangiwa mkutano.

**Kushinda Kukata Tamaa**

Usiku wa kwanza baada ya kufika mahali pa mkutano, nililemewa na hali ya kukata tamaa. Nilijaribu kuishinda, lakini ilionekana kuwa haiwezekani kudhibiti mawazo yangu. Watoto wangu wadogo walikuwa mzigo moyoni mwangu. Tulikuwa tumemwacha mmoja katika Jimbo la Maine akiwa na umri wa miaka miwili na miezi minane, na mtoto mwingine huko New York akiwa na umri wa miezi tisa. Tulikuwa tumetoka kufanya safari ngumu yenye mateso mengi, nami nikawaza juu ya wale waliokuwa wakifurahia ushirika wa watoto wao katika nyumba zao tulivu. Nilitafakari maisha yetu ya zamani, nikikumbuka maneno yaliyosemwa na dada mmoja siku chache kabla, ambaye alifikiri kwamba lazima ilikuwa jambo la kufurahisha sana kusafiri kupitia nchi bila kuwa na chochote cha kunisumbua. Alifikiri huo ndio ungekuwa maisha ambayo angefurahia. Lakini wakati huo huo moyo wangu ulikuwa ukiwatamani sana watoto wangu, hasa mtoto wangu mdogo aliyekuwa New York. Nilikuwa nimetoka katika chumba changu cha kulala, ambako nilikuwa nikipambana na hisia zangu, na kwa machozi mengi nilikuwa nimemsihi Bwana anipe nguvu ya kushinda kila kunung'unika na kwamba niweze kujikana nafsi kwa furaha kwa ajili ya Kristo. Katika hali hiyo ya moyo nililala, nami nikaota kwamba malaika mrefu alisimama karibu nami na kuniuliza kwa nini nilikuwa na huzuni. Nilimweleza mawazo yaliyokuwa yamenisumbua, nikasema: "Ninaweza kufanya mema machache sana; kwa nini tusikae pamoja na watoto wetu na kufurahia ushirika wao?" Akasema: **"**Umemtolea Bwana maua mawili mazuri, ambayo harufu yake ni kama uvumba mtakatifu mbele Zake, na ni ya thamani zaidi machoni Pake kuliko dhahabu au fedha, kwa maana ni zawadi ya moyo. Yanagusa kila nyuzi ya moyo kama hakuna dhabihu nyingine inavyoweza kufanya. Usitazame hali ya sasa tu, bali elekeza macho yako kwa wajibu wako, kwa utukufu wa Mungu, na ufuate katika uongozi Wake unaofunguka mbele yako; njia itazidi kung'aa. Kila kujikana nafsi, kila dhabihu, imeandikwa kwa uaminifu, na italeta thawabu yake."

**Kazi Huko Kanada**

Baraka za Bwana ziliambatana na mkutano wetu huko Sutton. Baada ya mkutano huo kumalizika, tuliendelea na safari yetu kuelekea Kanada Mashariki (*Canada East*). Koo langu lilinisumbua sana, na sikuweza kuzungumza kwa sauti kubwa, wala hata kunong'ona, bila kupata maumivu. Tulikuwa tukisafiri huku tukiomba ili tupate nguvu ya kuvumilia safari hiyo.

Hivyo tuliendelea mpaka tulipofika Melbourne. Tulitarajia kukutana na upinzani huko. Wengi waliodai kuamini katika ujio wa karibu wa Mwokozi wetu walipinga sheria ya Mungu. Tulihisi hitaji kubwa la nguvu kutoka kwa Mungu. Tuliomba kwamba Bwana ajidhihirishe kwetu. Ombi langu la dhati lilikuwa kwamba ugonjwa huo uondoke kooni mwangu na kwamba sauti yangu irudishwe. Nilipata ushahidi kwamba mkono wa Bwana ulinigusa mahali pale. Tatizo hilo liliondolewa mara moja, na sauti yangu ikawa wazi tena. Mshumaa wa Bwana

uliangaza juu yetu katika mkutano huo, nasi tulifurahia uhuru mkubwa katika Roho. Watoto wa Mungu waliimarishwa sana na kutiwa moyo.

**Mkutano Huko Johnson**

Muda mfupi baadaye tulirudi Vermont, na tukafanya mkutano wa pekee huko Johnson. Njiani tulisimama kwa siku kadhaa katika nyumba ya Ndugu E. P. Butler. Tuligundua kwamba yeye na baadhi ya ndugu zetu wa kaskazini mwa Vermont walikuwa wamechanganyikiwa sana na kujaribiwa kwa sababu ya mafundisho ya uongo na ushupavu wa kidini uliokithiri wa kikundi cha watu waliodai kuwa na utakaso kamili. Chini ya kivuli cha utakatifu mkubwa, watu hao walikuwa wakifuata mwenendo wa maisha uliokuwa aibu kwa jina la Kikristo.

Wanaume wawili waliokuwa viongozi wa ushupavu huo walikuwa katika maisha na tabia zao karibu sawa na wale tuliokutana nao miaka minne iliyopita huko Claremont, New Hampshire. Walifundisha fundisho la utakaso uliopitiliza, wakidai kwamba hawawezi kutenda dhambi na kwamba walikuwa tayari kwa ajili ya kunyakuliwa kwenda mbinguni. Walitumia ushawishi wa kishetani unaoteka akili (ushawishi wa akili unaodaiwa kuwa na nguvu za kiroho), na walidai kupokea nuru ya kimungu wakiwa katika hali fulani kama ya usingizi mzito au mawazo yaliyotenganishwa na hali ya kawaida (*trance*).

Hawakujishughulisha na kazi ya kawaida, bali pamoja na wanawake wawili ambao hawakuwa wake zao, walizunguka kutoka sehemu moja hadi nyingine, wakijilazimisha kupokelewa na watu na kupewa ukarimu. Kwa njia ya ushawishi wao wa siri wa ushawishi wa kishetani unaoteka akili, walikuwa wamepata kiwango kikubwa cha huruma na uungwaji mkono kutoka kwa baadhi ya watoto waliokuwa wamekua wa ndugu zetu waumini.

Ndugu Butler alikuwa mtu mwenye uadilifu wa nguvu. Alikuwa ameamshwa kabisa kuona ushawishi mbaya wa nadharia hizo za ushupavu, na alikuwa akipinga kwa bidii mafundisho yao ya uongo na madai yao ya kiburi. Zaidi ya hayo, alituweka wazi kwamba hakuwa na imani katika maono ya aina yoyote.

Kwa kusitasita kidogo, Ndugu Butler alikubali kuhudhuria mkutano uliokuwa nyumbani kwa Ndugu Lovejoy huko Johnson. Wale wanaume wawili waliokuwa viongozi wa ushupavu huo, ambao walikuwa wamewadanganya sana na kuwatesa watoto wa Mungu, walifika kwenye mkutano huo wakiwa wameandamana na wale wanawake wawili waliovaa mavazi meupe ya kitani, huku nywele zao ndefu nyeusi zikiwa zimetandazwa mabegani mwao. Mavazi hayo meupe ya kitani yalidaiwa kuwakilisha **haki ya watakatifu**.

Nilikuwa na ujumbe wa kukemea kwa ajili yao. Nilipokuwa nikizungumza, yule wa kwanza kati ya wale wanaume wawili aliendelea kunitazama kwa makini, kama vile wafanyavyo watu wanaotumia ushawishi wa kishetani unaoteka akili. Lakini sikuwa na hofu ya ushawishi

wake wa ushawishi wa kishetani unaoteka akili. Nguvu kutoka mbinguni ilikuja ili kutawala nguvu zao za kishetani. Watoto wa Mungu waliokuwa wameshikiliwa katika utumwa wa udanganyifu huo walianza kupumua kwa uhuru na kumshangilia Bwana.

Kadiri mkutano ulivyoendelea, wale washupavu walijaribu kusimama na kuzungumza, lakini hawakupewa nafasi. Walielezwa wazi kwamba uwepo wao haukutakiwa, lakini waliamua kubaki. Ndipo Ndugu Samuel Rhodes akashika sehemu ya nyuma ya kiti alichokuwa amekalia mmoja wa wale wanawake, akamvuta kutoka chumbani na kumpeleka kupitia barazani hadi kwenye nyasi nje. Aliporudi kwenye chumba cha mkutano, alimtoa mwanamke mwingine kwa namna hiyo hiyo. Wale wanaume wawili waliondoka chumbani, lakini walijaribu kurudi tena.

Wakati maombi yalipokuwa yakitolewa mwishoni mwa mkutano, yule mwanaume wa pili alifika mlangoni na kuanza kuzungumza. Mlango ulifungwa mbele yake. Akaufungua mlango tena na kuanza kuzungumza. Ndipo nguvu ya Mungu ikamshukia mume wangu. Rangi iliondoka usoni mwake alipoinuka kutoka kwenye magoti yake. Aliinua mikono yake mbele ya yule mwanaume, akisema: "Bwana hataki ushuhuda wako hapa. Bwana hataki uwepo wako hapa ili kuwavuruga na kuwaangusha watu Wake."

Nguvu ya Mungu iliijaza nyumba ile. Yule mwanaume alionekana kuogopa sana, akarudi nyuma kwa hofu kupitia ukumbi hadi chumba kingine. Alivuka chumba hicho huku akiyumba-yumba, akagonga ukuta, kisha akapata usawa wake na kutafuta mlango wa kutoka nje ya nyumba. Uwepo wa Bwana, ambao ulikuwa wenye uchungu kwa wale wenye dhambi waliokuwa katika ushupavu huo, uliwagusa wale waliokusanyika kwa heshima kubwa na hofu takatifu. Lakini baada ya watoto wa giza kuondoka, amani tamu kutoka kwa Bwana ilitulia juu ya kikundi chetu. Baada ya mkutano huo, wale waliodai kwa uongo na hila kuwa na utakatifu mkamilifu hawakuweza tena kurejesha nguvu zao juu ya ndugu zetu.

Uzoefu wa mkutano huu ulitupatia uaminifu na ushirika wa Ndugu Butler.

## 24. KUCHAPISHA TENA

Kutoka Oswego tulienda Centerport, pamoja na Ndugu na Dada Edson, na tukafanya makao yetu nyumbani kwa Ndugu Harris, ambako tulichapisha jarida la kila mwezi lililoitwa **Advent Review**.

### Review and Herald

Mnamo Novemba 1850, gazeti hilo lilianza kuchapishwa huko Paris, Maine. Huko lilipanuliwa, na jina lake likabadilishwa na kuwa lile linalojulikana hadi leo, **Advent Review and Sabbath Herald**. Tulikaa nyumbani kwa familia ya Ndugu A. Tulikuwa tayari kuishi kwa gharama ndogo ili gazeti liweze kuendelea. Marafiki wa kazi ya Mungu walikuwa wachache kwa idadi na maskini kwa mali za dunia, na bado tulilazimika kupambana na umaskini na kukata tamaa kukubwa. Tulikuwa na mizigo mingi ya mawazo, na mara nyingi tulikesha hadi saa sita za usiku, na wakati mwingine hadi saa nane au saa tisa za usiku, tukisahihisha kurasa za uchapishaji.

Kazi nyingi kupita kiasi, wasiwasi na mahangaiko, ukosefu wa chakula cha kutosha na chenye lishe, pamoja na kukabiliwa na baridi wakati wa safari zetu ndefu za majira ya baridi, vilikuwa mzigo mkubwa mno kwa mume wangu, naye akaanguka chini ya uzito huo. Alidhoofika sana hata hakuweza kutembea kwa urahisi kwenda kwenye ofisi ya uchapishaji. Imani yetu ilijaribiwa kwa kiwango cha juu kabisa. Kwa hiari tulivumilia upungufu, kazi ngumu, na mateso; lakini nia zetu zilieleweka vibaya, na tulitazamwa kwa mashaka na wivu. Wachache sana kati ya wale ambao tuliteseka kwa ajili ya manufaa yao walionekana kuthamini juhudi zetu.

Tulikuwa na huzuni nyingi kiasi kwamba hatukuweza kulala wala kupumzika. Saa ambazo zilipaswa kutupatia usingizi wa kutuburudisha mara nyingi zilitumika kujibu barua ndefu zilizosababishwa na wivu. Kwa saa nyingi, wakati wengine walipokuwa wamelala, tulikuwa tukimwaga machozi ya uchungu na kuomboleza mbele za Bwana. Hatimaye mume wangu alisema: “Mke wangu, hakuna maana ya kuendelea kujitahidi tena. Mambo haya yananivunja moyo, na hivi karibuni yatanipeleka kaburini. Siwezi kuendelea mbele. Nimeandika taarifa kwa

ajili ya gazeti, nikisema kwamba sitachapisha tena." Alipokuwa akitoka mlangoni kwenda kuipeleka taarifa hiyo kwenye ofisi ya uchapishaji, nilizimia. Alirudi ndani na kuniombea. Bwana akajibu maombi yake, nami nikapata nafuu.

Asubuhi iliyofuata, tulipokuwa katika ibada ya familia, nilichukuliwa katika maono na nikapewa maelekezo kuhusu mambo haya. Niliona kwamba mume wangu hakupaswa kuacha kuchapisha gazeti, kwa maana Shetani alikuwa akijaribu kumshawishi achukue hatua hiyo hasa, akifanya kazi kupitia kwa vyombo vyake ili afanye hivyo. Nilionyeshwa kwamba tulipaswa kuendelea kuchapisha, na kwamba Bwana angetutegemeza.

Muda mfupi baadaye tulipokea mialiko ya dharura ya kuhudhuria mikutano katika majimbo mbalimbali, nasi tukaamua kuhudhuria mikutano mikuu iliyofanyika Boston, Massachusetts; Rocky Hill, Connecticut; Camden na West Milton, New York. Mikutano hiyo yote ilikuwa ya kazi nyingi na juhudi kubwa, lakini ilikuwa ya manufaa makubwa kwa ndugu na dada wetu waliokuwa wametawanyika.

**Kuhamia Saratoga Springs**

Tulikaa Ballston Spa kwa majuma kadhaa, mpaka tulipofikia uamuzi wa kuchapisha huko Saratoga Springs. Kisha tukapangisha nyumba na kuwatumia ujumbe Ndugu na Dada Stephen Belden, pamoja na Dada Bonfoey, ambaye wakati huo alikuwa Maine akimtunza Edson mdogo. Kwa kutumia vyombo na samani za nyumbani tulizokopa, tukaanza kuishi katika nyumba yetu. Hapo mume wangu alichapisha juzuu ya pili ya *Advent Review and Sabbath Herald*.

Dada Annie Smith, ambaye sasa amelala katika Yesu, alikuja kuishi nasi ili atusaidie katika kazi. Msaada wake ulihitajika sana. Mume wangu alieleza hisia zake wakati huo katika barua aliyomwandikia Ndugu Howland, yenye tarehe Februari 14, 1852, akisema:

"Sote tunaendelea vizuri isivyo kawaida, isipokuwa mimi. Siwezi kuendelea kwa muda mrefu kuvumilia taabu za kusafiri na wajibu wa kazi ya uchapishaji. Jumatano usiku tulifanya kazi hadi saa nane za usiku, tukikunja na kufunga nakala ya 12 ya *Review and Herald*; kisha nikaenda kulala, lakini nikakohoa mpaka kulipopambazuka. Niombeeni. Kazi ya Mungu inaendelea kwa mafanikio makubwa sana. Huenda Bwana hatahitaji huduma yangu kwa muda mrefu zaidi, na ataniruhusu nipumzike kaburini. Ninatumaini kuachana na kazi ya gazeti hili. Nimesimama nalo wakati wa dhiki kuu sana; na sasa, wakati marafiki wake wamekuwa wengi, ninahisi niko huru kuliacha, ikiwa atapatikana mtu wa kulichukua. Ninatumaini njia yangu itafanywa wazi. Bwana na aongoze."

**Katika Rochester, New York**

Mnamo Aprili, 1852, tulihamia Rochester, New York, katika mazingira yaliyokuwa ya kukatisha tamaa sana. Katika kila hatua tulilazimika kusonga mbele kwa imani. Tulikuwa bado tumedhoofishwa na umaskini, na tulilazimika kuishi kwa kubana matumizi kwa kiwango cha juu sana na kujinyima mambo mengi. Nitatoa sehemu fupi ya barua niliyoiandikia familia ya Ndugu Howland, yenye tarehe Aprili 16, 1852:

"Ndiyo kwanza tunamalizia kupanga makazi yetu hapa Rochester. Tumepangisha nyumba kuukuu kwa dola mia moja sabini na tano kwa mwaka. Mashine ya uchapishaji iko ndani ya nyumba hiyo. Isingekuwa hivyo, tungelazimika kulipa dola hamsini kwa mwaka kwa ajili ya chumba cha ofisi. Mngelitabasamu kama mngeliweza kututembelea na kuona samani zetu. Tumenunua vitanda viwili vya zamani kwa senti ishirini na tano kila kimoja. Mume wangu aliniletea viti sita vya zamani, ambavyo hakuna hata viwili vilivyofanana, kwa gharama ya dola moja. Muda mfupi baadaye aliniletea tena viti vingine vinne vya zamani visivyokuwa na sehemu ya kukalia, ambavyo alivinunua kwa senti sitini na mbili. Miundo yake ilikuwa imara, nami nikavifuma upya sehemu za kukalia kwa kitambaa kizito. Siagi ni ghali sana kiasi kwamba hatuinunui, wala hatuwezi kumudu kununua viazi. Badala ya siagi tunatumia mchuzi, na badala ya viazi tunatumia turnipu. Milo yetu ya kwanza tuliila juu ya ubao uliowekwa juu ya mapipa mawili matupu ya unga. Tuko tayari kuvumilia upungufu na kujinyima ikiwa kazi ya Mungu inaweza kuendelezwa. Tunaamini kwamba mkono wa Bwana ulituongoza kuja mahali hapa. Hapa kuna uwanja mpana wa kazi, lakini watendakazi ni wachache. Sabato iliyopita mkutano wetu ulikuwa wa baraka nyingi. Bwana alituburudisha kwa uwepo Wake."

**Kusonga Mbele kwa Uthabiti**

Tuliendelea kufanya kazi kwa bidii huko Rochester katikati ya mashaka mengi na hali za kuvunja moyo. Kipindupindu kiliikumba mji huo, na wakati ugonjwa huo ulipokuwa ukienea, usiku kucha magari yaliyobeba maiti yalisikika yakiguruma barabarani yakielekea kwenye Makaburi ya Mount Hope. Ugonjwa huu haukuwaua maskini pekee, bali uliwachukua watu wa kila tabaka la jamii. Hata madaktari stadi walipatwa nao, wakaangushwa na ugonjwa huo, na kupelekwa katika Makaburi ya Mount Hope. Tulipokuwa tukipita katika mitaa ya Rochester, karibu kila kona tulikutana na magari yaliyobeba majeneza mepesi ya mbao za msonobari yaliyokuwa tayari kwa ajili ya kuwahifadhi wafu.

Edson wetu mdogo aliugua ugonjwa huo, nasi tukampeleka kwa Tabibu Mkuu. Nikambeba mikononi mwangu, na kwa jina la Yesu nikaukemea ugonjwa huo. Mara akapata nafuu, na dada mmoja alipoanza kumwomba Bwana amponye, yule mtoto wa miaka mitatu akatazama juu kwa mshangao, akasema, "Hawana haja ya kuendelea kuomba, kwa maana Bwana ameniponya." Alikuwa dhaifu sana, lakini ugonjwa haukuendelea tena. Hata hivyo, hakupata nguvu. Imani yetu ilikuwa bado inapaswa kujaribiwa. Kwa muda wa siku tatu hakula chochote.

**Kuandika na Kusafiri**

Tulikuwa tumepanga mikutano ya muda wa miezi miwili, kuanzia Rochester, New York, hadi Bangor, Maine; na safari hiyo tulipaswa kuifanya kwa gari letu la farasi lililokuwa na kifuniko, likivutwa na farasi wetu mzuri aitwaye Charlie, ambaye tulipewa na ndugu huko Vermont. Hatukuthubutu kumwacha mtoto akiwa katika hali hiyo ya hatari, lakini tuliamua kusafiri isipokuwa hali yake ingebadilika na kuwa mbaya zaidi. Ndani ya siku mbili tulipaswa kuanza safari yetu ili tufike kwenye mkutano wetu wa kwanza. Tuliweka jambo hilo mbele za Bwana, tukichukua kuwa ishara kwamba ikiwa mtoto angepata hamu ya kula, tungeendelea na safari. Siku ya kwanza hakukuwa na nafuu yoyote. Hakuweza kula hata chakula kidogo. Siku iliyofuata, yapata adhuhuri, aliomba supu, nayo ikampa nguvu.

Tulianza safari yetu alasiri hiyo. Yapata saa kumi jioni nilimbeba mtoto wangu mgonjwa juu ya mto, nasi tukasafiri maili ishirini. Usiku huo alionekana mwenye wasiwasi mwingi. Hakuweza kulala, nami nikamshika mikononi mwangu karibu usiku kucha.

Asubuhi iliyofuata tulishauriana ikiwa turudi Rochester au tuendelee na safari. Familia iliyokuwa imetukaribisha ilisema kwamba tukisonga mbele, tungezika mtoto njiani; na kwa jinsi ilivyoonekana, ndivyo ingekuwa. Lakini sikuthubutu kurudi Rochester. Tuliamini kwamba ugonjwa wa mtoto ulikuwa kazi ya Shetani, ili kutuzuia tusisafiri; nasi hatukuthubutu kumkubalia. Nikamwambia mume wangu, "Tukirudi, ninatarajia mtoto atakufa. Akienda mbele anaweza kufa pia. Na tuendelee na safari yetu, tukimtumaini Bwana."

Mbele yetu kulikuwa na safari yapata maili mia moja, ambayo ilitupasa kuikamilisha kwa siku mbili; hata hivyo tuliamini kwamba Bwana angefanya kazi kwa ajili yetu katika wakati huu wa dhiki kuu. Nilikuwa nimechoka sana, na niliogopa kwamba ningepitiwa na usingizi na kumwangusha mtoto kutoka mikononi mwangu; kwa hiyo nikamweka mapajani mwangu, nikamfunga kiunoni kwangu, nasi sote wawili tukalala kwa sehemu kubwa ya safari ya siku hiyo. Mtoto akaanza kupata nafuu na kuendelea kupata nguvu katika safari yote, nasi tukamrudisha nyumbani akiwa amepona vizuri.

Bwana alitubariki sana katika safari yetu ya Vermont. Mume wangu alikuwa na majukumu mengi na kazi nyingi. Katika mikutano mbalimbali alifanya sehemu kubwa ya mahubiri, akauza vitabu, na kufanya kazi ya kuongeza usambazaji wa gazeti. Mkutano mmoja ulipokwisha, tuliharakisha kwenda mwingine. Wakati wa adhuhuri tulimlisha farasi kando ya barabara na kula chakula chetu cha mchana. Kisha mume wangu, akiweka karatasi yake ya kuandikia juu ya kifuniko cha sanduku letu la chakula au juu ya kofia yake, aliandika makala kwa ajili ya *Review* na *Instructor*.

Katika majira ya kiangazi ya mwaka 1853 tulifanya ziara yetu ya kwanza huko Michigan. Muda mfupi baada ya kurudi Rochester, New York, mume wangu alianza kuandika kitabu cha

*Signs of the Times*. Alikuwa bado dhaifu, na aliweza kulala kwa shida sana, lakini Bwana alikuwa msaada wake. Wakati mawazo yake yalipokuwa yamevurugika na mwili wake ukiteseka, tulipiga magoti mbele za Mungu, na katika dhiki yetu tukamlilia. Alisikia maombi yetu ya bidii, na mara nyingi alimbariki mume wangu kiasi kwamba, akiwa na moyo ulioburudishwa, aliendelea na kazi. Mara nyingi kwa siku tulikwenda mbele za Bwana kwa maombi ya dhati. Kitabu hicho hakikuandikwa kwa nguvu zake mwenyewe.

**Ziara Huko Michigan na Wisconsin**

Katika majira ya kuchipua ya mwaka 1854 tulitembelea Michigan tena; na ingawa tulilazimika kupita katika njia zilizotengenezwa kwa magogo na kwenye matope mazito, nguvu zangu hazikupungua. Tulihisi kwamba Bwana alitaka tutembelee Wisconsin, nasi tukapanga kupanda treni huko Jackson usiku wa manane. Tulipokuwa tukijiandaa kupanda treni, tulihisi uzito mkubwa moyoni, tukapendekeza tuwe na wakati wa maombi; na tulipojikabidhi kwa Mungu, hatukuweza kujizuia kulia. Tulienda kituoni tukiwa na hisia za uchaji mkuu. Tulipopanda treni, tuliingia katika behewa la mbele lililokuwa na viti vyenye migongo mirefu, tukitumaini kwamba tungeweza kulala kidogo usiku huo. Behewa hilo lilikuwa limejaa, kwa hiyo tukarudi nyuma na kuingia kwenye behewa lililofuata, ambako tulipata viti. Sikuvua kofia yangu, kama nilivyokuwa nikifanya mara nyingi niliposafiri usiku, bali nilishika mkoba wangu wa mkononi, kana kwamba nilikuwa nikingoja jambo fulani. Sote wawili tulizungumza kuhusu hisia zetu za ajabu.

Treni ilikuwa imesafiri yapata maili tatu kutoka Jackson wakati mwendo wake ulipokuwa wa kutikisika sana, ukivuta mbele na nyuma kwa nguvu, na hatimaye ikasimama. Nikafungua dirisha, nikaona behewa moja limeinuliwa karibu wima. Nikasikia vilio vya maumivu, na kukawa na vurugu nyingi. Injini ilikuwa imetoka kwenye reli, lakini behewa tulilokuwa ndani yake lilikuwa bado kwenye reli, na lilikuwa limetenganishwa yapata futi mia moja kutoka kwa yale yaliyokuwa mbele yake. Kiunganishi hakikuwa kimekatika, lakini behewa letu lilikuwa limetenganishwa na lile lililokuwa mbele yake, kana kwamba malaika alikuwa amelitengeza hivyo. Behewa la mizigo halikuharibika sana, na sanduku letu kubwa la vitabu halikupata uharibifu wowote. Behewa la daraja la pili lilivunjika vibaya, na vipande vyake pamoja na abiria vilitupwa pande zote mbili za reli. Behewa ambalo hapo kwanza tulikuwa tumetaka kupata nafasi ndani yake liliharibika sana, na upande mmoja wake uliinuliwa juu ya lundo la mabaki. Watu wanne walikufa au walijeruhiwa vibaya kiasi cha kufa, na wengi walijeruhiwa sana. Hatukuweza kujizuia kuhisi kwamba Mungu alikuwa ametuma malaika kulinda maisha yetu.

Tulirudi nyumbani kwa Ndugu Cyrenius Smith, karibu na Jackson, na siku iliyofuata tukapanda treni kuelekea Wisconsin. Ziara yetu katika jimbo hilo ilibarikiwa na Mungu. Watu wengi walimgeukia Kristo kutokana na juhudi zetu. Bwana alinipa nguvu za kustahimili safari hiyo ndefu na ya kuchosha.

**Kurudi Rochester**

Tulirudi kutoka Wisconsin tukiwa tumechoka sana, tukitamani kupata mapumziko, lakini tulihuzunika tulipomkuta Dada Anna akiwa mgonjwa. Ugonjwa ulikuwa umemshika sana, na alikuwa amedhoofika mno. Majaribu yalizidi kutuzunguka. Tulikuwa na majukumu mengi ya kutuhangaisha. Wafanyakazi wa ofisi walikuwa wakila na kukaa nyumbani kwetu, na watu wa nyumbani kwetu walikuwa kati ya kumi na watano hadi ishirini. Mikutano mikubwa na mikutano ya Sabato ilifanyika nyumbani kwetu. Hatukuwa na Sabato za utulivu; kwa maana baadhi ya akina dada walikuwa wakikaa siku nzima pamoja nasi, wakiwa na watoto wao. Kwa ujumla ndugu na dada zetu hawakutambua usumbufu, kazi ya ziada, na gharama walizotuletea. Kadiri mmoja baada ya mwingine wa wafanyakazi wa ofisi walivyokuwa wakirudi nyumbani wakiwa wagonjwa, wakihitaji uangalizi wa pekee, niliogopa kwamba tungezidiwa na wasiwasi na mzigo wa majukumu. Mara nyingi nilifikiri kwamba hatungeweza kuvumilia zaidi; hata hivyo majaribu yaliendelea kuongezeka, na kwa mshangao niligundua kwamba hatukushindwa nayo. Tulijifunza somo kwamba tuliweza kustahimili mateso na majaribu mengi zaidi kuliko tulivyowahi kufikiri. Jicho la uangalizi la Bwana lilikuwa juu yetu, ili kuhakikisha kwamba hatuangamizwi.

Mnamo Agosti 29, 1854, jukumu jingine liliongezwa katika familia yetu kwa kuzaliwa kwa Willie. Hilo liliondoa mawazo yangu kwa kiasi fulani kutoka katika taabu zilizokuwa zimetuzunguka. Karibu na wakati huo tulipokea toleo la kwanza la gazeti lililoitwa kwa uongo *Messenger of Truth* ("Mjumbe wa Kweli"). Wale waliokuwa wakitusingizia kupitia gazeti hilo walikuwa wamekemewa kwa makosa na upotovu wao. Hawakukubali kukemewa; kwanza kwa siri, na baadaye waziwazi, walitumia ushawishi wao dhidi yetu.

Bwana alikuwa amenionyesha tabia ya kundi hilo na mwisho wake; kwamba chukizo Lake lilikuwa juu ya wale waliokuwa wameunganishwa na gazeti hilo, na kwamba mkono Wake ulikuwa dhidi yao. Ingawa kwa muda fulani wangeonekana kufanikiwa, na watu wengine waaminifu wangedanganywa, hata hivyo kweli hatimaye ingeshinda. Kila mtu mwaminifu angejitenga na udanganyifu uliokuwa umemshikilia, na kutoka akiwa huru kutokana na ushawishi wa watu hao waovu; kwa kuwa mkono wa Mungu ulikuwa dhidi yao, ilikuwa lazima waanguke.

## 25. KUHAMIA MICHIGAN

Mwaka **1855**, ndugu wa Michigan walifungua njia ili kazi ya uchapishaji ihamishiwe **Battle Creek**. Wakati huo mume wangu alikuwa anadai kati ya dola elfu mbili na elfu tatu; na kila kitu alichokuwa nacho, mbali na kiasi kidogo cha vitabu, kilikuwa ni madeni ya vitabu yaliyokuwa yanapaswa kulipwa kwake, na baadhi ya madeni hayo yalikuwa na matumaini hafifu ya kulipwa. Kazi ya Mungu ilionekana kana kwamba imesimama. Maagizo ya kuomba machapisho yalikuwa machache sana na madogo. Afya ya mume wangu ilikuwa mbaya sana. Alikuwa akisumbuliwa na kikohozi na maumivu ya mapafu, na mfumo wake wa neva ulikuwa umechoka sana. Tuliogopa kwamba angekufa akiwa bado ana madeni.

### Ahadi za Faraja

Hizo zilikuwa siku za huzuni. Niliwatazama wavulana wangu watatu wadogo, ambao, kama nilivyohofia, wangeachwa bila baba hivi karibuni; na mawazo kama haya yalinizonga: *Mume wangu atakufa kwa sababu ya kufanya kazi kupita kiasi katika kuendeleza kazi ya kweli ya wakati huu; na ni nani anayefahamu yale aliyoyateseka? Ni nani anayejua mizigo ambayo kwa miaka mingi ameibeba, na jinsi mahangaiko makubwa yalivyomvunja moyo na kuharibu afya yake, yakimpeleka kaburini kabla ya wakati wake, huku akiiacha familia yake ikiwa maskini na tegemezi?* Mara nyingi nilijiuliza swali hili: *Je, Mungu hajali mambo haya? Je, anayapita bila kuyatilia maanani?* Nilifarijiwa kujua kwamba yuko Mmoja ahukumuye kwa haki, na kwamba kila sadaka, kila kujinyima nafsi, na kila uchungu uliovumiliwa kwa ajili Yake, umeandikwa kwa uaminifu mbinguni, na utapata thawabu yake. Siku ya Bwana itatangaza na kufunua mambo ambayo bado hayajadhihirishwa.

Nilionyeshwa kwamba Mungu alikusudia kumrudishia mume wangu afya yake hatua kwa hatua; kwamba ilitupasa kuonyesha imani thabiti, kwa maana katika kila jitihada tungefanyiwa mashambulizi makali na Shetani; kwamba ilitupasa kuacha kutazama mambo ya nje na kuamini. Mara tatu kwa siku tulijitenga mbele za Mungu na kushiriki katika maombi ya dhati kwa ajili ya kupona kwa afya yake. Kwa neema Yake, Bwana alisikia kilio chetu cha bidii, na mume wangu akaanza kupata nafuu. Siwezi kueleza vizuri hisia zangu wakati huo kuliko jinsi zilivyoelezwa katika dondoo zifuatazo kutoka katika barua niliyomwandikia Dada Howland:

"Ninashukuru kwamba sasa ninaweza kuwa na watoto wangu pamoja nami, chini ya uangalizi wangu mwenyewe. [Waliporudi kutoka safari ya Mashariki kwenda nyumbani kwao Rochester katika majira ya kupukutika kwa majani ya mwaka 1853, Mzee na Bi. White walimleta pamoja nao mtoto wao mkubwa, Henry, ambaye kwa muda wa miaka mitano alikuwa ametunzwa kwa upendo mkubwa na Ndugu na Dada Howland.] Kwa majuma kadhaa nimekuwa nikihisi njaa na kiu ya wokovu, nasi tumefurahia ushirika na Mungu karibu bila kukatizwa. Kwa nini tubaki mbali na chemchemi, ilhali tunaweza kuja na kunywa? Kwa nini tufe kwa kukosa mkate, wakati kuna ghala lililojaa? Ni neema iliyo tele na ya bure. Ee nafsi yangu, jilishe kwa

wingi kutoka humo, na kila siku unywe furaha za mbinguni! Sitanyamaza. Sifa za Mungu zimo moyoni mwangu na ziko midomoni mwangu. Tunaweza kufurahia utimilifu wa upendo wa Mwokozi wetu. Tunaweza kushiba utukufu Wake ulio bora kabisa. Nafsi yangu inashuhudia jambo hili. Giza langu limeondolewa na nuru hii ya thamani, nami sitaweza kamwe kuisahau. Ee Bwana, nisaidie niihifadhi daima katika kumbukumbu iliyo hai. Amka, enyi nguvu zote za nafsi yangu! Amka, ukamwabudu Mkombozi wako kwa ajili ya upendo Wake wa ajabu!"

"Adui zetu wanaweza kushangilia ushindi. Wanaweza kusema maneno makali, na ndimi zao zikabuni kashfa, udanganyifu, na uongo; lakini hatutatikiswa. Tunamjua yule ambaye tumemwamini. Hatujakimbia bure, wala hatukufanya kazi bure. Siku ya hukumu inakuja, ambapo kila mmoja atahukumiwa kulingana na matendo aliyoyafanya akiwa katika mwili. Ni kweli kwamba ulimwengu umejaa giza. Upinzani unaweza kuongezeka. Watu wasiojali na wenye dhihaka wanaweza kuzidi kuwa hodari katika uovu wao. Lakini pamoja na hayo yote, hatutatikiswa, bali tutategemea mkono wa Mwenye Nguvu kwa ajili ya kupata nguvu."

**Utumwa Ulibadilishwa**

Tangu wakati tulipohamia **Battle Creek**, Bwana alianza kubadili hali yetu ya utumwa na mateso. Tulipata marafiki wenye huruma huko Michigan, waliokuwa tayari kushiriki mizigo yetu na kutupatia mahitaji yetu. Marafiki wa zamani waliokuwa wamejaribiwa katika eneo la kati la New York na New England, hasa huko Vermont, walituhurumia katika dhiki zetu na walikuwa tayari kutusaidia wakati wa shida. Katika mkutano mkuu uliofanyika Battle Creek mnamo Novemba, 1856, Mungu alitutendea mambo makuu. Uhai mpya ulitolewa kwa kazi ya Mungu, na juhudi za wahubiri wetu zikafanikiwa.

Machapisho yetu yakaanza kuhitajika sana, na yakathibitika kuwa ndiyo hasa yaliyohitajika kwa maendeleo ya kazi. Gazeti la *Messenger of Truth* ("Mjumbe wa Kweli") likafa upesi, na wale waliokuwa wakieneza roho za mgawanyiko kupitia humo wakatawanyika. Mume wangu aliwezeshwa kulipa madeni yake yote. Kikohozi chake kikaisha, maumivu na uchungu katika mapafu na koo vikapotea, naye akarudishiwa afya yake hatua kwa hatua, kiasi kwamba aliweza kuhubiri mara tatu siku ya Sabato na mara moja siku ya kwanza ya juma bila shida. Kazi hii ya ajabu ya kurejeshwa kwake ilikuwa ni ya Mungu, na utukufu wote unampasa Yeye.

## 26. NJIA MBILI

Katika mkutano mkuu uliofanyika **Battle Creek, Michigan**, tarehe 27 Mei, 1856, nilionyeshwa katika maono mambo kadhaa yanayolihusu kanisa kwa ujumla. Utukufu na ukuu wa Mungu vilipita mbele yangu. Malaika akasema: "Yeye ni wa kutisha katika ukuu Wake, lakini ninyi hamlitambui jambo hilo; ni wa kutisha katika hasira Yake, lakini kila siku mnamkosea. Jitahidini kuingia kwa mlango ulio mwembamba; kwa maana mlango ni mpana na njia ni pana iendayo upotevuni, nao wanaoingia kwa huo ni wengi; lakini mlango ni mwembamba na njia ni nyembamba iendayo uzimani, nao wanaoiona ni wachache." Njia hizi ni tofauti kabisa, zimetengana, na zinaelekea pande zinazopingana. Moja inaongoza kwenye uzima wa milele, na nyingine kwenye mauti ya milele. Niliona tofauti kati ya njia hizi, na pia tofauti kati ya makundi yanayosafiri katika njia hizo. Njia hizo zinapingana; moja ni pana na laini, nyingine ni nyembamba na yenye miamba na magumu. Vivyo hivyo, watu wanaozisafiri wanatofautiana katika tabia, maisha, mavazi, na mazungumzo yao.

Wale wanaosafiri katika njia nyembamba huzungumza juu ya furaha na shangwe watakayokuwa nayo mwishoni mwa safari yao. Nyuso zao mara nyingi huonekana zenye huzuni, lakini mara nyingi pia hung'aa kwa furaha takatifu na ya mbinguni. Hawavai kama wale walio katika njia pana, wala hawazungumzi au kutenda kama wao. Wamepewa kielelezo cha kufuata. **Mtu wa huzuni na ajuaye sikitiko** ndiye aliyefungua njia hiyo kwa ajili yao, naye Mwenyewe akaipitia. Wafuasi Wake wanaona nyayo Zake, na hivyo hufarijiwa na kutiwa moyo. Yeye alipita salama; na wao pia wanaweza kupita salama ikiwa watafuata nyayo Zake.

Katika njia pana, wote wanashughulika na nafsi zao, mavazi yao, na anasa za njiani. Wanajiachia katika vicheko na furaha, wala hawafikirii mwisho wa safari yao, yaani maangamizi ya hakika yaliyo mwisho wa njia hiyo. Kila siku wanakaribia zaidi maangamizi yao; lakini kwa upumbavu wanakimbilia mbele kwa kasi zaidi na zaidi. Ee, jambo hilo lilionekana la kutisha sana machoni pangu!

Niliona wengi wakisafiri katika njia hii pana wakiwa na maneno yaliyoandikwa juu yao: **"Tumekufa kwa mambo ya dunia. Mwisho wa mambo yote umekaribia. Ninyi nanyi jiwekeni tayari."** Walifanana kabisa na watu wengine wote waliokuwa na ubatili uliowazunguka, isipokuwa kivuli cha huzuni nilichokiona kwenye nyuso zao. Mazungumzo yao yalikuwa sawa kabisa na yale ya watu waliokuwa wachangamfu na wasiojali waliowazunguka; lakini mara kwa mara walikuwa wakionyesha kwa kuridhika sana maandishi yaliyokuwa kwenye mavazi yao, na kuwaomba wengine waandikiwe maneno hayo hayo kwenye mavazi yao. Walikuwa katika njia pana, lakini walidai kwamba walikuwa miongoni mwa wale waliokuwa wakisafiri katika njia nyembamba. Wale waliowazunguka walikuwa wakisema: "Hakuna tofauti kati yetu na ninyi. Sisi ni sawa; tunavaa sawa, tunazungumza sawa, na tunatenda sawa."

Kisha nilielekezwa kurudi nyuma katika miaka ya **1843 na 1844**. Wakati huo kulikuwa na roho ya wakfu ambayo haipo sasa. Ni nini kimewapata watu wa Mungu wanaodai kuwa taifa Lake la pekee? Niliona kufanana kwao na ulimwengu, kutokuwa tayari kuteseka kwa ajili ya kweli. Niliona ukosefu mkubwa wa kujitiisha kwa mapenzi ya Mungu. Nilielekezwa pia kwa wana wa Israeli baada ya kutoka Misri. Kwa rehema Yake, Mungu aliwaita watoke miongoni mwa Wamisri ili wamwabudu bila kuzuiwa wala kubanwa. Aliwatendea miujiza njiani; akawajaribu na kuwathibitisha kwa kuwaleta katika hali ngumu. Lakini baada ya matendo hayo ya ajabu ya Mungu na baada ya kuokolewa mara nyingi, walinung'unika walipojaribiwa au kuthibitishwa na Mungu. Walisema: "Laiti tungalikufa kwa mkono wa Bwana katika nchi ya Misri." Walitamani vitunguu na vitunguu maji vya Misri.

Niliona kwamba wengi wanaodai kuiamini kweli ya siku hizi za mwisho hushangaa kwamba wana wa Israeli walinung'unika walipokuwa safarini; kwamba baada ya Mungu kuwafanyia mambo makubwa namna hiyo, walikuwa hawana shukrani kiasi cha kusahau yote aliyowatendea. Malaika akasema: **"Ninyi mmefanya vibaya zaidi kuliko wao."** Niliona kwamba Mungu amewapa watumishi Wake kweli iliyo wazi na dhahiri kiasi kwamba haiwezi kupingwa. Popote wanapokwenda, wanakuwa na ushindi wa hakika. Adui zao hawawezi kuikwepa kweli yenye ushahidi wa wazi. Nuru imeng'aa kwa uwazi kiasi kwamba watumishi wa Mungu wanaweza kusimama mahali popote na kuiacha kweli, ikiwa wazi na yenye mpangilio, ichukue ushindi. Baraka hii kubwa haijathaminiwa, wala hata kutambuliwa kikamilifu. Jaribu lolote linapotokea, baadhi huanza kutazama nyuma na kufikiri kwamba maisha yao ni magumu. Baadhi ya wale wanaodai kuwa watumishi wa Mungu hawajui maana ya majaribu yanayotakasa. Wakati mwingine hujitengenezea majaribu wao wenyewe, huyawaza majaribu yasiyokuwapo, na hukata tamaa kwa urahisi sana; huumia kirahisi, na kujiheshimu kwao huathirika haraka kiasi kwamba hujidhuru wenyewe, huwadhuru wengine, na kuiumiza kazi ya Mungu. Shetani huyakuza majaribu yao na kuweka mawazo katika akili zao ambayo, yakikubaliwa, yataharibu ushawishi wao na manufaa yao katika kazi ya Mungu.

Baadhi wamejaribiwa kujiondoa katika kazi ya injili na kwenda kufanya kazi za mikono ili kujipatia riziki. Niliona kwamba kama mkono wa Mungu ungeondolewa kutoka kwao, na wakaachwa chini ya magonjwa na mauti, ndipo wangejua maana ya taabu ya kweli. Ni jambo la kutisha sana kumnung'unikia Mungu. Hawakumbuki kwamba njia wanayoisafiri ni njia yenye magumu, ya kujikana nafsi, na ya kujisulubisha nafsi; kwa hiyo hawapaswi kutarajia kwamba kila jambo litaenda kwa urahisi kana kwamba wanasafiri katika njia ile pana. **"Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao."** Waebrania 12:14.

Niliona kwamba baadhi ya watumishi wa Mungu, hata wahudumu, hukata tamaa kwa urahisi sana. Nafsi zao huumia upesi, na hudhani kwamba wamepuuzwa na kutendewa isivyo haki, wakati sivyo ilivyo. Hufikiri kwamba sehemu yao ni ngumu. Watu kama hao hawatambui jinsi ambavyo wangejisikia kama mkono wa Mungu unaowategemeza ungeondolewa, na wakapitia huzuni kuu ya nafsi. Ndipo wangeona kwamba sehemu yao ingekuwa ngumu mara

kumi zaidi kuliko ilivyokuwa walipokuwa wakifanya kazi ya Mungu, wakivumilia majaribu na upungufu, lakini wakiwa na kibali cha Bwana.

Baadhi ya wale wanaofanya kazi katika kazi ya Mungu hawajui wanapokuwa na wakati wa raha. Wamepitia upungufu mchache sana, na wanajua kidogo sana kuhusu uhitaji, kazi ngumu ya kuchosha, au mzigo wa nafsi. Hivyo, wanapokuwa na wakati wa utulivu, wanapobarikiwa na Mungu na karibu kuachiliwa kabisa na huzuni ya rohoni, hawatambui jambo hilo, bali hudhani kwamba majaribu yao ni makubwa. Niliona kwamba isipokuwa watu kama hao wawe na roho ya kujikana nafsi, na wawe tayari kufanya kazi kwa furaha bila kujisitiri wala kujihurumia, Mungu atawaondoa katika kazi hiyo. Hatawatambua kuwa watumishi Wake wanaojitoa kafara, bali atawaamsha wengine watakaofanya kazi kwa bidii, si kwa uvivu, na watakaojua wanapokuwa na wakati wa raha. Watumishi wa Mungu wanapaswa kubeba mzigo wa roho za watu, na kulia kati ya ukumbi na madhabahu wakisema, **“Ee Bwana, uwaachilie watu wako.”**

Baadhi ya watumishi wa Mungu wametoa maisha yao ili kuyatumia na kuyamaliza kwa ajili ya kazi ya Mungu, mpaka miili yao imechoka kabisa, na karibu imeharibika kwa kazi nyingi za akili, uangalifu usiokoma, taabu na upungufu. Wengine hawajawahi kubeba mzigo huo, wala hawakutaka kuubeba. Lakini watu kama hao hudhani kwamba wana wakati mgumu, kwa sababu hawajawahi kupitia shida za kweli. Hawajawahi kubatizwa katika mateso ya kazi ya Kristo, wala hawatabatizwa humo maadamu wanaonyesha udhaifu mwingi, ujasiri mdogo, na kupenda starehe zao.

Kutokana na yale Mungu aliyonionyesha, kunahitajika kuchujwa miongoni mwa wahudumu, ili wale wavivu, wazembe, na wanaojijali wenyewe waondolewe, na kubaki kundi safi, waaminifu, na wanaojitoa kafara, ambao hawatajitafutia raha zao wenyewe, bali watahudumu kwa uaminifu katika neno na mafundisho, wakiwa tayari kuteseka na kuvumilia mambo yote kwa ajili ya Kristo, na kuwaokoa wale ambao Kristo aliwafia. Watumishi hao na wahisi ole juu yao ikiwa hawatahubiri injili; lakini si wote wanaohisi jambo hilo.

## 27. TAJI MBILI

Katika maono niliyopewa huko Battle Creek, Michigan, Oktoba 25, 1861, nilionyeshwa dunia hii ikiwa yenye giza na huzuni. Malaika akasema, **"Tazama kwa makini!"** Ndipo nikaonyeshwa watu waliokuwa duniani. Wengine walikuwa wamezungukwa na malaika wa Mungu; wengine walikuwa katika giza nene, wamezungukwa na malaika waovu. Niliona mkono ukishuka kutoka mbinguni ukiwa umeshika fimbo ya enzi ya dhahabu. Juu ya fimbo hiyo kulikuwa na taji lililopambwa kwa almasi. Kila almasi ilitoa mwanga mkali, safi, na mzuri. Juu ya taji hilo kulikuwa na maandishi haya: "Wote wanaonipokea wana furaha, nao watakuwa na uzima wa milele."

Chini ya taji hilo kulikuwa na fimbo nyingine ya enzi, ambayo juu yake pia kulikuwa na taji. Katikati ya taji hilo kulikuwa na vito, dhahabu, na fedha, vikitoa mwanga kiasi. Maandishi juu yake yalikuwa: **"Hazina za duniani. Utajiri ni nguvu.** Wote wanaonipokea wana heshima na sifa." Niliona umati mkubwa ukikimbilia kupata taji hilo. Walikuwa wakipiga kelele na kusongana. Baadhi yao, kwa tamaa yao kubwa, walionekana kana kwamba wamepoteza akili. Walikuwa wakisukumana, wakiwarudisha nyuma walio dhaifu, na kuwakanyaga wale walioanguka kwa haraka yao. Wengi walizishika kwa nguvu hazina zilizokuwa ndani ya taji hilo, na hawakuziachia. Vichwa vya baadhi yao vilikuwa vyeupe kama fedha, na nyuso zao zilikuwa zimejaa mikunjo ya wasiwasi na taabu. Hata jamaa zao wenyewe, mfupa wa mifupa yao na nyama ya nyama yao, hawakuwajali. Walipoonyeshwa nyuso za kuomba msaada, walizikumbatia zaidi hazina zao, kana kwamba waliogopa kupoteza hata sehemu ndogo, au kushawishiwa kuwagawia wengine. Macho yao yenye tamaa yalilitazama mara kwa mara taji la duniani, wakihesabu na kuhesabu tena hazina zake.

Niliona picha za umaskini na mateso miongoni mwa umati huo. Waliyatazama yale mali kwa shauku, lakini waligeuka kwa kukata tamaa, kwa kuwa wenye nguvu waliwasukuma na kuwaondoa walio dhaifu. Hata hivyo hawakuacha kujaribu; pamoja na watu wengi waliokuwa vilema, wagonjwa, na wazee, waliendelea kusukumana kuelekea kwenye taji la duniani. Wengine walikufa wakijaribu kulifikia. Wengine walianguka walipokuwa karibu kulishika. Wengi walikuwa wamekwisha kuligusa tu walipoanguka chini. Miili ya wafu ilikuwa imetapakaa ardhini, lakini umati uliendelea kukimbia, ukiwakanyaga waliokuwa wameanguka na waliokufa. Kila aliyefanikiwa kulifikia taji hilo alipata sehemu yake, na alipigiwa makofi kwa sauti kubwa na kundi la watu waliokuwa wakilitazama kwa shauku.

Kundi kubwa la malaika waovu lilikuwa likifanya kazi kwa bidii. Shetani alikuwa katikati yao, na wote walionyesha furaha kubwa walipowaona watu wakihangaikia taji hilo. Alionekana kuwa na mvuto wa pekee juu ya wale walioutafuta kwa shauku kubwa.

Wengi waliokuwa wakilitafuta taji hili la duniani walikuwa Wakristo kwa jina. Baadhi yao walionekana kuwa na nuru kidogo. Mara kwa mara walilitazama taji la mbinguni kwa shauku, na walivutiwa na uzuri wake; lakini hawakuwa na ufahamu wa kweli wa thamani na utukufu wake. Wakati kwa mkono mmoja walikuwa wakijinyoosha kwa uzembe kulifikia taji la mbinguni, kwa mkono mwingine walikuwa wakijitahidi kwa nguvu kulipata taji la duniani, wakiwa wameazimia kulimiliki. Walipozidi kujitahidi kulipata taji la duniani, walipoteza kabisa kuliona lile la mbinguni. Waliachwa gizani, lakini waliendelea kupapasa kwa bidii ili walipate taji la duniani.

Baadhi yao walichoshwa na kundi lililokuwa likilitafuta kwa tamaa hiyo kubwa. Walitambua hatari yao, wakaligeukia kisogo, na kwa bidii wakaanza kulitafuta taji la mbinguni. Mara nyuso zao zikabadilika kutoka gizani kwenda nuruni, kutoka huzuni kwenda furaha na shangwe takatifu.

Kisha niliona kundi jingine likisonga mbele kupitia katika umati huo, macho yao yakiwa yamekazia taji la mbinguni. Walipokuwa wakisonga kwa bidii kupitia katikati ya umati ule wenye vurugu, malaika waliwaandama na kuwafungulia njia ili wasonge mbele. Walipokaribia taji la mbinguni, nuru iliyokuwa ikitoka ndani yake iliwaangazia wao na mazingira yao, ikifukuza giza lao, na kuendelea kuwa angavu zaidi na zaidi, hata walionekana kubadilishwa na kufanana na malaika. Hawakutazama hata mara moja taji la duniani kwa shauku yoyote. Wale waliokuwa wakilitafuta taji la duniani waliwadhihaki, na kuwatupia mipira myeusi. Lakini mipira hiyo haikuwadhuru maadamu macho yao yalikuwa yamekazia taji la mbinguni. Ila wale waliogeuza macho yao na kuitazama mipira hiyo myeusi walichafuliwa nayo. Ndipo Maandiko yafuatayo yakawekwa mbele yangu:

**"***Msijiwekee hazina duniani, nondo na kutu viharibupo, na wevi huvunja na kuiba; bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusikoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wevi hawavunji wala hawaibi; kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako. Taa ya mwili ni jicho; basi jicho lako likiwa safi, mwili wako wote utakuwa na nuru. Lakini jicho lako likiwa bovu, mwili wako wote utakuwa na giza. Basi ile nuru iliyomo ndani yako ikiwa giza; si giza hilo! Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia huyu, na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu, na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali***."** Mathayo 6:19–24.

Kisha yale niliyokuwa nimeyaona yakafafanuliwa kwangu hivi: Umati uliokuwa ukijitahidi kwa shauku kuu kupata taji la duniani ni wale wanaopenda hazina za ulimwengu huu, na wanaodanganywa na kuvutwa na vivutio vyake vya muda mfupi. Niliona kwamba baadhi ya wale wanaodai kuwa wafuasi wa Yesu wana tamaa kubwa ya kupata mali za duniani kiasi kwamba wanapoteza upendo wao kwa mbingu, wanaishi kama ulimwengu, na Mungu huwahesabu kuwa ni wa ulimwengu. Wanadai kwamba wanatafuta taji lisiloharibika, yaani hazina iliyo mbinguni; lakini shauku yao na shughuli yao kuu ni kujipatia hazina za duniani. Wale walio na hazina zao katika ulimwengu huu, na wanaopenda utajiri wao, hawawezi

kumpenda Yesu. Wanaweza kudhani kwamba wako sawa, lakini ingawa wanang'ang'ania mali zao kwa mshiko wa mchoyo, hawawezi kufanywa kuona wala kuhisi kwamba wanapenda fedha kuliko kazi ya kweli au kuliko hazina ya mbinguni.

**"Basi ikiwa nuru iliyo ndani yako ni giza, giza hilo ni kuu namna gani!"** Kulikuwa na wakati katika maisha ya watu kama hao ambapo nuru waliyopewa hawakuithamini, nayo ikageuka kuwa giza. Malaika akasema, **"Hamwezi kupenda na kuabudu hazina za duniani, huku mkimiliki utajiri wa kweli."**

Yule kijana alipomjia Yesu na kusema, **"Mwalimu mwema, nifanye jambo gani jema ili nipate uzima wa milele?"** Yesu alimpa uchaguzi: aachane na mali zake apate uzima wa milele, au azishike na kuupoteza uzima huo. Utajiri wake ulikuwa wa thamani zaidi kwake kuliko hazina ya mbinguni. Sharti la kuachana na mali zake na kuwapa maskini ili awe mfuasi wa Kristo na apate uzima wa milele lilipoelezwa kwake, shauku yake ilipoa, naye akaenda zake akiwa mwenye huzuni.

Wale nilioonyeshwa wakililia kwa tamaa taji la duniani ni wale watakaotumia njia yoyote ile kujipatia mali. Katika jambo hilo wanakuwa kama waliopoteza akili. Mawazo yao yote na nguvu zao zote huelekezwa katika kutafuta utajiri wa duniani. Wanawakanyaga wengine haki zao, huwadhulumu maskini, na humwonea mfanyakazi katika ujira wake. Wakipata nafasi ya kuwazidi akili walio maskini na wasio werevu, na hivyo kuongeza mali zao, hawatasita hata kidogo kuwaonea, na hata kuwaacha wafikie umaskini wa kutupwa.

Wale watu ambao vichwa vyao vilikuwa vimejaa mvi za uzee, na nyuso zao zimekunjwa na mashaka, lakini bado walikuwa wakishikilia kwa tamaa hazina zilizokuwa ndani ya taji, walikuwa ni wazee waliobakiwa na miaka michache tu ya kuishi. Hata hivyo walikuwa na hamu kubwa ya kuongeza hazina zao za duniani. Kadiri walivyokuwa wakikaribia kaburini, ndivyo walivyozidi kushikamana nazo.

Hata jamaa zao wenyewe hawakunufaika. Wanafamilia wao waliruhusiwa kufanya kazi kupita nguvu zao ili kuokoa fedha kidogo. Hawakuzitumia kwa manufaa ya wengine wala hata kwa manufaa yao wenyewe. Ilitosha kwao kujua kwamba walikuwa nazo. Walipoonyeshwa wajibu wao wa kuwasaidia maskini na kuunga mkono kazi ya Mungu, walihuzunika. Wangependa kupokea zawadi ya uzima wa milele, lakini hawakuwa tayari iliwagharimu chochote. Masharti yaliwaonekana kuwa magumu mno. Lakini Ibrahimu hakumzuilia Mungu mwanawe wa pekee. Kwa kumtii Mungu, aliweza kumtoa sadaka mtoto huyo wa ahadi kwa urahisi zaidi kuliko ambavyo wengi wangetoa baadhi ya mali zao za duniani.

Ilikuwa jambo la kuhuzunisha kuona wale ambao walipaswa kuwa wakikomaa kwa ajili ya utukufu, na kila siku wakijiandaa kwa ajili ya kutokufa, wakitumia nguvu zao zote kulinda hazina zao za duniani." Niliona kwamba watu kama hao hawawezi kuthamini hazina ya mbinguni. Upendo wao mkuu kwa mambo ya duniani huonyesha kwa matendo yao kwamba hawaithamini urithi wa mbinguni kiasi cha kuwafanya watoe sadaka yoyote kwa ajili yake.

Yule **“kijana”** alionyesha utayari wa kuzishika amri, lakini Bwana wetu alimwambia kwamba alikuwa amepungukiwa na jambo moja. Alitamani uzima wa milele, lakini alipenda mali zake kuliko alivyopenda uzima huo. Wengi wanajidanganya wenyewe. Hawajaitafuta kweli kama mtu anavyotafuta hazina iliyofichwa. Hawajatumia kikamilifu uwezo wao. Akili zao, ambazo zingeweza kuangaziwa na nuru ya mbinguni, zimejaa wasiwasi na fadhaa. **“Mahangaiko ya dunia hii, na udanganyifu wa mali, na tamaa za mambo mengine ziingiapo, hulisonga lile neno, likawa halizai.”** Malaika akasema, **“Watu hao hawana udhuru.”** Niliona nuru yao ikizidi kufifia. Hawakutaka kuelewa kweli nzito na muhimu za wakati huu, na walidhani kwamba wako salama hata bila kuzielewa. Nuru yao ikazimika, nao wakaanza kupapasa gizani.

Umati wa watu waliokuwa vilema na wagonjwa, waliokuwa wakisongamana kuelekea kwenye taji la duniani, ni wale ambao maslahi yao na hazina zao ziko katika ulimwengu huu. Ingawa wanakatishwa tamaa kila upande, hawataweka mioyo yao mbinguni ili kujipatia hazina na makao huko. Wanakosa mali za duniani; na huku wakiendelea kuzikimbiza, wanapoteza pia za mbinguni. Licha ya kuona kukatishwa tamaa, maisha ya huzuni, na mwisho mbaya wa wale waliokuwa wamejitoa kabisa kutafuta utajiri wa duniani, wengine bado hufuata njia hiyo hiyo. Wanakimbilia mbele kwa wazimu, bila kujali mwisho wa kusikitisha wa wale wanaowaiga.

Wale waliolifikia taji hilo, wakapata sehemu ndani yake na kusifiwa kwa makofi, ni wale wanaopata kile ambacho ndicho lengo kuu la maisha yao—utajiri. Wanapokea heshima ambayo ulimwengu huwapa matajiri. Wanakuwa na ushawishi katika ulimwengu. Shetani na malaika zake waovu hufurahia jambo hilo. Wanajua kwamba watu kama hao ni mali yao hakika; kwa maana maadamu wanaishi katika uasi dhidi ya Mungu, wao ni mawakala wenye nguvu wa Shetani.

Wale waliochukizwa na kundi lililokuwa likigombania kwa hamu taji la kidunia, ni wale ambao wameutazama mwenendo na mwisho wa wote wanaojitahidi kutafuta utajiri wa dunia. Wanaona kwamba watu hao hawatosheki kamwe, bali hawana furaha; nao wanaingiwa na hofu, kisha wanajitenga na kundi hilo lisilo na furaha, na kutafuta utajiri wa kweli na udumuo.

Wale waliokuwa wakijisukuma kupita katikati ya umati kwa ajili ya taji la mbinguni, wakiwa wameandamana na malaika watakatifu, nilionyeshwa kwamba hao ni watu waaminifu wa Mungu. Malaika huwaongoza mbele, nao wanatiwa moyo kwa bidii kusonga mbele kwa ajili ya hazina ya mbinguni.

Mipira myeusi iliyokuwa ikitupwa nyuma ya watakatifu, ilikuwa ni uongo wa lawama uliosambazwa dhidi ya watu wa Mungu na wale wanaopenda na kutenda uongo. Tunapaswa kuwa waangalifu sana kuishi maisha yasiyo na lawama, na kujiepusha na kila sura ya uovu; kisha ni wajibu wetu kusonga mbele kwa ujasiri, bila kujali uongo wa lawama wa waovu. Wakati macho ya wenye haki yanapoelekezwa kwenye hazina ya mbinguni isiyo na thamani, watazidi kufanana na Kristo, na hivyo watabadilishwa na kufanywa tayari kwa ajili ya kuhamishwa.

## 28. UMIZIMU WA KISASA

Mnamo Agosti 24, 1850, Nilitambua kwamba ule 'upigaji wa ajabu wa sauti' ulikuwa ni nguvu ya Shetani; baadhi yake ilitoka kwake moja kwa moja, na baadhi yake kwa njia isiyo ya moja kwa moja kupitia mawakala wake, lakini yote yalitokana na Shetani. Ilikuwa kazi yake ambayo aliifanya kwa njia mbalimbali; hata hivyo wengi katika makanisa na ulimwenguni walikuwa wamefunikwa na giza kubwa kiasi kwamba walifikiri na kudai kwamba ilikuwa nguvu ya Mungu. Malaika alisema: je! Haiwapasi watu kutafuta habari kwa Mungu wao? Je! Waende kwa watu waliokufa kwa ajili ya watu walio hai? Je, walio hai watawaendea wafu ili kupata maarifa? Wafu hawajui neno lolote. Je, kwa ajili ya Mungu aliye hai mtawaendea wafu? Wameacha Mungu aliye hai ili kuzungumza na wafu ambao hawajui lolote. Tazama Isaya 8:19, 20.

Niliona kwamba hivi karibuni ingekuwa jambo linaloonekana kuwa ni kufuru kuzungumza dhidi ya upigaji wa sauti wa namna hiyo, na kwamba ingeenea zaidi na zaidi; kwamba nguvu za Shetani zingezidi kuongezeka, na kwamba baadhi ya wafuasi wake waliomfuata kwa kujitoa wangekuwa na uwezo wa kufanya miujiza, hata kuleta moto kutoka mbinguni mbele ya macho ya wanadamu. Nilionyeshwa kwamba kupitia upigaji wa sauti wa namna hiyo na nguvu za ushawishi wa kishetani unaoteka akili, wachawi hawa wa kisasa wangeweza baadaye kueleza miujiza yote iliyofanywa na Bwana wetu Yesu Kristo, na kwamba wengi wangeamini kuwa kazi zote kuu za Mwana wa Mungu alipokuwa duniani zilifanywa kwa nguvu hiyo hiyo. Nilielekezwa nyuma hadi wakati wa Musa, na nikaona ishara na maajabu ambayo Mungu aliyafanya kupitia yeye mbele ya Farao; mengi kati ya hayo yaliigwa na wachawi wa Misri. Nikaona kwamba kabla tu ya ukombozi wa mwisho wa watakatifu, Mungu atafanya kazi kwa nguvu kwa ajili ya watu Wake, na wachawi hawa wa kisasa wataruhusiwa kuiga kazi ya Mungu.

Wakati huo utakuja hivi karibuni, na itatupasa kushikilia mkono wenye nguvu wa Yehova; kwa maana ishara hizi zote kuu na maajabu makubwa ya Shetani yamekusudiwa kuwadanganya watu wa Mungu na kuwaangusha. Akili zetu lazima zikae imara kwa Mungu, wala hatupaswi kuogopa hofu ya waovu, yaani, kuogopa yale wanayoogopa na kuheshimu yale wanayoyaheshimu; bali tunapaswa kuwa jasiri na hodari kwa ajili ya kweli. Kama macho yetu yangefunguliwa, tungeona sura za malaika waovu zikituzunguka, wakijaribu kubuni njia mpya

za kutusumbua na kutuangamiza. Pia tungeona malaika wa Mungu wakitulinda dhidi ya nguvu zao; kwa maana jicho la Mungu linalochunga daima liko juu ya Israeli kwa ajili ya mema, naye atawalinda na kuwaokoa watu Wake ikiwa watamtumaini. Adui atakapokuja kama mafuriko, Roho wa Bwana atasimamisha bendera dhidi yake.

Malaika alisema: **"**Kumbuka, uko katika eneo la udanganyifu wa Shetani**."** Niliona kwamba tunapaswa kukesha, kuvaa silaha zote za Mungu, na kuchukua ngao ya imani; ndipo tutaweza kusimama, na mishale yenye moto ya yule mwovu haitatudhuru.

## 29. MITEGO YA SHETANI

Niliona kwamba Shetani aliwaamuru malaika zake kuweka mitego hasa kwa wale waliokuwa wakitazamia marejeo ya pili ya Kristo, na wanaozishika amri zote za Mungu. Shetani aliwaambia malaika zake kwamba makanisa yalikuwa usingizini. Angeongeza nguvu zake na maajabu ya uongo, naye angeweza kuwashikilia. Lakini alisema: "Tunalichukia kundi la washika Sabato; wanaendelea kufanya kazi dhidi yetu, na wanatunyakulia watu wetu ili wazishike sheria za Mungu tunazozichukia." "Nendeni, wale wenye mashamba na fedha mkawafanye walewe na mahangaiko. Mkiweza kuwafanya waweke mapenzi yao juu ya vitu hivyo, tutakuwa tumewapata. Wanaweza kudai chochote wanachotaka; wafanyeni tu wajali zaidi fedha kuliko mafanikio ya ufalme wa Kristo au kuenea kwa kweli tunazozichukia. Waonyesheni ulimwengu katika hali ya kuvutia sana, ili waupende na kuuabudu."

"Lazima tuweke katika safu zetu njia zote ambazo tunaweza kupata udhibiti wake. Kadiri watu wanaomfuata Kristo wanavyoweka mali zao nyingi katika huduma Yake, ndivyo watakavyoharibu ufalme wetu kwa kuwanyakua raia wetu. Wanapopanga mikutano katika sehemu mbalimbali, tuko hatarini. Kwa hiyo mwe waangalifu sana. Leteni machafuko na vurugu ikiwa inawezekana. Haribuni upendo wao kwa wao. Wakatisheni tamaa na kuwavunja moyo wahudumu wao; kwa maana tunawachukia. Wawekeni wale walio na mali kila sababu inayowezekana ili wasitoe fedha zao. Dhibiti mambo ya fedha ikiwa mnaweza, na wasukumeni wahudumu wao katika uhitaji na dhiki. Hili litadhoofisha ujasiri wao na bidii yao. Pigana kwa kila inchi ya ardhi. Fanyeni tamaa ya mali na upendo wa vitu vya dunia kuwa sifa kuu zinazotawala tabia zao. Maadamu tabia hizi zinatawala, wokovu na neema vitabaki nyuma.

Wazungusheni kila aina ya mvuto wa dunia, nao hakika watakuwa wetu. Na si kwamba tutakuwa na wao tu, bali ushawishi wao mbaya hautatumika kuwaongoza wengine kwenda mbinguni. Wakati mtu yeyote atakapojaribu kutoa, wekeni ndani yao roho ya uchoyo, ili watoe kidogo iwezekanavyo."

Niliona kwamba Shetani anatekeleza mipango yake vizuri. Watumishi wa Mungu wanapoweka mikutano, Shetani pamoja na malaika zake huwa pale ili kuzuia kazi hiyo. Daima anaweka mawazo katika akili za watu wa Mungu. Huwaongoza wengine katika njia moja na wengine katika njia nyingine, akitumia kila mara udhaifu na tabia mbaya zilizopo ndani ya

ndugu na dada, akichochea na kuamsha mielekeo yao ya asili. Wanapovutwa kwnye mwelekeo wa ubinafsi na tamaa, Shetani husimama kando yao, na kwa nguvu zake zote hujaribu kuwaongoza waendelee na dhambi zao zinazowatawala. Neema ya Mungu na nuru ya kweli vinaweza kuyeyusha kwa muda hisia zao za tamaa na ubinafsi; lakini ikiwa hawapati ushindi kamili, Shetani huingia wakati hawapo chini ya ushawishi wa wokovu, na kuondoa kila kanuni ya heshima na ukarimu ndani yao. Kisha wanaanza kufikiri kwamba wanatakiwa mambo mengi sana. Wanachoka kutenda mema, na kusahau dhabihu kubwa ambayo Yesu aliitoa ili kuwakomboa kutoka katika nguvu za Shetani na kutoka katika taabu isiyo na tumaini.

Shetani alitumia tabia ya Yuda ya tamaa na ubinafsi, akamfanya anung'unike wakati Mariamu alipomimina marhamu ya thamani juu ya Yesu. Yuda aliona jambo hilo kuwa ni upotevu mkubwa, akasema kwamba marhamu hiyo ingeweza kuuzwa na fedha zake kuwapa maskini. Lakini hakujali maskini; bali aliona sadaka hiyo ya ukarimu kwa Yesu kuwa ni matumizi yasiyofaa. Yuda alimthamini Bwana wake kiasi cha kutosha tu kumuuza kwa vipande vichache vya fedha. Nami nikaona kwamba wapo baadhi kama Yuda miongoni mwa wale wanaodai kumngojea Bwana wao. Shetani anawatawala, lakini wao hawalitambui hilo.

Mungu hawezi kukubali hata kiwango kidogo kabisa cha tamaa ya mali au ubinafsi, Naye huchukia maombi na maonyo ya wale wanaojiruhusu kuwa na tabia hizi mbaya. Shetani anapoona kwamba muda wake ni mfupi, huwaongoza wanadamu kuwa wabinafsi na wenye tamaa zaidi na zaidi; kisha hushangilia anapowaona wamejifungia ndani yao wenyewe, wakiwa wachoyo, wagumu kutoa, na wenye kujifikiria wao wenyewe. Kama macho ya watu wa namna hiyo yangefunguliwa, wangemwona Shetani akishangilia kwa furaha ya kuzimu juu yao, akicheka upumbavu wa wale wanaokubali mapendekezo yake na kuingia katika mitego yake.

Shetani na malaika zake huandika kila tendo la unyonge na tamaa la watu hawa, kisha humletea Yesu na malaika zake watakatifu, wakisema kwa dharau: **"Hawa ndio wafuasi wa Kristo! Wanajiandaa kwa ajili ya kunyakuliwa!"** Shetani hulinganisha mwenendo wao na mafungu ya Maandiko ambayo yanawakemea waziwazi, kisha huwadhihaki malaika wa mbinguni akisema: **"Hawa ndio wanaomfuata Kristo na neno Lake! Haya ndio matunda ya dhabihu na ukombozi wa Kristo!"** Malaika hugeuka wakiwa wamechukia katika tukio hilo.

Mungu anahitaji watu Wake wawe na matendo mema daima; na wanapochoka kutenda mema, Mungu naye huchoshwa nao. Niliona kwamba Yeye hafurahishwi kabisa hata na dalili ndogo kabisa ya ubinafsi kwa upande wa watu Wake wanaodai kuwa Wake, ambao Yesu hakukataa kutoa hata maisha Yake ya thamani kwa ajili yao. Kila mtu mwenye ubinafsi na tamaa ataanguka njiani. Kama Yuda aliyemuuza Bwana wake, watauza kanuni njema na tabia ya heshima na ukarimu kwa ajili ya faida ndogo ya dunia. Watu wote wa namna hiyo watachujwa kutoka miongoni mwa watu wa Mungu. Wale wanaotaka mbingu lazima, kwa nguvu zote walizonazo, wahimize kanuni za mbinguni. Badala ya kudumaa na kunyauka kwa sababu ya ubinafsi, mioyo yao inapaswa kupanuka kwa ukarimu. Kila nafasi inapaswa kutumiwa kufanya

mema kwa mmoja na mwingine, na hivyo kudumisha kanuni za mbinguni. Yesu alionyeshwa kwangu kama mfano mkamilifu. Maisha Yake hayakuwa na maslahi ya kibinafsi, bali kila mara yalijulikana kwa ukarimu usio na ubinafsi.

## 30. PEPETO (KUTIKISWA)

Niliona baadhi ya watu wakiwa na imani yenye nguvu na vilio vya uchungu wakimsihi Mungu. Nyuso zao zilikuwa zimepauka, na zilionyesha huzuni kubwa, ikidhihirisha mapambano yao ya ndani. Uthabiti na bidii kubwa vilionekana katika nyuso zao; matone makubwa ya jasho yalitiririka kutoka kwenye vipaji vyao. Mara kwa mara nyuso zao zingeng'aa kwa alama za kibali cha Mungu, kisha tena sura ile ile ya huzuni, bidii na wasiwasi mkubwa ingewakaa.

Malaika waovu walikuwa wamewazunguka kwa wingi, wakileta giza juu yao ili kumficha Yesu wasimwone, ili macho yao yaelekezwe kwenye giza lililowazunguka, na hivyo waongozwe kumtilia Mungu mashaka na kumnung'unikia. Usalama wao pekee ulikuwa katika kuyaelekeza macho yao juu. Malaika wa Mungu walikuwa wamepewa jukumu la kuwalinda watu Wake; na wakati hewa yenye sumu ya malaika waovu ilipokuwa ikiwazunguka watu hawa wenye wasiwasi, malaika wa mbinguni waliendelea kupiga mabawa yao juu yao ili kutawanya giza zito.

Wakati wale waliokuwa wakiomba waliendelea na vilio vyao vya bidii, mara kwa mara mwanga wa nuru kutoka kwa Yesu uliwafikia, ukitia moyo mioyo yao na kuangaza nyuso zao. Niliona kwamba baadhi yao hawakushiriki katika kazi hii ya kuhangaika na kuomba. Walionekana kutokuwa na shughuli wala kujali. Hawakupinga giza lililowazunguka, nalo liliwafunika kama wingu zito. Malaika wa Mungu waliwaacha hawa, na wakaenda kuwasaidia wale waliokuwa wakiomba kwa bidii. Niliona malaika wa Mungu wakiharakisha kuwasaidia wote waliokuwa wakipambana kwa nguvu zao zote dhidi ya malaika waovu, na waliokuwa wakijaribu kujisaidia kwa kumwita Mungu kwa uvumilivu. Lakini malaika Wake waliwaacha wale ambao hawakufanya juhudi yoyote ya kujisaidia, nami nikawaacha wasionekane tena.

Niliuliza maana ya pepeto (kutikiswa) nilikokuwa nimeona, nikaonyeshwa kwamba kutasababishwa na **ushuhuda wa moja kwa moja** unaotokana na ushauri wa **Shahidi wa Kweli kwa Walaodikia**. Hili litakuwa na matokeo moyoni mwa anayelipokea, na litamwongoza kuinua kiwango na kutangaza kweli iliyo wazi. Wengine hawatavumilia ushuhuda huu wa moja kwa moja. Watainuka dhidi yake, na jambo hili ndilo litakalosababisha pepeto miongoni mwa watu wa Mungu.

Niliona kwamba ushuhuda wa Shahidi wa Kweli haujazingatiwa hata nusu yake. Ushuhuda wa kutisha ambao juu yake hatima ya kanisa inategemea umepuuzwa kwa urahisi, kama sio kutupiliwa mbali kabisa. Ushuhuda huu lazima ufanye kazi ya toba ya ndani kabisa; wote wanaoupokea kwa kweli watautii na kutakaswa.

Malaika alisema: **"Sikilizeni!"** Mara nikasikia sauti kama ya vyombo vingi vya muziki, vyote vikitoa sauti kamilifu, tamu na yenye upatanifu. Ilizidi muziki wowote niliowahi kusikia, ikiwa imejaa rehema, huruma, furaha iliyoinua moyo, na utakatifu. Ilipenya katika nafsi yangu yote. Malaika alisema: **"Tazama!"** Kisha mawazo yangu yalielekezwa kwa kundi nililokuwa nimeona likitikiswa sana. Nilionyeshwa wale ambao hapo awali niliwaona wakilia na kuomba kwa uchungu wa roho. Idadi ya malaika walinzi waliowazunguka ilikuwa imeongezeka mara mbili, nao walikuwa wamevikwa silaha kuanzia kichwani hadi miguuni. Walitembea kwa utaratibu kamili, kama jeshi la askari. Nyuso zao zilionyesha mapambano makali waliyopitia na vita vya uchungu walivyovumilia. Lakini sura zao, zilizokuwa zimeonyesha mateso makubwa ya ndani, sasa ziling'aa kwa nuru na utukufu wa mbinguni. Walikuwa wamepata ushindi, nao ushindi huo uliwafanya watoe shukrani kuu na furaha takatifu. Idadi ya kundi hili ilikuwa imepungua. Baadhi yao walikuwa wametikiswa na kuachwa njiani. Wale waliokuwa wazembe na wasiojali, ambao hawakuungana na wale waliothamini ushindi na wokovu kiasi cha kuendelea kusihi na kuhangaika kwa ajili yake, hawakuupata; nao waliachwa nyuma katika giza, na nafasi zao mara moja zilijazwa na wengine waliolishika kweli na kuingia katika safu. Malaika waovu waliendelea kuwazunguka, lakini hawakuwa na uwezo wowote juu yao.

Niliwasikia wale waliovikwa silaha wakisema kweli kwa nguvu kubwa. Ilikuwa na matokeo. Wengi walikuwa wamefungwa; baadhi ya wake kwa waume zao, na baadhi ya watoto kwa wazazi wao. Wale waaminifu waliokuwa wamezuiwa kusikia kweli sasa waliishika kwa hamu kubwa. Hofu yote waliyokuwa nayo kwa sababu ya ndugu zao iliondoka, na kweli pekee ndiyo iliyotukuzwa kwao. Walikuwa na njaa na kiu ya kweli; nayo ilikuwa ya thamani na ya kupendeza zaidi kuliko maisha. Niliuliza ni nini kilichosababisha mabadiliko haya makubwa. Malaika akajibu: **"Ni mvua ya masika, kuburudishwa kutoka mbele za Bwana, na kilio kikuu cha malaika wa tatu."**

Nguvu kubwa ilikuwa pamoja na hawa wateule. Malaika alisema: **"Tazama!"** Mawazo yangu yakageuzwa kwa waovu, au wale wasioamini. Wote walikuwa katika hali ya msukosuko. Bidii na nguvu vilivyokuwa pamoja na watu wa Mungu viliwaamsha na kuwakasirisha. Machafuko, machafuko yalikuwa kila mahali. Niliona hatua zikichukuliwa dhidi ya kundi lililokuwa na nuru na nguvu za Mungu. Giza lilizidi kuwazunguka, lakini walisimama imara, wakikubaliwa na Mungu na kumtumaini Yeye. Niliwaona wakiwa katika hali ya mashaka; kisha nikawasikia wakimlilia Mungu kwa bidii. Mchana na usiku kilio chao hakikukoma: **"Mapenzi Yako, Ee Mungu, yatimizwe! Kama itakupendeza, fanya njia ya kuwaokoa watu Wako! Tuokoe kutoka kwa mataifa yanayotuzunguka. Yametuweka tayari kwa kifo; lakini mkono Wako unaweza kuleta wokovu."** Hayo ndiyo maneno yote ninayoweza kuyakumbuka. Wote

walionekana kuwa na ufahamu mkubwa wa kutostahili kwao, na walionyesha kujisalimisha kabisa kwa mapenzi ya Mungu; lakini kama Yakobo, kila mmoja bila ubaguzi alikuwa akisihi na kushindana kwa bidii ili aokolewe.

Mara tu baada ya kuanza kilio chao cha dhati, malaika, kwa huruma, walitamani kwenda kuwaokoa. Lakini malaika mmoja mrefu na mwenye mamlaka aliwazuia. Alisema: **"Mapenzi ya Mungu bado hayajatimia. Lazima wakinywe kikombe. Lazima wabatizwe kwa ubatizo."**

Muda mfupi baadaye nilisikia sauti ya Mungu, iliyotikisa mbingu na dunia. Kulikuwa na tetemeko kubwa la nchi. Majengo yalitikiswa na kuanguka kila upande. Kisha nikasikia kelele ya ushindi, yenye sauti kubwa, tamu kama muziki, na iliyo wazi. Niliangalia lile kundi ambalo muda mfupi kabla lilikuwa katika huzuni kubwa na utumwa. Utumwa wao ulikuwa umegeuzwa. Nuru tukufu iliwaangazia. Jinsi walivyokuwa wazuri wakati huo! Alama zote za uchovu na huzuni zilikuwa zimeondoka, na afya na uzuri vilionekana katika kila uso. Maadui zao, mataifa yaliyowazunguka, walianguka kama watu waliokufa; hawakuweza kuvumilia nuru iliyokuwa ikiangaza juu ya wale waliokombolewa na watakatifu. Nuru hii na utukufu vilibaki juu yao mpaka Yesu alipoonekana katika mawingu ya mbinguni. Ndipo kundi hilo la waaminifu waliokuwa wamejaribiwa lilibadilishwa kwa muda mfupi, kufumba na kufumbua, kutoka utukufu hata utukufu. Na makaburi yakafunguliwa, nao watakatifu wakatoka wakiwa wamevikwa kutokufa, wakilia: **"Ushindi juu ya mauti na kaburi!"** Kisha pamoja na watakatifu walio hai walichukuliwa juu kumlaki Bwana wao angani, huku sauti nyingi za utukufu na ushindi zikisikika kutoka katika kila ulimi usiokufa.

## 31. KUSAFIRI KATIKA NJIA NYEMBAMBA

Nilipokuwa Battle Creek, Michigan, mwezi wa Agosti, 1868, niliota ndoto kwamba nilikuwa pamoja na umati mkubwa wa watu. Sehemu ya mkusanyiko huo ilianza safari ikiwa imejiandaa kwa ajili ya kusafiri. Tulikuwa na mabehewa yaliyokuwa yamebebeshwa mizigo mizito. Tulipokuwa tukisafiri, njia ilionekana kupanda juu. Upande mmoja wa njia hiyo kulikuwa na korongo refu lenye kina kirefu; upande mwingine kulikuwa na ukuta mrefu, laini na mweupe....

Tulipoendelea na safari yetu, njia ilizidi kuwa nyembamba na yenye mteremko mkali zaidi. Katika sehemu fulani ilionekana kuwa nyembamba sana kiasi kwamba tuliamua kwamba hatungeweza tena kuendelea na mabehewa yaliyokuwa yamebeba mizigo mizito. Ndipo tukayafungua mabehewa kutoka kwa farasi, tukachukua sehemu ya mizigo kutoka katika mabehewa hayo na kuiweka juu ya farasi, kisha tukaendelea na safari tukiwa tumepanda farasi.

Tulipoendelea mbele, njia iliendelea kuwa nyembamba zaidi. Tulilazimika kujisogeza karibu sana na ukuta ili kujiepusha na kuanguka kutoka katika njia hiyo nyembamba kwenda chini kwenye korongo lenye mteremko mkali. Tulipofanya hivyo, mizigo iliyokuwa juu ya farasi iligusana na ukuta, na kutufanya tugeuke upande wa korongo. Tuliogopa kwamba tungeanguka na kuvunjika vipande vipande juu ya miamba. Ndipo tukakata mizigo kutoka kwa farasi, nayo ikaanguka chini kwenye korongo. Tukaendelea mbele tukiwa tumepanda farasi, tukiwa na hofu kubwa, kwa sababu tulipofikia sehemu nyembamba zaidi za njia, tuliogopa kwamba tungepoteza usawaziko wetu na kuanguka. Katika nyakati hizo, mkono fulani ulionekana kushika hatamu za farasi na kutuongoza katika njia hiyo yenye hatari.

Kadiri njia ilivyozidi kuwa nyembamba, tuliamua kwamba hatungeweza tena kusafiri kwa usalama tukiwa juu ya farasi. Kwa hiyo tuliwaacha farasi na kuendelea kwa miguu, mmoja baada ya mwingine katika mstari mmoja, kila mmoja akifuata nyayo za aliyemtangulia. Katika hatua hii, kamba ndogo zilishushwa kutoka juu ya ukuta ule mweupe safi; nasi kwa hamu tukazishika ili zitusaidie kudumisha usawaziko wetu katika njia ile. Tulipokuwa tukisonga mbele, kamba hiyo iliendelea kusogea pamoja nasi. Hatimaye njia ikawa nyembamba sana kiasi kwamba tuliamua kwamba tungeweza kusafiri kwa usalama zaidi bila viatu vyetu. Kwa hiyo tulivivua kutoka miguuni mwetu, na tukaendelea kwa umbali fulani bila viatu. Baadaye

ikaamuliwa kwamba tungeweza kusafiri kwa usalama zaidi bila soksi zetu; hivyo nazo zikavuliwa, nasi tukaendelea mbele tukiwa na miguu mitupu.

Ndipo tukawakumbuka wale ambao hawakuwa wamejizoesha kwa kujinyima na kuvumilia taabu. Walikuwa wapi sasa? Hawakuwa tena katika kundi hilo. Katika kila mabadiliko ya safari, baadhi yao waliachwa nyuma, na wale waliobaki walikuwa ni wale tu waliozoea kuvumilia magumu. Mateso na kujinyima kwa njia hiyo yaliwafanya wale waliobaki wawe na hamu zaidi ya kusonga mbele mpaka mwisho.

Hatari yetu ya kuanguka kutoka katika njia ile iliongezeka. Tulijisogeza karibu sana na ukuta ule mweupe, lakini hatukuweza kuweka miguu yetu yote juu ya njia hiyo; kwa maana ilikuwa nyembamba mno. Tulisimamisha karibu uzito wetu wote juu ya zile kamba, tukisema kwa sauti: **"Tumeshikilia kutoka juu! Tumeshikilia kutoka juu!"** Maneno hayo hayo yalisemwa na watu wote waliokuwa katika njia ile nyembamba.

Tuliposikia sauti za furaha na sherehe zilizoonekana kutoka kwenye shimo kubwa lililokuwa chini, tulitetemeka. Tulisikia viapo vya makufuru, mizaha michafu, na nyimbo za chini na chafu. Tulisikia nyimbo za vita na nyimbo za kucheza. Tulisikia muziki wa vyombo, na vicheko vikubwa, vilivyochanganyika na laana, vilio vya uchungu, na maombolezo makali. Hivyo tukawa na shauku kubwa zaidi kuliko hapo awali ya kubaki katika njia ile nyembamba na ngumu. Mara nyingi tulilazimika kusimamisha uzito wetu wote juu ya zile kamba, ambazo ziliongezeka ukubwa kadiri tulivyokuwa tukisonga mbele.

Niligundua kwamba ukuta ule mzuri mweupe ulikuwa umechafuliwa kwa damu. Nilihuzunika nilipoona ukuta huo ukiwa na madoa ya damu. Hata hivyo, hisia hiyo ilidumu kwa muda mfupi tu, kwa sababu mara moja nilifikiri kwamba jambo hilo lilikuwa kama lilivyopaswa kuwa. Wale wanaofuata baada yetu watajua kwamba wengine walitangulia kupita katika njia hii nyembamba na ngumu, nao watahitimisha kwamba ikiwa wengine waliweza kuendelea mbele, basi wao pia wanaweza kufanya vivyo hivyo. Na wakati damu itakapomwagika kutoka kwenye miguu yao iliyoumia kwa maumivu, hawatakata tamaa kwa kuvunjika moyo; bali watakapoiona damu juu ya ukuta, watajua kwamba wengine walivumilia maumivu hayo hayo.

Hatimaye tulifika kwenye ufa mkubwa, mahali ambapo njia yetu iliishia. Hakukuwa tena na kitu cha kuongoza miguu yetu, wala kitu cha kukanyagia. Tegemeo letu lote lilipaswa kuwa juu ya zile kamba, ambazo zilikuwa zimeongezeka ukubwa mpaka zilikuwa kama miili yetu. Hapo tulipatwa na mashaka na huzuni kwa muda. Tukauliza kwa sauti za hofu na kunong'ona: **"Kamba hii imefungwa wapi?"** Mume wangu alikuwa mbele yangu. Matone makubwa ya jasho yalikuwa yakimtiririka kutoka kwenye paji la uso wake. Mishipa ya shingo yake na sehemu za pembeni za uso kati ya jicho na sikio zilikuwa imevimba na kuongezeka ukubwa mara mbili ya kawaida. Alitoa miguno iliyozuiwa ya uchungu mkubwa. Jasho lilikuwa likinitoka usoni mwangu, nami nilihisi mateso makubwa ambayo sikuwahi kuyapata kabla. Mapambano ya kutisha yalikuwa mbele yetu. Ikiwa tungeshindwa hapa, matatizo yote tuliyopitia katika safari yangekuwa yamekuwa bure.

Mbele yetu, upande mwingine wa ufa huo, kulikuwa na shamba zuri la majani mabichi, yenye urefu wa karibu sentimita kumi na tano. Sikuweza kuuona mwanga wa jua, lakini miale myepesi na yenye kung'aa, iliyofanana na dhahabu na fedha safi, ilikuwa ikilitanda shamba hilo. Hakuna kitu nilichowahi kuona duniani ambacho kingeweza kulinganishwa na uzuri na utukufu wa shamba hilo. Lakini swali lililokuwa mioyoni mwetu lilikuwa: **Je, tutaweza kufika huko?** Ikiwa kamba ingekatika, tungeangamia. Tukauliza tena kwa sauti za uchungu: **"Ni nini kinachoshikilia kamba hii?"**

Kwa muda mfupi tulisita kuendelea. Ndipo tukasema: **"Tumaini letu pekee ni kutegemea kabisa kamba hii. Imekuwa tegemeo letu katika njia hii yote ngumu. Haitatuangusha sasa."** Lakini bado tulikuwa na mashaka na huzuni. Ndipo maneno yakasikika: **"Mungu ndiye anayeshikilia kamba hii. Hatuna haja ya kuogopa."** Maneno hayo yalirudiwa na wale waliokuwa nyuma yetu, pamoja na kusema: **"Hatatutelekeza sasa. Ametuleta salama mpaka hapa."**

Ndipo mume wangu akajirusha juu ya ufa huo wa kutisha na kufika katika lile shamba zuri upande mwingine. Mara moja nami nikamfuata. Lo, ni hisia gani ya faraja na shukrani kwa Mungu tuliyokuwa nayo! Nilisikia sauti zikinyanyuka kwa sifa za ushindi kwa Mungu. Nilikuwa mwenye furaha, mwenye furaha kabisa.

Nikaamka, na nikagundua kwamba kwa sababu ya wasiwasi niliokuwa nimeupitia katika kuvuka njia hiyo ngumu, kila mshipa wa mwili wangu ulikuwa kama unatetemeka. Ndoto hii haihitaji maelezo zaidi. Ilifanya mvuto mkubwa sana katika akili yangu kiasi kwamba huenda kila sehemu yake itaendelea kuwa wazi mbele yangu muda wote ambao kumbukumbu yangu itaendelea kuwepo.

## 32. KUJITAYARISHA KWA AJILI YA HUKUMU

"Naye akalia masikioni mwangu kwa sauti kuu, akisema, Wakaribieni wale wenye kuangalia mji, kila mtu akiwa na silaha yake ya kuangamiza mkononi mwake." "Naye akamwita yule mtu aliyevaa mavazi ya kitani, aliyekuwa na kidau cha wino cha mwandishi ubavuni mwake; naye Bwana akamwambia, Pita katikati ya mji, katikati ya Yerusalemu, ukatie alama katika vipaji vya nyuso za watu wale wanaougua na kulia kwa sababu ya machukizo yote yanayofanyika katikati yake. Naye akawaambia wengine kwa kusikia kwangu, Nendeni nyuma yake katikati ya mji, mkapige; jicho lenu lisihurumie, wala msiwe na huruma; waueni kabisa wazee na vijana, wasichana na watoto wadogo na wanawake; lakini msimkaribie mtu yeyote aliye na hiyo alama; anzeni katika patakatifu pangu. Basi wakaanza na wale wazee waliokuwa mbele ya nyumba."
**Ezekieli 9:1, 3-6.**

Yesu yuko karibu kuondoka katika kiti cha rehema cha patakatifu pa mbinguni, ili kuvaa mavazi ya kisasi, na kumwaga ghadhabu yake katika hukumu juu ya wale ambao hawajaipokea nuru ambayo Mungu amewapa. "Kwa sababu hukumu juu ya tendo baya haitekelezwi upesi, mioyo ya wanadamu huthibitishwa ndani yao ili kutenda mabaya." **Mhubiri 8:11.** Badala ya kulainishwa na uvumilivu na ustahimilivu mrefu ambao Bwana amewaonyesha, wale wasiomcha Mungu wala wasioipenda kweli, wanaifanya mioyo yao kuwa migumu zaidi katika njia zao mbaya. Lakini kuna mipaka hata kwa uvumilivu wa Mungu, na wengi wanavuka mipaka hiyo. Wamezidi mipaka ya neema; kwa hiyo Mungu lazima aingilie kati na kutetea heshima Yake.

Kuhusu Waamori, Bwana alisema: "Na kizazi cha nne kitarudi hapa, maana haujatimia uovu wa Waamori bado." **Mwanzo 15:16.** Ingawa taifa hili lilijulikana sana kwa ibada yake ya sanamu na upotovu wake, bado halikuwa limekijaza kikombe cha uovu wake, na Mungu hakuwa tayari kutoa amri ya kuangamizwa kwake kabisa. Watu hao walipaswa kuona nguvu ya Mungu ikidhihirishwa kwa namna ya pekee, ili wasiwe na udhuru. Muumba mwenye huruma alikuwa tayari kuvumilia uovu wao mpaka kizazi cha nne. Kisha, ikiwa hakungeonekana mabadiliko yoyote ya kuwa bora, hukumu zake zingewaangukia.

Kwa usahihi usiokosea, Yeye asiye na mwisho bado anaendelea kuhesabu matendo ya mataifa yote. Wakati rehema Yake inapowasilishwa pamoja na mwito wa kutubu, hesabu hiyo

itaendelea wazi; lakini wakati hesabu hiyo itakapofikia kiwango fulani ambacho Mungu amekipanga, kazi ya ghadhabu Yake itaanza. Hesabu inafungwa. Uvumilivu wa Mungu unafikia mwisho. Hakutakuwa tena na maombi ya rehema kwa ajili yao.

Mgogoro mkubwa unakaribia haraka. Wakati wa Mungu wa kuleta hukumu umekaribia. Ingawa Mungu hataki kuadhibu, bado ataadhibu, na kwa haraka. Wale wanaotembea katika nuru wataona ishara za hatari inayokaribia; lakini hawapaswi kukaa kimya, bila kujali, wakisubiri uharibifu, wakijifariji kwa mawazo kwamba Mungu atawalinda watu Wake katika siku ya hukumu. La hasha! Wanapaswa kutambua kwamba ni wajibu wao kufanya kazi kwa bidii ili kuwaokoa wengine, wakimtazamia Mungu kwa imani kubwa ili awasaidie. "*Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana,akiomba kwa bidii*." **Yakobo 5:16.**

Chachu ya utauwa bado haijapoteza nguvu yake yote. Wakati ule ambapo hatari na huzuni ya kanisa vitakapokuwa vikubwa zaidi, kundi dogo linalosimama katika nuru litalia na kuugua kwa sababu ya machukizo yanayofanyika katika nchi. Lakini zaidi sana maombi yao yatainuka kwa ajili ya kanisa, kwa sababu washiriki wake wanafuata mfano wa dunia.

Maombi ya dhati ya kundi hili waaminifu hayatatupwa bure. Wakati Bwana atakapokuja kama mlipiza kisasi, atakuja pia kama mlinzi wa wote waliodumisha imani katika usafi wake, na kujilinda wasichafuliwe na dunia. Ni wakati huu ambapo Mungu ameahidi kulipiza kisasi kwa wateule Wake ambao wanamlilia mchana na usiku, ingawa amewavumilia kwa muda mrefu.

Siku ya kisasi cha Mungu iko karibu sana. Muhuri wa Mungu utawekwa katika vipaji vya nyuso vya wale tu wanaougua na kulia kwa sababu ya machukizo yanayofanyika katika nchi. Wale wanaojiunganisha kwa huruma na dunia, wakila na kunywa pamoja na walevi, hakika wataangamizwa pamoja na watenda maovu. "Macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, Na masikio yake hukielekea kilio chao. Uso wa Bwana ni juu ya watenda mabaya, Aliondoe kumbukumbu lao duniani." **Zaburi 34:15, 16.**

Mwendo wetu wenyewe utaamua kama tutapokea muhuri wa Mungu aliye hai, au tutakatwa kwa silaha za maangamizi. Tayari matone machache ya ghadhabu ya Mungu yameanguka juu ya dunia; lakini wakati mapigo saba ya mwisho yatakapomiminwa bila kuchanganywa na rehema katika kikombe cha hasira Yake, ndipo itakuwa ni kuchelewa milele kutubu na kutafuta mahali pa kujificha. Hakutakuwa tena na damu ya upatanisho itakayoweza kuosha madoa ya dhambi.

"Wakati huo Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako; na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo; na wakati huo watu wako wataokolewa; kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile." **Danieli 12:1.**

Wakati huu wa taabu utakapokuja, kila kesi itakuwa imeamuliwa; hakutakuwa tena na kipindi cha majaribu, wala rehema kwa wale wasiotubu. Muhuri wa Mungu aliye hai utakuwa juu ya watu Wake.

Kundi hili dogo lililosalia, ambalo haliwezi kujilinda katika mapambano ya kifo dhidi ya mamlaka za dunia zilizoandaliwa na jeshi la joka, litamfanya Mungu kuwa ulinzi wao. Amri itakuwa imetolewa na mamlaka kuu ya kidunia kwamba wanapaswa kumwabudu mnyama na kupokea chapa yake, vinginevyo wakabili mateso na kifo. Mungu awasaidie watu Wake sasa, kwa maana wataweza kufanya nini katika pambano hilo la kutisha bila msaada wake?

Ujasiri, uthabiti, imani, na kumtumaini Mungu bila masharti katika uwezo Wake wa kuokoa, haviji kwa muda mfupi. Neema hizi za mbinguni hupatikana kwa uzoefu wa miaka mingi. Kwa maisha ya juhudi takatifu na kushikamana kwa uthabiti na yaliyo sawa, watoto wa Mungu walikuwa wakifunga hatima yao. Wakiwa wamezungukwa na majaribu yasiyohesabika, walijua kwamba walipaswa kuyapinga kwa uthabiti, la sivyo wangeshindwa. Walihisi kwamba walikuwa na kazi kubwa ya kufanya, na kwamba wakati wowote wangeweza kuitwa kuweka chini silaha zao; na ikiwa wangefika mwisho wa maisha yao kazi yao ikiwa haijakamilika, hilo lingekuwa hasara ya milele. Kwa hamu walipokea nuru kutoka mbinguni, kama wanafunzi wa kwanza walivyoipokea kutoka midomoni mwa Yesu. Wakati Wakristo wa kwanza walipofukuzwa kwenda milimani na nyikani, walipoachwa katika magereza kufa kwa njaa, baridi, na mateso, wakati kifo cha kishahidi kilipoonekana kuwa njia pekee ya kutoka katika shida zao, walifurahi kwa sababu walihesabiwa kustahili kuteseka kwa ajili ya Kristo, ambaye alisulubishwa kwa ajili yao. Mfano wao wa thamani utakuwa faraja na moyo kwa watu wa Mungu watakaoletwa katika wakati wa taabu ambao haujawahi kuwapo.

Sio wote wanaodai kushika Sabato watakaotiwa muhuri. Wapo wengi hata miongoni mwa wale wanaowafundisha wengine kweli ambao hawatapokea muhuri wa Mungu katika vipaji vya nyuso zao. Walikuwa na nuru ya kweli, walijua mapenzi ya Bwana wao, walielewa kila jambo la imani yetu, lakini hawakuwa na matendo yanayolingana na imani hiyo. Wale waliokuwa wamezoea sana unabii na hazina za hekima ya Mungu walipaswa kuishi kulingana na imani yao. Walipaswa kuziongoza nyumba zao baada yao, ili kupitia familia iliyo na utaratibu mzuri waweze kuonyesha kwa ulimwengu matokeo ya kweli juu ya moyo wa mwanadamu.

Hakuna hata mmoja wetu atakayepokea muhuri wa Mungu wakati tabia zetu zina doa au unajisi wowote. Ni jukumu letu kurekebisha mapungufu katika tabia zetu, na kusafisha hekalu la roho kutoka kila uchafu. Ndipo mvua ya masika itakapomwagika juu yetu kama mvua ya kwanza ilivyowashukia wanafunzi siku ya Pentekoste.

Tumeridhika kwa urahisi sana na mafanikio yetu. Tunajiona kuwa sisi ni matajiri na tumeongezeka mali, wala hatujui kwamba sisi ni: “maskini, vipofu, na uchi.” **Ufunuo 3:17.** Sasa ni wakati wa kuzingatia onyo la Shahidi wa Kweli: “Nakupa shauri, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona.” **Ufunuo 3:18.**

Katika maisha haya lazima tukabiliane na majaribu ya moto na kutoa dhabihu za gharama kubwa, lakini amani ya Kristo ndiyo thawabu. Kumekuwa na kujikana nafsi kidogo sana, na kuteseka kidogo sana kwa ajili ya Kristo, kiasi kwamba msalaba karibu umesahaulika kabisa. Ni lazima tushiriki mateso ya Kristo ikiwa tunataka kuketi pamoja Naye katika ushindi juu ya kiti Chake cha enzi. Kadiri tunavyochagua njia rahisi ya kujifurahisha wenyewe, na kuogopa kujikana nafsi, ndivyo imani yetu itakosa kuwa imara. Hatuwezi kuijua amani ya Yesu wala furaha inayotokana na ushindi unaotambuliwa moyoni. Wale walioinuliwa zaidi miongoni mwa kundi la waliokombolewa wanaosimama mbele ya kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo, wakiwa wamevaa mavazi meupe, wanaijua vita ya kushinda, kwa maana wametoka katika dhiki kuu. Wale ambao walikubali mazingira badala ya kuingia katika mapambano haya hawatajua jinsi ya kusimama siku ile ambapo uchungu utakuwa juu ya kila nafsi. Hata kama Nuhu, Ayubu, na Danieli wangekuwa katika nchi hiyo, hawangeweza kuwaokoa wana wao wala binti zao; kwa maana kila mmoja atalazimika kuokoa nafsi yake kwa haki yake mwenyewe.

Hakuna anayepaswa kusema kwamba hali yake haina tumaini, au kwamba hawezi kuishi maisha ya Kikristo. Maandalizi kamili yamefanywa kupitia kifo cha Kristo kwa ajili ya kila nafsi. Yesu ndiye msaada wetu wa daima wakati wa uhitaji. Mwite kwa imani, Naye ameahidi kusikia na kujibu maombi yako.

Lo, tunahitaji imani iliyo hai na inayotenda! Tunahitaji kuwa nayo; ni lazima tuwe nayo, la sivyo tutazimia na kushindwa siku ya majaribu. Giza litakalokuwa juu ya njia yetu wakati huo lisituvunje moyo wala kutupeleka katika kukata tamaa. Ni pazia ambalo Mungu analitumia kufunika utukufu Wake anapokuja kutuletea baraka nyingi. Tunapaswa kujua jambo hili kupitia uzoefu wetu wa zamani. Katika siku ile ambapo Mungu atakuwa na mashindano na watu Wake, uzoefu huu utakuwa chanzo cha faraja na tumaini.

Sasa ndiyo wakati wa kujilinda sisi wenyewe na watoto wetu wasichafuliwe na dunia. Sasa ndiyo wakati wa kufua mavazi yetu ya tabia na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo. Sasa ndiyo wakati wa kushinda kiburi, tamaa mbaya, na uvivu wa kiroho. Sasa ndiyo wakati wa kuamka na kufanya juhudi thabiti ili kuwa na tabia kamilifu. “Leo, kama mtaisikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu.” **Waebrania 4:7.** Tuko katika hali ya kujaribiwa sana, tukingojea na kukesha kwa ajili ya kuonekana kwa Bwana wetu. Dunia iko gizani. Lakini Paulo anasema: “Bali ninyi, ndugu, hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwivi.” **1 Wathesalonike 5:4.** Daima ni kusudi la Mungu kuleta nuru kutoka gizani, furaha kutoka huzuni, na pumziko kutoka uchovu kwa ajili ya nafsi inayongoja na kutamani.

**Ndugu, mnafanya nini katika kazi hii kubwa ya kujiandaa?** Wale wanaojiunganisha na dunia wanapokea namny la dunia, na wanajiandaa kwa chapa ya mnyama. Wale wasiojitumaini wenyewe, wanaojinyenyekeza mbele za Mungu, na kutakasa nafsi zao kwa kutii kweli—hao wanapokea namna ya mbinguni, na wanajiandaa kwa muhuri wa Mungu katika

vipaji vya nyuso zao. Wakati amri itakapotolewa, na muhuri utakapowekwa, tabia zao zitabaki safi na zisizo na doa milele.

Sasa ndiyo wakati wa kujiandaa. Muhuri wa Mungu hautawahi kuwekwa juu ya paji la uso wa mwanaume au mwanamke asiye safi. Hautawahi kuwekwa juu ya paji la uso wa mtu mwenye tamaa ya cheo au anayependa dunia. Hautawahi kuwekwa juu ya paji la uso wa watu wenye ndimi za uongo au mioyo yenye udanganyifu. Wote wanaopokea muhuri lazima wasiwe doa mbele za Mungu—wawe wataradhia wa mbingu. **Jifunzeni Maandiko kwa ajili yenu wenyewe, ili mpate kuelewa uzito wa kutisha wa saa hii tuliyopo.**

## 33. MUUNDO NA MAENDELEO

Imekuwa karibu miaka arobaini tangu muundo wa kanisa ulipoanzishwa miongoni mwetu kama watu. *(Kauli hii ilitolewa mwaka 1892.)* Nilikuwa miongoni mwa wale waliokuwa na uzoefu katika kuanzisha muundo huo tangu mwanzo. Ninajua matatizo ambayo yalipaswa kukabiliwa, maovu ambayo muundo huo ulikusudiwa kuyarekebisha, na nimefuatilia ushawishi wake kuhusiana na ukuaji wa kazi ya Mungu. Katika hatua za mwanzo za kazi, Mungu alitupatia nuru maalumu kuhusu jambo hili, na nuru hiyo, pamoja na masomo ambayo uzoefu umetufundisha, vinapaswa kuzingatiwa kwa makini.

Tangu mwanzo kazi yetu ilipaswa kusonga mbele kwa nguvu. Idadi yetu ilikuwa ndogo, na wengi wetu tulitoka katika tabaka la watu maskini. Maoni na mafundisho yetu hayakujulikana sana kwa ulimwengu. Hatukuwa na nyumba za ibada, tulikuwa na machapisho machache tu, na vifaa vya kuendeleza kazi yetu vilikuwa vichache sana. Kondoo walikuwa wametawanyika katika njia kuu na njia za pembeni, mijini, vijijini, na misituni. Amri za Mungu na imani ya Yesu ndiyo iliyokuwa ujumbe wetu.

### Umoja Katika Imani na Mafundisho

Mume wangu, pamoja na Wazee Joseph Bates, Stephen Pierce, Hiram Edson, na wengine waliokuwa wenye akili timamu, waungwana, na waaminifu, walikuwa miongoni mwa wale ambao, baada ya muda kupita mwaka 1844, walitafuta ukweli kama hazina iliyofichwa.

Tulikuwa tukikutana tukiwa tumelemewa mioyoni mwetu, tukiomba kwamba tupate kuwa wamoja katika imani na mafundisho; kwa maana tulijua kwamba Kristo hajagawanyika. Jambo moja baada ya jingine lilifanywa kuwa somo la uchunguzi. Maandiko yalifunguliwa kwa hofu kuu na heshima. Mara nyingi tulifunga, ili tuweze kufaa zaidi kuelewa ukweli. Baada ya maombi ya dhati, ikiwa jambo fulani halikueleweka, lilijadiliwa, na kila mmoja alitoa maoni yake kwa uhuru; kisha tulipiga magoti tena katika maombi, na dua za dhati zilipaa kwenda

mbinguni kwamba Mungu atusaidie kuona jambo moja kwa mtazamo mmoja, ili tupate kuwa wamoja, kama Kristo na Baba walivyo wamoja. Machozi mengi yalimwagika.

Tulitumia masaa mengi kwa kazi hii. Wakati mwingine usiku mzima ulitumika katika uchunguzi wa Maandiko kwa utulivu na heshima kuu, ili tupate kuelewa ukweli kwa ajili ya wakati wetu. Katika baadhi ya nyakati Roho wa Mungu alinijilia, na sehemu ngumu zilifanywa wazi kupitia njia iliyowekwa na Mungu; ndipo kukawa na upatanifu mkamilifu. Sote tulikuwa na nia moja na roho moja.

Tulijitahidi sana kwamba Maandiko yasipotoshwe ili kuendana na mawazo ya mtu yeyote. Tulijaribu kufanya tofauti zetu ziwe ndogo iwezekanavyo kwa kutokazia mambo ambayo hayakuwa ya msingi, ambayo juu yake kulikuwa na maoni tofauti. Lakini mzigo wa kila moyo ulikuwa kuleta hali miongoni mwa ndugu ambayo ingeweza kujibu sala ya Kristo kwamba wanafunzi Wake wawe na umoja kama Yeye na Baba walivyo.

Wakati mwingine ndugu mmoja au wawili walijishikilia kwa ukaidi dhidi ya mtazamo uliokuwa umetolewa, na kuonyesha hisia za asili za moyo; lakini tabia hii ilipojitokeza, tulisitisha uchunguzi wetu na kuahirisha mkutano wetu, ili kila mmoja apate nafasi ya kwenda kwa Mungu katika maombi, na bila mazungumzo na wengine, achunguze jambo hilo lililokuwa tofauti, akiomba nuru kutoka mbinguni. Kwa maneno ya urafiki tuliagana, ili tukutane tena haraka iwezekanavyo kwa uchunguzi zaidi. Wakati mwingine nguvu za Mungu zilikuja juu yetu kwa namna ya pekee, na wakati nuru ya wazi ilipofunua mambo ya ukweli, tulilia na kufurahi pamoja. Tulimpenda Yesu; tulipendana sisi kwa sisi.

**Kuanzishwa kwa Utaratibu wa Kanisa**

Idadi yetu iliongezeka taratibu. Mbegu iliyopandwa ilinyunyiziwa na Mungu, Naye akaikuza. Mwanzoni tulikusanyika kwa ajili ya ibada, na kuwasilisha ukweli kwa wale waliokuja kusikiliza, katika nyumba za watu binafsi, jikoni, maghalani, vichakani, na katika nyumba za shule; kwa muda mfupi kabla hatujaweza kujenga nyumba za ibada za heshima.

Kadiri idadi yetu ilivyoongezeka, ilikuwa wazi kwamba bila aina fulani ya utaratibu wa kanisa kungekuwa na machafuko makubwa, na kazi isingeweza kusonga mbele kwa mafanikio. Ili kutoa mahitaji ya huduma ya injili, kuendeleza kazi katika maeneo mapya, kulinda makanisa pamoja na huduma dhidi ya washiriki wasiostahili, kushikilia mali za kanisa, kuchapisha ukweli kupitia vyombo vya habari, na kwa mambo mengine mengi, muundo ulikuwa wa lazima.

Hata hivyo, kulikuwa na hisia kubwa za kupinga jambo hili miongoni mwa watu wetu. Waadventista wa Siku ya Kwanza walipinga utaratibu wa kanisa, na wengi wa Waadventista wa Sabato walikuwa na mawazo hayo hayo. Tulimtafuta Bwana kwa maombi ya dhati ili tupate kuelewa mapenzi Yake, na nuru ilitolewa kupitia Roho Wake kwamba lazima kuwe na utaratibu

na nidhamu kamili katika kanisa—kwamba muundo ulikuwa wa muhimu sana. Mfumo na utaratibu vinaonekana katika kazi zote za Mungu katika ulimwengu mzima. Utaratibu ni sheria ya mbingu, na unapaswa kuwa sheria ya watu wa Mungu duniani.

**Kuingia Katika Miradi Mipya**

Tulikuwa na mapambano makubwa katika kuanzisha utaratibu wa kanisa. Licha ya kwamba Bwana alitoa ushuhuda baada ya ushuhuda kuhusu jambo hili, upinzani ulikuwa mkubwa sana, na ulipaswa kukabiliwa tena na tena. Lakini tulijua kwamba Bwana Mungu wa Israeli alikuwa akituongoza na kutuongoza kwa njia ya majaliwa Yake. Tuliingia katika kazi ya kuanzisha utaratibu, na maendeleo makubwa yaliambatana na hatua hii ya kusonga mbele.

Kadiri maendeleo ya kazi yalivyotuhitaji kuingia katika miradi mipya, tulikuwa tayari kuianzisha. Bwana alielekeza mawazo yetu kwenye umuhimu wa kazi ya elimu. Tuliona hitaji la shule, ili watoto wetu waweze kupata mafundisho yaliyo huru kutokana na makosa ya falsafa za uongo, na ili mafunzo yao yawe katika upatanifu na kanuni za Neno la Mungu. Hitaji la taasisi ya afya lilikuwa limesisitizwa kwetu, kwa ajili ya msaada na mafundisho kwa watu wetu wenyewe, na pia kama njia ya kuwa baraka na kuleta nuru kwa wengine. Mradi huu pia uliendelezwa. Yote haya yalikuwa kazi ya umisionari ya kiwango cha juu kabisa.

**Matokeo ya Juhudi za Umoja**

Kazi yetu haikuendelezwa kwa kutegemea zawadi kubwa au urithi; kwa maana tulikuwa na watu wachache wenye mali nyingi miongoni mwetu. Ni siri gani ya mafanikio yetu? Tumesonga mbele chini ya maagizo ya Kiongozi wa wokovu wetu. Mungu amebariki juhudi zetu za umoja. Ukweli umeenea na kustawi. Taasisi zimeongezeka. Mbegu ya haradali imekua na kuwa mti mkubwa. Mfumo wa utaratibu wa kanisa umeonyesha kuwa ni mafanikio makubwa. Utoaji kwa mpango (*systematic benevolence*) uliingizwa kulingana na mpango wa Biblia. Mwili "umeunganishwa kwa kile ambacho kila kiungo hutoa." Kadiri tulivyosonga mbele, mfumo wetu wa utaratibu umeendelea kuthibitika kuwa wenye ufanisi.

**Kuepuka Hatari za Machafuko**

Mtu yeyote hapaswi kushabikia la wazo kwamba tunaweza kuachana na utaratibu wa kanisa. Umetugharimu mawazo mengi, na maombi mengi ya kutafuta hekima ambayo tunajua Mungu ameyajibu, ili kujenga muundo huu. Umejengwa kwa maelekezo Yake, kupitia kujitoa sana, dhabihu nyingi, na mapambano. Ndugu zangu msidanganyike kiasi cha kujaribu kuubomoa; kwa maana kwa kufanya hivyo mtaleta hali ambayo hamuiwazi. Kwa jina la Bwana nawatangazia kwamba utaratibu huu lazima udumu, ukiimarishwa, ukiwekwa imara, na kusimamishwa kwa uthabiti. Kwa amri ya Mungu, "Songa mbele," tuliendelea wakati matatizo yaliyopaswa kushindwa yalipoonekana kufanya hatua hiyo isiwezekane. Tunajua ni gharama

gani iliyolipwa katika kutekeleza mipango ya Mungu hapo zamani, ambayo imetufanya kuwa vile (watu) tulivyo leo. Kwa hiyo, kila mmoja awe mwangalifu sana asiwasumbue au kuwavuruga watu katika mambo ambayo Mungu ameyaweka kwa ajili ya ustawi wetu na mafanikio yetu katika kuendeleza kazi Yake.

Malaika hufanya kazi kwa upatano. Utaratibu mkamilifu hutawala mienendo yao yote. Kadiri tunavyoiga kwa karibu zaidi upatano na utaratibu wa jeshi la malaika, ndivyo juhudi za wajumbe hawa wa mbinguni zitakavyokuwa na mafanikio zaidi kwa ajili yetu. Ikiwa hatuoni umuhimu wa kutenda kwa umoja na kwa upatano, na tukawa watu wasio na utaratibu, wasio na nidhamu, na wasio na mpangilio katika mwenendo wetu wa kazi, malaika ambao wamepangwa kikamilifu na wanaotenda kwa utaratibu mkamilifu, hawawezi kufanya kazi kwa mafanikio kwa ajili yetu. Wao huondoka kwa huzuni, kwa maana hawajaidhinishwa kubariki machafuko, vurugu, na ukosefu wa mpangilio. Wote wanaotamani ushirikiano wa wajumbe wa mbinguni lazima wafanye kazi kwa umoja pamoja nao. Wale walio na upako kutoka juu, katika juhudi zao zote watahimiza utaratibu, nidhamu, na umoja wa matendo; ndipo malaika wa Mungu wataweza kushirikiana nao. Lakini kamwe, kamwe wajumbe hawa wa mbinguni hawataweka kibali chao juu ya hali ya kutokuwa na utaratibu, kutokuwepo kwa mpangilio, na machafuko. Maovu haya yote ni matokeo ya juhudi za Shetani za kudhoofisha nguvu zetu, kuharibu ujasiri wetu, na kuzuia matendo yenye mafanikio.

Shetani anajua vizuri kwamba mafanikio yanaweza kupatikana tu kwa utaratibu na utendaji wenye upatano. Anajua kwamba kila kitu kinachohusiana na mbingu kiko katika utaratibu mkamilifu, kwamba utii na nidhamu kamili vinaonekana katika mienendo ya jeshi la malaika. Ni juhudi zake za makusudi kuwaongoza Wakristo wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo mbali kadiri awezavyo kutoka katika mpango wa mbinguni. Kwa hiyo huwadanganya hata watu wanaodai kuwa wa Mungu, na kuwafanya waamini kwamba utaratibu na nidhamu ni maadui wa hali ya kiroho; kwamba usalama wao pekee ni kila mmoja kufuata njia yake mwenyewe, na kujitenga hasa na makundi ya Wakristo waliooungana na wanaojitahidi kuimarisha nidhamu na upatano wa matendo. Juhudi zote zinazofanywa kuanzisha utaratibu huonekana kuwa hatari, kana kwamba ni kuzuia uhuru unaostahili; kwa hiyo huogopwa kama vile upapa. Roho hizi zinazodai kujitoa kwa Mungu huona ni sifa kujivunia uhuru wao wa kufikiri na kutenda kwa kujitegemea. Hawataki kukubali maoni ya mtu yeyote. Hawawajibiki kwa mtu yeyote. Nilionyeshwa kwamba ni kazi maalumu ya Shetani kuwaongoza watu kuhisi kwamba ni mpango wa Mungu kwao kujitenga na wengine, kuchagua njia yao wenyewe, bila kujali ndugu zao.

**Wajibu Binafsi na Umoja wa Kikristo**

Mungu anawaongoza watu kutoka katika ulimwengu na kuwaweka juu ya jukwaa tukufu la ukweli wa milele, yaani amri za Mungu na imani ya Yesu. Atawafundisha na kuwaandaa watu Wake. Hawatakuwa katika hali ya kutokubaliana, mmoja akiamini jambo fulani na mwingine akiwa na imani na mtazamo unaopingana kabisa; kila mmoja akifanya kazi kivyake bila kujali

mwili wa kanisa. Kupitia utofauti wa karama na huduma alizoweka katika kanisa, wote wataufikia umoja wa imani. Ikiwa mtu mmoja atachukua mtazamo wake kuhusu ukweli wa Biblia bila kujali maoni ya ndugu zake, na kutetea njia yake kwa kusema kwamba ana haki ya kuwa na mtazamo wake binafsi, kisha akausukuma kwa wengine, atawezaje kutimiza sala ya Kristo? Na ikiwa mwingine na mwingine watajitokeza, kila mmoja akidai haki yake ya kuamini na kusema kile apendacho bila kujali imani ya mwili wa kanisa, utapatikana wapi ule upatano uliokuwepo kati ya Kristo na Baba Yake, ambao Kristo aliomba uwepo kati ya ndugu Zake?

Ingawa tuna kazi binafsi na wajibu binafsi mbele za Mungu, hatupaswi kufuata hukumu zetu wenyewe bila kujali maoni na hisia za ndugu zetu; kwa maana njia hiyo ingeleta machafuko katika kanisa. Ni wajibu wa wahudumu kuheshimu maamuzi ya ndugu zao; lakini mahusiano yao wao kwa wao, pamoja na mafundisho wanayofundisha, yanapaswa kupimwa kwa sheria na ushuhuda; ndipo, ikiwa mioyo iko tayari kufundishwa, hakutakuwa na migawanyiko kati yetu. Wengine wana mwelekeo wa kutokuwa na utaratibu, na wanaanza kuachana na alama kuu za imani; lakini Mungu anafanya kazi kwa watumishi Wake ili wawe wamoja katika mafundisho na katika roho.

Ni muhimu kwamba umoja wetu leo uwe wa aina itakayoweza kustahimili majaribu. Tuna masomo mengi ya kujifunza, na mengi sana ya kuyaacha. Mungu na mbingu pekee ndio hawakosei. Wale wanaofikiri kwamba hawatawahi kuacha mtazamo waliouzoea, wala hawatawahi kubadilisha maoni yao, watakatishwa tamaa. Kadiri tunavyoshikilia mawazo na maoni yetu wenyewe kwa ukaidi, hatuwezi kuwa na ule umoja ambao Kristo aliomba.

Ikiwa ndugu anapopokea nuru mpya kutoka katika Maandiko, anapaswa kueleza msimamo wake kwa uwazi; na kila mhudumu anapaswa kuyachunguza Maandiko kwa moyo wa uaminifu ili kuona kama mambo yanayowasilishwa yanaweza kuthibitishwa kwa Neno lililoongozwa na Roho. “Tena haimpasi mtumwa wa Bwana kuwa mgomvi; bali kuwa mwanana kwa watu wote, awezaye kufundisha, mvumilivu; akiwaonya kwa upole wao washindanao naye, ili kama ikiwezekana, Mungu awape kutubu na kuijua kweli.” **2 Timotheo 2:24, 25**

**Kile Mungu Alichotenda!**

Tunapotazama historia yetu ya zamani, baada ya kupitia kila hatua ya maendeleo hadi kufikia hali tuliyo nayo sasa, naweza kusema: **Mungu Atukuzwe!** Ninapoona yale ambayo Mungu ametenda, najazwa na mshangao na imani katika Kristo kama Kiongozi wetu. Hatuna chochote cha kuogopa kwa wakati ujao, isipokuwa tusahau jinsi Bwana alivyotuongoza, pamoja na mafundisho Yake katika historia yetu ya zamani.

Sasa sisi ni watu wenye nguvu, ikiwa tutamtumaini Bwana; kwa maana tunashughulikia kweli kuu za Neno la Mungu. Tuna kila sababu ya kushukuru. Ikiwa tutatembea katika nuru inayotuangazia kutoka katika maneno yaliyo hai ya Mungu, tutakuwa na majukumu makubwa

yanayolingana na nuru kuu tuliyopewa na Mungu. Tuna wajibu mwingi wa kutekeleza, kwa sababu tumewekwa kuwa watunzaji wa ukweli mtakatifu ambao unatakiwa kutolewa kwa ulimwengu katika uzuri wake wote na utukufu wake. Tuna deni kwa Mungu kutumia kila fursa aliyotukabidhi ili kuuvika ukweli kwa utakatifu wa tabia, na kuupeleka ujumbe wa onyo, faraja, tumaini, na upendo kwa wale walio katika giza la makosa na dhambi.

Mshukuruni Mungu kwa yale ambayo tayari yamefanyika katika kuwapatia vijana wetu vituo kwa ajili ya mafunzo ya kidini na kiakili. Wengi wameelimishwa ili kushiriki katika sehemu mbalimbali za kazi, si katika Amerika pekee, bali pia katika nchi za kigeni. Mashine ya uchapishaji imetoa machapisho ambayo yameeneza maarifa ya ukweli mbali na karibu. Hebu zawadi zote ambazo, kama vijito vidogo vilivyoongezeka na kuwa mto mkubwa wa ukarimu, zitambuliwe kuwa sababu ya kumshukuru Mungu.

Leo tunalo jeshi la vijana ambalo linaweza kufanya mengi ikiwa litaelekezwa na kutiwa moyo ipasavyo. Tunataka watoto wetu wauamini ukweli. Tunataka wabarikiwe na Mungu. Tunataka washiriki katika mipango iliyopangwa vizuri kwa ajili ya kuwasaidia vijana wengine. Hebu wote wafundishwe ili waweze kuuwakilisha ukweli kwa usahihi, wakitoa sababu ya tumaini lililo ndani yao, na kumheshimu Mungu katika tawi lolote la kazi ambalo wamehitimu kulifanyia kazi.

Kama wanafunzi wa Kristo, ni wajibu wetu kueneza nuru ambayo tunajua kwamba ulimwengu hauna. Hebu watu wa Mungu: “Watende mema, wawe matajiri kwa kutenda mema, wawe tayari kutoa mali zao, washirikiane na wengine kwa moyo; huku wakijiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate uzima ulio kweli kweli.” **1 Timotheo 6:18, 19.**

## 34. UPENDO WA MUNGU KWA KANISA

**George's Terrace, St. Kilda Road, Melbourne, Desemba 23, 1892.**

**Ndugu wapendwa wa Konferensi Kuu:**

Ninawashuhudia ndugu na dada zangu kwamba kanisa la Kristo, ingawa ni dhaifu na lenye mapungufu, ndio chombo pekee duniani ambacho Kristo hukipatia kipaumbele na kulijali kwa kiwango cha juu kabisa. Wakati anapoutolea ulimwengu wote mwaliko wa kuja Kwake na kuokolewa, anawaagiza malaika Wake kutoa msaada wa kimungu kwa kila nafsi inayokuja Kwake kwa toba na unyenyekevu. Naye mwenyewe huja kwa njia ya Roho Wake Mtakatifu na kukaa katikati ya kanisa Lake. "Bwana, kama Wewe ungehesabu maovu, Ee Bwana, nani angesimama? Lakini kwako kuna msamaha, Ili Wewe uogopwe. Nimemngoja Bwana, roho yangu imengoja, Na neno lake nimelitumainia. Nafsi yangu inamngoja Bwana, Kuliko walinzi waingojavyo asubuhi, Naam, walinzi waingojao asubuhi." **Zaburi 130:3-6** "Ee Israeli, umtarajie Bwana; Maana kwa Bwana kuna fadhili, Na kwake kuna ukombozi mwingi. Yeye atamkomboa Israeli na maovu yake yote." **Zaburi 130:7-8**

Watumishi na kanisa lote, hebu maneno haya yawe kauli yetu, yakitoka katika mioyo inayojibu wema mkuu na upendo wa Mungu kwetu kama watu na kwetu binafsi: "Israeli na amtumaini Bwana tangu sasa na hata milele." "Ninyi msimamao nyumbani mwa Bwana, Nyuani mwa nyumba ya Mungu wenu. Msifuni Bwana kwa kuwa Bwana ni mwema, Liimbieni jina lake kwa maana lapendeza. Kwa sababu Bwana amejichagulia Yakobo, Na Israeli, wawe watu wake hasa. Maana najua mimi ya kuwa Bwana ni mkuu, Na Bwana wetu yu juu ya miungu yote." Zaburi 135:2-5 Ndugu na dada zangu, tafakarini jambo hili: Bwana anao watu Wake, watu waliochaguliwa, yaani kanisa Lake, ambalo ni Lake mwenyewe. Kanisa hilo ni ngome Yake mwenyewe, ambayo anaishikilia katikati ya ulimwengu uliojaa dhambi na uliomwasi Mungu. Na Mungu amekusudia kwamba ndani ya kanisa hilo kusiwe na mamlaka nyingine inayotambuliwa, wala sheria nyingine inayokubalika, isipokuwa mamlaka na sheria Zake mwenyewe.

Shetani ana ushirika mkubwa, yaani kanisa lake. Kristo analiita **sinagogi la Shetani**, kwa sababu washiriki wake ni watoto wa dhambi. Washiriki wa kanisa la Shetani wamekuwa wakifanya kazi daima ili kuiondoa sheria ya Mungu, na kuchanganya tofauti kati ya mema na mabaya. Shetani anafanya kazi kwa nguvu kubwa ndani na kupitia watoto wa uasi, ili kuinua usaliti na uasi dhidi ya Mungu kuwa ukweli na uaminifu. Na wakati huu nguvu ya uvuvio wake wa kishetani inawasukuma mawakala walio hai kutekeleza uasi mkuu dhidi ya Mungu ambao ulianzia mbinguni.

Katika wakati huu, kanisa linapaswa kuvaa mavazi yake mazuri: **"Kristo, Haki Yetu."** Tofauti zilizo wazi na thabiti zinapaswa kurejeshwa na kuonyeshwa mbele ya ulimwengu, kwa kuinua juu amri za Mungu na imani ya Yesu. Uzuri wa utakatifu unapaswa kuonekana katika mng'ao wake wa asili, ukitofautiana na ubaya na giza la wale wasio waaminifu, yaani wale waliomwasi Mungu na kuasi sheria Yake. Kwa njia hii tunamtambua Mungu, na kutambua sheria Yake, ambayo ndiyo msingi wa serikali Yake mbinguni na katika falme Zake zote duniani. Mamlaka Yake yanapaswa kuwekwa wazi na kutofautishwa mbele ya ulimwengu; na hakuna sheria zinazopaswa kukubaliwa ambazo zinapingana na sheria za Yehova. Ikiwa, kwa kukaidi mipango ya Mungu, ulimwengu utaruhusiwa kuathiri maamuzi au matendo yetu, kusudi la Mungu litakuwa limeangushwa. Haijalishi kisingizio hicho kinaonekana kuwa cha kuvutia kiasi gani, ikiwa kanisa litasita katika jambo hili, limeandikwa dhidi yake katika vitabu vya mbinguni kuwa ni **usaliti wa amana takatifu kabisa**, na ni **hiana kwa ufalme wa Kristo**. Kanisa linapaswa kushikilia kwa uthabiti na kwa uamuzi kanuni zake mbele ya ulimwengu wote wa mbinguni na falme zote za dunia. Uaminifu thabiti katika kulinda heshima na utakatifu wa sheria ya Mungu utavuta macho na hata mshangao wa ulimwengu, na wengi wataongozwa, kwa matendo mema watakayoyaona, kumtukuza Baba yetu aliye mbinguni. Waaminifu na wa kweli wanabeba alama za mamlaka ya mbinguni, si za watawala wa duniani. Watu wote watajua ni akina nani walio wanafunzi wa Kristo, waliochaguliwa na waaminifu; na watawatambua watakapotiwa taji na kutukuzwa kuwa wale waliomheshimu Mungu, na ambao Mungu amewaheshimu, akiwaingiza katika urithi wa **utukufu wa milele usio na kifani**.

Bwana amelipatia kanisa Lake uwezo na baraka, ili liweze kuuonyesha ulimwengu mfano wa utoshelevu Wake mwenyewe. Na ili kanisa Lake liwe kamili ndani Yake, likiwa uwakilishi wa kudumu wa ulimwengu mwingine, yaani ulimwengu wa milele, wenye sheria zilizo juu kuliko sheria za duniani. Kanisa Lake linapaswa kuwa hekalu lililojengwa kwa mfano wa kimungu. Mjenzi mkuu wa kimalaika ameleta kutoka mbinguni kipimo chake cha dhahabu, ili kila jiwe lichongwe na kusawazishwa kwa kipimo cha Mungu, na kung'arishwa ili ling'ae kama alama ya mbingu, likitoa pande zote miale angavu na safi ya **Jua la Haki**. Kanisa linapaswa kulishwa kwa mana kutoka mbinguni, na kuwekwa chini ya ulinzi pekee wa neema Yake. Likiwa limevikwa silaha kamili za nuru na haki, linaingia katika pambano lake la mwisho. Mabaki machafu, vitu visivyofaa, vitateketezwa, na mvuto wa ukweli utashuhudia kwa ulimwengu tabia yake ya kutakasa na kuinua.

Bwana Yesu anafanya majaribio katika mioyo ya wanadamu kwa kuonyesha rehema Yake na neema Yake nyingi. Analeta mabadiliko ya ajabu kiasi kwamba Shetani, pamoja na majivuno yake yote ya ushindi, na pamoja na ushirika wake wote wa uovu ulioungana dhidi ya Mungu na sheria za serikali Yake, anasimama akiyaona kama ngome isiyoweza kupenywa kwa hila na udanganyifu wake. Kwa Shetani, haya ni siri isiyoeleweka. Malaika wa Mungu—maserafi na makerubi, pamoja na mamlaka zilizowekwa kushirikiana na wanadamu—hutazama kwa mshangao na furaha kwamba wanadamu walioanguka, ambao zamani walikuwa watoto wa ghadhabu, kupitia mafunzo ya Kristo wanajenga tabia inayofanana na ya Mungu. Wanakuwa wana na binti za Mungu, ili washiriki sehemu muhimu katika kazi na furaha za mbinguni.

Kristo amelipa kanisa Lake uwezo wa kutosha ili apokee utukufu mwingi kutoka kwa wale aliowakomboa na kuwanunua. Kanisa, likiwa limevikwa haki ya Kristo, ni ghala Lake, mahali ambapo utajiri wa rehema Yake, upendo Wake, na neema Yake unapaswa kuonekana kwa utimilifu na udhihirisho wa mwisho. Tangazo katika sala Yake ya maombezi kwamba: upendo wa Baba kwetu ni mkubwa kama ule aliokuwa nao kwa Mwanawe pekee, na kwamba tutakuwa pamoja Naye pale alipo, tukiwa wamoja milele na Kristo pamoja na Baba, ni jambo la kushangaza kwa jeshi la mbinguni, na ni furaha yao kuu. Kipawa cha Roho Wake Mtakatifu—kilicho kwa wingi, kamili, na tele—kitakuwa kwa kanisa Lake kama **ukuta wa moto unaolizunguka**, ambao nguvu za kuzimu hazitaweza kuushinda. Katika usafi wake usiochafuliwa na ukamilifu wake usio na doa, Kristo anawaona watu Wake kama: thawabu ya mateso Yake yote, matokeo ya udhalilishaji Wake, tunda la upendo Wake, na nyongeza ya utukufu Wake. Kristo ndiye kitovu kikuu ambacho kutoka Kwake hutoka utukufu wote. **“Heri walioalikwa kwenye karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo.”** (Ufunuo 19:9)

## 35. KAZI YA UMISHONARI

Mnamo Desemba 10, 1871, nilionyeshwa kwamba Mungu angefanya kazi kubwa kupitia kweli, ikiwa watu waliojitolea, wenye kujikana nafsi, wangejitoa bila masharti katika kazi ya kuiwasilisha kwa wale walio gizani. Wale walio na ujuzi wa kweli ya thamani, na ambao wamewekwa wakfu kwa Mungu, wanapaswa kutumia kila fursa ambapo kuna nafasi ya kuingia na kuisukuma kweli mbele. Malaika wa Mungu wanafanya kazi katika mioyo na dhamiri za watu wa mataifa mengine, na nafsi zaaminifu zinasumbuliwa wanapoona ishara za nyakati katika hali ya kutotulia ya mataifa. Swali linazuka mioyoni mwao: **"Mwisho wa mambo haya yote utakuwa nini?"** Wakati Mungu na malaika wanafanya kazi ya kugusa mioyo, watumishi wa Kristo wanaonekana kuwa wamelala. Ni wachache sana wanaofanya kazi kwa umoja na wajumbe wa mbinguni.

Ikiwa wahudumu na watu wangeamka vya kutosha, wasingebaki katika hali hiyo ya kutojali, wakati Mungu amewaheshimu kwa kuwafanya kuwa washika sheria Yake, kwa kuiandika katika akili zao na kuiweka katika mioyo yao. Kweli hizi zenye umuhimu wa milele zinapaswa kuwa kipimo kwa ulimwengu; lakini hata katika nchi yetu wenyewe kuna miji, vijiji, na maeneo ambayo hayajawahi kusikia ujumbe wa onyo. Vijana wanaochochewa na mwito uliotolewa wa kusaidia katika kazi hii kubwa ya kusogeza mbele kazi ya Mungu, hufanya hatua fulani za mwanzo, lakini hawapati mzigo wa kazi moyoni mwao kiasi cha kutimiza kile ambacho wangeweza kufanya.

Ikiwa vijana wanaoanza kufanya kazi katika kazi hii wangekuwa na roho ya kimisionari, wangeonyesha kwamba kwa hakika Mungu amewaita katika kazi hiyo. Lakini wanapokataa kwenda katika maeneo mapya, na kuridhika tu kuhama kutoka kanisa moja kwenda kanisa jingine, wanaonyesha kwamba mzigo wa kazi hauko juu yao. Mawazo ya wahubiri wetu vijana hayajapanuka vya kutosha. Bidii yao ni dhaifu sana. Ikiwa vijana wangekuwa macho na wamejitoa kwa Bwana, wangekuwa na bidii kila dakika ya wakati wao, na wangetafuta kujitayarisha ili wawe watenda kazi katika eneo la umishonari.

Vijana wanapaswa kujitayarisha kwa kujifunza lugha nyingine, ili Mungu aweze kuwatumia kama vyombo vya kuwasilisha kweli Yake ya wokovu kwa watu wa mataifa mengine. Vijana hawa wanaweza kupata ujuzi wa lugha nyingine hata wakati wanapokuwa wakifanya kazi ya kuwavuta wenye dhambi kwa Kristo. Ikiwa watatumia muda wao kwa uangalifu na kwa uchumi, wanaweza kuendeleza akili zao, na kujitayarisha kwa matumizi makubwa zaidi. Ikiwa wanawake vijana ambao wamebeba majukumu machache wangejitoa kwa Mungu, wangeweza kujitayarisha kwa manufaa kwa kujifunza na kufahamu lugha nyingine. Wangeweza kujitoa katika kazi ya kutafsiri.

Machapisho yetu yanapaswa kuchapishwa katika lugha nyingine, ili mataifa ya kigeni yaweze kufikiwa. *(Wakati maneno haya yaliandikwa mwaka 1871, mwanzo tu ulikuwa umefanywa katika kuandaa na kuchapisha machapisho ya dhehebu katika lugha mbalimbali za Ulaya na nchi nyingine.)* Mengi yanaweza kufanywa kupitia njia ya uchapishaji, lakini bado mengi zaidi yanaweza kutimizwa ikiwa ushawishi wa kazi ya wahubiri walio hai utaambatana na machapisho yetu. Wamishonari wanahitajika kwenda katika mataifa mengine ili kuhubiri kweli kwa njia yenye tahadhari na uangalifu. Kazi ya kweli ya sasa inaweza kupanuliwa sana kupitia juhudi binafsi.

Wakati makanisa yatakapowaona vijana wenye bidii wakijitayarisha ili kupanua kazi zao katika miji, vijiji, na maeneo ambayo hayajawahi kuchochewa kusikia kweli, na wamishonari wakijitolea kwenda katika mataifa mengine ili kuwapelekea kweli, makanisa yatahamasishwa na kutiwa nguvu zaidi kuliko kama yangepokea tu huduma za vijana wasio na uzoefu. Wanapoona mioyo ya wahudumu wao ikiwa imewaka kwa upendo na bidii kwa ajili ya kweli, pamoja na shauku ya kuokoa nafsi, makanisa yataamka na kuchochewa. Kwa kawaida, makanisa haya yana karama na nguvu ndani yao wenyewe za kujibariki na kujitia nguvu, na kukusanya kondoo na wana-kondoo katika zizi. Yanahitaji kuwekwa katika hali ya kutumia uwezo wao wenyewe, ili karama zote zilizolala bila kutumika ziweze kuitwa katika huduma hai.

Bwana amefanya kazi mioyoni mwa watu wa lugha nyingine, na amewaleta chini ya ushawishi wa kweli, ili waweze kustahili kufanya kazi katika kazi Yake. Amewaleta karibu na ofisi ya uchapishaji, ili wasimamizi wake waweze kutumia huduma zao, ikiwa wangekuwa macho kwa mahitaji ya kazi ya Mungu. Machapisho yanahitajika katika lugha nyingine, ili kuamsha shauku na roho ya kuuliza maswali miongoni mwa mataifa mengine.

Kama vile mahubiri ya Nuhu yalivyowaonya, kuwajaribu, na kuwathibitisha wenyeji wa ulimwengu kabla ya gharika ya maji kuwaangamiza kutoka juu ya uso wa dunia, vivyo hivyo kweli ya Mungu kwa siku hizi za mwisho inafanya kazi kama hiyo ya kuonya, kujaribu, na kuthibitisha ulimwengu. Machapisho yanayotoka katika ofisi ya uchapishaji yana muhuri wa Yule wa Milele. Yanasambazwa katika nchi yote, na yanaamua hatima za nafsi. Sasa wanahitajika sana watu wanaoweza kutafsiri na kuandaa machapisho yetu katika lugha nyingine, ili ujumbe wa onyo uweze kuwafikia mataifa yote, na kuwajaribu kwa nuru ya kweli; ili

wanaume na wanawake, wanapoiona nuru hiyo, wageuke kutoka katika uasi na kuingia katika utii wa sheria ya Mungu.

Kila nafasi inapaswa kutumiwa ili kupeleka kweli katika mataifa mengine. Hili litahitaji gharama kubwa kwa kiasi fulani, lakini gharama hiyo haipaswi kamwe kuwa kizuizi cha kufanya kazi hii. Fedha zina thamani tu pale zinapotumiwa kusogeza mbele maslahi ya ufalme wa Mungu. Bwana amewakopesha watu fedha kwa kusudi hili hasa, ili wazitumie kupeleka kweli kwa wanadamu wenzao.

Sasa ndio wakati wa kutumia mali kwa ajili ya Mungu. Sasa ndio wakati wa kuwa **matajiri katika matendo mema**, tukijiwekea hazina msingi mzuri kwa ajili ya wakati ujao, ili tupate kuushika uzima wa milele. Nafsi moja iliyookolewa katika ufalme wa Mungu ina thamani kubwa kuliko utajiri wote wa dunia. Tunawajibika mbele za Mungu kwa ajili ya nafsi za wale tunaokutana nao, na kadiri uhusiano wetu na wanadamu wenzetu unavyokuwa karibu, ndivyo uwajibikaji wetu unavyokuwa mkubwa zaidi. Sisi ni undugu mmoja mkubwa wa wanadamu, na ustawi wa wenzetu unapaswa kuwa jambo letu kuu. Hatuna hata muda mmoja wa kupoteza. Ikiwa tumekuwa wazembe katika jambo hili, ni wakati wa sasa kuwa na bidii, ili kukomboa muda, isije damu ya nafsi ikaonekana juu ya mavazi yetu. Kama watoto wa Mungu, hakuna hata mmoja wetu aliye na udhuru wa kutoshiriki katika kazi kubwa ya Kristo ya kuokoa wanadamu wenzetu.

Itakuwa kazi ngumu kushinda chuki zilizojengwa na kuwashawishi wasioamini kwamba juhudi zetu za kuwasaidia hazina ubinafsi. Lakini jambo hili halipaswi kuzuia kazi yetu. Hakuna amri katika Neno la Mungu inayotuambia tufanye mema kwa wale tu wanaothamini na kuitikia juhudi zetu, au kuwasaidia wale tu watakaotushukuru kwa ajili yake. Mungu ametutuma kufanya kazi katika shamba Lake la mizabibu. Jukumu letu ni kufanya yote tunayoweza. “Asubuhi panda mbegu zako, Wala jioni usiuzuie mkono wako. Kwa maana wewe hujui ni zipi zitakazofanikiwa, kama ni hii au hii, au kama zote zitafaa sawasawa.” **Mhubiri 11:6**

Tuna imani ndogo sana. Tunamwekea mipaka Mtakatifu wa Israeli. Tunapaswa kushukuru kwamba Mungu anajishusha kutumia yeyote miongoni mwetu kama vyombo Vyake. Kwa kila ombi la dhati linalotolewa kwa imani kwa ajili ya jambo lolote, majibu yatarudi. Huenda yasije kama tulivyotarajia; lakini yatakuja—labda si kwa namna tuliyopanga, bali kwa wakati ule ule ambao tunayahitaji zaidi. Lakini, ole, jinsi gani kutokuamini kwetu kulivyo dhambi! “Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa..”
**Yohana 15:7**.

## 36. MIPANGO MIKUBWA ZAIDI

Nilipokuwa California katika mwaka wa 1874, nilipewa ndoto yenye kuvutia sana, ambayo ndani yake ilionyeshwa jinsi chombo cha uchapishaji kinavyotumika katika kazi ya kupeleka ujumbe wa malaika wa tatu kwa ulimwengu.

Niliota kwamba baadhi ya ndugu huko California walikuwa katika mkutano wa mashauriano, wakifikiria mpango bora wa kufanya kazi katika msimu uliokuwa unakuja. Baadhi yao walifikiri kwamba ingekuwa busara kuepuka miji mikubwa, na kufanya kazi katika maeneo madogo. Mume wangu alikuwa akisisitiza kwa bidii kwamba mipango mipana zaidi iwekwe, na juhudi zilizopanuliwa zaidi zifanywe, ambazo zingelingana vizuri zaidi na tabia ya ujumbe wetu.

Ndipo kijana mmoja ambaye mara nyingi nilikuwa nimemwona katika ndoto zangu, akaingia katika mkutano huo wa mashauriano. Alisikiliza kwa shauku kubwa maneno yaliyokuwa yakisemwa, kisha, baada ya kutafakari kwa makini, alisema kwa ujasiri wenye mamlaka:

**"**Miji na vijiji ni sehemu ya shamba la mizabibu la Bwana. Lazima isikie ujumbe wa onyo. Adui wa kweli anafanya juhudi kubwa za kukata tamaa ili kuwageuza watu kutoka katika kweli ya Mungu na kuwaelekeza kwenye uongo.... Mnapaswa kupanda mbegu kando ya maji yote.

Huenda msione mara moja matokeo ya kazi yenu, lakini jambo hili lisiwavunje moyo. Mfanye Kristo kuwa mfano wenu. Alikuwa na wasikilizaji wengi, lakini wafuasi wachache. Nuhu alihubiri kwa miaka mia moja na ishirini kwa watu kabla ya gharika; lakini kati ya makundi mengi ya watu waliokuwa duniani wakati huo, ni watu wanane tu waliookolewa."

Mjumbe huyo aliendelea kusema: **"**Mna mawazo madogo sana kuhusu kazi ya wakati huu. Mnajaribu kupanga kazi kwa namna ambayo mnaweza kuishika yote mikononi mwenu. Lazima muwe na mtazamo mpana zaidi. Nuru yenu haipaswi kuwekwa chini ya pishi wala chini

ya kitanda, bali iwekwe juu ya kinara, ili iangaze kwa wote waliomo nyumbani. Nyumba yenu ni ulimwengu."

"Uhakika na ukweli wa madai yanayowafunga watu ya amri ya nne lazima viwasilishwe kwa watu kwa uwazi kabisa. 'Ninyi ni mashahidi Wangu.' Ujumbe utaenda kwa nguvu katika sehemu zote za ulimwengu, kwenda Oregon, Ulaya, Australia, visiwa vya baharini, kwa mataifa yote, lugha zote, na watu wote. Dumisheni heshima ya kweli. Itakua na kufikia kiwango kikubwa. Nchi nyingi zinangojea nuru ya ziada ambayo Bwana anayo kwa ajili yao; lakini imani yenu ina mipaka, ni ndogo sana. Mtazamo wenu kuhusu kazi hii unahitaji kupanuliwa sana. Oakland, San Francisco, Sacramento, Woodland, na miji mikubwa katika Marekani lazima isikie ujumbe wa kweli. Songeni mbele. Mungu atafanya kazi kwa nguvu kuu ikiwa mtatembea mbele Zake kwa unyenyekevu wote wa moyo. Si imani kuzungumza juu ya mambo yasiyowezekana. Hakuna lisilowezekana kwa Mungu. Nuru ya madai yanayowafunga watu ya sheria ya Mungu itakuwa kipimo na jaribio kwa ulimwengu."

Katika maono yangu ya mwisho nilionyeshwa kwamba tunapaswa kuwa na sehemu ya kufanya katika California katika kupanua na kuimarisha kazi ambayo tayari imeanzishwa. Nilionyeshwa kwamba kazi ya umishonari lazima ifanywe katika California, Australia, Oregon, na maeneo mengine kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko watu wetu walivyowahi kufikiria, kutazamia, au kupanga. Nilionyeshwa kwamba kwa sasa hatuendi kwa kasi ile ambayo uongozi wa Mungu katika majaliwa Yake unatufungulia njia. Nilionyeshwa kwamba **kweli ya sasa** inaweza kuwa nguvu kubwa katika California ikiwa waumini wa ujumbe huu hawatampa adui nafasi kwa njia ya kutokuamini na ubinafsi, bali wataelekeza juhudi zao kwenye lengo moja—yaani, **kujenga na kuimarisha kazi ya kweli ya sasa.**

Niliona kwamba kungekuwa na gazeti litakalochapishwa katika pwani ya Pasifiki. Kungeanzishwa taasisi ya afya huko, na nyumba ya uchapishaji ingeundwa.

Muda ni mfupi; na wote wanaoamini ujumbe huu wanapaswa kuhisi wajibu mtakatifu ulio juu yao wa kuwa wafanyakazi wasio na ubinafsi, wakitumia ushawishi wao upande ulio sahihi, na kamwe wasipatikane kwa neno au tendo wakiwa wamejipanga dhidi ya wale wanaotafuta kusogeza mbele maslahi ya kazi ya Mungu. Mawazo ya ndugu zetu ni madogo mno. Wanatarajia mambo machache sana. Imani yao ni ndogo mno.

Gazeti litakalochapishwa katika pwani ya Pasifiki lingetia nguvu na kutoa ushawishi kwa ujumbe. Nuru ambayo Mungu ametupa haina thamani kubwa kwa ulimwengu ikiwa haiwezi kuonekana kwa kuwasilishwa mbele yao. Ninawaambia kwamba **maono yetu lazima yapanuliwe.** Tunaona mambo yaliyo karibu, lakini hatuoni yaliyo mbali.

## 37. KUPANUA KAZI KATIKA NCHI ZA KIGENI

Neno linanijia wakati wa usiku ili niseme kwa makanisa yanayojua kweli: **"Ondoka, uangaze; kwa maana nuru yako imekuja, na utukufu wa Bwana umekuzukia." Isaya 60:1.**

Maneno ya Bwana katika sura ya hamsini na nne ya Isaya ni kwa ajili yetu: "Panua mahali pa hema yako, na wayatandaze mapazia ya maskani yako; usiwakataze; ongeza urefu wa kamba zako; vikaze vigingi vya hema yako. Kwa maana utaenea upande wa kuume na upande wa kushoto; na wazao wako watawamiliki mataifa; wataifanya miji iliyokuwa ukiwa kukaliwa na watu. Usiogope; maana hutatahayarika; wala usifadhaike; maana hutaaibishwa; kwa kuwa utaisahau aibu ya ujana wako, pia mashutumu ya ujane wako hutayakumbuka tena. Kwa sababu Muumba wako ni mume wako; Bwana wa majeshi ndilo jina lake; na Mtakatifu wa Israeli ndiye Mkombozi wako; Yeye ataitwa Mungu wa dunia yote." Isaya 54:2-5.

Na maneno ya Kristo kwa wanafunzi Wake pia ni kwa ajili ya watu Wake leo: "Hamsemi ninyi, Bado miezi minne, ndipo yaja mavuno? Tazama, mimi nawaambieni, Inueni macho yenu myatazame mashamba, ya kuwa yamekwisha kuwa meupe, tayari kwa mavuno. Naye avunaye hupokea mshahara, na kukusanya matunda kwa uzima wa milele, ili yeye apandaye na yeye avunaye wapate kufurahi pamoja." Yohana 4:35, 36.

Watu wa Mungu wana kazi kubwa iliyo mbele yao, kazi ambayo lazima iendelee kuongezeka katika umuhimu na upana. Juhudi zetu katika kazi za kimisionari lazima ziwe pana zaidi sana. Kazi iliyo thabiti zaidi kuliko ile iliyofanyika tayari lazima ifanywe kabla ya kuonekana mara ya pili kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Watu wa Mungu hawapaswi kuacha kazi yao mpaka watakapouzunguka ulimwengu mzima.

Shamba la mizabibu linajumuisha ulimwengu wote, na kila sehemu yake inapaswa kufanyiwa kazi. Kuna maeneo ambayo sasa ni nyika za kiroho, na hayo yanapaswa kufanywa kuwa kama bustani ya Bwana. Maeneo ya dunia yaliyo ukiwa yanapaswa kulimwa, ili yaweze kuchipua na kuchanua kama waridi. Maeneo mapya yanapaswa kufanyiwa kazi na watu waliojazwa na Roho Mtakatifu. Makanisa mapya lazima yaanzishwe, na makundi mapya yapangwe na kuundwa. Kwa wakati huu, kunapaswa kuwa na wawakilishi wa **kweli ya sasa** katika kila mji na katika sehemu za mbali za dunia. Dunia yote inapaswa kuangazwa kwa utukufu wa kweli ya Mungu. Nuru inapaswa kung'aa katika nchi zote na kwa watu wote. Na nuru hiyo inapaswa kutoka kwa wale ambao wameipokea. Nyota ya asubuhi imewachomozea, na tunapaswa kuangaza nuru yake katika njia za wale walio gizani.

Mgogoro uko karibu sana nasi. Sasa tunapaswa, kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, kutangaza kweli kuu za siku hizi za mwisho. Muda si mrefu kila mtu atakuwa amesikia onyo na kufanya uamuzi wake. Ndipo mwisho utakapokuja.

Kiini kabisa cha imani yote ya kweli ni **kufanya jambo lililo sahihi kwa wakati unaofaa.** Mungu ndiye Mtaalamu Mkuu wa kazi, na kwa majaliwa Yake huandaa njia ili kazi Yake itimizwe. Yeye huandaa nafasi, hufungua njia za ushawishi, na njia za kufanya kazi. Ikiwa watu Wake wataangalia ishara za uongozi Wake katika majaliwa, na kuwa tayari kushirikiana Naye, wataona kazi kubwa ikikamilishwa. Juhudi zao, zikiwa zimeelekezwa kwa usahihi, zitaleta matokeo mara mia zaidi kuliko yale ambayo yangeweza kupatikana kwa kutumia njia na rasilimali zilezile katika eneo jingine ambalo Mungu hafanyi kazi kwa namna hiyo ya wazi. Kazi yetu ni kazi ya **matengenezo na uamsho**, na ni kusudi la Mungu kwamba ubora wa kazi katika kila eneo uwe somo la mfano kwa watu. Katika maeneo mapya hasa, ni muhimu kwamba kazi ianzishwe kwa namna ambayo itatoa mfano sahihi wa kweli. Katika mipango yetu yote ya shughuli za kimisionari, kanuni hizi zinapaswa kuwekwa akilini....

Walinzi wa Mungu wanapaswa kusimama juu ya kuta za Sayuni, na kutoa onyo hili: **"Asubuhi inakuja, na pia usiku,"** — usiku ambao ndani yake hakuna mtu awezaye kufanya kazi....

Kilio kinakuja kutoka katika nchi za mbali: **"Vuka uje utusaidie."** Maeneo haya hayafikiwi kwa urahisi, wala hayako tayari kwa mavuno kama yalivyo mashamba yaliyo karibu zaidi na macho yetu; lakini hayapaswi kupuuzwa....

Ndugu zetu hawajatambua kwamba kwa kusaidia kusogeza mbele kazi katika nchi za kigeni, wangekuwa wanasaidia pia kazi ya nyumbani. Kile kinachotolewa kuanzisha kazi katika eneo moja kitasababisha kuimarishwa kwa kazi katika maeneo mengine. Wakati wafanyakazi wanapowekwa huru kutoka katika hali ya vikwazo na matatizo, juhudi zao zinaweza kupanuliwa zaidi. Kadiri nafsi zinavyoletwa katika kweli, na makanisa yanapoanzishwa, nguvu za kifedha zitaongezeka. Hivi karibuni makanisa hayo yataweza si tu kuendeleza kazi ndani ya mipaka yao wenyewe, bali pia kusaidia maeneo mengine. Hivyo mzigo unaobebwa na makanisa ya nyumbani utagawanywa.

Kazi ya umishonari ya nyumbani itaendelea mbele kwa kila namna wakati roho ya ukarimu zaidi, kujikana nafsi, na kujitoa mhanga itaonekana kwa ajili ya ustawi wa kazi ya utume ugenini. Kwa maana ustawi wa kazi ya nyumbani, chini ya Mungu, unategemea kwa kiasi kikubwa ushawishi unaorudi kutoka katika kazi ya injili inayofanyika katika nchi za mbali. Ni kwa kufanya kazi kwa bidii ili kukidhi mahitaji ya kazi ya Mungu ndipo tunapowasiliana na Chanzo cha nguvu zote.

Ingawa kazi katika nchi za kigeni haijasonga mbele kama ilivyopaswa kusonga, bado kile kilichofanyika kinatupa sababu ya kumshukuru Mungu na msingi wa kutiwa moyo. Fedha chache sana zimetumika katika maeneo hayo ukilinganisha na maeneo ya nyumbani, na kazi imefanyika chini ya shinikizo kubwa zaidi na bila vifaa vinavyostahili. Lakini tunapozingatia msaada uliotumwa katika maeneo hayo, matokeo yake kwa kweli yanashangaza. Mafanikio yetu katika umishonari yamekuwa sawia kabisa na juhudi zetu za kujikana nafsi na kujitoa mhanga.

Mungu pekee ndiye awezaye kukadiria kazi iliyotimizwa wakati ujumbe wa injili umetangazwa kwa njia iliyo wazi na ya moja kwa moja. Maeneo mapya yameingiliwa, na kazi ya kusonga mbele kwa nguvu imefanyika. Mbegu za kweli zimepandwa, nuru imeangaza katika akili nyingi, na kuleta mtazamo mpana zaidi juu ya Mungu pamoja na uelewa sahihi zaidi kuhusu tabia inayopaswa kujengwa. Maelfu wameletwa katika ujuzi wa kweli iliyo ndani ya Kristo Yesu. Wamejazwa imani itendayo kazi kwa upendo na kuitakasa nafsi.

Thamani ya faida hizi za kiroho iko juu ya uwezo wetu wa kuelewa. Ni kipimo gani kinaweza kupima kina cha neno lililohubiriwa? Ni mizani gani inayoweza kupima kwa usahihi ushawishi wa wale waliogeuzwa kuingia katika kweli? Nao kwa upande wao wanakuwa wamishonari, wakifanya kazi kwa ajili ya wengine. Katika maeneo mengi nyumba za ibada zimejengwa. Biblia, Biblia ya thamani sana, inasomwa. Maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye anakaa pamoja nao.

Na tushangilie kwamba kazi ambayo Mungu anaweza kuikubali imefanyika katika maeneo haya. Kwa jina la Bwana, na tuinue sauti zetu kwa sifa na shukrani kwa ajili ya matokeo ya kazi iliyofanyika ng'ambo.

Na bado Jemadari wetu, ambaye kamwe hafanyi kosa, anatuambia: **"Songeni mbele. Ingieni katika maeneo mapya. Inueni juu bendera katika kila nchi. 'Ondoka, uangaze; kwa maana nuru yako imekuja, na utukufu wa Bwana umekuzukia.'"**

Neno letu la vita linapaswa kuwa: **"Mbele, daima mbele."** Malaika wa Mungu watatutangulia ili kutuandalia njia. Mzigo wetu kwa ajili ya **"maeneo yaliyo nje zaidi"** haupaswi kamwe kuondolewa mpaka dunia yote itakapong'aa kwa utukufu wa Bwana.

## 38. **KUSAMBAZA UKURASA ULIOCHAPISHWA**

Wasemaji kadhaa walikuwa wamehubiri mbele ya makutano makubwa na yenye usikivu katika mkutano wa hema huko Roma, New York, siku ya kwanza ya juma, tarehe 12 Septemba 1875. Usiku uliofuata niliota kwamba kijana mmoja mwenye sura ya heshima aliingia katika chumba nilichokuwa, mara tu baada ya mimi kumaliza kuzungumza. Alisema:

**"**Umeelekeza mawazo ya watu kwenye mambo muhimu, ambayo kwa idadi kubwa ya watu ni mageni na mapya. Kwa wengine mambo hayo yanawavutia sana. Watendakazi katika neno na mafundisho wamefanya walichoweza katika kuwasilisha kweli. Lakini isipokuwa juhudi kamili zaidi ifanywe ili kuyaimarisha mawazo haya katika akili za watu, juhudi zenu zitakuwa karibu bure. Shetani ana vivutio vingi vilivyo tayari kuvuta akili; na mahangaiko ya maisha haya pamoja na udanganyifu wa mali vyote vinashirikiana kukaba mbegu ya kweli iliyopandwa moyoni."

**"**Katika kila juhudi kama hii mnayofanya sasa, matokeo makubwa zaidi yangepatikana kupitia kazi zenu ikiwa mngekuwa na machapisho yanayofaa tayari kwa ajili ya kusambazwa. Vipeperushi vinavyohusu mambo muhimu ya kweli kwa wakati huu vinapaswa kutolewa kwa uhuru kwa wote watakaovipokea. Mnapaswa kupanda mbegu kando ya maji yote."

"Uchapishaji ni njia yenye nguvu ya kusogeza akili na mioyo ya watu.Watu wa ulimwengu huu wanaitumia sana mashine ya uchapishaji, na hutumia kila nafasi kuweka mbele ya watu maandishi yenye sumu. Ikiwa watu walio chini ya ushawishi wa roho ya ulimwengu na wa Shetani wana bidii katika kusambaza vitabu, vipeperushi, na magazeti yenye tabia ya kuharibu, ninyi mnapaswa kuwa na bidii zaidi katika kuwapelekea watu maandishi yenye tabia ya kuinua na kuokoa."

"Mungu amewaweka watu Wake katika nafasi ya kutumia faida zinazopatikana kupitia uchapishaji, ambazo zikiunganishwa na vyombo vingine, zitafanikiwa katika kueneza maarifa ya kweli. Vipeperushi, magazeti, na vitabu, kulingana na mahitaji, vinapaswa kusambazwa katika miji yote na vijiji vyote vya nchi. Hapa ndipo kuna kazi ya umishonari kwa wote."

"Kunapaswa kuwepo na watu waliozoezwa kwa ajili ya tawi hili la kazi ambao watakuwa wamisionari, na ambao watasambaza machapisho. Wanapaswa kuwa watu wenye mwenendo mzuri, ambao hawatawafukuza wengine wala kukataliwa na wengine. Hii ni kazi ambayo inawastahili watu kuitoa muda wao wote na nguvu zao kadiri hali inavyohitaji. Mungu amelikabidhi watu Wake nuru kuu. Hii si kwa ajili yao kuifurahia kwa ubinafsi peke yao, bali ni kwa ajili ya kuziacha miale yake iangaze kwa wengine walio katika giza la upotovu.

Hamfanyi kama watu hata sehemu moja ya ishirini ya kile mnachoweza kufanya katika kueneza maarifa ya kweli. Mambo mengi zaidi yanaweza kutimizwa na mhubiri hai akiwa pamoja na usambazaji wa magazeti na vijitabu kuliko kwa kuhubiri Neno pekee bila machapisho. Chombo cha uchapishaji ni chombo chenye nguvu ambacho Mungu amekikusudia kiunganishwe na nguvu za mhubiri hai ili kupeleka kweli mbele ya mataifa yote, makabila yote, lugha zote, na watu wote. Akili nyingi zinaweza kufikiwa kwa njia hii pekee.

Hapa kuna kazi halisi ya kimisionari ambayo ndani yake nguvu na mali vinaweza kuwekezwa na kupata matokeo bora zaidi. Kumekuwa na hofu kubwa sana ya kuchukua hatua kwa imani, na kupanda mbegu kando ya maji yote. Fursa zimekuwa zikitolewa lakini hazijakamatwa wala kutumiwa ipasavyo. Kumekuwa na hofu kubwa mno ya kuthubutu. Imani ya kweli si kujitumainia kupita kiasi, bali ni kuthubutu mambo makubwa. Nuru ya thamani na kweli yenye nguvu vinapaswa kutolewa katika machapisho bila kuchelewa.

Akasema: "Mume wako hapaswi kuvunjwa moyo katika juhudi zake za kuwahimiza watu kuwa wafanyakazi, na kuwajibika kwa kazi muhimu. Kila mtu ambaye Mungu atamtumia, Shetani atamshambulia. Ikiwa watajitenga na mbingu, na kulihatarisha kazi ya Mungu, kushindwa kwao hakutahesabiwa kwake wala kwako, bali kutahesabiwa kwa ukaidi na upotovu wa asili ya wale walalamikaji ambao hawakutaka kuelewa na kushinda tabia zao. Watu hawa ambao Mungu amewajaribu kuwatumia kufanya kazi Yake, lakini wakashindwa, na hivyo kuwaletea mizigo mikubwa wale waliokuwa wasio na ubinafsi na waaminifu, wamezuia na kukatisha tamaa zaidi kuliko mema yote waliyoyafanya. Hata hivyo, jambo hili lisizuie kusudi la Mungu la kuwa na kazi hii inayokua, pamoja na mizigo yake ya majukumu, igawanywe katika matawi mbalimbali, na kuwekwa juu ya watu wanaopaswa kufanya sehemu yao na kubeba mizigo inapopaswa kubebwa. Watu hawa lazima wawe tayari kufundishwa, ndipo Mungu aweze kuwaandaa na kuwatakasa, na kuwapa hukumu takatifu, ili kile wanachokifanya waweze kukitekeleza kwa jina Lake.

## 39. MTAZAMO WA PAMBANO

Katika maono niliona majeshi mawili yakiwa katika mapambano makali sana. Jeshi moja liliongozwa na bendera zilizokuwa na alama ya dunia; jeshi lingine liliongozwa na bendera yenye damu ya Mfalme Emmanueli. Bendera moja baada ya nyingine ilianguka mavumbini, wakati kundi baada ya kundi kutoka katika jeshi la Bwana lilipojiunga na adui, na kabila baada ya kabila kutoka katika safu za adui lilijiunga na watu wa Mungu wanaozishika amri. Malaika aliyekuwa akiruka katikati ya mbingu aliweka bendera ya Emmanueli katika mikono ya watu wengi, huku jemadari mkuu akipaza sauti kwa nguvu: Ingieni katika mstari. Wale walio waaminifu kwa amri za Mungu na ushuhuda wa Kristo sasa na wachukue nafasi zao. Tokeni kati yao, mjitenge, wala msiguse kitu kilicho najisi, nami nitawapokea, nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa wanangu wa kiume na wa kike. Wote wanaotaka, na waje kusaidia kazi ya Bwana, kusaidia kazi ya Bwana dhidi ya wenye nguvu.

Vita viliendelea kwa ukali. Ushindi ulibadilika kutoka upande mmoja kwenda mwingine. Mara askari wa msalaba walirudi nyuma: "kama vile mchukuzi wa bendera azimiavyo." **Isaya 10:18.** Lakini kurudi kwao nyuma kulikuwa kwa muda tu ili kupata nafasi bora zaidi ya kushambulia. Kelele za furaha zilisikika. Wimbo wa kumsifu Mungu ulipanda juu, na sauti za malaika zikaungana katika wimbo huo, wakati askari wa Kristo walipoinua bendera Yake juu ya kuta za ngome zilizokuwa zikishikiliwa na adui. Nahodha wa wokovu wetu alikuwa akiongoza vita, akituma msaada kwa askari Wake. Nguvu Zake zilionyeshwa kwa namna kuu, zikiwatia moyo kusukuma vita hadi malangoni. Aliwafundisha mambo ya kutisha katika haki alipokuwa akiwaongoza hatua kwa hatua, wakishinda na kuendelea kushinda.

Hatimaye ushindi ulipatikana. Jeshi lililofuata bendera yenye maandishi: **"Amri za Mungu, na imani ya Yesu,"** lilishinda kwa utukufu mkubwa. Askari wa Kristo walikuwa karibu na malango ya mji, na kwa furaha mji ulimkaribisha Mfalme wake. Ufalme wa amani, furaha, na haki ya milele ukawekwa imara.

### Kanisa Lenye Ushindi

Sasa kanisa liko katika hali ya kupigana vita. Sasa tunakabiliana na ulimwengu ulio katika giza kuu la usiku wa manane, karibu wote ukiwa umejitoa kwa ibada ya sanamu. Lakini siku inakuja ambayo vita vitakuwa vimepigwa, na ushindi utakuwa umepatikana. Mapenzi ya Mungu yatatendeka duniani kama yanavyotendeka mbinguni. Ndipo mataifa hayatakuwa na sheria nyingine isipokuwa sheria ya mbinguni. Wote watakuwa familia yenye furaha na umoja, wakiwa wamevikwa mavazi ya sifa na shukrani—vazi la haki ya Kristo. Asili yote, katika uzuri wake mkuu usioelezeka, itamtolea Mungu sifa na ibada daima. Dunia itajawa na nuru ya mbingu. Miaka itaendelea katika furaha. Nuru ya mwezi itakuwa kama nuru ya jua, na nuru ya jua

itakuwa mara saba zaidi kuliko ilivyo sasa. Juu ya mandhari hiyo, nyota za asubuhi zitaimba pamoja, na wana wa Mungu watapiga kelele kwa furaha, wakati Mungu na Kristo watakapoungana kutangaza: “Hapatakuwa na dhambi tena, wala hapatakuwa na mauti tena.”

**Kusimama Katika Ulinzi**

Hii ndiyo mandhari niliyoonyeshwa. Lakini kanisa lazima lipigane, na litapigana, dhidi ya maadui wanaoonekana na wasioonekana. Mawakala wa Shetani katika umbo la kibinadamu wako duniani. Wanadamu wameungana ili kumpinga Bwana wa majeshi. Muungano huu utaendelea mpaka Kristo atakapoondoka katika nafasi Yake ya uombezi mbele ya kiti cha rehema, na kuvaa mavazi ya kisasi. Mawakala wa kishetani wako katika kila mji, wakifanya kazi kwa bidii kupanga makundi ya wale wanaopinga sheria ya Mungu. Wale wanaodai kuwa watakatifu na wale wasioamini waziwazi wanasimama pamoja katika makundi haya. Huu si wakati wa watu wa Mungu kuwa dhaifu. Hatuwezi kuruhusu kuwa bila ulinzi hata kwa muda mmoja.

**“***Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake. Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani. Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama. Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani, na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani; zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu*” **Waefeso 6:10-17.**

**“***Na hii ndiyo dua yangu, kwamba pendo lenu lizidi kuwa jingi sana, katika hekima na ufahamu wote; mpate kuyakubali yaliyo mema; ili mpate kuwa na mioyo safi, bila kosa, mpaka siku ya Kristo; hali mmejazwa matunda ya haki, kwa njia ya Yesu Kristo, kwa utukufu na sifa ya Mungu.* **Wafilipi 1:9-11.**

**“***Lakini mwenendo wenu na uwe kama inavyoipasa Injili ya Kristo, ili, nikija na kuwaona ninyi, au nisipokuwapo, niyasikie mambo yenu, kama mnasimama imara katika roho moja, kwa moyo mmoja mkiishindania imani ya Injili; wala hamwaogopi adui zenu, katika neno lo lote; kwao hao ni ishara mathubuti ya kupotea, bali kwenu ninyi ni ishara ya wokovu, huo utokao kwa Mungu.9 Maana mmepewa kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu, ila na kuteswa kwa ajili yake***”** **Wafilipi 1:27-29.**

Katika siku hizi za mwisho, maono ya utukufu wa wakati ujao yamefunuliwa—mandhari zilizochorwa kwa mkono wa Mungu—na mambo haya yanapaswa kuwa ya thamani kwa kanisa Lake. Ni nini kilichomtegemeza Mwana wa Mungu wakati wa kusalitiwa Kwake na

kuhukumiwa Kwake? Aliona matokeo ya mateso ya nafsi Yake, naye akaridhika. Aliona ukubwa wa milele, na akaona furaha ya wale ambao kupitia kudhalilishwa Kwake wangepokea msamaha na uzima wa milele. Alijeruhiwa kwa ajili ya makosa yao, alichubuliwa kwa ajili ya maovu yao. Adhabu iliyowaletea amani ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake waliponywa. Sikio Lake lilisikia sauti ya furaha ya waliokombolewa. Alisikia aliokombolewa wakiimba wimbo wa Musa na Mwana-Kondoo.

Lazima tuwe na maono ya wakati ujao na baraka za mbingu. Simama kwenye kizingiti cha milele, na usikie ukaribisho wa neema unaotolewa kwa wale ambao katika maisha haya walishirikiana na Kristo, wakiona kuwa ni heshima na pendeleo kuteseka kwa ajili Yake. Wanapoungana na malaika, wanatupa taji zao miguuni mwa Mkombozi wakisema: **"***Astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, kuupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka. Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya nchi ya juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake, nalivisikia, vikisema, Baraka na heshima na utukufu na uweza una yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele***."** **Ufunuo 5:12, 13.**

Huko waliokombolewa wanawasalimu wale waliowaelekeza kwa Mwokozi aliyeinuliwa. Wanaungana katika kumsifu Yeye aliyekufa ili wanadamu waweze kuwa na uzima unaolingana na uzima wa Mungu. Vita vimekwisha. Dhiki zote na mapambano yote yamekwisha. Nyimbo za ushindi zinajaza mbingu yote wakati waliokombolewa wanaposimama kuzunguka kiti cha enzi cha Mungu. Wote wanaimba wimbo wa furaha: **"Astahili, astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, naye anaishi tena, mshindi mwenye ushindi."**

**"***Baada ya hayo nikaona, na tazama, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele za Mwana-Kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao; wakilia kwa sauti kuu wakisema, Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo."* **Ufunuo 7:9, 10.**

**"***Nikamwambia, Bwana wangu, wajua wewe. Akaniambia, Hao ndio wanatoka katika dhiki ile iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo. Kwa hiyo wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu lake, na yeye aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema yake juu yao. Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote. Kwa maana huyo Mwana-Kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga, naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao." "wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita***."** **Ufunuo 7:14-17; 21:4.**

## 40. THAWABU YA JUHUDI ZA DHATI

*"Kazi ya mtu aliyoijenga juu yake ikikaa, ... atapokea thawabu."* **1 Wakorintho 3:14.** Itakuwa tukio la utukufu jinsi gani thawabu itakayotolewa wakati watendakazi waaminifu watakapokusanyika kuzunguka kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo. Yohana, alipokuwa bado katika hali yake ya kibinadamu, alipoona utukufu wa Mungu, alianguka kama mtu aliyekufa; hakuweza kustahimili maono hayo. Lakini wakati watoto wa Mungu watakapovaa kutokufa, **"watamwona kama alivyo." 1 Yohana 3:2.** Watasimama mbele ya kiti cha enzi, wakiwa wamekubaliwa katika Mpendwa. Dhambi zao zote zimefutwa. Makosa yao yote yameondolewa. Sasa wanaweza kuutazama utukufu usio na pazia wa kiti cha enzi cha Mungu. Wamekuwa washirika pamoja na Kristo katika mateso Yake, wamekuwa watendakazi pamoja Naye katika mpango wa ukombozi, na sasa wanashiriki pamoja Naye katika furaha ya kuona roho zikiokolewa katika ufalme wa Mungu, ambako watamsifu Mungu milele yote.

### Furaha za Waliokombolewa

Ndugu yangu, dada yangu, ninakusihi ujitayarishe kwa ajili ya kuja kwa Kristo katika mawingu ya mbingu. Kila siku acha kuipenda dunia moyoni mwako. Elewa kwa uzoefu maana ya kuwa na ushirika pamoja na Kristo. Jitayarishe kwa ajili ya Hukumu, ili Kristo atakapokuja, ili kutukuzwa katika wote waaminio, uwe miongoni mwa wale watakaokutana Naye kwa amani. Katika siku hiyo, waliokombolewa wataangaza katika utukufu wa Baba na wa Mwana. Malaika, wakigusa vinubi vyao vya dhahabu, watamkaribisha Mfalme na nyara Zake za ushindi—wale ambao wameoshwa na kufanywa weupe katika damu ya Mwana-Kondoo. Wimbo wa ushindi utasikika, ukijaza mbingu yote. Kristo ameshinda. Anaingia katika nyua za mbinguni, akiwa ameandamana na waliokombolewa Wake, ambao ni mashahidi kwamba kazi Yake ya mateso na kujitoa haikuwa bure.

Ufufuo na kupaa kwa Bwana wetu ni ushahidi hakika wa ushindi wa watakatifu wa Mungu juu ya mauti na kaburi, na ni ahadi kwamba mbingu iko wazi kwa wale wanaofua mavazi yao ya tabia na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo. Yesu alipaa kwenda kwa Baba kama mwakilishi wa jamii ya wanadamu, na Mungu atawaleta wale wanaodhihirisha sura Yake ili wamwone na kushiriki pamoja Naye utukufu Wake.

Kuna makao kwa ajili ya wasafiri wa duniani. Kuna mavazi kwa ajili ya wenye haki, pamoja na taji za utukufu na mitende ya ushindi. Kila jambo ambalo limetutatiza katika matendo ya Mungu litaelezwa wazi katika ulimwengu ujao. Mambo ambayo yalikuwa magumu kueleweka ndipo yatakapopata maelezo yake. Siri za neema zitafunuliwa mbele yetu. Mahali ambapo akili zetu zenye mipaka ziliona tu mkanganyiko na ahadi zilizovunjika, tutaona

upatanifu mkamilifu na uzuri mkuu. Tutajua kwamba upendo usio na mwisho uliongoza mambo yaliyokuwa yanaonekana kuwa majaribu makubwa zaidi. Tunapotambua utunzaji wa upendo wa Yeye afanyaye mambo yote kufanya kazi pamoja kwa ajili ya mema yetu, tutafurahi kwa furaha isiyosemeka na iliyojaa utukufu. Maumivu hayawezi kuwepo katika mazingira ya mbingu. Katika makao ya waliokombolewa hakutakuwa na machozi, wala misafara ya mazishi, wala alama za huzuni. **"***Wala hapana mwenyeji atakayesema, Mimi mgonjwa; watu wakaao humo watasamehewa uovu wao.***"** **Isaya 33:24.** Mto mmoja wenye utajiri wa furaha utazidi kutiririka na kuongezeka kadiri umilele unavyoendelea.

Bado tuko katikati ya vivuli na misukosuko ya shughuli za duniani. Hebu tuyatafakari kwa bidii zaidi mambo ya baraka yatakayokuja. Hebu imani yetu ipenye kupitia kila wingu la giza, na tumtazame Yeye aliyekufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Amefungua malango ya Paradiso kwa wote wanaompokea na kumwamini. Kwao anawapa uwezo wa kuwa wana na binti za Mungu. Hebu mateso yanayotuumiza sana yawe masomo yenye kutufundisha, yakitufundisha kusonga mbele kuelekea lengo la tuzo ya mwito wetu mkuu katika Kristo. Hebu kutiwe moyo na wazo kwamba Bwana yu karibu kuja. Tumaini hili na lifurahishe mioyo yetu. **"Kwa kuwa bado kitambo kidogo sana, Yeye ajaye atakuja, wala hatakawia." Waebrania 10:37.** Heri wale watumishi ambao, Bwana wao atakapokuja, atawakuta wakikesha.

**Tunaelekea Nyumbani**

Tunaelekea nyumbani. Yeye aliyetupenda sana hata kufa kwa ajili yetu, ametujengea mji. Yerusalemu Mpya ndio mahali petu pa pumziko. Hapatakuwa na huzuni katika mji wa Mungu. Hakutakuwa tena na kilio cha majonzi, wala wimbo wa huzuni unaotokana na matumaini yaliyovunjika na wapendwa waliozikwa. Hivi karibuni mavazi ya uzito na huzuni yatabadilishwa kuwa vazi la arusi. Hivi karibuni tutashuhudia kutawazwa kwa Mfalme wetu. Wale ambao maisha yao yamefichwa pamoja na Kristo, wale ambao katika dunia hii wamevipiga vita vile vizuri vya imani, wataangaza kwa utukufu wa Mkombozi katika ufalme wa Mungu.

Si muda mrefu tutamwona Yeye ambaye ndani Yake matumaini yetu ya uzima wa milele yamejikita. Na mbele ya uwepo Wake, majaribu yote na mateso yote ya maisha haya yatakuwa kama kitu kisicho na maana. **"***Basi msiutupe ujasiri wenu, kwa maana una thawabu kuu. Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi. Kwa kuwa bado kitambo kidogo sana, Yeye ajaye atakuja, wala hatakawia."* **Waebrania 10:35-37.** Tazameni juu, tazameni juu, na hebu imani yenu izidi kuongezeka daima. Hebu imani hii iwaongoze katika njia nyembamba inayoelekea kupitia malango ya mji wa Mungu, kuingia katika upeo mkubwa usio na mipaka wa wakati ujao wa utukufu ambao umeandaliwa kwa ajili ya waliokombolewa. **"***vumilieni, hata kuja kwake Bwana. Tazama, mkulima hungoja mazao ya nchi yaliyo ya thamani, huvumilia kwa ajili yake hata yatakapopata mvua ya kwanza na ya mwisho. Nanyi vumilieni, mthibitishe mioyo yenu, kwa maana kuja kwake Bwana kunakaribia***."** **Yakobo 5:7, 8.**

**Kiambatisho**

**Karama ya Unabii**

Mwanzoni, wakati mwanadamu alipoumbwa na kuwekwa katika bustani ya Edeni, aliweza kuzungumza na Muumba wake pamoja na malaika uso kwa uso. Lakini dhambi ilipoingia, pendeleo hili liliondolewa. Mwanadamu akawa chini ya hukumu ya mauti, na hakuweza kuuona utukufu wa ajabu wa Mungu wala kuishi katika uwepo Wake.

Lakini ingawa mwanadamu aliyeanguka hangeweza tena kuzungumza moja kwa moja na Mungu, bado Baba yetu wa mbinguni mwenye upendo ameendelea kudumisha mawasiliano na familia ya wanadamu. Kupitia huduma ya malaika watakatifu, amewapatia wanaume na wanawake ulinzi dhidi ya nguvu za uovu, na msaada wa kuishi kulingana na mapenzi Yake. Na kupitia utendaji wa Roho Wake Mtakatifu, Mungu amezungumza na mioyo ya wanadamu, na amewezesha hata wale walio wenye dhambi nyingi na wasiojua kupata njia iendayo katika kutenda haki na uzima wa milele.

Mungu pia amesema na jamii ya wanadamu walioanguka kupitia vyombo vya kibinadamu alivyochagua, ambao kwao aliwasilisha ujuzi wa kusudi Lake katika maono na ndoto. Wajumbe hawa wa mapenzi Yake wamejulikana kama watu watakatifu, au manabii, waliotengwa na Bwana Mwenyewe kwa kazi maalumu ya kupokea na kuwasilisha ukweli kutoka mbinguni kwa wanadamu. "*Akiwapo nabii kati yenu,Mimi,Bwana,nitajifunua kwake katika maono,Nitasema naye katika ndoto*." **Hesabu 12:6.**

Maandiko Matakatifu yaliandikwa kutokana na maandishi ya watu waliotukuzwa kwa namna hii. Kwa watu walioishi katika siku zao, watu hawa walipeleka ujumbe kutoka kwa Mungu; na pia walifundisha kweli za kiroho na kutoa mashauri na maonyo kwa ajili ya kanisa la nyakati zijazo. Kwa "manabii" "Wakafunuliwa ya kuwa si kwa ajili yao wenyewe, bali kwa ajili yenu walihudumu katika mambo hayo, ambayo sasa yamehubiriwa kwenu na wale waliowahubiri ninyi Injili kwa Roho Mtakatifu aliyetumwa kutoka mbinguni. Mambo hayo malaika wanatamani kuyachungulia." 1 Petro 1:10-12.

**Katika Kipindi cha Wazee wa Imani**

Karama ya unabii haikuzuiliwa kwa kizazi kimoja tu. Mapema katika kumbukumbu iliyoongozwa na Mungu tunapata mifano ya udhihirisho wake. Henoko, wa saba kutoka kwa Adamu, alikuwa nabii. Akitazama mbele kupitia karne nyingi, aliona kwa maono ya kinabii kuja kwa Bwana na kutekelezwa kwa hukumu za mwisho juu ya waovu. **Yuda 14, 15.**

Kwa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo Bwana alijidhihirisha katika maono, akitabiri baraka ambazo zingekuja kwa uzao wao. Pamoja nao alifanya upya agano Lake, na waliwezeshwa kutazamia thawabu ya mwisho ya wenye haki, na kuuona utukufu wa mji ule wa mbinguni ambao mjenzi na muumba wake ni Mungu. **Waebrania 11:10.**

Musa, ambaye alichaguliwa na Mungu kuwaongoza Waisraeli kutoka utumwani Misri kwenda katika nchi ya Kanaani, alikuwa nabii mkuu. Akitabiri kuja kwa Masihi, alisema: "Bwana, Mungu wako, atakuondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zako kama nilivyo mimi; msikilizeni yeye." **Kumbukumbu la Torati 18:15.** Mungu alimpa mtu huyu mwaminifu mafunuo mengi; na ingawa utukufu wa Mungu haukufunuliwa kwake kikamilifu, bado Neno lasema kwamba Mungu alizungumza naye "uso kwa uso." Kumbukumbu la Torati 34:10.

Baada ya wana wa Israeli kukaa katika nchi ya Kanaani, ushawishi wa waabudu sanamu waliowazunguka uliwageuza kutoka kwa Mungu wa kweli, wakaanza kuabudu jua, mwezi, na nyota, pamoja na sanamu zilizochongwa zilizotengenezwa kwa dhahabu, fedha, miti, na mawe. Kwa kufanya hivyo walizivunja amri za Mungu zilizotoka mbinguni, ambazo zilitolewa kwa ajili ya mema yao wenyewe. Moyo wa Mungu wenye upendo ulihuzunika alipoliona taifa teule likiongozwa mbali na Muumba na Mtoaji wake wa mema, na kuingia katika njia ya matendo iliyokuwa ikielekea kwenye uharibifu.

Katika hali ya uasi mkuu kulikuwa na baadhi ya watu waliodumisha uaminifu wao kwa Yehova; na kutoka miongoni mwao, Mungu aliwachagua manabii aliowatuma kuwaita watu watubu, na kuwaonya juu ya maovu ambayo mwenendo wao ungewaletea kwa hakika. "*Bwana, Mungu wa baba zao, akatuma kwao kwa mikono ya wajumbe wake, akiondoka mapema, na kutuma; kwa sababu aliwahurumia watu wake, na makao yake*." **2 Mambo ya Nyakati 36:15.**

Miongoni mwa manabii mashuhuri wa Israeli walikuwa Samweli, Eliya, Elisha, Isaya, Yeremia, Ezekieli, na Danieli. Kwa maneno yenye nguvu waliwaita watu waache njia zao mbaya, wakiwapa hakikisho kwamba Bwana angewapokea kwa neema na kuwabariki, na kuponya kurudi nyuma kwao. Baadhi ya maandishi ya manabii hawa yana matumizi maalumu kwa wakati tunaoishi sasa. Waliandika juu ya mambo ambayo yangetokea "katika siku za mwisho," au katika "wakati wa mwisho." Isaya 2:2; Danieli 12:4.

**Wakati wa Kuja kwa Kristo Mara ya Kwanza**

Nabii wa mwisho wa Agano la Kale alikuwa Malaki. Katika kipindi cha desturi za kidini za nje kabla ya ujio wa Kristo, kwa kadiri kumbukumbu zilivyo, hakukuwa na udhihirisho wa karama ya unabii. Lakini manabii walitumwa ili kuandaa njia kwa ajili ya Masihi. Zakaria, baba yake Yohana Mbatizaji, "alijazwa na Roho Mtakatifu, naye akatabiri." Luka 1:67. Simeoni, mtu "mwenye haki na mcha Mungu," ambaye alikuwa "akitarajia faraja ya Israeli," alikuja kwa uongozi wa Roho hekaluni, naye akatabiri kuhusu Yesu kwamba angekuwa: "Nuru ya

kuwaangazia Mataifa, na utukufu wa watu wako Israeli.” Luka 2:25, 32. Anna, nabii mke, “alisema habari zake kwa watu wote waliokuwa wakitazamia ukombozi katika Yerusalemu.” Luka 2:38. Na hapakuwa na nabii mkuu kuliko Yohana Mbatizaji katika kizazi chochote, ambaye alichaguliwa na Mungu kutangaza kwa Israeli ujio wa: “Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu.” Yohana 1:29.

**Katika Siku za Mitume**

Mwanzo wa kipindi cha Ukristo ulidhihirishwa kwa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu na udhihirisho wa karama mbalimbali za kiroho. Miongoni mwa karama hizo kulikuwa na karama ya unabii. Katika kitabu cha Matendo tunasoma maneno yaliyoongozwa na Mungu yaliyotolewa na Petro, Stefano, na wengine waliokuwa sehemu ya kanisa la kwanza la Kikristo; pia tunasoma habari za binti wanne wa Filipo, “waliokuwa mabikira, waliotabiri,” na pia nabii mmoja aliyeitwa Agabo. Matendo 21:9, 10.

Mtume Paulo alikuwa na maono ya utukufu wa mbinguni. Tazama 2 Wakorintho 12:1-7. Aliandika kwa kirefu katika sura ya kumi na mbili ya kitabu cha kwanza cha Wakorintho kuhusu karama za Roho zilizotolewa, ambazo hazikutolewa kwa ajili ya kizazi kimoja tu, bali: “*hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo*.” **Waefeso 4:13.** *“Na Mungu ameweka wengine katika Kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha.”* **1 Wakorintho 12:28.**

Yohana, aliyekuwa wa mwisho kuishi kati ya wale mitume kumi na wawili wa Yesu, alikuwa nabii. Katika kitabu cha mwisho cha Biblia, anaeleza juu ya maono aliyopewa alipokuwa uhamishoni katika kisiwa cha Patmo. Katika kuyaandika maono hayo alisema kwamba yalikuwa: “Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu, awaonyeshe watumwa wake mambo ambayo hayana budi kutukia upesi.” Na anasema kwamba Kristo: “1 Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu awaonyeshe watumwa wake mambo ambayo kwamba hayana budi kuwako upesi; naye akatuma kwa mkono wa malaika akamwonyesha mtumwa wake Yohana; aliyelishuhudia Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu Kristo, yaani, mambo yote aliyoyaona.” Ufunuo 1:1, 2.

**Kutoweka kwa Karama ya Unabii Wakati wa Uasi Mkuu**

Maandiko yalitabiri juu ya uasi mkubwa ambao hata katika siku za mitume ulikuwa umeanza kujidhihirisha miongoni mwa baadhi ya ndugu wa uongo katika kanisa, na ambao hatimaye ungeendelea kuwa: “kuasi,” na kufunuliwa kwa: “mtu yule wa kuasi, mwana wa uharibifu,” ambaye Paulo aliandika habari zake kwa Wathesalonike. 2 Wathesalonike 2:1-7.

Katika kutimizwa kwa unabii huu, ni jambo lililothibitishwa katika historia kwamba baada ya kifo cha mtume wa mwisho wa Yesu, baadhi ya washiriki wa kanisa la Kikristo walianza kuacha urahisi wa kweli kama ulivyofundishwa na Kristo; na taratibu waumini hao waliongozwa kuungana na ulimwengu katika desturi za kipagani.

Kadiri miaka ilivyopita, na kanisa lilivyoongezeka kwa idadi na umaarufu, wengi walizidi kuwa wazembe katika utii wao kwa mafundisho ya Biblia, mpaka hatimaye, katika karne ya tano na ya sita baada ya Kristo, sehemu kubwa ya wale waliodai kuwa Wakristo kwa kweli hawakuwa wakiishi kwa kupatana na mafundisho ya Kristo. Kwa karne nyingi zilizofuata, aina ya Ukristo iliyoasi ilitawala. Ukweli ulikandamizwa na kusahaulika, na ujinga ukaenea.

Karne hizi za uasi zinaitwa kwa usahihi katika historia kuwa: **"Zama za Giza" (Dark Ages).** Katika kipindi hiki, juhudi zilifanywa kubadilisha au kuondoa mafundisho mengi ya msingi ya Biblia. Katika mazingira kama haya, si jambo la kushangaza kwamba katika kipindi hicho, kama vile pia katika karne zilizotangulia kuja kwa Kristo mara ya kwanza, udhihirisho wa karama ya unabii ulipotea karibu kabisa.

**Kurejeshwa Katika Siku za Mwisho**

Lakini Maandiko, wakati yakitabiri juu ya uasi huu wa kutisha, pia yanafundisha wazi kwamba kabla ya kuja kwa Kristo mara ya pili, wengi wataokolewa kutoka katika giza la makosa na ushirikina. Kwa mara nyingine tena dunia itaangazwa kwa utukufu wa Mungu. Kweli safi za Biblia zitaangaza. Na katika wakati huu wa nuru ya mbinguni unaoonyesha kukaribia kwa mwisho wa kizazi, karama za Roho zitaonekana tena katika kanisa la kweli. "Hata itakuwa, baada ya hayo, ya kwamba nitamimina roho yangu juu ya wote wenye mwili; na wana wenu, waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono; tena juu ya watumishi wenu, wanaume kwa wanawake, katika siku zile, nitamimina roho yangu." Yoeli 2:28, 29; Matendo 2:17, 18.

Kwa maneno yaliyo wazi, nabii Yohana anazungumza juu ya: "masalio," au kanisa la mwisho, kuwa ni wale ambao: "wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu Kristo." Ufunuo 12:17. Katika kifungu kingine, mwandishi huyu huyu anatoa ufafanuzi wa wazi kuhusu maana ya: "ushuhuda wa Yesu." Wakati mmoja Yohana alipojaribu kumwabudu malaika aliyemtokea katika maono, malaika huyo alisema:

"Angalia, usifanye hivi; mimi ni mjoli wako na wa ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu. Msujudie Mungu. Kwa maana ushuhuda wa Yesu ndio roho ya unabii." Ufunuo 19:10.

Katika hali kama hiyo hiyo, malaika huyo alisema mahali pengine:

"Angalia, usifanye hivi; mimi ni mjoli wako, na wa ndugu zako manabii." Ufunuo 22:9.

Wazo linaloelezwa katika vifungu hivi viwili ni lilelile. Katika kifungu kimoja, "ndugu" wa Yohana wanasemekana kuwa na: "ushuhuda wa Yesu;" na katika kifungu kingine, "ndugu" hao wanaitwa: "manabii."

Kwa hiyo ni manabii walio na: "ushuhuda wa Yesu." Na malaika aliyemtokea Yohana kwa hakika alikuwa mjumbe maalumu anayewasilisha maelekezo kwa manabii wote—bila shaka malaika Gabrieli, ambaye ametajwa kuwa alimtokea Danieli. Tazama Danieli 8:16; 9:21. Malaika huyo huyo alimwambia Yohana zaidi: "Ushuhuda wa Yesu ndio roho ya unabii." Ufunuo 19:10.

Kwa kulinganisha maneno ya Biblia: "ushuhuda wa Yesu" na kauli ya Ufunuo 12:17 kuhusu: "masalio wale wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu Kristo," tunafikia hitimisho kwamba kabla ya kuja kwa Kristo mara ya pili, kanisa Lake la kweli litakuwa likizishika amri Zake, na litakuwa na Roho ya unabii.

Kutimia kwa haraka kwa unabii wa Maandiko Matakatifu kuhusu ishara na matukio ambayo yangetambulisha matukio ya mwisho ya historia ya dunia ni ushahidi wa hakika kwamba sasa tunaishi katika siku za mwisho. Kwa hiyo, kundi la Wakristo wanaozishika amri za Mungu na walio na ushuhuda wa Yesu Kristo—yaani Roho ya unabii—linapaswa kuwepo leo. **Je, linaweza kupatikana wapi?**

**Kupimwa kwa Neno**

Kwa sababu ya ushupavu wa kidini uliotokana na kazi za watu wanaodai kwa uongo kwamba wamefundishwa na Mungu, watu wengi wema wamekuwa na mashaka makubwa au hata kutokuamini kabisa madai ya mtu yeyote anayesema amepokea ufunuo wa Mungu. Lakini mtafutaji wa kweli anapaswa kujilinda kwa usawa dhidi ya kudanganywa na manabii wa uongo au walimu wa uongo, na pia dhidi ya kushindwa kuitambua kweli ya Mungu. Mtume anaandika: "msitweze unabii; jaribuni mambo yote; lishikeni lililo jema;" 1 Wathesalonike 5:20, 21.

Kwa kupatana na agizo hili, waamini katika Kristo wanahimizwa kutoa uangalifu wa kweli kwa ushahidi wa uongozi wa Mungu katika harakati ya Marejeo (Advent movement) ya siku hizi, na kwa udhihirisho wa karama ya unabii inayohusiana na harakati hii. Kupuuza kazi ya Roho Mtakatifu, kama inavyoonekana kupitia karama hii, ni jambo la hatari. Hata hivyo, tunaonywa: "Jihadharini na manabii wa uongo, wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, lakini kwa ndani ni mbwa-mwitu wakali." Na kipimo kimetolewa: "Mtawatambua kwa matunda yao."

Kama vile wanadamu wasivyoweza kutarajia kuvuna: "zabibu katika miiba, au tini katika michongoma," vivyo hivyo hawawezi kupata ukweli usiochanganywa na nguvu itakasayo kutoka kwa mdanganyifu mwovu. "kila mti mwema huzaa matunda mazuri; na mti mwovu huzaa matunda mabaya. Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mwovu kuzaa matunda

mazuri. Kila mti usiozaa tunda zuri hukatwa ukatupwa motoni. Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua." **Mathayo 7:15-20.**

Kazi hai za Ellen G. Harmon, ambaye baada ya ndoa yake alijulikana kama Bi. E. G. White, zilichukua kipindi cha miaka sabini. Miaka sitini ya kipindi hicho aliifanya kazi huko Amerika, na miaka kumi huko Ulaya na Australasia. Katika kipindi hiki kirefu aliheshimiwa kwa kupewa mafunuo mengi, ambayo yeye aliamini kwamba yalitoka mbinguni, na ambayo alijitahidi kwa uaminifu kuyaandika kwa ajili ya mafundisho ya kanisa. Vitabu vingi vya maandishi yake vimechapishwa na vinaenezwa duniani kote. Maelfu mengi ya watu, wakiwa wameshawishika kupitia Maandiko kwamba tunaishi karibu na mwisho wa historia ya dunia hii, wameamini kwamba Bi. White alikuwa chombo ambacho kupitia kwake Mungu alizungumza kwa njia ya Roho ya unabii kwa kanisa Lake la masalio. Imani kama hiyo kwa hakika inastahili kuchunguzwa. Tabia ya kazi yake inapaswa kupimwa kwa maisha yake mwenyewe, kwa mafundisho yake, na kwa asili ya mafunuo aliyopokea.

Bi. White daima alitamani kwamba kazi yake na mafundisho yake yapimwe kwa kiwango cha Neno la Mungu kama lilivyofunuliwa katika Maandiko Matakatifu. Aliandika: "Acheni ushuhuda upimwe kwa matunda yake. Roho ya mafundisho yake ni ipi? Matokeo ya ushawishi wake yamekuwa nini? ... Mungu ama analifundisha kanisa Lake, akilikemea makosa yake, na kulitia nguvu imani yake, au hafanyi hivyo. Kazi hii ni ya Mungu, au siyo. Mungu hafanyi chochote kwa ushirikiano na Shetani. Kazi yangu ... ina muhuri wa Mungu, au ina muhuri wa adui. Hakuna kazi ya katikati katika jambo hili."

"Bwana alipokuwa amejidhihirisha kwangu kupitia Roho ya unabii, mambo ya zamani, ya sasa, na yajayo yalipita mbele yangu. Nilionyeshwa nyuso ambazo sikuwahi kuziona, na miaka mingi baadaye nilizitambua nilipokutana nazo. Nimeamshwa kutoka usingizini nikiwa na ufahamu ulio wazi wa mambo yaliyokuwa yameonyeshwa kwangu hapo awali; na nimeandika, katikati ya usiku, barua ambazo zilivuka bara zima, na zilipofika wakati wa hatari, ziliokoa madhara makubwa kwa kazi ya Mungu. Hii imekuwa kazi yangu kwa miaka mingi. Nguvu fulani imenichochea kukemea na kuonya makosa ambayo sikuwa nimeyafikiria. Je, kazi hii ... imetoka juu au chini? ... Wale wanaotamani kweli kuijua kweli watapata ushahidi wa kutosha wa kuamini." — *Testimonies for the Church*, Juzuu ya 5, uk. 671, 672.

**Kristo Atukuzwe**

Kufanyika mwili kwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu wa kiungu, "Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu," ndilo jambo kuu la Injili. "Maana ndani yake unakaa utimilifu wote wa Uungu kwa jinsi ya kimwili. Nanyi mmetimilika katika yeye." Wakolosai 1:27; 2:9, 10. Kukubali au kukataa ukweli huu muhimu ni mojawapo ya vipimo vilivyowekwa na Mungu kwa mtu yeyote anayesema kuwa ana karama ya unabii.

Mtume Yohana anaandika: “Wapenzi, msiiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani. Katika hili mwamjua Roho wa Mungu; kila roho ikiriyo kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu. Na kila roho isiyomkiri Yesu haitokani na Mungu.” 1 Yohana 4:1-3.

Manabii wa uongo hawamtukuzi Kristo. Badala yake, huvuta watu wawaangalie wao wenyewe. Kwa kusema: “mambo yaliyopotoka,” huwavuta wanafunzi wawafuate wao wenyewe. (Matendo 20:30). Ili kutimiza kusudi hili, hufundisha kwa namna inayopendeza akili ya tamaa ya kibinadamu ya wale ambao mioyoni mwao husema: “Msione; na manabii, Msitoe unabii wa mambo ya haki, tuambieni maneno laini.” (Isaya 30:10). Walimu hawa wanaodai kuwa manabii: “Hao ni wa dunia; kwa hiyo wanena ya dunia na dunia huwasikia.”
(1 Yohana 4:5).

Katika mafundisho ya Bi. White, Kristo anatambuliwa na kuinuliwa kama **Mwokozi pekee wa wenye dhambi**. Kwa Kristo: “Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.” (Matendo 4:12). Katika kazi yake mwenyewe kwa ajili ya Bwana, alidhihirisha maagizo yafuatayo aliyowapa ndugu zake waliokuwa katika huduma:

“Kristo aliyesulubiwa, Kristo aliyefufuka, Kristo aliyepaa mbinguni, Kristo anayekuja tena, anapaswa kuufanya moyo wa mhudumu ulainike, kufurahi, na kujazwa kiasi kwamba atawasilisha kweli hizi kwa watu kwa upendo na bidii kuu. Mhudumu atasahaulika, na Yesu ataonekana. Mwinueni Yesu, ninyi mnaowafundisha watu; mwinueni katika mahubiri, katika nyimbo, na katika maombi. Nguvu zenu zote zielekezwe katika kuwaelekeza roho zilizochanganyikiwa, zilizopotea njia, na zilizopotea kabisa kwa ‘Mwana-Kondoo wa Mungu.’ Mwinueni Mwokozi aliyefufuka, na kuwaambia wote wanaosikia, njoo Kwake yeye ambaye ‘alitupenda, akajitoa kwa ajili yetu.’ Hebu sayansi ya wokovu iwe mzigo wa kila mahubiri, mada ya kila wimbo. Ijazwe katika kila ombi. Msilete chochote katika mahubiri yenu kitakachoongeza juu ya Kristo, hekima na nguvu ya Mungu. Shikeni mbele neno la uzima, mkimwonyesha Yesu kuwa tumaini la mwenye kutubu na ngome ya kila mwamini. Onyesheni njia ya amani kwa walio na shida na waliokata tamaa, na dhihirisheni neema na ukamilifu wa Mwokozi.” — *Gospel Workers*, uk. 159, 160.

**“Kwa Sheria na Ushuhuda”**

Daima imekuwa juhudi ya adui wa haki kuwaongoza watu kupuuza madai ya sheria ya Yehova. Na kupitia manabii Wake, Mungu daima amejitahidi kuwaongoza watu watambue madai yenye nguvu ya sheria Yake ya milele na isiyobadilika. Kuhusu watu Wake wa zamani imeandikwa: “Bwana aliwashuhudia Israeli, na Yuda, kwa kinywa cha kila nabii, na cha kila mwonaji, akisema, Geukeni, na kuziacha njia zenu mbaya, mkazishike amri zangu na hukumu

zangu, sawasawa na ile sheria yote niliyowaamuru baba zenu, nikawapelekea kwa kinywa cha manabii watumishi wangu.” (2 Wafalme 17:13).

Katika siku zetu, wakati ambapo kuna mwelekeo mkubwa wa kutupilia mbali kizuizi cha sheria ya Mungu, Bi. White amejitahidi kwa uthabiti na bila woga kuleta mbele ya dhamiri za watu utakatifu wa matakwa ya Mungu. Kutobadilika kwa sheria hiyo, na umuhimu wa utii kupitia nguvu ya Kristo kwa kila hitaji lake, pamoja na **amri ya nne**, kumesisitizwa daima katika kazi yake ya hadharani. Kuhusu uhusiano kati ya sheria na injili, aliandika:

“Katika maisha ya Kristo kanuni za sheria zimewekwa wazi; na Roho Mtakatifu wa Mungu anapougusa moyo; nuru ya Kristo inapowaonyesha wanadamu hitaji lao la damu Yake yenye kutakasa na haki yake ihesabiwayo kuwa yao, sheria bado ni chombo cha kutuleta kwa Kristo, ili tupate kuhesabiwa haki kwa imani. ‘Sheria ya Bwana ni kamilifu, huiburudisha nafsi.’

‘Mpaka mbingu na nchi zitakapopita,’ alisema Yesu, ‘hakuna hata nukta moja wala herufi moja ya sheria itakayopita, hata yote yatimie.’ Jua linalong’aa mbinguni, na dunia imara mnayoishi juu yake, ni mashahidi wa Mungu kwamba sheria Yake haibadiliki na ni ya milele. Ingawa vinaweza kupita, maagizo ya Mungu yatadumu. ‘Ni rahisi zaidi mbingu na nchi kupita kuliko nukta moja ya sheria kushindwa.’ Mfumo wa mifano uliokuwa ukimwelekeza Yesu kama Mwana-Kondoo wa Mungu ulipaswa kuondolewa wakati wa kifo Chake; lakini maagizo ya amri kumi ni maagizo yasiyobadilika kama kiti cha enzi cha Mungu.” — *The Desire of Ages*, uk. 308.

**Maandiko Matakatifu Kuheshimiwa**

Maandishi ya Bi. White daima yanaelekeza kwenye Biblia kama chanzo kikuu cha kweli yote ya kiroho. Yamejaa nukuu za Maandiko, ambayo hayapewi tafsiri za kubuni au zisizo na msingi. Waadventista Wasabato hawayaoni maandishi yake kama nyongeza ya Biblia, wala hawafundishi kwamba kuyasoma kunachukua nafasi ya kujifunza Biblia. Yeye mwenyewe aliandika:

“Neno la Mungu linatosha kuangaza akili iliyofunikwa na giza zaidi, na linaweza kueleweka na wale wanaotamani kulielewa. Lakini, licha ya hayo yote, baadhi ya watu wanaodai kulifanya Neno la Mungu kuwa somo lao wanaonekana kuishi kinyume kabisa na mafundisho yake yaliyo wazi. Basi, ili kuwaacha wanaume na wanawake bila udhuru, Mungu huwapa ushuhuda ulio wazi na wenye nguvu, akiwavuta tena kwenye neno ambalo walipuuza kulifuata.” Aliendelea: “Shuhuda hazijatolewa ili kulidhoofisha Neno la Mungu, bali kulikuza na kuvuta akili za watu Kwake, ili uzuri wa unyenyekevu wa kweli uweze kuwagusa wote.”

Kauli yetu kuu inapaswa kuwa: **“kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi.”** Tunayo Biblia iliyojaa kweli za thamani sana. Ndani yake mna **chanzo na kilele cha maarifa yote**. Maandiko Matakatifu, yaliyotolewa

kwa uvuvio wa Mungu: "*lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema*." **2 Timotheo 3:16-17** Ifanyeni Biblia kuwa kitabu chenu cha kujifunza.

Kwa ndugu zake katika huduma, aliandika: "Msitete nadharia au vipimo ambavyo Kristo hajawahi kuvizungumzia, na ambavyo havina msingi katika Biblia. Tunayo kweli kuu na ya kutisha kwa ajili ya watu. 'Imeandikwa' ndicho kipimo kinachopaswa kuletwa mbele ya kila nafsi. Twende kwenye Neno la Mungu kwa ajili ya mwongozo. Tutafute 'asema hivi Bwana.'

Tumekuwa na mbinu za kibinadamu za kutosha. Akili iliyofundishwa tu katika sayansi ya ulimwengu itashindwa kuelewa mambo ya Mungu; lakini akili hiyo hiyo, inapobadilishwa na kutakaswa, itaona nguvu ya Mungu katika neno Lake." — *Gospel Workers*, uk. 309, 310.

**Unabii Uliotimia**

Moja ya mambo yanayomtambulisha Mungu wa kweli tofauti na miungu yote ya uongo ni uwezo Wake wa kuwasiliana na wanadamu kuhusu mambo ya zamani na yajayo. Kupitia nabii Isaya, Yehova anatoa changamoto kwa miungu inayotambuliwa na wapagani: "*Wayatangaze na kutujulisha yatakayokuwa; watuonyeshe mambo ya zamani, ni mambo gani, tukapate kuyatia moyoni, tukajue mwisho wake; au wamdhihirishie yatakayotokea baadaye. Tujulisheni yatakayokuwa baadaye, nasi tutakiri ya kuwa ninyi ni miungu*." **Isaya 41:22-23** Na kwa sababu miungu hiyo ya uongo haikuwa na uwezo wa kufanya hivyo, Yehova anasema: "Tazameni, ninyi si kitu, tena kazi yenu si kitu; awachaguaye ninyi ni chukizo." **Isaya 41:24**

Moja ya vipimo vilivyowekwa na Mungu kwa nabii wa kweli ni **kutimia kwa usahihi kwa maneno yake**. Kwa Israeli ya kale Mungu alisema kupitia Musa, ambaye alikuwa nabii mkuu: "Nawe ukisema moyoni mwako, Tutajuaje neno asilolinena Bwana? Atakaponena nabii kwa jina la Bwana, lisifuate jambo lile wala kutimia, hilo ndilo neno asilolinena Bwana; kwa kujikinai amelinena huyo nabii, usimwogope." (Kumbukumbu la Torati 18:21, 22).

Matukio mengi yanaweza kutajwa ambapo uwezo wa kuona mambo yajayo kwa njia ya unabii aliopewa Bi. White. Mara nyingi aliona katika maono watu ambao hakuwafahamu. Baadaye katika safari zake alikutana na watu hao, na kuwapa ujumbe ambao alikuwa amepewa katika maono kwa ajili yao—ujumbe uliodhihirisha ujuzi wa matendo yao au nia zao ambazo hangeweza kuzipata kutoka kwa chanzo chochote cha kibinadamu.

Katika miaka ya mwanzo ya kazi yake, wakati ambapo yeye, mume wake, na Mzee **Joseph Bates** walikuwa karibu watu pekee waliokuwa wakihubiri ukweli wa Sabato, alionyeshwa katika maono ukuaji wa baadaye wa harakati hiyo ambayo wakati huo ilikuwa dhaifu na ambayo wao walikuwa waanzilishi wake. Mnamo **Novemba 1, 1848**, katika mkutano

uliofanyika **Dorchester, Massachusetts**, Bi. White alipokea maono ambapo aliona ujumbe huo, uliowakilishwa kwa mfano wa jua linalochomoza, ukiongezeka nguvu mpaka ulipoangaza dunia yote.

Baada ya kutoka katika maono hayo, alimwambia mume wake kwamba Bwana alitaka aanze kuchapisha gazeti dogo, na kwamba kazi ya kuchapisha ukweli ingeongezeka mpaka machapisho hayo yangekuwa kama mito ya nuru inayozunguka dunia. Kwa mtazamo wa kibinadamu, huu ulikuwa unabii wa ujasiri sana. Waumini walikuwa wachache sana kwa idadi, walikuwa maskini kwa mali za dunia, na mafundisho yao hayakupendwa na wengi. Lakini Mungu, ambaye Kwake mambo yote yanawezekana, ametimiza neno hili kwa njia ya ajabu. Tangu wakati huo, uchapishaji wa vitabu na machapisho yenye kweli na ujumbe wa Biblia kupitia dhehebu hili umeendelea kuongezeka, mpaka kufikia kusambazwa kwake katika sehemu mbalimbali za dunia, jumla ikiwa kama $7,000,000 kwa mwaka.

Katika kueleza maono yake ya awali, Bi. White alieleza kwa uwazi uzoefu ambao watu wa Kiadventista wangepitia kabla ya Bwana kuja. Wakati ambapo udhihirisho wa **umizimu (spiritualism)** ulikuwa bado umejikita katika matukio ya ajabu ya: "sauti kugonga bila kumwona mtu" (mysterious rappings: Sauti za ajabu za kugonga ambazo chanzo chake hakikuonekana na zilidaiwa kuwa zinatoka kwa ulimwengu wa roho.) iliyotokea huko **Rochester, New York**, alionyeshwa ukuaji wa haraka na wa kushangaza ambao harakati hiyo ingefanya katika siku zijazo. Alitabiri pia kuwepo kwa sheria zinazolazimisha **ibada ya Jumapili** katika nchi ambazo wakati huo zilikuwa na uhuru kamili wa dini. Unabii huu wote, pamoja na mingine mingi, ulichapishwa na kusambazwa kwa upana. Mabadiliko ya matukio yaliyotokea tangu unabii huo ulipoandikwa yamedhihirisha ukweli wa sehemu kubwa ya unabii huo, na utimilifu wake umeongeza imani kwamba unabii wake kuhusu ushindi wa mwisho wa kazi ya Waadventista Wasabato nao utatimia. Mafanikio ya harakati hii yameendelezwa kwa kiwango kikubwa kupitia mashauri na maonyo yaliyokuja kwa viongozi na watenda kazi wake kupitia sauti na kalamu ya Bi. White.

### *Hali Wakati wa Maono*

Hasa katika miaka ya mwanzo ya kazi yake, maono ya Bi. White mara nyingi yalitolewa mbele ya mashahidi wengi. Wakati wa udhihirisho huo, alikuwa **hajitambui kabisa kuhusu mazingira yake ya duniani**. Hata hivyo, mara nyingi alikuwa akitembea huku akifanya ishara zenye utulivu na uzuri, wakati akieleza matukio aliyokuwa akiyaona. Nguvu yake katika nyakati hizo ilikuwa ya ajabu sana. Wanaume wenye nguvu walijaribu kusogeza mkono wake au kuushusha kutoka katika nafasi aliyokuwa ameushikilia, lakini walishindwa. Katika tukio moja, nyumbani kwa **Bwana Curtis**, huko **Topsham, Maine**, mwaka **1845**, alichukua kutoka kwenye kabati Biblia kubwa ya familia iliyokuwa na uzito wa karibu **pauni kumi na nane** (takribani kilo 8). Aliiinua juu kwa mkono wake wa kushoto akiwa ameunyoosha, kisha akageuza kurasa kwa mkono wake wa kulia. Wakati huo macho yake yalielekezwa juu, mbali na kitabu, lakini aliweza

kusoma kwa usahihi vifungu vingi vya Maandiko, huku akionyesha mistari kwa kidole chake cha chanda cha mkono wake wa kulia. Kwa nguvu zake za kawaida ingekuwa ngumu hata kuinua kitabu hicho kizito. Lakini alipokuwa amepewa nguvu isiyo ya kawaida wakati wa maono, aliweza kukishikilia juu kwa mkono uliounyoshwa kwa zaidi ya nusu saa.

Katika kueleza maono yake, Bi. White mara nyingi alimtaja yule aliyekuwa akimfundisha kwa maneno kama: **"malaika wangu anayeandamana nami," "mwalimu wangu,"** au **"kiongozi wangu."** Kwa maneno hayo alimaanisha malaika mwenye nuru na utukufu mkuu, ambaye daima alikuwa akimwongoza na kumfundisha.

Ingawa Bi. White mara nyingi alikuwa akizungumza akiwa katika maono, bado **hakukuwa na pumzi iliyotoka midomoni mwake**. Mnamo **Juni 26, 1854**, huko **Rochester, New York**, wakati alipokuwa katika maono, madaktari wawili walijaribu kuthibitisha kwamba lazima kuwe na pumzi katika mapafu yake. Miongoni mwa majaribio waliyofanya, waliweka mshumaa uliowashwa karibu sana na midomo yake bila kumchoma. Lakini ingawa wakati huo alikuwa akizungumza kwa nguvu, mwali wa moto wa mshumaa haukutikisika hata kidogo. Dalili ya kwanza ya kutoka kwake katika maono ilikuwa **kuvuta pumzi kwa nguvu**. Labda sekunde kadhaa zilipita kabla hajavuta pumzi nyingine. Baada ya kuvuta pumzi kadhaa kwa kina, alianza tena kupumua kwa kawaida.

Hali hizi za mwili zinafanana na uzoefu wa nabii **Danieli** alipokuwa katika maono, kama alivyoandika katika sura ya kumi ya unabii wake. Danieli anaeleza kuhusu kupoteza nguvu na kuonekana kwa malaika aliyempa nguvu isiyo ya kawaida: *"mara hazikusalia nguvu ndani yangu, wala pumzi haikusalia ndani yangu. Kisha mmoja mfano wa mwanadamu akanigusa tena, akanitia nguvu." (Danieli 10:17, 18).*

**Ushuhuda wa Shahidi Aliyeona**

Mzee **Uriah Smith**, aliyekuwa msaidizi wa muda mrefu wa Bi. White na mume wake, alitoa ushuhuda ufuatao kuhusu karama yake ya pekee:

"Kila kipimo kinachoweza kutumika kuchunguza udhihirisho wa aina hii kinaonyesha kuwa ni wa kweli. Ushahidi unaounga mkono udhihirisho huo, wa ndani na wa nje, ni wa hakika. Unapatana na Neno la Mungu na pia unapatana wenyewe kwa wenyewe. Umetolewa, isipokuwa kama wale walio na uwezo mkubwa wa kuhukumu wamejidanganya daima, wakati Roho wa Mungu alipokuwa hasa akidhihirika. Kwa utulivu, heshima, na mvuto mkubwa, mambo haya yanajionyesha kwa kila mtazamaji kuwa ni kinyume kabisa na mambo ya uongo au ushupavu wa kupita kiasi." Aliendelea kusema:

"Matunda yake yanaonyesha kwamba chanzo chake ni kinyume na uovu."

1. Huleta Maadili Safi Zaidi

“Kwanza, yanaelekeza kwenye maadili yaliyo safi kabisa. Yanapinga kila aina ya uovu, na yanahimiza utendaji wa kila wema. Yanaonyesha hatari tunazopaswa kupitia kabla ya kufikia ufalme. Yanafichua hila za Shetani. Yanatuonya dhidi ya mitego yake. Yamezuia mapema mpango mmoja baada ya mwingine wa ushupavu wa kidini ambao adui alijaribu kuingiza kati yetu. Yamefunua uovu uliofichika, yameleta wazi makosa yaliyofichwa, na yameonyesha nia mbaya za watu wasio waaminifu. Yametuchochea tena na tena kujitoa zaidi kwa Mungu, juhudi kubwa zaidi kwa ajili ya utakatifu wa moyo, na bidii zaidi katika kazi na huduma ya Bwana wetu.”

2. Humwelekeza Mtu kwa Kristo

“Pili, yanatuongoza kwa Kristo. Kama Biblia, yanamwonyesha Kristo kuwa tumaini pekee na Mwokozi pekee wa wanadamu. Yanatuonyesha maisha Yake matakatifu na mfano Wake wa Uungu kwa namna iliyo hai, na kwa maombi yenye nguvu yanatuhimiza kufuata nyayo Zake.”

3. Hutuongoza kwenye Biblia

“Tatu, yanatupeleka kwenye Biblia. Yanakiweka kitabu hicho mbele yetu kama Neno la Mungu lililoongozwa na Roho na lisilobadilika. Yanatusihi tulichukue Neno hilo kuwa mshauri wetu na kuwa kanuni ya imani na mwenendo wetu. Kwa nguvu ya pekee yanatusihi tujifunze kurasa zake kwa muda mrefu na kwa bidii, na kuzoea mafundisho Yake, kwa maana ndilo litakalotuhukumu katika siku ya mwisho.”

4. Yameleta Faraja kwa Mioyo Mingi

“Nne, yameleta faraja na matumaini kwa mioyo mingi. Yamewaimarisha walio dhaifu, yamewatia moyo waliokata tamaa, na yamewainua waliolemewa. Yameleta mpangilio kutoka katika machafuko, yamenyoosha mahali palipopinda, na yameleta nuru katika mambo yaliyokuwa meusi na yasiyoeleweka. Na hakuna mtu mwenye akili isiyo na chuki anayeweza kusoma maonyo yake yenye nguvu kwa ajili ya maadili safi na ya juu, kuinuliwa kwake kwa Mungu na Mwokozi, kukemea kwake kila uovu, na wito wake kwa kila jambo lililo takatifu na lenye sifa njema, bila kulazimika kusema: ‘Haya si maneno ya mtu aliye na pepo.’”

**Thamani ya Kazi Yake**

Baada ya miaka sabini kamili ya kazi yenye bidii katika nchi nyingi, katika kuandika na kuhubiri, Bi. White alilala katika Yesu kwa utulivu nyumbani kwake karibu na **St. Helena, California**, tarehe **16 Julai 1915**. Alizikwa kando ya mume wake katika **Oak Hill Cemetery, Battle Creek, Michigan**, tarehe **24 Julai**. Katika mahubiri ya mazishi, Mzee **A. G. Daniells**,

aliyekuwa Mwnyekiti wa **Konferensi Kuu ya Waadventista Wasabato**, alisema kuhusu kazi ya maisha yake:

"Labda hatuna hekima ya kutosha kusema kwa hakika ni sehemu gani ya kazi ya maisha ya Bi. White iliyokuwa na thamani kubwa zaidi kwa ulimwengu, lakini inaonekana kwamba wingi mkubwa wa maandishi ya kidini yenye kina aliyoyaacha ungekuwa msaada mkubwa zaidi kwa wanadamu. Vitabu vyake vinazidi zaidi ya juzuu ishirini. Baadhi ya vitabu hivyo vimetafsiriwa katika lugha nyingi katika sehemu mbalimbali za dunia. Vimefikia usambazaji wa zaidi ya nakala milioni mbili, na bado vinaendelea kuwafikia watu kwa maelfu."

"Tunapotazama sehemu yote ya kweli ya injili—uhusiano wa mwanadamu na Bwana wake pamoja na wanadamu wenzake—ni lazima ionekane kwamba kazi ya maisha ya Bi. White imezipa misingi hii mikuu msaada chanya na wenye kujenga. Amegusa ubinadamu katika kila eneo muhimu la mahitaji yake, na ameuinua hadi kiwango cha juu zaidi."

"Sasa amepumzika. Sauti yake imenyamaza; kalamu yake imewekwa kando. Lakini ushawishi mkubwa wa maisha yale yenye nguvu, yenye bidii, na yaliyojazwa na Roho utaendelea. Maisha hayo yaliunganishwa na umilele; yalifanywa ndani ya Mungu. Ujumbe uliotangazwa na kazi iliyofanywa vimeacha kumbukumbu ambayo haitaoza wala kuangamia." "Juzuu nyingi alizoacha, zinazogusa kila sehemu ya maisha ya mwanadamu, zikihimiza kila matengenezo yanayohitajika kwa ajili ya kuboresha jamii, kama inavyoonekana katika familia, mji, serikali, na taifa, zitaendelea kuunda maoni ya jamii na tabia za mtu binafsi. Ujumbe wake utathaminiwa zaidi kuliko ulivyokuwa hapo awali." "Kazi ambayo maisha yake yalijitoa kwake, na ambayo maisha hayo yaliikuza na kuiendeleza kwa kiwango kikubwa, itaendelea kusonga mbele kwa nguvu na kasi inayoongezeka kadiri miaka inavyopita. Sisi tuliohusika nayo hatupaswi kuwa na hofu yoyote isipokuwa hofu ya kushindwa kutekeleza sehemu yetu kwa uaminifu kama tunavyopaswa."

**Maelezo ya Chini ya Ukurasa**

**[1]** Makala mbili katika kiambatisho hiki:

1. **"The Prophetic Gift" (Karama ya Unabii)**
2. **"Tested by the Word" (Likipimwa kwa Neno)** ziliandikwa katika majira ya vuli ya mwaka **1914** na wachungaji:

- **R. W. Munson**
- **D. E. Robinson**

.

**MWISHO WA KIAMBATISHO: "karama ya unabii"** imeeleza mambo makuu yafuatayo:

1. **Mungu ameendelea kuwasiliana na wanadamu baada ya anguko la mwanadamu.**
2. **Karama ya unabii imeonekana katika vipindi vyote vya historia ya Biblia:**
    - Enoko,
    - Ibrahimu,
    - Isaka,
    - Yakobo,
    - Musa,
    - Manabii wa Israeli,
    - Yohana Mbatizaji,
    - Mitume,
    - Yohana wa Ufunuo.
3. **Karama ya unabii ilipungua wakati wa uasi mkubwa wa kanisa**, lakini kulingana na unabii wa Biblia ingerejeshwa katika siku za mwisho.
4. **Kanisa la masalia linatambulishwa kwa:**
    - kushika amri za Mungu,
    - kuwa na ushuhuda wa Yesu Kristo, yaani Roho ya unabii.
5. **Karama ya unabii inapaswa kupimwa kwa Biblia**, si kwa hisia au madai ya kibinadamu.
6. **Kristo ndiye kiini cha kila ujumbe wa kweli wa unabii.**
7. **Sheria ya Mungu na Maandiko Matakatifu vinaendelea kuwa kiwango cha mwisho cha kweli.**
8. **Matunda ya huduma ya nabii wa kweli yanaonekana katika:**
    - kumwinua Kristo,
    - kuongoza watu kwenye Biblia,
    - kuleta toba na utakatifu,
    - kuimarisha imani.
9. **Maisha na kazi ya Ellen G. White vinawasilishwa kama udhihirisho wa karama ya Roho ya unabii katika siku za mwisho.**

**REJEA (VYANZO)**

Maudhui ya sura arobaini fupi zilizounda kitabu hiki zimechaguliwa kutoka katika maandishi ya Bi. White, kama yanavyopatikana kwenye vitabu vyake: *"Life Sketches of Ellen G. White*," "*Early Writings*," and "*Testimonies for the Church*," Volumes 1-9, na kutoka kwenye nakala zake za *Review and Herald*, na ripoti za mahudhurio yake ya mikutano ya Konferensi Kuu, kama zilivyozachapwa katika *General Conference Bulletin*.

Sura ya 1-6 na 8-12 zimechukuliwa kutoka kwenye *Life Sketches of Ellen G. White*, 17-103.

Sura ya 7 na 13-18 zimechukuliwa kutoka kwenye "*Early Writings*," sura zinazoonekana kwa wingi, pia sura 21

Sura ya 19, 20, na 22-25 zimechaguliwa kutoka kwenye *Life Sketches of Ellen G. White*, 105-159.

Sura ya 26 inatoka kwenye "*Testimonies for the Church* 1:127-131.

Sura ya 27 inatoka kwenye "*Testimonies for the Church* 1:347-353.

Sura 28-30 zinatoka kwenye "*Early Writings*."

Sura ya 31 inatoka kwenye "*Testimonies for the Church* 2:594-597.
Sura ya 32 inatoka kwenye *Testimonies for the Church* 5:207-216.

Sura ya 33, "Muundo nna Maendeleo," imechaguliwa kutoka kwenye *General Conference Daily Bulletin*, January 29, 1893; *Review and Herald*, June 3, 1884; Review *and Herald*, July 26, 1892; *Testimonies for the Church* 3:446, 447; *Testimonies for the Church* 2:56 na 57, Series B; na *Gospel Workers*, 303.

Sura ya 34 inatoka kwenye *General Conference Daily Bulletin*, February 27, 1893.

Sura ya 35, 36, na 38 zinatoka kwenye "*Life Sketches*,"

Sura ya 37 inatoka kwenye *Testimonies for the Church* 6:23-29.
Sura 39 inatoka kwenye *Testimonies for the Church* 8:41-45.
Sura ya 40 inatoka kwenye *Testimonies for the Church* 9:285-288.

Maada ndogondogo zimeandikwa pamoja na Kiambatanisho kuhusu "Karama ya Unabii" ili kumsaidia msomaji,